**29 MEI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Thelathini na Tano – Tarehe 29 Mei, 2023

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Daniel B. Sillo) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**MHE. MINZA S. MJIKA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaanza Ofisi ya Rais TAMISEMI,namwita Mheshimiwa Jafar Chaurembo Mbunge wa Mbagala sasa aulize swali lake kwa niaba yake Mheshimiwa Dorothy Kilave.

Na. 452

**Ujenzi wa Stendi ya Mabasi yaendayo Mikoa ya Kusini**

**MHE. DOROTHY G. KILAVE K.n.y. MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga Stendi ya Mabasi yaendayo Mikoa ya Kusini katika eneo la Mbagala?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI Mheshimiwa Deo Ndejembi majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Jimbo la Mbagala kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na stendi ya mabasi yaendayo kusini katika eneo la

Mbagala. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Temeke imetenga kiasi cha shilingi bilioni mbili kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya kuanza ujenzi wa stendi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Temeke inaendelea na taratibu za kupata eneo la kujenga stendi hiyo katika Kata ya Mbagala. Pindi eneo litakapopatikana ujenzi utaanza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali langu la kwanza; kwa kuwa fedha za ujenzi zilitengwa tangu 2023/2024 na kwa kuwa eneo hakuna;

Je, ni kwa nini hizo fedha zisitumike sasa kufidia eneo la kujenga stendi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; kutokana na umuhimu wa stendi hiyo juu ya Serikali pamoja na wananchi wa Temeke;

Je, haioni sasa kuna umuhimu wa kuwa na sababu ya kuipa fedha za miradi ya mikakati Halmashauri yetu ya Temeke ili kuendeleza ujenzi huu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Chaurembo; la kwanza, hili la mwaka wa fedha 2024/2025 hii ni fedha ambayo wameitenga. Kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, fedha hii bilioni mbili imetengwa katika mwaka wa fedha tunaoenda kuanza, yaani *July* mwaka 2023/2024 sasa ni maamuzi yao wenyewe kupitia kikao chao cha *finance* na maamuzi ya halmashauri, kama wataweza kufanya fidia kutokana na fedha hii wanaweza wakalipa ili wa-secure ili lile eneo liwe ni la kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali la pili, umuhimu wa Serikali kuipa fedha, Halmashauri ya Manispaa ya

Temeke. Tunatambua kwamba ni jambo la muhimu sana kuwa na maeneo ya miradi ya kimkakati hapa nchini ili kuziwezesha halmashauri zetu kuongeza uwezo wa kipato. Tutawapatia fedha wakiandika andiko na kulileta Ofisi ya Rais TAMISEMI na kisha sisi kulichakata na kulipeleka katika Wizara ya Fedha ambapo ndio wanaotoa fedha hizi. Kwa hiyo niwaatoe hofu wana Temeke na wana Mbagala kwamba pale tutakapo pokea andiko lao basi tutatenga fedha hizo kwa ajili ya ujenzi wa stendi hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Florent Kyombo, swali la nyongeza.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakazi wa Mkoa wa Kagera wamekuwa wakipata adha kwa kukosa stendi ambayo iko ndani ya Manispaa ya Bukoba, ambayo Mbunge wa Jimbo ndugu yangu Steven Byabato amekuwa akifatilia.

Je, ni lini sasa Stendi hiyo itajengwa ili kuweza kusaidia wananchi wa Mkoa wa Kagera?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kyombo kuhusu stendi ya Manispaa ya Bukoba. Serikali itapeleka fedha hizo pale maandiko haya yatakuwa yamepitiwa na kuona *sustainability*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni miradi ya kimkakati, na kwa kuwa ni ya kimkakati lazima ioneshe *sustainability,* kwamba watakapopatiwa fedha na kujenga miradi hii basi halmashauri itaweza kuingiza mapato ya kujiendesha. Kwa hiyo pale ambapo tutamaliza mchakato wa ku-*review* andiko hili lililoletwa na Manispaa ya Bukoba tutawasilisha Wizara ya Fedha ili nao waweze kutenga fedha kwa ajili ya stendi hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuulizwa swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halmashauri ya Wilaya ya Karatu pia ina mpango wa kujenga stendi ya kisasa, na kwenye bajeti ijayo, halmashauri umetenga fedha kidogo, tunajua haitaweza kutosheleza.

Je, Serikali kuu iko tayari sasa ku *top-up* hicho kidogo kilichotengwa na halmashauri ili malengo yaweze kufikiwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Paresso la Stendi ya Karatu. Kwanza ni pongeze jitihada za halmashauri ya Karatu kwa kutenga fedha zao kwenye mapato ya ndani kwa ajili ya ujenzi wa stendi hii. Ni dhamira ya Serikali hasa hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha inawezesha halmashauri zetu zote nchini kuwa na uwezo wa kupata mapato, kama nilivyosema awali, ambayo ni *sustainable* kwa ajili ya uendeshaji wa halmashauri hizi. Hivyo tutakapo pokea andiko kutoka Halmashuri ya Karatu juu ya ujenzi wa stendi hii basi tutaangalia tutachakata andiko hilo na kuliwasilisha Wizara ya Fedha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Kiswaga Mbunge wa Kalenga kwa niaba yake atauliza Mheshimiwa Tumaini Magesa.

Na. 453

**Kuimarisha Vituo vya Afya vya zamani**

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA K.n.y. MHE. JACKSON G. KISWAGA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha Vituo vya Afya vya zamani ikiwa ni pamoja na kujenga Chumba cha kuhifadhi Maiti?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, Mbunge wa Jimbo la Kalenga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya. Tayari Ofisi ya Rais TAMISEMI, imekwishakusanya orodha ya vituo vya afya vinavyohitaji ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais TAMISEMI, ilipoanza kusimamia mpango maalum wa kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya ya msingi mwezi Oktoba 2023, jumla ya vituo vya afya 379 kati ya vituo vya afya 697 vimekarabatiwa na kuongezewa miundombinu iliyopungua ikiwemo wodi za uzazi, vyumba vya upasuaji na majengo ya kuhifadhia maiti. Jumla ya majengo 117 ya kuhifadhia maiti yamejengwa na kuwekewa majokofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imepanga kukarabati vituo vya afya 50 kupitia fedha za Mfuko wa Afya wa Dunia, ili kuviwezesha vituo hivyo kutoa huduma za dharura na upasuaji kwa mama mjamzito. Serikali, itaendelea kutoa fedha kwa ajili ya kukarabati vituo vya afya ili kuviwezesha kutoa huduma zinazokosekana likiwemo jimbo la Kalenga.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tumaini Magesa swali la nyongeza.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hali iliyoko Kalenga ni sawa sawa na hali iliyoko Busanda tunavyo vituo viwili vya Chikobe na Bukori. Nini mkakati wa Serikali wa kuviboresha vituo hivyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu swali lake la nyongeza la lini Serikali itatenga fedha za katika Vituo vya Afya vya Chikobe na Bukoli. Ni lengo la

Serikali kuhakikisha inajenga vituo vya afya vya kimkakati kote nchini; na ndiyo maana katika mwaka wa fedha huu ambao unamalizika tarehe 30 Juni mwaka huu Serikali ilitenga bilioni 117 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati kote nchini. Hivyo basi tutaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi huo. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pale ambapo fedha zitapatikana tutavitenga vituo hivi vya afya vya Chikobe na Bukoli.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Songe swali la nyongeza.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kituo cha Afya cha Kiloreli kilipandishwa hadhi, kutoka zahanati na baadaye kikawa kituo cha afya, lakini bado hakina majengo yoyote yenye kukidhi kuwa kituo cha afya;

Je, Serikali ina mpango wowote kuleta fedha kwa ajili ya kuongeza majengo pale?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba inajenga majengo yote ambayo yanahitajika kwenye vituo vya afya hapa nchini, kikiwemo ambacho amekitaja Mheshimiwa Songe cha kule Wilayani Busega. Hivyo basi kadri ya upatikanaji wa fedha tutahakikisha tunapeleka fedha katika kituo hiki cha afya ili kiweze kuapata majengo yanayohitajika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wananchi wa Bunda Mjini katika Kata ya Manyamanyama walianza ujenzi wa nyumba mbili za watumishi kwa nguvu zao;

Je, ni lini Serikali sasa mtakamilisha maboma hayo ya nyumba za watumishi ambayo yamekaa kwa muda mrefu kwenye Hospitali ya Manyamanyama?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi hii kuwapongeza sana wananchi wa Bunda Mjini na wa Kata hii ya Manyamanyama kwa kuweza kujitoa na kuanza ujenzi wa majengo ya nyumba za watumishi. Serikali itafanya tathmini ya majengo hayo kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Bunda Mjini, na pale tathmini itakapokamilika tutaona ni namna gani tunatenga fedha katika mwaka wa fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege Mbunge wa Kalambo sasa aulize swali lake.

Na. 454

**Ujenzi wa Kituo cha Afya Kasanga – Kalambo**

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza: -

Je, ni lini ahadi ya kujenga Kituo cha Afya Kata ya Kasanga itatekelezwa?

**MWENYEKITI:**Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Jimbo la Kalambo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itatekeleza ahadi ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kasanga kama iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alivyotembelea Kata ya Kasanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati kote nchini

kikiwemo Kituo cha Afya Kasanga kama ilivyoelekezwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Josephati Sinkamba swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nipongeze majibu mazuri ya Serikali. Lakini pamoja na pongezi hiyo naomba niulize maswali madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhitaji wa vituo vya afya kwa ajili ya kutoa huduma za afya unahitajika sana katika Wilaya ya Kalambo na Halmashauri ya Kalambo na wananchi kwa kulijua hilo wameweza kujenga zahanati nane na ziko usawa wa *lintel*. Zahanati hizo ni pamoja na Uyumi, Sengakalonje, Limba, *just to mention*. Je, Serikli haioni kwamba iko sababu ya kuhakikisha kwamba inapeleka fedha ili kumalizia juhudi kubwa zilizofanywa na wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, uhitaji wa kujenga kituo cha afya katika Kata ya Katete ni wa muhimu sana kwa kuzingatia jiografia yake; Je, Serikali haioni kwamba iko sababu ya kuhakikisha kwamba katika bajeti inayokuja maeneo haya yanapelekewa fedha ili vituo vya afya vijengwe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kandege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza juu ya hizi zahanati ambazo zimejengwa kwa jitihada za wananchi wa kule Kalambo. Kwanza nitoe pongezi tena kwa wananchi wa kule Kalambo kwa jitihada zao za kujenga maboma haya ya zahanati, lakini vile vile niseme mbele ya Bunge lako tukufu kwamba ni azma ya Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha ina boresha afya za Watanzania kwa kujenga zahanati na vituo vya afya, hospitali za wilaya na hospitali za mikoa na rufaa kadri ya

upatikanaji wa fedha. Hivyo basi sisi kama Serikali tutaangalia zahanati hizi na kuona ni namna gani tunaweza tuka-*support* katika mwaka wa fedha wa 2024/2025 katika umaliziaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda katika swali lake la pili la kujenga Kituo cha Afya cha Katete. Tutatuma timu kule Kalambo kwenda kufanya tathmini ya Kituo hiki cha Afya cha Katete, na tutaona ni namna gani tunaweza tuka-*support* jitihada hizi ambazo Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa kule Kalambo wote wamezifanya, za kupata kituo cha afya hapa. Mara tu tathmini itakapokamilika basi tutaona ni namna gani tunatenga fedha katika mwaka wa fedha wa 2024/2025.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Kwa kuwa nilishaomba Kata ya Mgombasi tunashida ya kuwa na kituo cha afya ilhali ni kata ambayo ina watu wengi sana.

Je, Serikali iko tayari kutuambia ni lini au iko katika mpango wa bajeti hii kujenga kituo cha afya kata ya Mgombasi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotoka kujibu swali la Mheshimiwa Kandege la kutuma timu kufanya tathmini ya kuona wingi wa watu na uhitaji wa kituo cha afya, basi pia nichukue nafasi hii kusema kwamba timu hii tutahakikisha pia inafika kwa Mheshimiwa Kawawa kule katika kata ya Mgombasi na kufanya tathmini na kuona idadi ya watu waliokuwa pale na uhitaji uliopo ili Serikali iweze kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho cha afya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kata za Kia, Muungano, Uroki, Mnadani na Weruweru ni kata ambazo hazina vituo vya afya na wananchi

wanatembea umbali mrefu sana kwenda kufata huduma kule Bomang'ombe.

Je, ni lini Serikali itajenga vituo vya afya kwenye kata hizi muhimu sana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itajenga vituo vya afya hivi muhimu katika Kata za Kia, Muungano, Uroki katika halmashauri ya Wilaya ya Hai kadri ya upatikanaji wa fedha. Lakini vile vile nichukue nafasi hii mbele ya Bunge lako Tukufu kumwelekeza Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro kuweza kufanya tathmini ya zahanati hizi zilizoko katika kata alizozitaja Mheshimiwa Saashisha ili kuona ni namna gani zinakidhi vigezo vya kupandishwa hadhi na kuwa vituo vya afya ndipo tuweze kuona ni namna gani tunatenga fedha katika mwaka wa fedha wa 2024/2025.

**MWENYEKITI:**Mheshimiwa Asha Abdullah Juma swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa juhudi kubwa za Serikali zimefanyika kujenga hospitali vituo vya afya vya kileo;

Je, Serikali ina mpango gani kuhimarisha huduma ya kinywa na meno katika vituo vya afya na zahanati zote nchini, kwa sababu sehemu hiyo inaonekana kusahaulika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni azma ya Serikali kuhakikisha inaboresha afya za Watanzania ikiwemo afya ya kinywa na meno. Na ndio maana Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imetenga fedha nyingi sana katika ununuzi wa vifaa tiba vikiwemo hivi vya kinywa na meno. Tayari tuna timu ya Ofisi ya Rais TAMISEMI ambayo inazunguka kwenye maeneo yote yaliyopatiwa vifaa tiba

kutoa mafunzo kwa wataalam wetu kuona ni namna gani wanaweza kuanza kutumia vifaa hivi kutoa huduma ya kinywa na meno kwenye hospitali zetu za wilaya na kwenye vituo vyetu vya afya vya kimkakati.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida, swali la nyongeza.

**MHE AIDA J. KHENAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kituo cha Afya Kabwe kikikamilika kinategemea kuhudumia zaidi ya kata tatu. Je, ni lini sasa Serikali itapeleka fedha ili kumalizia kituo hiki kifanye kazi katika hizo kata tatu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itapeleka fedha katika Jimbo la Nkasi kwa Mheshimiwa Aida kule kwa ajili ya kujenga kituo cha afya ambacho amekitaja kadri ya upatikanaji wa fedha. Vilevile nitumie nafasi hii kusema tutatuma timu ambayo nimeisema pia itaelekea kule Kalambo kwa sababu ni mkoa mmoja timu hii pia iweze kufika katika kituo hiki cha afya na kufanya tathmini na kuona ni namna gani tunaweza tukatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hiki cha afya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu alipofanya ziara kwenye Wilaya ya Chemba kwenye Kijiji cha Itwalo aliahidi Serikali kujenga kituo cha afya, lakini hivyo hivyo kwenye Kata ya Tarangi. Naomba kujua ni lini utekelezaji wa ujenzi huu utafanyika? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Monni kwanza nilitaarifu Bunge lako kwamba, Serikali inatoa kipaumbele cha

kukamilisha ahadi zote za Viongozi wetu wa Kitaifa kuanzia Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi tutaangalia katika kata hizi mbili ambazo Mheshimiwa Monni amezitaja ni namna gani tunaweza tukatenga fedha ama kama imetengewa fedha kwenye mwaka huu wa fedha unaoenda kuanza wa 2023/2024, tuweze kuanza ujenzi huu mara moja na kama fedha haijatengwa, basi tutenge fedha kwenye mwaka wa fedha wa 2024/2025.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake

Na. 455

**Hitaji la Stendi – Chemba**

**MHE. KUNTI Y. MAJALA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha za ujenzi wa stendi ya Wilaya ya Chemba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba kuwa na Stendi ya Mabasi na kwa kuzingatia umuhimu huo tayari imetenga eneo lenye ukubwa wa ekari 22 na tathmini ya gharama za ujenzi wa stendi hiyo ni takribani milioni 643.82.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuanza na kukamilisha stendi hiyo, Halmashauri ya Wilaya ya Chemba inashauriwa kuandaa andiko la mradi huo ili liweze kutumika kutafuta fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa mradi huo kutoka vyanzo mbalimbali vya fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti, swali la nyongeza.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Suala la andiko tayari Wilaya ya Chemba mwaka 2020/2021 tulishaandika hilo andiko na likaenda TAMISEMI na TAMISEMI wakatushauri tuanze kwa mapato yetu ya ndani. Mpaka sasa tumeshatumia zaidi ya milioni 36 kwa ajili ya ulipaji wa fidia pamoja na kufanya usafi katika eneo hilo. Sasa tunataka kujua, je, ni lini Serikali inakwenda kutekeleza maagizo yake kwenye suala zima la ujenzi wa stendi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, stendi hii pia mwaka 2020 Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati John Pombe Magufuli alipopita Wilaya ya Chemba wananchi wa Wilaya ya Chemba walimwomba ujenzi wa stendi hii na akaahidi itajengwa haraka iwezekanavyo. Sasa na Mheshimiwa Waziri umesema hapa kwamba mko kwenye mchakato wa kukamilisha ahadi zote za viongozi. Je, ni lini Serikali inakwenda kutekeleza ahadi hii ya Hayati John Pombe Magufuli ili tuweze kumuenzi wananchi wa Wilaya ya Chemba? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kunti Majala, hili la kwanza la andiko. Mpaka sasa Ofisi ya Rais, TAMISEMI haijapokea andiko lolote kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Chemba juu ya ujenzi wa stendi hii, si kusema kwamba Serikali haijapokea, andiko hili huenda liliandikwa likapelekwa moja kwa moja Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutafuatilia juu ya andiko hili la Chemba na nitakaa na Mheshimiwa Mbunge kuweza kuona andiko hili limefikia wapi na kama kuna marekebisho yoyote, basi yaweze kufanyika na kurejeshwa tena kufanyiwa tathmini ili fedha iweze kutafutwa kadri ya upatikanaji wake kwenda kujenga stendi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali lake la pili la ahadi ya Mheshimiwa Rais, nirejee tena kusema ni kipaumbele cha Serikali kuhakikisha inatekeleza ahadi zote za Viongozi wetu Wakuu wa Nchi kuanzia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu kadri ya upatikanaji wa fedha na tutaangalia ili tuone tunatenga fedha kwenye mwaka upi wa fedha kadri bajeti itakavyoruhusu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wiliam Mbunda, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Serikali ina mpango wa kujenga miradi ya kimkakati katika halmashauri mbalimbali, Halmashauri ya Mji wa Mbinga ni moja ya halmashauri ambayo inatakiwa ipate miradi hiyo ya kimkakati, nataka nijue kupitia mradi wa *TACTIC* ni lini serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kujenga mradi huo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii ya kimkakati upatikanaji wake unaendana sambamba na tutakavyopokea maandiko kutoka kwa wataalam wetu kwenye halmashauri mbalimbali nchini ikiwemo Halmashauri ya Mbinga na Mradi wa *TACTIC* alioutaja upo unaratibiwa na Taasisi ya *TARURA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakaa na Mheshimiwa Mbunge kuona kama *TACTIC phase one* mradi wa mkakati wote upo katika halmashauri ile, kama haupo tuone ni *phase two,* kama haupo tuone kama ni *phase three,* lakini nitumie jukwaa hili la Bunge lako Tukufu kusema tu kwamba kuwaasa wataalam wetu Maafisa Mipango na Wakurugenzi wa Halmashauri kuwa wabunifu wanapofanya maandiko haya ya miradi ya kimkakati. Lengo la Serikali kutoa miradi hii ya kimkakati ni ili halmashauri ziweze kupata uwezo wa kimapato, wasibuni tu mradi ili mradi halmashauri fulani imefanya na wao wakataka, waangalie jiografia yao, eneo lao, ni mambo gani ambayo wakiyafanya basi miradi hii itawaingizia kipato.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Halmashauri ya Wilaya ya Momba ni miongoni mwa halmashauri 56 ambazo zimewekwa kwenye kundi ambalo tutapangiwa hela za maendeleo asilimia 20. Je ni upi mkakati wa TAMISEMI kutujengea stendi kwenye Kata ya Kamsamba ukanda wa chini, Kata ya Ikana ukanda wa juu kwa sababu sehemu zote hizi zinaunganisha Mkoa wa Songwe na Mkoa wa Rukwa na kuna uhitaji kubwa sana wa stendi ili zitumike kaka chanzo cha mapato kwenye halmashauri.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Sichalwe amekuwa akilifuatilia sana hili na amekuja mara kadhaa Ofisi ya rais TAMISEMI kulifuatilia hili jambo na tutaendelea kutenga fedha kadri ya upatikanaji wake ili tuweze kuwajengea wananchi wa Momba stendi hizi na kuiwezesha Halmashauri ya Momba kuwa na uwezo wa kupata fedha ya mapato kutokana na miradi hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, swali la Mheshimiwa Asya Sharif Omar, Mbunge wa Viti Maalum, litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Maimuna Mtanda

Na. 456

**Kutoa mafunzo ya kuogelea kwa wakulima wa mwani – Zanzibar**

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA K.n.y. MHE. ASYA SHARIF OMAR** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kutoa mafunzo ya kuogelea kwa wakulima wa Mwani Zanzibar?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asya Sharif Omar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa zao la mwani katika kuongeza kipato, ajira na kukuza uchumi katika ukanda wa pwani na Taifa kwa ujumla. Vilevile, inatambua kuwa, zaidi ya asilimia 90 ya wakulima wa mwani ni wanawake. Ili kuwa na kilimo endelevu na kulinda usalama wa wakulima wa mwani wawapo katika shughuli zao, ni muhimu wakulima hawa kuwa na ujuzi wa kuogelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimekuwa na mikakati mbalimbali kuhakikisha wakulima wa mwani wanapatiwa nyenzo bora za kuhakikisha usalama mahali pa kazi. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zitatoa mafunzo ya kuogelea kwa wakulima wa mwani pamoja na kununua na kusambaza vifaa vya kulinda usalama wakiwa kwenye maji wakishughulika na kilimo cha mwani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA SALUM MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Serikali imekiri kabisa kwamba asilimia kubwa ya wakulima wa zao hili ni wanawake, je, mkakati wa kutoa elimu pia kuwahusisha wanaume ili na wao waweze kujiongezea kipato kupitia zao hili ukoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa *product* itokanayo na zao la mwani ni muhimu sana kwa afya ya wananchi wote wakiwemo wanaume pamoja na wanawake. Je Serikali haioni haja sasa ya kutumia Vyombo vya Habari kuujulisha umma umuhimu wa zao hili ili wananchi wengi waweze kulilima na kupata mazao au kupata ajira zitokanazo na zao hili? Ahsante

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kutambua umuhimu wa zao hili na jitihada mojawapo ya sasa na mkakati ambao tulionao katika maeneo ambayo yanazunguka Ukanda wa Pwani na wamekuwa wakituona maeneo mbalimbali ni kutangaza kwa makundi yote mawili wanawake na wanaume kuhakikisha wanashiriki katika zao hili la mwani. Kwa hiyo kazi hiyo tunaifanya na tutaongeza jitihada kuifanya ili ongezeko la watu wanaojihusisha na shughuli hizo wawe wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutumia Vyombo vya Habari, sasa hivi tumekuwa tukifanya ukiangalia *TBC* kuna vipindi vinavyohusisha kilimo cha mwani, lakini tutaongeza mara dufu zaidi ili tutanue wigo mpana ili vyombo vya Habari viweze kuwafikia wananchi katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo jambo hilo tumelipokea na tutalifanya, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Wilaya ya Kigamboni ina ukanda wa bahari takribani kilomita 70, nataka kujua nini mkakati wa Serikali wa kukuza kilimo cha mwani na jongoo bahari katika Wilaya ya Kigamboni kama mkakati wa kuchochea uchumi wa bluu na kuongeza ajira nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwondoe shaka Mheshimiwa Mbunge kwamba moja ya mkakati wetu mkubwa ni kuhakikisha tunafikia maeneo

yote ya ukanda wa pwani na ndio maana hivi karibuni tumepata fedha kutoka maeneo mbalimbali. Juzi tumesaini mkataba wa fedha karibu dola milioni 13 na watu wa *USAID* na sehemu ya hizo fedha ni pamoja na kuhamasisha kilimo cha mwani na majongoo bahari katika Ukanda wa Pwani ikiwemo Kigamboni. tumefanya hivyo Ifani, Tanga, kwa hiyo ni jambo ambalo lipo katika mchakato. Ahsante

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Sasa tunaenda Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 457

**Ukosefu wa masoko ya uhakika kwa mazao nchini**

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto ya bei ndogo za mazao pamoja na ukosefu wa masoko ya uhakika nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Anthony Mavunde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ya kuhakikisha wakulima wanapata bei shindani na masoko ya uhakika. Mikakati hiyo ni pamoja na kuongeza tija kwenye uzalishaji kupitia uwekezaji katika miundombinu ya umwagiliaji, pembejeo, utafiti, huduma za ugani, matumizi ya teknolojia na kurasimisha Sekta ya Kilimo Mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali inaendelea kuhamasisha kilimo cha kibiashara kinachozingatia mahitaji ya soko; kushiriki makongamano na maonesho ya kibiashara na uwekezaji kwa lengo la kutangaza bidhaa na maeneo ya uwekezaji katika sekta ya kilimo; kushirikiana na Sekta Binafsi katika ujenzi wa miundombinu ya masoko; kuimarisha mifumo ya kielektroniki ambayo itawezesha upatikanaji wa taarifa za masoko kwa wakati; kutoa mafunzo kuhusu kilimo biashara kwa Maafisa Ugani na Wakulima na kuendelea kufungua masoko mapya katika nchi mbalimbali kwa kufanya tafiti za mahitaji kwa nchi husika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nimshukuru waziri kwa majibu yake mazuri sana aliyoyatoa hapa hivi sasa, lakini nina maswali yangu mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa suala hili ni la muda mrefu, je, Serikali inaweza kutuambia nini hali halisi kwa sasa pamoja na mifano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; kwa kuwa ongezeko la thamani, mazao yetu hapa nchi kuna maboresho ya mazao yetu, je, Serikali iko tayari kutengeneza viwanda vidogovidogo katika wilaya zetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali halisi ya upatikanaji wa masoko ya mazao yetu. Nataka nikiri mbele ya Bunge lako kwamba hivi sasa katika baadhi ya mazao hasa mazao ya nafaka soko la mazao haya limekuwa ni kubwa ndani na nje ya mipaka ya Tanzania na hivyo kuwawezesha wakulima wetu wengi kuwa na masoko ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hivyo katika matunda na mbogamboga pia na kwenyewe tunafanya vizuri hivi

sasa parachichi letu limepata nafasi ya kwenda katika masoko ya Hispania, China, Marekani, pamoja na Afrika ya Kusini hii ni ishara njema kuonesha kwamba kuna kazi imefanyika kwenye kutangaza mazao yetu, lakini pia kwenye kahawa na korosho na mazao mengine pia tunafanya vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili la kuongeza thamani, ni mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba tunaendelea kuongeza thamani ya mazao yetu ya kilimo. Mkakati uliopo hivi sasa ni kuhakikisha kwamba tunajenga uwezo kwa uanzishaji wa viwanda vidogovidogo kuanzia kule katika eneo la korosho na mazao mengine ya nafaka. Hivi sasa bodi ya mazao mchanganyiko yenyewe tu imeshaendelea kuwekeza katika vinu vingi vya kusaga mazao ya nafaka ili kuongeza thamani ya mazao yetu. Hii ni hatua ya Serikali lakini pia na sekta binafsi wanatuunga mkono.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Leah Komanya, swali la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Nataka kujua kauli ya Serikali kuhusu kuporomoka kwa zaidi ya asilimia 50 kwa bei ya alizeti kwa wakulima na hali nchi ina upungufu mkubwa wa kujitosheleza katika uzalishaji wa mafuta ya kula?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli bei ya alizeti imeporomoka na imesababisha kuwakatisha tamaa wakulima, lakini sisi Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Fedha tumekaa chini na kuangalia namna bora ya kuweza kutatua changamoto hii ikiwemo kuangalia sera zetu za fedha na hasa katika kuliboresha eneo la kuongeza kodi kwa mafuta ambayo yanaagizwa kutoka nje ya nchi ili kuweza kuwalinda wakulima wetu wa ndani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali la nyongeza

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa kuwa asilimia 72 ya zao la tangawizi inalimwa ndani ya Jimbo

la Same Mashariki na kwa kuwa bei ya zao hili kwa wananchi bado siyo rafiki kabisa. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri aniambie watatumia mkakati gani wa kuwafanya hawa wananchi wapate bei ambayo itawatia moyo wa kuendelea kulima zao hili muhimu nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua kwamba tunao wajibu kama Serikali kuhakikisha kwamba wakulima wanapata bei bora ya mazao yao, Serikali imeanzisha mamlaka maalum ambayo inaitwa *COPRA* kwa ajili ya usimamizi wa masoko na bei ya wakulima ikiwemo wakulima wa tangawizi. Nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutahakikisha tunashirikiana sisi na yeye ili wakulima wake waweze kupata bei bora na kilimo kiweze kuimarika katika eneo lake hilo la Same.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi ya kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri, Chuo cha *TARI* Naliendele zaidi ya miaka 20 sasa wamekamilisha utafiti unaoonesha kwamba kutokana na *nipa* inayopatikana kwenye korosho ina uwezo wa kuzalisha *ethanol methanol* pamoja na *alcohol* kwa matumizi ya burudani pamoja na hospitali, lakini pia kuongezea kipato wakulima na kupunguzia Taifa hili hasara. Je nini mkakati wa Serikali kuhakikisha sasa *nipa* inakuwa rasmi kwa ajili ya kupunguzia hasara Taifa letu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia hoja ya Mbunge, tutaishirikisha *TAR*I pamoja na Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali ili ikibainika kwamba *nipa* hiyo inaweza ikatumika katika maeneo ambayo ameyataja, basi sisi kama Serikali kwa kushirikiana na *TARI* tutasaidia kuongeza mnyororo wa thamani wa zao la korosho.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Edward Kisau, swali la nyongeza.

**MHE EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuwa wakulima walihamasika sana kuhusu alizeti na bei imeteremka na wakati wanaangalia sheria ili wazuie mafuta yanayotoka nje, kwa nini Serikali isifanye *commitment* au kununua alizeti yote ambayo wakulima wamelima?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumepata changamoto ya bei kuporomoka na ndiyo maana kwenye bajeti yetu Mheshimiwa Waziri alitamka kwenye kitabu chake cha bajeti uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo *(ADF) Agricultural Development Fund* ambayo kazi yake nyingine ni kwa ajili ya *price stabilization*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari njema ni kwamba tumeshapata amri kutoka Wizara ya Fedha ya uanzishwaji wa Mfuko huu na Mfuko utaanza kufanya kazi, natumai katika changamoto ambazo zitajitokeza baadaye basi Serikali kupitia Mfuko huu inaweza kufanya kazi hiyo kwa ajili ya kuwa *rescue* wakulima. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, sasa aulize swali lake.

Na. 458

**Mikopo kwa Wakulima wa Korosho**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuhakikisha kuwa wakulima wa korosho wanapata mikopo nafuu ili waweze kugharamia kilimo hicho?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Jimbo la Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania inaratibu uwezeshaji wa wakulima wa korosho kupata mikopo ya kuendeleza zao la korosho ikiwemo pembejeo na utunzaji wa mashamba. Uwezeshwaji huo utafanyika kupitia Vyama Vikuu vya Ushirika kuwawekea dhamana wakulima ili waweze kupata mikopo kutoka katika taasisi za fedha

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali inaendelea na jitihada mbalimbali za kuwaunganisha wakulima na taasisi za fedha ili waweze kupata mikopo yenye riba nafuu kuanzia asilimia tisa kushuka chini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Dadi, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza baada ya Serikali kuanza kutoa ruzuku za pembejeo baadhi ya benki zimeacha kabisa kutoa mikopo kwa wakulima wakati gharama ya zao la korosho sio pembejeo tu, kuna gharama ya matayarisho ya mashamba na gharama za uvunaji.

Je, Serikali inatoa tamko gani kwa benki hizo? *(Makofi)*

Swali langu la pili, changamoto ambazo zinawakabili wakulima wa mazao ya kimkakati, pamba, korosho, chai, alizeti zingeweza kutatuliwa na mfuko wa maendeleo ya kilimo.

Serikali inaweza kutoa tamko, je, ni lini sasa Mfuko huo utaanza kufanya kazi rasmi ili kuwasaidia wakulima hawa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwezeshwaji wakulima kupitia taasisi za fedha, kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi Serikali pamoja na Tume ya Maendeleo ya Ushirika, tutakaa kwa pamoja na taasisi za kifedha kuona namna bora ya kuweza kuwawezesha wakulima hasa wa korosho na hivi sasa tumeanza hatua za awali, tumeshakaa na benki, ziko changamoto ambazo zimejitokeza hasa za urejeshaji wa mikopo hii, lakini hii ilitokana na changamoto kwamba wakulima wengi walikuwa hawajasajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tumeanza kuwasajili wakulima, kila mkulima atatambulika eneo lake alipo, shamba lake lilipo na ukubwa wa shamba ili kuirahishia benki namna bora ya kuweza kuwapatia mikopo na tunaamini kupitia njia hii wakulima wengi zaidi watapata mikopo katika taasisi za fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa mujibu wa Sheria za Fedha za Umma Sura Namba 347 Kifungu cha 17 (1) cha Sheria ile, kimetoa amri ya uanzishwaji wa Mfuko wa maendeleo ya kilimo. Mfuko tayari tumeshapata amri ya kuanzisha, umeanza kazi na tumeshateua na Meneja wa Mfuko na Mhasibu Mkuu, punde tutaendelea kuhakikisha kwamba tunapata vile vyanzo vya kuutunisha Mfuko huu ili basi inapotokea changamoto mbalimbali na hasa katika kuwawezesha wakulima kuweza kupata huduma mbalimbali Mfuko huu uweze kutumika.

**MWENYEKITI:** Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, karibu Mheshimiwa.

Na. 459

**Hitaji la kuwa na ujazo tofauti na kilo 50 wa mbolea**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza:-

Je, Serikali ipo tayari kuzungumza na wenye viwanda vya mbolea ili kuwe na ujazo wa kilo tofauti na 50?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyeketi, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 32, (4) na (5) pamoja na Kanuni ya 33(1) ya Kanuni za Mbolea za mwaka 2011, wazalishaji au waingizaji wa mbolea wanaruhusiwa kufungasha mbolea katika ujazo unaofaa kwa watumiaji mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbolea zilizo katika hali ya yabisi *(solid fertilizers)* zinapaswa kufungashwa katika ujazo wa kilo tano, 10, 25 na 50. Mbolea zilizo katika hali ya kimiminika *(liquid fertilizers)* zinapaswa kuwa katika ujazo wa mililita tano, 10, 20, 50 na 100. Aidha, visaidizi vingine vya mbolea kama vile chokaa mazao *(agricultural lime)* na jasi *(gypsum)* hufungashwa katika ujazo wa kilo tano, 10, 20, 50 na 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kusimamia wazalishaji wa mbolea kuzalisha mbolea kulingana na mahitaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Josephine, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Sswali la kwanza, kama ni hivyo ni kwa nini sasa mbolea hizo kwa vifungashio ulivyovitaja hazipo madukani? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa mvua za kwanza ni za kupandia. Je, katika Mkoa wa Kigoma kwa mwaka huu mbolea zitafika Mkoa wa Kigoma mwezi gani? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mbolea hizi za ujazo tofauti tofauti hutokana na mahitaji halisi ya maeneo husika

na aina ya mazao yanayolimwa. Kwa sababu imeonekana kuna mahitaji hayo, kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Ubora wa Mbolea Tanzania - *TFRA* tutatoa maelekezo kwa wazalishaji na waingizaji wa mbolea hapa nchini kuhakikisha kwamba wanatoa mbolea kulingana na mahitaji na hasa katika hoja ambayo Mheshimiwa Mbunge ameisema ya kuanzia kilo tano, 20, mpaka 10 na kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusu mbolea kufika lini. Tulishasema ndani ya Bunge lako Tukufu ya kwamba tunataka tuhakikishe changamoto za msimu uliopita safari hii zisijirudie na mbolea ifike nchini kwa wakati, wakati wakulima wetu wakiwa bado wana nguvu ya kuweza kununua hasa baada ya kuwa wametoka kuuza mazao yao. Ni *commitment* ya Serikali kwamba tutahakikisha ndani ya mwezi wa Saba mbolea imefika hapa nchini na wakulima waanze kununua kwa ajili ya msimu ujao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea Wizara ya Madini, Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 460

**Mikataba ya sekta ya uziduaji kuwa wazi**

**MHE. JESCA D. KISHOA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaweka wazi mikataba ya sekta ya uziduaji kama *The Extractive Industries Transparency Initiative* inavyotutaka?

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni mwanachama wa Asasi ya Kimataifa ya *EITI (Extractive Industries Transparency Initiative)*. Ambalo jukumu lake kuu ni kuhamasisha Serikali kuweka mifumo ya

uwazi katika rasilimali madini, mafuta na gesi asilia ili kuboresha mapato na manufaa yanayotokana na shughuli za utafutaji na uchimbaji wa rasilimali hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza takwa la uwekaji wazi wa mikataba Taasisi ya *TEITI* imeandaa Mpango kazi *(Roadmap)* kwa ajili ya utekelezaji wa kazi ya uwekaji wazi mikataba. Mpango huo umewekwa wazi kwa ajili ya utekelezaji kulingana na matwaka ya Kimataifa ya Taasisi ya *EITI*. Kwa hivyo, katika mwaka wa fedha 2023/2024 *TEITI* imeweka mkakati wa kuhakikisha kuwa mikataba inawekwa wazi, ikiwa ni pamoja na kushauriana na mamlaka nyingine za Serikali namna bora ya kutekeleza mikataba na takwa hili. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jesca David Kishoa, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tunayo Sheria Tanzania *Extractive Industry Transparency Initiative Act* ya mwaka *2016, Section Number 16* ambayo inataka mikataba yote ya Sekta ya Uziduaji iwekwe wazi na iwekwe wazi kwenye *website* pamoja na vyombo vya habari *media* zote Tanzania. Nataka kujua *commitment* ya Serikali, kwa sababu *EITI* wanakuja *validation* Tanzania mwaka huu.

Serikali imejipangaje kuhakikisha kwamba mnalinda *reputation* ya nchi kwa kuwa na sheria ambayo haitekelezeki kwa muda mrefu toka 2016? *(Makofi)*

Swali la pili, nataka *commitment* ya Serikali ni lini suala hili linakwenda kukamilika kwa sababu limekaa kwa muda mrefu sana? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimjibu Mheshimiwa Jesca Kishoa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa swali lake la kwanza, Wizara yetu ya Madini na wakifanya kazi pamoja na *TEITI* na mamlaka nyingine ya Serikali ikiongozwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali wako katika mchakato ambao unachambua na kufanya kazi kwa kushirikiana na kampuni zote zilizowekeza katika sekta za rasilimali hizi ili kuona namna bora ya kuweka wazi hiyo mikataba kwa mujibu wa matakwa ya Sheria ya Taasisi ya Kimataifa ya *EITI*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kwamba ni lini? Kwa ratiba tuliyonayo tunategemea kwamba kufika Mwezi wa Kumi mwaka huu taratibu zote zitakuwa zimekamilika na hivyo mikataba hiyo itakuja kuwekwa wazi kwa mujibu wa matakwa ya Taasisi ya Kimataifa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Luhaga Mpina, swali la nyongeza.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Kwa kuwa, Serikali imeendelea kukaidi na kukiuka sheria katika uingiaji na usimamizi wa mikataba ya uziduaji ambayo ni madini gesi na mafuta na pamoja na matakwa yale ya *TEITI* lakini pia kuna matakwa ya Sheria Kifungu 12 cha *(The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) No. (5) Act, 2017*) ambayo…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa swali.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ambayo inataka mikataba yote iletwe hapa Bungeni. Kwa nini Serikali inaendelea kukiuka matakwa haya ya kisheria? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali haina mpango wala haifanyi maksudi kwamba lazima sheria iliyowekwa ikiukwe. Sheria zote zinasimamiwa na Serikali na Wabunge wote nasi Watendaji wote wa Serikali tumeapa kusimamia sheria ya nchi na Katiba ya nchi, kwa hivyo kama kuna ambayo haitekelezwi ni suala lingine la kuangalia tu mikakati ya Serikali ya kujisimamia na kuhakikisha

kwamba sheria zinatekelezwa kwa mujibu wa jinsi zilivyotungwa lakini hakuna utaratibu wowote wa kwamba Serikali inakusudia na inavunja sheria yeyote.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, swali la Mheshimiwa Jonas Van Zeeland litaulizwa na Mheshimiwa Kwagilwa Reuben.

Na. 461

**Ujenzi wa barabara ya Turiani - Mziha**

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO K.n.y. MHE. JONAS V. ZEELAND** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Turiani hadi Mziha kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, Mbunge wa Mvomero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Turiani hadi Mziha, yenye urefu wa kilometa 35.5 kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami imekamilika. Serikali imepanga kujenga ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kwa awamu katika mwaka wa fedha 2023/2024. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kwagilwa Reuben, swali la nyongeza.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kwenye swali hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii inaunganisha Mkoa wa Tanga na Mkoa wa Morogoro pia imekuwepo kwenye Ilani za

Uchaguzi za CCM tangu enzi za Mzee Mkapa, Mzee Kikwete, Hayati Magufuli na sasa Rais Samia. Je, kwa nini Serikali isiweke Wakandarasi Mwaka wa Fedha 2023/2024 kwa barabara nzima kilometa 104 yaani Turiani – Mziha – Handeni badala ya kuweka kipande hicho kidogo? *(Makofi)*

Swali la pili la nyongeza, kwenye bajeti za Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2020/2021, 2021/2022, 2022/2023 na sasa 2023/2024 barabara hii imekuwa ikitengewa kiasi hiki cha fedha cha bilioni moja na majibu ya Serikali yamekuwa ni haya haya.

Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Mkoa wa Tanga na Mkoa wa Morogoro kuhusu barabara hii na ahadi zake zisizotekelezeka? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Reuben Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli barabara aliyoitaja ipo kwenye Ilani na ni kweli kwamba inaunganisha Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Tanga, ni barabara ambayo kwa kweli ina historia yake na kwa maana hiyo Serikali ilishaanza kuijenga hadi Turiani, kwa sasa Serikali imedhamiria kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kuanzia Turiani, Mziha hadi Handeni, Kilometa 104, lakini kuweka Wakandarasi zaidi ya mmoja utaharakisha lakini kutategemea sana na upatikani wa fedha ili kuweza kuweka Wakandarasi zaidi ya mmoja kwa kipindi kimoja. Dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba kwa mwaka ujao wa fedha tunaendelea pale tulipoishia kukamilisha barabara hii hadi Handeni. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oliver, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona.

Je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi wa barabara ya Katoma hadi Bukoli kwa kiwango cha lami ndani ya Wilaya ya Misenyi, Mkoani Kagera?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Semuguruka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Katoma kwenda Bukoli ipo inaendelea kujengwa lakini kwa awamu. Mwaka huu wa fedha imetengewa pia fedha ambapo tunategemea kwamba tutajenga zaidi ya kile tulichokuwa tunakijenga ili kuikamilisha barabara yote kwa kiwango cha lami. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itasaini mkataba wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, barabara kuanzia Kongwa – Kiteto – Simanjiro hadi Arusha na Tanga – Kiteto hadi Singida? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu swali moja.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti tulitaja barabara aliyoitaja Kongwa - Kibaya – Orkesumet - Losinyai hadi Arusha ambayo tunachosubiri sasa ni baada tu ya Bunge hili sasa ambalo tunategemea kabla ya Mwezi Juni barabara hiyo iwe imesainiwa kwa mpango wa *EPC + F.* Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Masasi – Nachingwea - Liwale itajengwa kwa utaratibu wa *EPC + F* tuliambiwa Mkandarasi amepatikana. Ni lini mkataba utatiwa saini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kama nilivyojibu katika swali ambalo nimeulizwa barabara hizi ziko saba na moja ya barabara hiyo ni ya Masasi – Nachingwea hadi Liwale. Mikataba ilishakamilika kinachosubiriwa ni muda na kwa sasa kwa sababu ni miradi mikubwa *signing* itafanyika muda wowote iko tayari kwa ajili ya *signing* na tunategemea kabla ya mwisho wa mwezi Juni barabara hii ya Masasi – Liwale – Nachingwea kilometa 175 itakuwa imesainiwa. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Barabara ya Utegi – Shirati mpaka Kirongwe kwa kuwa upembuzi yakinifu umekwishakamilika na barabara imeingizwa kwenye bajeti. Nataka nijue nini mpango wa Serikali sasa kuanza ujenzi wa barabara hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaisikia barabara aliyoitaja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge rudia swali lako.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Utegi – Shirati mpaka Kirongwe kwa kuwa upembuzi yakinifu umekamilika na nimeona imewekwa kwenye bajeti mwaka huu, nilitaka nijue sasa mpango wa Serikali wa kuitangaza na kuanza barabara hii ujenzi wa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ndiyo imetengewa fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi, tunajua upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ulishakamilika, kwa hiyo taratibu za manunuzi kuanza ujenzi wa barabara hiyo zitaanza mwaka wa fedha wa 2023/2024 kama ilivyopitishwa na Bunge hili kwa maana ya mwaka ujao wa fedha. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendela na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mbunge wa Iramba Mashariki swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Dkt. Chaya.

Na. 462

**Fidia kwa wananchi waliopisha uanzishaji wa Kambi ya Gereza la Kilimo Singa**

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA K.n.y. MHE. FRANCIS I. MTINGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamaliza kulipa fidia kwa baadhi ya wananchi waliopisha uanzishaji wa Kambi ya Gereza la Kilimo Singa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mbunge wa Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Singa ilianzishwa mwaka 1983 katika Kijiji cha Singa chini ya Magereza ya Mkoa wa Singida ikiwa na eneo la ekari 500 kama ilivyoombwa kutoka Serikali ya Kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ardhi *(Land Ordinance 03, Cap 113)* ya mwaka 1923 iliyokoma mwaka 2003 haikuruhusu ulipwaji wa fidia kwa maeneo yanayotwaliwa na Serikali ambayo hayajaendelezwa. Kwa kuzingatia sheria hiyo, wananchi walio na maeneo yaliyoendelezwa (kwa kupanda mazao ya kudumu) katika eneo lililogawiwa kwa gereza walilipwa fidia zao shilingi 300,000 kwa eneo lenye ukubwa wa ekari 10 na malipo ya mwisho yalifanyika mwaka 1997. Taratibu za umilikishaji rasmi wa eneo hilo kwa Jeshi la Magereza zinakamilishwa na Mamlaka husika, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Chaya, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongeza. Katika Wilaya ya Manyoni, tuna Gereza la Wilaya na gereza hili wanajishughulisha sana na kilimo, lakini kuna changamoto sana ya zana za kilimo za kisasa. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba tunaliwezesha Jeshi la Magereza la Manyoni ili waweze kujikita kwenye kilimo cha kisasa hususan kupeleka matrekta?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Katika Gereza hilo hilo la Wilaya ya Manyoni tuna upungufu mkubwa sana wa nyumba za watumishi. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba sasa tunawajengea Maafisa Magereza nyumba za kisasa ili nao wajione ni sehemu ya Tanzania? Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umuhimu wa kuwa na zana za kilimo za kisasa ikiwemo matrekta, huo ndio mwelekeo mpya wa Wizara ya Mambo ya Ndani kupitia Jeshi la Magereza kuimarisha vikosi vyake ili viweze kulima kwa tija. Kwa kufanya hivyo tumeimarisha Shirika la Uchumi la Magereza kwa maana ya SHIMA ili lianze kuzalisha kwa tija hatimaye magereza mengine ambayo hayajaingizwa katika utaratibu huu yaweze kuiga kutokana na kazi inayofanywa na SHIMA na moja ya vitendeakazi wanavyotumia ni matrekta. Kwa hiyo, Mheshimiwa atupe muda tu, tutakapokuwa tumeboresha, Gereza la Manyoni litafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umuhimu wa kuwa na nyumba bora za watumishi pia ni kipaumbele cha Jeshi la Magereza na kwa sasa wanatumia nguvukazi ya Jeshi la Magereza ili kujiimarisha kwa kujenga nyumba zinazofaa. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kumwomba Mkuu wa Magereza Mkoa wa Singida awasiliane na wenzie wa Magereza yake ndani ya mkoa waanze miradi ya kujenga nyumba za maafisa ili Serikali kwa maana ya Magereza Makao Makuu yaweze kuwa–*support* vifaa vya kukamilishia majengo hayo, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Salim Mussa Omar, Mbunge wa Gando, sasa aulize swali lake.

Na. 463

**Kupunguza kodi kwa kampuni changa**

**MHE. SALIM MUSSA OMAR** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza kodi kwa kampuni changa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salim Mussa Omar, Mbunge wa Jimbo la Gando kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na utaratibu wa kuzingatia misingi ya utozaji kodi, Serikali imetoa unafuu kwa biashara na kampuni changa kwa kuzitoza kodi miezi sita baada ya kuanzishwa kwake na kodi ya mapato kwa kampuni hizo huanza kutozwa baada ya kuanza kutengeneza faida ambayo hukokotolewa kulingana na faida iliyopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na zoezi la mapitio ya mfumo wa kodi ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya bajeti ya mwaka 2023/2024. Mwelekeo wa Serikali ni kuboresha zaidi mazingira ya kufanya biashara na kuvutia uwekezaji hasa kwa kampuni changa ikiwemo uboreshaji wa mifumo ya usimamizi wa kodi, kufanya tathmini ya tozo mbalimbali zilizopo kwa lengo la ama kupunguza viwango au kuzifuta kabisa pale ambapo zinaonekana ni kero kwa biashara au kampuni changa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salim Mussa, swali la nyongeza.

**MHE. SALIM MUSSA OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nachukua fursa hii kuwaombea tu kwa Mwenyezi Mungu waweze kutimiza yale ambayo wananchi wana-*wish*. Nina swali lingine la nyongeza: Je, utaratibu huu ambao unafanyika kwa makampuni katika kujikadiria kodi yao kwa kufanya ukokotoaji wa kile ambacho wanaingiza, ni lini utaenda kwa maduka ya kawaida ya *retails? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nina ushauri kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa nini sasa kutokana na sintofahamu kubwa iliyojitokeza ndani ya nchi yetu baina ya mlipa kodi na mtoza kodi, kwa nini sasa usiwepo mfumo wa kutengeneza *activities* za kimichezo baina yao hata kutengeneza ligi baina ya wafanyabiashara pamoja na *TRA* na viwanja tunavyo pale Kariakoo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri hilo moja ni ushauri, wewe jibu swali moja la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge. Kabla ya kujibu naomba nimpongeze sana kwa namna anavyojitahidi kutetea kampuni changa vile vile na wafanyabiashara wadogo wadogo. Swali lake anasema ni lini? Namwomba tu Mheshimiwa Salim awe na subira, mchakato huu unaendelea kufanywa na Serikali kwa nia safi. Mara tu baada ya kumalizika tutaleta katika Bunge lako tukufu, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, sasa namwita Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini, aulize swali lake.

Na. 464

**Serikali imejipangaje kuhusu udhibiti wa ubora wa nguo na viatu vya mitumba vinavyotoka nje ya nchi**

**MHE. PRISCUS J. TARIMO** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kusimamia ubora wa nguo na viatu vya mtumba vinavyotoka nje ya nchi ambavyo havina ubora na bei ni kubwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Shirika la Viwango Tanzania inatekeleza majukumu ya udhibiti wa ubora na usalama wa bidhaa zinazoingia na kutoka nchini kupitia Kitengo cha Udhibiti wa Ubora wa Bidhaa zinazoingia na kutoka nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa zote zinazotoka nje ya nchi zilizoainishwa kwa vigezo mbalimbali zikiwemo nguo na viatu vya mtumba hukaguliwa chini ya mfumo wa ukaguzi wa shehena kabla ya kuingia nchini *(Pre-Shipment Verification of Conformity to Standards),* ukaguzi ambao unafanywa na mawakala waliopewa dhamana na shirika. Pamoja na kukagua ubora, vilevile usalama wa nguo na viatu vya mitumba hukaguliwa kwa vigezo vya kiafya na kutoa cheti cha afya *(Fumigation Certificate)*. Endapo bidhaa hizo zitakidhi vigezo vilivyowekwa na kuhakikiwa na Maafisa Afya,

pale shehena husika inapofika bandarini Dar es Salaam au katika mpaka wowote, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, swali la nyongeza.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini kwanza niseme tu wamejibu upande mmoja, upande wa *quality,* yaani ubora lakini upande wa bei hawajagusia. Ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu sisi ambao tuko *field* tumeona kabisa utaratibu huu wa kukagua haufanyi kazi, kwa maana marobota yanayokuja sasa nchini yamejaa nguo chakavu ambazo haziwezi hata kuuzika; je, Serikali haioni namna ya kutafuta utaratibu mwingine wa kuhakikisha wanafanya ukaguzi mzuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili. Kwa kuwa bei imeonekana bado ni kubwa kutokana na kuwepo kwa madalali, lakini pia ubora unakuwa *compromised* kutokana na zile nchi nazo zimepigwa na uchumi: Serikali haina mpango mwingine wa kudhibiti biashara hii ili tusiwe dampo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ufanisi wa ukaguzi wa mawakala tuliowapa kazi hiyo kwa mujibu wa maelezo ya Mheshimiwa Mbunge ambaye naamini anawakilisha wafanyabiashara wanaofanya biashara hii ni kwamba ziko chini ya kiwango. Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia *TBS* itafanya uthamini juu ya utendaji wa mawakala waliopewa na kama itathibitika kwamba wanaleta mavazi ambayo yako chini ya kiwango kwa maana ya ubora, lakini na uchakavu hatua zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kuwafutia hizo leseni na kuwatafuta watu wengine wanaoweza kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bei kubwa ya bidhaa inayotoka kwenye hizo nchi alizozibainisha ambako ndiko wafanyabiashara wetu huchukua mizigo, Serikali kupitia Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji itafanya tathmini na kuangalia

masoko mengine kwa maana ya nchi nyingine zinazozalisha bidhaa kama hizo zinazotafutwa na wawekezaji au wafanyabiashara kutoka Tanzania ili wale ambao watakuwa na bei nzuri, basi mwelekeo uwe katika nchi hizo kuliko kuendelea kutumia masoko ya zamani ambayo bei yake ni kubwa, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 465

**Vituo vya uwekezaji na masoko kwa wanawake katika kila kata**

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanzisha Vituo Maalum vya Masuala ya Uwekezaji na Masoko kwa Wanawake katika kila Kata?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji nchini kwa ajili ya wazawa na wageni wakiwemo wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanzisha majukwaa ya kiuchumi mahususi kwa ajili ya wanawake. Majukwa haya yanatoa fursa kwa ajili ya wanawake kuona fursa za uwekezaji na biashara na kuzitumia ikiwemo masoko ya bidhaa wanazozalisha. Aidha, Serikali imeendelea kutambua kundi la wanawake na kuwapa fursa ya kukopeshwa mikopo mbalimbali ikiwemo mikopo ya 10% kutoka kwenye halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuangalia fursa mbalimbali kwa ajili ya kuwawezesha wanawake na pale itakapoonekana kuna haja ya kuanzisha vituo vya uwekezaji wa masoko mahususi kwa wanawake, basi kazi hiyo itafanyika katika ngazi ya kata, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, swali la nyongeza.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nilikuwa na maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza: Je, Serikali haioni haja sasa ya kuwasaidia wajasiriamali wadogo kutafuta masoko nje ya nchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Nini mkakati wa Serikali kuwaandaa wajasiriamali hawa wadogo kuwa wawekezaji ndani ya nchi yao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuwatafutia masoko nje ya nchi, ndiyo maana utaona kuna majukwaa mbalimbali ya akina mama pamoja na makongamano yanayowakutanisha wafanyabiashara wanawake na wakati mwingine husafirishwa kwenda katika nchi mbalimbali kuhudhuria makongamano kama hayo kama njia ya kuwajengea uwezo na kutafuta masoko kwa ajili ya bidhaa wanazozalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la pili la kuwawezesha wawe wafanyabiashara wakubwa, nimesema katika jibu la msingi kwamba Serikali imetoa fursa mbalimbali za kuwakopesha wafanyabiashara wakiwemo akina mama ili waweze hatimaye kuimarisha mitaji yao kuikuza na hatimaye wawe wafanyabiashara wakubwa. Ni matarajio yetu fursa mbalimbali zinazotolewa na Serikali hususan hii Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan itawezesha akina mama kuendelea kuongezeka katika idadi ya wafanyabiashara wakubwa katika nchi yetu, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Wahesimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali na majibu asubuhi hii. Naomba niwaletee matangazo machache, tunaanza na wageni walioko Bungeni asubuhi hii.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza ni wageni waliopo jukwaa la Spika ambao ni wageni wa Mheshimiwa Mhandisi Hamad Masauni, Mbunge na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni Ndg. Kaspar Kaspar Mmuya ambaye ni Katibu Mkuu, Dkt. Maduhu Kazi Naibu Katibu Mkuu, Ndg. Camillus Wambura ambaye ni Mkuu wa Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. Mzee Ramadhani Nyamka, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, ahsanteni sana. Ndugu John William Masunga ambaye ni Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, ahsanteni. Dkt. Anna Makakala ambaye ni Kamishna Jenerali wa Jeshi la Uhamiaji. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana, ahsante sana.

Tunaye Ndugu Ismail Rumatila ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA),* tunaye Prof. Suffian Bukurura ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Uzalishaji Mali wa Jeshi la Polisi, tunaye Balozi Khamis Kaghasheki, Mwenyekiti wa Bodi ya *Parole,* tunaye Bwana Moremi Marwa ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Shirika la Magereza (SHIMA), tunaye Ndugu Abdallah Mmanga, Mkurugenzi wa *NIDA* kwa upande wa Zanzibar, tunaye Ndg. Hamadi Hamadi ambaye ni Kamishna wa Polisi Zanzibar, tunaye Ndg. Wanja Mtawazo ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Magereza *(SHIMA),* ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni hawa wameambatana na wafuatao: Tunao Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, Makamishna, Watendaji na Wataalam kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa ujumla wenu msimame. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia Wajumbe wa Baraza la Usalama Barabarani wasimame, ahsante. Yuko mgeni mwingine

wa Mheshimiwa Hamad Masauni, Mbunge na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ambaye ni mke wake, Ndg. Thaniya Abdallah. Ahsante sana. Karibu sana wifi na shemeji yetu. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tuna mgeni wa Mheshimiwa Jumanne Sagini, Mbunge na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kutoka Musoma, Mkoa wa Mara, ahsante. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 16 wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni Umoja wa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa kutoka Jijini Dar es Salaam, wote msimame, ahsanteni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tunao wageni 60 wa Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mbunge, ambao ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Jimbo la Ndanda Mkoa wa Mtwara. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Jafari Chege Mbunge ambao ni Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Rorya kutoka Mkoa wa Mara wakiongozwa na Ndugu Ongujo Nyamarwa ambaye ni Mwenyekiti wa Chama, Wilaya ya Rorya, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunao wanafunzi 150 na walimu 10 kutoka Shule ya *St. Mathew* ya Jijini Dar es Salaam, ahsante na karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo mengine; ninalo tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge ambapo Katibu wa Bunge anawakumbusha Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii itaendesha semina kuhusu Uhifadhi na Utangazaji Utalii. Semina hii itafanyika leo siku ya Jumatatu tarehe 29 Mei, 2023 mara baada ya kusitisha Shughuli za Bunge saa saba mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wote wanakaribishwa kuhudhuria semina hii muhimu ili kupata uelewa wa masuala yahusuyo uhifadhi na utalii ili kusaidia kutoa elimu kwa wananchi kuhusu uhifadhi endelevu.

Waheshimiwa Wabunge, liko tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge; Katibu wa Bunge anawakumbusha Waheshimiwa Wabunge wote kuwa malipo yote yatalipwa

kutokana na kusaini mahudhurio kwenye *biometric* na siyo vinginevyo. Waheshimiwa Wabunge wanatakiwa kusaini kwa kutumia mashine zilizopo ndani ya jengo la Bunge na siyo magetini. Vilevile ni muhimu kila Mbunge kuhakikisha kuwa baada ya kusaini anapokea ujumbe wenye maneno *verified* ili kujiridhisha kwamba taarifa zake zimepokelewa na ofisi.

Tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge; Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo itaendesha semina kuhusu *COSOTA* ilipotoka, ilipo na inapoelekea pamoja na fursa zilizopo katika biashara ya ubunifu. Semina hii itafanyika siku ya Jumanne tarehe 30 Mei, 2023 mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa saba mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, wote mnakaribishwa kuhudhuria semina hii muhimu ili kuwajengea uelewa kuhusu manufaa yaliyopatikana katika kuimarisha ulinzi wa kazi za kiubunifu zinazolindwa na Sheria ya Haki Miliki na Haki Shirikishi Na. 7 ya mwaka 1999.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club;* Waheshimiwa Wabunge, Mwenyekiti wetu wa *Bunge Sports Club* anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote matokeo ya mechi ya mpira wa miguu iliyofanyika tarehe 27 Mei, 2023 kati ya *Bunge Sports Club* na timu ya Umoja ya Wamachifu kama ifuatavyo: -

Waheshimiwa Wabunge, timu ya *Bunge Sports Club* ilipata magoli saba na timu ya Umoja wa Machafu haikupata goli. Wafungaji wa magoli kwa upande wa *Bunge Sports Club* alikuwa ni Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, Mheshimiwa Makame Mlenge Haji na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana, nawashukuru.

Katibu.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mwongozo wa Spika, nani? Mheshimiwa Luhaga Mpina.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo kwa Kanuni ya 79 kuhusu kuahirisha mjadala unaoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mjadala unaoendelea usimame kwa muda ili kuweza kujadili jambo kubwa hili la dharula ambalo kadri siku zinavyo endelea linazidi kuleta athari kubwa katika uendeshaji na usimamizi wa shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 38 (2)(b) (i) na kifungu cha 38 (3) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008 na marekebisho yake ya mwaka 2020 kinaitaka Serikali wakati taarifa ya *CAG* inawekwa mezani ije sambamba na majibu ya Serikali kuhusu taarifa ya *CAG* inayowasilishwa Bungeni kwa Waheshimiwa Wabunge. Lakini leo hii imezidi sasa miezi miwili Serikali haijaweka mezani majibu ya hoja za Mkaguzi, haijaweka mezani taarifa ya mpango kazi ya shughuli za kujibu hoja za mkaguzi na hivyo kulifanya Bunge lako kupata wakati mgumu sana katika kuisimamia Serikali. Kwa mfano wakati unazungumzia majukumu yaliyotekelezwa na Serikali katika wakati husika halafu majibu ya *CAG* hayajawekwa hapa mezani, inaleta changamoto kubwa sana kwa Waheshimiwa Wabunge kuweza kuenenda na hili suala.

Sasa kwa sababu sheria ilipitishwa na Bunge hili tukufu na sheria inatakiwa kufuata na kuzingatiwa, nikaona kuna haja sasa leo hii Wabunge wenzangu waniunge mkono ili tulijadili hili jambo ambalo ni muhimu sana katika utekelezaji wa majukumu yetu hapa. Kwa sababu bila kupata haya majibu ya Serikali na Taarifa ya *CAG* iko mezani na ni *public document* inatupa wakati mgumu sana katika kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wabunge wenzangu waniunge mkono hoja hii tuijadili ili tuweze kusonga mbele, kwa mujibu wa sheria za nchi yetu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Luhaga Mpina kwa kuomba Mwongozo wa Kiti kwa kanuni ya 79. Lakini kanuni ya Mwongozo ni Kanuni ya 76 ili kuona jambo lilitokea mapema kama linaruhusiwa ama haliruhusiwi lakini ametaja dharura kwa maana kama ni dharura angeenda Kanuni ya 54. Sasa kwa kuwa jambo hili si la dharura na kwa kuwa utaratibu za kujadili hoja za *CAG* zinafahamika basi Mheshimiwa Luhaga utapata Mwongozo baadaye. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO – KATIBU MEZANI**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.**

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tuna hoja mbele yetu sasa ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Sasa namuomba nimkaribishe Mheshimiwa Waziri awasilishe hoja yake. Mheshimiwa *Eng.* Masauni karibu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2022/2023 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kunipa afya njema ya kuweza kusimama katika Bunge hili kuwasilisha Hotuba hii pamoja na Muhtasari nitakao wasilisha. Naomba Hotuba yangu yote iingizwe katika *Hansard* za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee namshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini kuendelea kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuiongoza vyema nchi yetu inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi. Wote tunashuhudia hali

ya amani, utulivu na usalama ikiendelea kuwepo nchini ikiwa ni miongoni ya misingi ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi zangu pia nazitoa kwa viongozi wote wa kitaifa akiwemo Makamu wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Isdor Mpango, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa na Spika wa Bunge wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wote hawa wako pamoja, wanaonesha uwezo mkubwa katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kuliongoza Taifa letu. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itaendelea kutekeleza maelekezo ya viongozi hawa yenye lengo la kuimarisha utendaji wa Wizara hii, kuongeza ufanisi katika kuhudumia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kufanya uteuzi wa baadhi ya viongozi wa Wizara hii. Tarehe 9 Desemba, 2022 Mhe. Rais alimteua Bw. Kaspar Mmuya kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Tarehe 20 Agosti, 2022 alimteua Kamishna wa Polisi Camillus Wambura kuwa Inspekta Jenerali wa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tarehe 24 Agosti, 2022 Mhe. Rais alimpandisha cheo na kumteua Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Magereza Mzee Ramadhani Nyamka kuwa Kamishna Jenerali wa Magereza. Kwa niaba ya watumishi wote wa Wizara hii nawapongeza kwa uteuzi huo, hongereni Sana. Pia, tarehe 18 Aprili, 2023 Mheshimiwa Rais alimteua Mheshimiwa Balozi Khamis Sued Kagasheki kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya *Parole,* naye pia nampongeza kwa uteuzi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia nafasi hii pia kuwapongeza na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ikijumuisha wajumbe mahiri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya uongozi wa Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, Makamu Mwenyekiti Vincent Paul Mbogo Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kusini. Kamati hii imekuwa na mchango muhimu katika kutoa maoni, ushauri na ushirikiano

mkubwa uliosaidia kuboresha bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2023/2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya mapato ya matumizi ya fedha kwa mwaka 2022/2023; katika mwaka 2022/2023 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya shiling trilioni 1.21. Hadi kufikia mwezi Mei, 2023 jumla ya shilingi bilioni 996.87 zilipokelewa na Wizarani sawa na asilimia 80.61 ya bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge. Aidha Wizara imepokea jumla ya jumla ya shilingi bilioni 82.52 kwa kwa ajili ya kulipa madeni ya watumishi, wakandarasi, wazabuni na watoa huduma. Pia Wizara imekusanya jumla ya shilingi bilioni 264.66 zilizokusanywa ambayo ni sawa na asilimia 72 ya lengo ya kukusanya shilingi bilioni 367.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yaliyopatikana katika bajeti ya mwaka 2022/2023. Kupitia utekelezaji wa mpango wa bajeti ya mwaka 2022/2023, Wizara imefanikiwa kukamilisha jumla ya miradi 23 ambayo ni ujenzi wa majengo mawili ya makazi ya familia 24 ya askari Polisi Mabatini – Mwanza, nyumba nne za kuishi familia nane askari Polisi Kusini Pemba, jengo moja la kuishi familia nne askari Polisi Kaskazini Pemba, Ofisi tatu ya Makamanda Polisi Mkoa wa Kusini Unguja, Kaskazini Unguja na Mkoa wa Polisi Tarime Rorya, nyumba tatu za kuishi Makamishna wa Jeshi la Polisi Jijini Dodoma, Vituo vitatu vya Polisi daraja A vilivyopo Lushoto – Tanga, Wanging'ombe – Njombe, Kigamboni Dar es salaam na Kituo cha Polisi daraja B Ruangwa – Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine iliyokamilika ni vituo viwili vya Polisi daraja C Kizimkazi – Kusini Unguja na Kirongwe Mkoa wa Kipolisi Tarime – Rorya, ujenzi wa wodi ya wazazi na chumba cha upasuaji katika Zahanati ya *FFU* Ukonga – Dar es Salaam, ujenzi wa vituo vitatu vya zimamoto na uokoaji vilivyopo Nzuguni na Chamwino – Dodoma na kituo kikuu cha zimamoto na uokoaji *TAZARA* – Dar es Salaam, Ofisi ya Uhamiaji Mikoa ya Geita, Lindi na Manyara na Ofisi ya Uhamiaji za Wilaya ya Masasi, Nanyumbu, Newala na Tandahimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa miradi 23 ambayo mingi ilikuwa haijakamilika kwa muda mrefu, kumeweka historia ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Historia hii ni matokeo ya dhamira ya dhati aliyonayo Mheshimiwa Dkt. Samia

Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu ya kuleta mageuzi katika Wizara hii kwa kuviwezesha na kuviimarisha vyombo vyake vya usalama ili viweze kuhudumia wananchi kwa weledi na ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imefanikiwa kupokea jumla ya magari 162, ambayo magari 156 ni ya Jeshi la Polisi, manne ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, mawili ya Makao Makuu ya Wizara. Mafanikio mengine ni kuanza kutoa huduma za Polisi katika Kata 3,956 za Tanzania Bara na Shehia 388 Zanzibar. Wakimbizi 10,335 walipatiwa suluhisho la kudumu, ambapo wakimbizi 5,324 walirejeshwa kwa hiari yao nchini Burundi na wakimbizi 5,011 walihamishiwa katika mataifa ya Marekani, Canada, Ufaransa na Australia na kuanza kutumika kwa mfumo wa *NIDA* wa kielektroniki katika kuwasilisha maombi ya usajili na utambuzi wa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya kipaumbele katika Bajeti ya mwaka ya 2023/2024. Wizara kwa mwaka 2023/2024 imeweka kipaumbela katika maeneo yafuatayo; kuendelea kudumisha amani na usalama wa raia na mali zao kwa kufanya doria, misako na operesheni maalum, kuendeleza ushirikishwaji jamii kwenye ulinzi wa umma, kukamilisha miradi ya maendeleo inayoendelea kutekelezwa, kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali na kuboresha mazingira ya kazi na makazi kwa watumishi na askari na kuongeza vitendea kazi vya kisasa katika kutoa huduma ikiwemo magari, boti, helkopta, pikipiki pamoja na mitandao na dhana za kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine ya kipaumbele ni kuimarisha ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo, kuimarisha usimamizi wa Sheria ya Usalama Barabarani ili kupunguza matukio ya ajali na kufanya mapitio ya sheria nyingine zinazohusu Wizara, kuandaa kanuni, kuboresha huduma za urekebu kwa wafungwa, kuimarisha uzalishaji katika mashamba ya magereza kwa ajili ya mahitaji ya chakula cha wafungwa na mahabusu, kuimarisha mashirika yaliyopo chini ya Wizara, kutoa mafunzo kwa watumishi, raia na askari, kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala yanayohusu Wizara na kuimarisha utunzaji wa mazingira kwenye Magereza na Makambi ya Wakimbizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Wizara itaendelea kusimamia maboresho yanayoendelea kwenye vyombo vyake vya usalama pamoja na kuendelea kuyafanyia kazi maelekezo ya Mheshimiwa Rais anayoyatoa na yatakayotolewa kupitia Tume ya Uboreshaji wa Haki Jinai, inayohusisha masuala ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya mwaka 2022/2023 na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2023/2023; upandishaji wa vyeo; jumla ya watumishi 1,696 wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi walipandishwa vyeo. Idadi hiyo inajumuisha maafisa wakaguzi na askari 622 wa Jeshi la Polisi, 130 wa Jeshi la Magereza, 762 wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na 182 wa Idara ya Uhamiaji. Katika mwaka 2023/2024 Wizara itaendelea kuwapandisha vyeo maafisa wakaguzi, askari na watumishi raia katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira kwa askari na watumishi raia; katika mwaka 2022/2023 Serikali imetoa kibali cha kuajiri jumla ya watumishi 6,608 kwa majeshi yaliyopo chini ya Wizara kati ya hao ni 1158 na 57 ni watumishi raia, 1995 ni askari wa Jeshi la Magereza, askari 79 kwa ajili ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ambao watapelekwa katika kikosi maalum cha kuzuia magendo KMKM – Zanzibar kwa ajili ya kupata mafunzo ya uogeleaji na uokoaji. Idara ya Uhamiaji imeajiri askari 818 ambao wameanza kazi mwezi Septemba, 2022 na wengine 521 wameanza mafunzo ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2023/2024 Wizara inatarajia kuajiri jumla ya askari 3,117 kwa lengo la kuboresha utendaji kazi. Kati ya hao, askari 2,000 ni wa Jeshi la Polisi, 517 wa Jeshi la Magereza, 200 wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na 400 wa Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo ya watumishi. Jumla ya maafisa, wakaguzi, askari na watumishi raia 7,282 wameendelea kupatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo. Kati ya hao, 69 ni wa Makao Makuu ya Wizara, 5,041 Jeshi la Polisi, 662 Jeshi la Magereza, 764 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na 751 Idara ya Uhamiaji. Mafunzo hayo yatagharamiwa na Serikali kwa asilimia 100 bila kuwa na makato yoyote kutoka kwenye posho za askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara itaendelea kuwapatia mafunzo ya kuwajengea uwezo na kiutendaji askari na watumishi raia, ambapo jumla ya shilingi bilioni 29.93 zimetengwa ili kuwezesha mafunzo hayo. Hivyo, napenda kusisitiza kuwa askari wote wa Vyombo vya Usalama chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi wataendelea kupata mafunzo bila kukatwa posho zao kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ununuzi wa sare za maafisa na askari; katika mwaka 2022/2023 Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 10.25 kwa ajili ya ununuzi wa sare za maafisa na askari wa vyombo vya usalama vilivyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Zabuni za ununuzi wa Sare hizo zimetolewa kwa Shirika la uzalishaji mali la Jeshi la Polisi na Shirika la Magereza. Aidha, jumla ya shilingi bilioni 2.87 zimetolewa kwa ajili ya kununua jozi za viatu vya maafisa na askari. Viatu hivyo vilinunuliwa na vitaendelea kununuliwa kutoka katika kampuni ya kutengeneza bidhaa za ngozi Kilimanjaro *International Leather Company.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2023/2024 Serikali imetoa jumla shilingi bilioni 16.02 kwa ajili ya ununuzi wa sare za maafisa na askari. Aidha, ninahamasisha mashirika yaliyopo chini ya Wizara yaendelee kushiriki katika zabuni za ununuzi wa sare za vyombo vya usalama chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa lengo la kupata sare zenye ubora na bei nafuu pamoja na kuwezesha mashirika kujiimarisha kwa kuzingatia fursa zilizopo kwenye vyombo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya sheria, kanuni na itifaki. Wizara imefanikiwa kufanya mapitio ya kanuni zifuatazo; Kanuni ya Kuzuia Ugaidi ya mwaka 2022, Kanuni ya Usajili na Utambuzi wa Watu ya mwaka 2014, Kanuni ya Viza za Uhamiaji ya mwaka 2016 na Marekebisho ya Amri ya uanzishwaji wa Bodi ya Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza ya mwaka 2006. Aidha, Kanuni za Kudumu za Idara ya Uhamiaji ya 2023 zimetungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali iliridhia Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi ya mwaka 2004. Azimio la Itifaki hiyo liliridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi

Septemba, 2022. Pia, Serikali iliridhia Itifaki ya Uwezeshaji wa Uingiaji na Utokaji wa Watu ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika ya mwaka 2005. Azimio la Itifaki hili litahusishwa Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa kwa mujibu wa Ibara 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2023/2024 Wizara itafanya mapitio ya baadhi ya Sheria ili kuimarisha usimamizi ikiwemo Sheria ya Uhamiaji Sura Na. 54, Sheria ya *Parole* Sura Na. 400, Sheria ya Jumuiya Sura Na. 337, Sheria ya Wakimbizi Na. 9 ya mwaka 1998 na Sheria ya Usajili wa Utambuzi wa Watu ya Mwaka 1986 rejeo la mwaka 2012. Mabadiliko hayo ya sheria yataenda sambamba na marekebisho ya kanuni za sheria husika na utekelezaji wa programu ya maboresho yanayoendelea ndani ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi, hali ya usalama nchini; wajibu wa msingi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni kuhakikisha usalama wa watu na mali zao unaendelea kuwepo ili amani na utulivu wa nchi yetu uendelee kudumu. Hali hii inawezesha shughuli za kiuchumi na kijamii kufanyika na kuchangia maendeleo ya Taifa letu. Katika kutekeleza wajibu huo, Wizara hushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama, jamii na wadau wengine ili kuhakikisha uhalifu wa aina zote unadhibitiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwepo hali ya usalama nchini, uhalifu wa makosa dhidi ya binadamu, maadili ya jamii na kuwania mali umeendelea kuwepo. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 makosa makubwa ya jinai yaliyotolewa taarifa katika vituo vya polisi yalikuwa ni 45,455 ikilinganishwa na makosa 43,771 yaliyotolewa taarifa katika kipindi kama hicho mwaka 2021/2022. Sababu ya kuongezeka kwa makosa hayo ni pamoja na watu kujichukulia sheria mkononi, migogoro ya ardhi na mirathi, ubakaji, ulawiti, mmomonyoko wa maadili, tamaa ya mapenzi na imani za kishirikina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ni kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu kuzingatia sheria, kuhamasisha jamii kutoa taarifa za makosa hayo kwa wakati kwa kushirikisha viongozi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji na

kushirikisha viongozi wa dini katika kutoa elimu ya maadili mema kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya usalama barabarani. Hali ya usalama barabarani imeendelea kuimarika kutokana na Jeshi la Polisi kuendelea kusimamia Sheria za Usalama Barabarani kwa kushirikiana na wadau. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 matukio ya ajali za barabarani imepungua kutoka matukio 1,283 ikilinganishwa na matukio 1,731 kwa kipindi kama hicho mwaka 2021/2022, sawa na asilimia 25.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupungua kwa matukio ya ajali kunatokana na kuimarika kwa usimamizi wa sheria, kufanyika kwa operesheni maalum, doria na misako nchi nzima. Aidha, elimu ya usalama barabarani imeendelea kutolewa kwa makundi yote yanayotumia barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia mabadiliko hayo chanya na maoni ya wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, utayari wa wamiliki wa madereva wa mabasi kuzingatia sheria na kanuni za usalama barabarani, utimamu wa Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya ulinzi na usalama, Baraza la Usalama Barabarani limefanyia kazi suala la mabasi ya abiria kusafiri masaa 24 na kutoa mapendekezo yake. Serikali inayafanyia kazi mapendekezo hayo na itatoa uamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kudhibiti ajali za barabarani katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Jeshi la Polisi litaangalia upya mfumo mzima wa utoaji wa leseni kwa kushirikiana na taasisi nyingine zinazohusika katika utoaji wa leseni. Hatua nyingine ni pamoja na kufanya uhakiki wa leseni za madereva nchini, aidha Serikali itaharakisha taratibu za kuweka kamera za barabarani ambazo zitasaidia kubaini matukio ya uvunjifu wa sheria katika barabara kuu za maeneo ambayo hayana askari polisi. Pia, operesheni maalum zitafanyika katika barabara kuu kwa lengo la kufuatilia nyendo za madereva wanaovunja sheria na kuchukua hatua stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea kuchukua hatua za kinidhamu kwa askari yoyote atakayejihusisha kwa vitendo vya ukiukwaji wa maadili na rushwa. Pia Wizara itaendelea kutambua

kazi zinazofanywa na askari waadilifu kama Koplo Hamisi R. Masana ambaye leo nimemwalika hapa Bungeni. Askari huyu alikataa rushwa wakati akitekeleza majukumu yake. Alikuwa ni miongoni mwa wageni ambao tumewawasilisha ili uweze kuwatambulisha, lakini natumai utalifanyia hilo kazi itakapokupendeza baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, operesheni ya kupambana na uhalifu; Wizara imeendelea kutekeleza Ibara 105A ya Ilani ya CCM ya mwaka 2020/2025 inayoelekeza kuimarishwa kwa usalama wa raia na mali zao. Misako, doria na operesheni zimefanyika kwa ajili ya kupambana na uhalifu wa aina zote. Matokeo ya operesheni hizo ni kukamatwa kwa risasi 442 na silaha 198. Aidha, Wizara kupitia Jeshi la Polisi iliratibu kampeni za usalimishaji wa silaha haramu kwa hiari ikiwa ni utekelezaji wa Makubaliano ya Umoja wa Afrika ya mwaka 2017 ambapo jumla ya silaha 1,220 zilisalimishwa.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine za Serikali limefanya operesheni za kupambana na uhalifu wa Nyara za Serikali. Ushirikiano huo ulifanikisha kukamata Nyara za Serikali 2,201 zenye uzito wa kilo 17,211 na gramu 913 zikiwa na thamani ya shilingi bilioni 9.55. Jumla ya watuhumiwa 917 walikamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uboreshaji wa Huduma ya Polisi Jamii; kuanzia mwezi Julai, 2022 Jeshi la Polisi limepeleka askari katika Kata 3,956 na Shehia 388 ili kushirikiana na Maafisa Watendaji katika Kata katika masuala ya ulinzi na usalama. Pia kurahisisha mawasiliano kati ya Jeshi la Polisi na mananchi katika kuzuia na kupambana na uhalifu. Askari hao wakishirikiana na watendaji wa kata kuanzisha vikundi vya ulinzi shirikishi katika maeneo hayo. Naomba kutoa wito kwa Kamati za Usalama za Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji kuwatambua Askari Kata na Shehia na kuwapa ushirikiano stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza Ibara ya 105E ya Ilani ya CCM ya mwaka 2020 – 2025, elimu ya uhamasishaji juu ya masuala ya ulinzi, uzalendo kwa Taifa na usalama wa nchi yetu imeendelea kutolewa kwa jamii. Elimu hiyo imetolewa kwa kutumia vyombo vya habari, shuleni, nyumba za ibada kupitia Maafisa wa Polisi Jamii, Wakaguzi na Askari waliopo kwenye kata ya shehia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena vile vile nitumie nafasi hii kuwapongeza Askari Kata na Askari Shehia ambao wanatekeleza majukumu yao kwa kujituma na kwa ubunifu wa hali ya juu. Miongoni mwao ni Wakaguzi Wasaidizi wa Polisi ambao nao vile vile nimewaalika hapa leo akiwemo Dkt. M. Lwena, Khalfani A. Ussi, Daniel, Mbebela, Msike F. Banda, Fransis S. Msuku ambao nao vile vile imani yangu ikikupendeza utawatambulisha hapo baadaye hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha katika mwaka 2023/2024, tathmini ya mpango wa Wizara ya ujenzi wa vituo ofisi na nyumba za makazi ya askari itafanyika ili kuzingatia mahitaji ya ujenzi wa nyumba za polisi katika ngazi ya kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dawati la Jinsia la Watoto; hadi kufikia Mei, 2023 jumla ya mashauri 14,184 ya matukio ya ukatili wa kijinsia na watoto yalitolewa taarifa katika vituo vya polisi ikilinganishwa na matukio 12,642 yaliyotokea kipindi kama hicho mwaka 2021/2022. Katika hatua zaidi za kudhibiti vitendo hivyo elimu ya kuzuia na kutoa taarifa juu ya ukatili na unyanyasaji katika jamii imeendelea kutolewa katika shule za msingi na sekondari, vyuo vikuu na kati, nyumba za ibada na kupitia vyombo vya habari. Aidha Jeshi la Polisi limefanya mapitio ya mitaala yake na kuongeza somo la *gender and child protection.* Mitaala hiyo imepitishwa na *NACTE* kwa ajili ya kutoa mafunzo ya kada zote za vyuo vya polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2023/2024 Wizara kupitia Jeshi la Polisi itaanzisha maabara maalum kwa ajili ya kushughulikia makosa ya kimtandao juu ya unyanyasaji wa watoto. Aidha, mafunzo ya kushughulikia makosa ya ukatili wa kijinsia na unyanyasaji dhidi ya watoto yataendelea kutolewa na Maafisa na Askari. Vilevile elimu itaendelea kutolewa kwa jamii katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar kuhusu kuzuia na kutoa taarifa juu ya masuala ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa vitendea kazi kwa Jeshi la Polisi; Jeshi la Polisi limepokea magari 150 kati ya magari 369 ikiwa ni utekelezaji wa Mkataba kati ya Serikali na Kampuni ya *Ashok Leyland* ya India. Magari yaliyopokelewa yamepelekwa katika Vituo vya Polisi vyenye uhitaji mkubwa. Magari 219 yaliyobaki

yatapokelewa kabla ya Septemba, 2023. Vilevile Jeshi la Polisi limepata msaada wa magari 13 na pikipiki 14 kutoka kwa wadau mbalimbali. Natumia fursa hii kuwashukuru wadau wote waliohusika kulipatia Jeshi la Polisi vitendea kazi ikiwemo Kamati za Usalama Barabarani za Mikoa ambazo Wenyeviti wake leo hapa wamejumuika na sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2022/2023, Serikali ilitenga Shilingi Bilioni 15.0 kwa ajili ya kununua magari 111 na pikipiki 336 za Jeshi la Polisi. Hadi kufikia mwezi Mei, 2023 Shilingi Bilioni 7.5 zilishapokelewa ili kuwezesha ununuzi wa magari 53 na pikipiki 56, ambazo taratibu za ununuzi zinaendelea. Katika kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, magari hayo yatasambazwa kwenye wilaya zote nchi nzima na pikipiki hizi zitasambazwa kwenye kata zote nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2023/2024, Serikali imepanga kununua magari 24 kwa gharama ya shilingi bilioni 7.68 kwa ajili ya Jeshi la Polisi. Shilingi Bilioni 2.1 zitatumika kununua pikipiki 21 kwa kuongoza misafara ya Viongozi Wakuu wa Serikali. shilingi bilioni 4.5 zitatumika kununua boti 10 kwa ajili ya doria katika Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo katika mwaka 2022/2023, Serikali ilitenga jumla shilingi bilioni 3.33 kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ili kuwezesha huduma za polisi katika ngazi ya wilaya, ambayo hupelekwa hadi katika ngazi ya kata. Serikali inaendelea kuongeza fedha hizo, ambapo katika mwaka 2023/2024, jumla ya shilingi bilioni 16.76 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya magari na pikipiki ili kuwezesha huduma za polisi katika ngazi za wilaya, mikoa mpaka kwenye kata. Lengo la Serikali ni kuongeza huduma za polisi kuwafikia wananchi kwa haraka katika ngazi zote ikiwemo kata, vijiji na shehia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya kipaumbele ya Jeshi la Polisi katika mwaka 2023/2024; Serikali imedhamiria kuendelea kuboresha utendaji wa Jeshi la Polisi kwa kuongeza kasi ya ujenzi wa makazi ya askari. Majengo ya ofisi, vituo vya polisi na ununuzi wa vitendea kazi. Katika mwaka 2023 /2024 Serikali imetenga jumla ya Shilingi Bilioni 27.19 kutekeleza miradi ya kipaumbele ifuatayo: Kukamilisha ujenzi wa jengo la ghorofa tatu askari eneo la Buyekera

– Kagera; Kumalizia ujenzi wa nyumba tatu za askari eneo la Tunguu, Kusini Unguja; na Kukamilisha ujenzi wa Ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine ni kumalizia ujenzi wa Vituo viwili vya Polisi Daraja "B'' vya Bariadi – Simiyu pamoja na Mkuranga – Pwani; Kumalizia ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja "C'' Igoma – Mbeya; Ujenzi wa jengo la ghorofa la Askari katika kambi *FFU* Dodoma; Ujenzi wa *Rest House* ya Polisi Mkoa wa Arusha; Ujenzi wa jengo la Maktaba Chuo cha Polisi Zanzibar; na Ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje awamu ya pili katika Hospitali ya Polisi Kilwa *Road* – Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati wa makazi ya askari kutoka vituo na ofisi utafanyika kama ifuatavyo: Majengo mawili ya ghorofa moja na nyumba mbili za Askari 12 Makunduchi, Kusini Unguja – Zanzibar; Majengo matatu yenye ghorofa moja ya Askari 12 Wete Pemba; Majengo 10 ya kuishi askari familia 40 Kambi ya Polisi Ziwani– Zanzibar; na Jengo la ghorofa mbili la Askari Kambi la Polisi Ziwani Mjini Magharibi Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, ukarabati utafanyika katika maghorofa 90 ya kuishi familia Askari 360 katika Kambi ya Polisi Kilwa Road – Dar es Salaam; Ofisi ya *FFU* Kambi ya Polisi Ziwani – Zanzibar; Kituo cha Polisi Daraja B Malindi, Mjini Magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nyingine zilizotekelezwa kwa mwaka 2023/2024 ni kununua vifaa vya uchunguzi kwa ajili ya maabara ya uchunguzi wa sayansi ya jinai pamoja na vifaa vingine vya kijeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maboresho ya Mfuko wa Tuzo na Tozo; Mfuko huu ulianzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 66(1) cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi, Sura ya 322. Kwa mujibu wa kifungu cha 66(4) cha Sheria hiyo malengo ya Mfuko huo ilikuwa ni pamoja na kutoa msaada kwa familia za askari waliofariki wakiwa wanatekeleza majukumu yao ya kazi; kutoa tuzo kwa matendo ya kishujaa kwa askari na ujenzi wa miundombinu ya polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliunda timu ya wataalam kwa ajili ya kufanya uchambuzi wa Mfuko wa Tuzo na Tozo uliopo chini ya Jeshi la Polisi na kutoa mapendekezo ya kuboresha. Pamoja na masuala yaliyopendekezwa na timu Wizara imepanga kufanya mambo yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kugawanya mapato ya Mfuko kwa kulindwa kwa mgawanyo wa 40% kwa matumizi ya askari na 60% kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya Jeshi la Polisi. Shirika la Jeshi la Polisi litatafuta mkopo katika taasisi za fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa miundombinu na mrejesho wa mkopo utafanyika kupitia fedha za Mfuko wa tuzo na tozo. Aidha tutaweka mikakati thabiti ya kulinda vyanzo vya mapato ya Mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maboresho hayo pia yanahusisha kutunga kanuni za Mfuko wa Tuzo na Tozo ambapo rasimu ya kanuni hizo zimeandaliwa na kufanya maboresho ya menejimenti ya uendeshaji wa Shirika la Polisi kwa jumla. Lengo ni kuimarisha utendaji kazi wa shirika ili kuliwezesha Jeshi la Polisi kubaki na jukumu la msingi la ulinzi na usalama wa raia na mali zao. Aidha, maboresho hayo yatawezesha kuongeza kasi ya ujenzi wa miundombinu ya Jeshi la Polisi kipaumbele kikiwa ni ujenzi wa vituo vya polisi katika ngazi ya kata na shehia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kuhamasisha wananchi kuanza maandalizi ya kutafuta maeneo ya kuanza hatua za awali za ujenzi wa Vituo vya Polisi katika kata zao. Baada ya taratibu zote za kisheria kukamilika kipaumbele kitatolewa katika kata zitakazoonesha mwamko wa wito huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ambayo Serikali imepanga kukamilisha kupitia Mfuko wa Tuzo na Tozo katika mwaka 2023/2024 kwa ujumla ni shilingi bilioni 4.24 ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa jengo la Kamandi ya Polisi Mtwara; ujenzi wa Kituo cha Polisi daraja B Namtumbo, Ruvuma; ujenzi wa jengo la *RPC* Rufiji; Ujenzi wa bweni la wanafunzi wa Kidatu; kujenga Kituo cha Polisi Daraja C Kitangari, Newala – Mtwara; na ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja B Misungwi – Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine itakayokamilishwa katika mwaka 2023/2024 kupitia fedha hizo ni:-

Ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja B Chang'ombe – Dodoma; Kukarabati Kituo cha Polisi Micheweni – Zanzibar; Ukarabati wa Makao Makuu ya Polisi Zanzibar; Ukarabati wa jengo la Maabara ya Uchunguzi wa Kisayansi – Dar es Salaam; Kukamilisha nyumba tano za makazi ya familia 20 za Askari Polisi eneo la Mfikiwa – Kaskazini Pemba; Kukamilisha nyumba saba za makazi ya familia 14 za Askari Polisi, eneo la Finya – Kusini Pemba; Ukarabati wa Shule ya Polisi Moshi – Kilimanjaro na Kuendelea na upimaji wa viwanja vya Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi; Shirika hili linaendelea na utekelezaji wa miradi ya kimkakati iliyopo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ikiwemo Mradi wa Usindikizaji Fedha *(Cash in Transit)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2022/2023 utekelezaji wa Mradi wa Usindikizaji Fedha umeanza kwa Benki ya *NMB*. Naipongeza Benki ya NMB kwa kushirikiana na Shirika hilo katika kazi hiyo. Nitumie fursa hii kuzihamasisha Taasisi nyingine za fedha za umma na kampuni binafsi, vituo vya mafuta, Taasisi za Dini na watu binafsi kwa ujumla kutumia huduma za Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi katika usafirishaji wa fedha kwa njia salama na za uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Ukaguzi wa Ulazima wa Vyombo vya Moto; katika mwaka 2022/2023 Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi limekamilisha andiko la Mradi wa Ukaguzi wa Vyombo vya Moto. Mradi utatekelezwa kwa ubia na sekta binafsi kuanzia mwaka 2023/2024 na vituo vya ukaguzi 40 vitatumika katika mikoa yote vikiwemo vituo hamishika *(Mobile Centers)*. Lengo ni kutumia teknolojia ya kisasa bila mwingiliano mkubwa wa kibinadamu katika kukagua vyombo vya moto. Mfumo huu utasaidia kupunguza ajali zinazotokana na uchakavu wa vyombo vya moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Miji Salama *(Safer Cities);* katika mwaka 2022/2023 Shirika limekamilisha andiko la Mradi wa Miji Salama utakaotumia kamera zenye mifumo ya utambuzi wa

sura. Katika awamu ya kwanza kamera hizo zitafungwa Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Dodoma pamoja na kwenye barabara, maduka, majengo na mitaa ili kubaini na kudhibiti kukabiliana na matishio na mianya ya uhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali ipo katika hatua za kukamilisha majadiliano na Serikali ya Falme za Kiarabu kwa ajili ya upatikanaji wa mkopo wa Dola za Marekani milioni 105 za kutekeleza mradi huu. Naomba nitumie fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa msukumo wake katika upatikanaji wa nyenzo na vifaa vya kisasa vya kubaini, kushughulikia na kuzuia uhalifu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Magereza; Hali ya Ulinzi na Usalama Magerezani; hadi kufikia mwezi Mei, 2023, jumla ya wahalifu 30,901 walikuwepo katika magereza yote nchini ambapo wafungwa ni 18,887 na mahabusu ni 12,044. Hali ya msongamano magerezani imeendelea kudhibitiwa kwa kuchukua hatua zikiwemo utekelezaji wa adhabu mbadala kama vile Mpango wa *Parole,* kifungo cha nje na huduma kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Mei, 2023 jumla ya wafungwa 780 walitolewa magerezani kupitia utaratibu wa Kifungo cha Nje na wafungwa 3,719 walihukumiwa kutumikia adhabu zao kwenye jamii. Pia Jeshi la Magereza limeendelea kudhibiti msongamano wa magereza yaliyopo katika Miji Mikuu kwa kuhamisha wafungwa na mahabusu 2,027 kwenda katika magereza yenye nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa msamaha uliowanufaisha wafungwa 1,637 waliokuwepo magerezani. Mheshimiwa Rais alitoa msamaha huo katika siku ya Maadhimisho ya Sherehe za Miaka 61 ya Uhuru wa Tanzania Bara, zilizofanyika tarehe 19 Desemba mwaka 2022 na Sherehe za Maadhimisho ya Muungano wa Miaka 59 ya Tanganyika na Zanzibar ya tarehe 26, Aprili 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hizi zimewezesha kupunguza kwa idadi ya wafungwa magerezani kutoka 32,671 katika kipindi cha mwezi Julai, 2021 hadi Mei, 2022, kufikia wafungwa 30,901

katika kipindi kama hicho mwaka 2022/2023. Hivyo kuwezesha kupungua kwa msongamano kwa wafungwa kutoka 9.2% hadi 6.2% ikilinganishwa na uwezo wa kuhifadhi wafungwa 29,902.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinzi na usalama magerezani unaendelea kuimarishwa kwa kutumia vifaa vya kiusalama vya kielektroniki, vifaa hivyo vimefungwa katika Gereza la Butimba Mwanza. Aidha, shilingi bilioni 1.59 zimepokelewa kwa ajili ya ununuzi na usimikaji wa vifaa vya kielektroniki katika Magereza ya Ruanda, Mbeya; Maweni, Tanga; Uyui, Tabora; Karanga, Kilimanjaro; na Gereza la Arusha. Pia, mkataba wa ununuzi wa vifaa vya upekuzi vyenye thamani ya shilingi 990,950,000 umesainiwa mwezi Machi, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2023/2024, shilingi 600,000,000 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya usalama vya kielektroniki na usimikaji wa mifumo ya ulinzi na usalama katika Gereza Lilungu – Mtwara, Gereza Lindi na Gereza Bukoba na vifaa vya kisasa vya kielektroniki vitaendelea kufungwa katika magereza mengine kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Huduma ya Urekebu; huduma hii inatolewa kwa wafungwa waliopo magerezani kwa kuwapatia stadi za kazi, huduma za kiroho, ushauri wa kisaikolojia na michezo, elimu ya ufundi stadi hutolewa kupitia Vyuo vya Ufundi vya Magereza vilivyosajiliwa na Serikali. Hadi Mei, 2023, jumla ya wafungwa 126 wamepatiwa mafunzo ya ufundi stadi katika Chuo cha Ufundi Ruanda – Mbeya na Wami Vijana – Morogoro. Katika mwaka 2023/2024, huduma za urekebu zitaendelea kuimarishwa katika magereza yote ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Magereza litafanya maboresho katika mitaala ya mafunzo ya urekebu kuanzia ngazi za mafunzo ya awali hadi mafunzo ya uongozi kwa ngazi zote. Lengo ni kuimarisha shughuli za urekebu na usalama magerezani. Shilingi 300,000,000 zimetengwa kwa ajili ya kuboresha mitaala hiyo na shilingi 67,000,000 zitatumika kuandaa mpango wa mafunzo wa Jeshi la Magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha 2023/2024, shilingi bilioni 2.76 zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Magereza

ya Gairo, Kilosa, Morogoro; Kakonko, Kigoma; Kaliua, Tabora; Karatu, Arusha; Msalato na Isanga Dodoma; Igunga, Tabora; Kwa Mturuki, Bagamoyo, Pwani; pamoja na kuanza ujenzi wa magereza mapya ya Kiabakari, Mara; Mpimbwe, Katavi; Sengerema, Mwanza; Kyerwa, Kagera; Kingurungundwa, Lindi; na Mlolo, Iringa. Shilingi 800,000,000 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Ofisi za Magereza katika Mikoa mitano ya Geita, Kigoma, Lindi, Songwe na Tanga. Jeshi litaendelea kujenga miundombinu ya magereza na majengo ya ofisi kwa kuzingatia mahitaji na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Magereza; Jeshi la Magereza limefanya ukarabati katika mabweni ya wafungwa katika Gereza la Wanawake Kingolwira; Gereza la Mbigiri, Morogoro; Gereza la Shinyanga; Gereza la Kongwa, Dodoma; Gereza la Wanawake, Ruvuma; Gereza la Lindi; na Gereza la Lilungu, Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati mwingine umefanyika kwa kujenga ukuta wa ngome katika Gereza la Ileje, Songwe; Idete na Mbigiri, Morogoro; na Kalilankulukulu, Katavi. Katika mwaka 2023/2024, Shilingi Bilioni 2.13 zimetengwa katika maeneo ambayo nimeshayataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuboresha Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo katika Mashamba ya Magereza; katika mwaka 2023/2024, Jeshi la Magereza limeweka lengo la kulima mazao katika jumla ya ekari 15,000. Kati ya hizo, ekari 5,245, zitalimwa mahindi; ekari 1,434, mpunga; ekari 2,553, alizeti; ekari 790, maharage; na ekari 4,998, mazao mengine. Mavuno yanayotarajiwa kupatikana ni tani 4,420 kwa mchanganuo ambao unaonekana kwenye kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya nishati na utunzaji wa mazingira. Katika kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais la kutumia nishati safi ya kupikia chakula cha wafungwa badala ya kutumia kuni, Jeshi la Magereza limeanza kutumia gesi katika Gereza la Keko, Chuo cha Taaluma ya Urekebishaji Tanzania, Dar es Salaam, pia mfumo wa gesi asilia umeanza kufungwa katika Gereza la Ukonga, Dar es Salaam kwa ajili ya kupika chakula cha wafungwa. Aidha. Serikali, imetenga shilingi bilioni moja katika bajeti ya mwaka

2023/2024 kwa ajili ya kuendeleza matumizi ya gesi kwa ajili ya kupikia katika magereza 19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza (SHIMA). Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imefanya mabadiliko ya Kanuni za Shirika la Magereza ili kuhakikisha linajiendesha kibiashara. Aidha, uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi Inspekta Jenerali wa Polisi Mstaafu Said Ally Mwema, Bodi mpya ya Wakurugenzi na Afisa Mtendaji Mkuu Ndugu Moremi Marwa umefanyika na ilizinduliwa rasmi tarehe 1 Novemba, 2022, kufanyika kwa mabadiliko haya kunachochea ufanisi katika utendaji wa shirika na kuwezesha kufikia malengo ya uanzishwaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko haya yamewezesha kupatikana na mafanikio makubwa katika shirika hilo kwa muda mfupi, ikiwemo kuandaliwa kwa mpango wa biashara wa miaka mitatu 2023/2024 – 2025/2026. Mpango huo unatoa dira ya ukuaji wa biashara ya SHIMA kwa kuzingatia utatuzi wa changamoto za kiutendaji kwa miradi inayohusu shughuli za msingi za shirika, kufanya marekebisho ya miongozo ya uendeshaji wa miradi na kuboresha matumizi ya rasilimali zilizopo ili ziweze kuleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shirika limepanga kufanya maboresho ya viwanda vya samani na ushonaji Ukonga na Kiwanda cha samani Uyui, maboresho hayo yatafanyika kwa kufanya matengenezo na ununuzi wa mashine mpya, lengo ni kuongeza ufanisi wa shughuli zinazotekelezwa kwenye viwanda hivyo katika utengenezaji wa bidhaa. Ili kufanikisha shughuli hizo, kiasi cha shilingi 165,000,000 kimepangwa kutumika katika mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio mengine ni kuboreshwa kwa utunzaji wa kumbukumbu za hesabu na matumizi ya mifumo ya teknolojia katika makusanyo ya mapato, ambapo katika kipindi cha Novemba, 2022 hadi Machi, 2023 mizania ya hesabu ya mali ya shirika imeongezeka kutoka shilingi bilioni 29 hadi kufikia Shilingi bilioni 49.44 kutoka Novemba 2022 hadi Machi 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kurudia: Mizania ya hesabu ya hesabu ya Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Magereza imeongezeka kutoka shilingi bilioni 29 hadi kufikia shilingi bilioni 49.44

sawa na ongezeko la takriban Shilingi bilioni 20 kwa muda huu mfupi. Hii inawezesha shirika kuongeza mtaji na kuwezesha ushirikiano wa kibiashara na sekta za kifedha na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha shughuli za kilimo katika msimu wa mwaka 2022/2023 shirika limelima ekari 5,306 ambapo ekari 3,925 zimelimwa mahindi, 865 mpunga, 197 maharage, 230 alizeti, 89 miwa, matarajio ni kuvuna tani 5,228 za mahindi na 973 za mpunga, tani 99 za maharage, tani 138 alizeti, tani 2,670 miwa. Mavuno haya yatasaidia kuongeza chakula cha wafungwa kinachozalishwa na shirika kutoka wastani wa tani 2,900 za mahindi na tani 973 za mpunga kwa mwaka 2022/2023 hadi kufikia tani 4,800 za mahindi na tani 1,486 za mpunga kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Mwentekiti, pia, itasaidia Serikali kupunguza gharama zitakazotumika kununua chakula kwa wazabuni wa nje. Mpango wa shirika ni kuwezesha kufikia zaidi ya asilimia 70 ya kujitosheleza na chakula cha wafungwa kwa mazao ya mahindi, mpunga, maharage ifikapo mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni Tanzu ya SHIMA *(Guard Security Company)*. Shirika kupitia kampuni yake tanzu ya *SHIMA Guard Security Company Limited* imeendelea kutoa huduma za ulinzi wa watu na mali kwa taasisi za umma pamoja na watu binafsi. Hadi kufikia mwezi Mei, 2023 vijana wa kitanzania zaidi ya 650 wamepatiwa mafunzo na kuajiriwa kwa ajili ya kazi za ulinzi. Kuanzishwa kwa Kampuni hii kumewezesha shirika kupata mapato ya wastani wa Shilingi bilioni 2.6 kwa mwaka. Katika mwaka 2023/2024 shirika litaendelea kutoa huduma za ulinzi na hivyo kuchangia katika mapato ya Shirika na kutoa ajira kwa Watanzania. Na ninatoa rai kwa taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma na binafsi pamoja na watu binafsi kutumia huduma ya ulinzi kupitia kampuni mahiri hii ya kizalendo kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limezima moto na kufanya uokoaji katika matukio 2,405. Katika matukio hayo Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kushirikiana na wadau wengine wameweza kuokoa majeruhi 71 na kilometa za mraba 719.33 za uoto wa asili wa Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na madhara makubwa yanayosababishwa na majanga ya moto, Serikali imenunua maboti mawili ya uokoaji na ununjuzi wa magari matatu ya kuzima moto. Boti moja linafanya kazi katika Mkoa wa Dar es Salaam na jingine moja Mkoa wa Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2022/2023 Serikali imetenga Shilingi bilioni 1.96 kwa ajili ya ununuzi wa magari 15 ya utawala na shughuli za ukaguzi wa kinga na tahadhari dhidi ya moto. Hadi kufikia mwezi Mei, 2023 shilingi bilioni 1.88 zimepokelewa na taratibu za ununuzi zinaendelea. Vilevile katika mwaka 2023/2024 Serikali imetenga Shilingi bilioni 1.96 kwa ajili ya ununuzi wa magari 12 ya utawala na ukaguzi wa kinga na tahadhari ya moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada nyingine Serikali imepata mkopo wa masharti nafuu wa *Euro* milioni 4.9 sawa na takribani shilingi bilioni 12.79 kutoka Serikali ya Austria kwa ajili ya ununuzi wa magari 12 ya kuzima moto, ikiwemo magari mawili ya ngazi yenye uwezo wa kuzima moto kwenye majengo yenye zaidi ya ghorofa 20. Magari hayo yanatarajia kuletwa nchini kuanzia Disemba, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali inakamilisha taratibu zitakazowezesha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kupata vitendea kazi vingi na vya kisasa kwa mkopo wa Dola za Marekani milioni 100, sawa na shilingi bilioni 232.61. Mkopo huu utatolewa na *Abu dhabi Export Credit (ADEX)* kutoka Serikali ya Falme za Kiarabu *(UAE)*. Kwa sasa Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango ipo katika hatua za juu majadiliano na Serikali ya Falme za Kiarabu *(UAE)* kupitia *ADEX* kuhusu upatikanaji wa mkopo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena nampongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi yote ya Ulinzi na Usalama kwa azma yake ya kutaka kuweka uwekezaji mkubwa wa kihistoria katika Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ambao haujawahi kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Mradi wa ujenzi wa kituo kikuu cha Zimamoto na Uokoaji *TAZARA* – Dar es Salaam umekamilika na ulizinduliwa rasmi na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango tarehe 28 Aprili, 2023. Miradi mingine iliyokamilika ni ujenzi wa Vituo vya Zimamoto na Uokoaji Nzuguni na Chamwino, miradi hiyo ilizinduliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa siku ya tarehe 26 Aprili, 2023. Aidha, ukarabati wa Kituo cha Zimamoto na Uokoaji Ilala - Dar es Salaam unaendelea na umefikia asilimia 74.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya maendeleo ya mwaka 2023/2024 Jeshi litafanya yafuatayo:-

(i) Ununuzi wa vifaa vya Zimamoto na Uokoaji shilingi milioni 500;

(ii) Ujenzi wa majengo mawili ya ghorofa Kikombo, Dodoma kwa shilingi bilioni 2.5;

(iii) Ukarabati wa nyumba 10 za makazi ya Askari katika Mikoa ya Arusha, Iringa na Morogoro kwa shilingi bilioni 400; na

(iv) Utekelezaji wa ujenzi wa Chuo cha Zimamoto na Uokoaji, Chogo, Tanga shilingi bilioni 1.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Idara ya Uhamiaji; udhibiti wa uingiaji na utokaji wa wageni na raia nchini; Idara ya Uhamiaji inatekeleza majukumu yake ya msingi ya utoaji wa huduma ya kiuhamiaji kwa wageni na raia. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2022 hadi Mei, 2023 jumla ya wageni 1,442,404 waliingia nchini ikilinganishwa na wageni 1,129,844 waliongia nchini kwa kipindi kama hicho mwaka 2021/2022. Ongezeko la wageni walioingia na kutoka nchini linatokana na Sera ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuwavutia wawekezaji kutembelea Tanzania kwa shughuli ya uwekezaji, utalii, biashara na shughuli za kijamii. Kwa mara nyingine tena, naomba kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa jitihada zake za kuvutia wageni kuingia nchini kwa shughuli za kiuchumi na kijamii hasa kupitia filamu yake *ya Royal Tour*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, operesheni, misako, doria na ukaguzi; operesheni, misako, doria na ukaguzi zimefanyika ili kuwadhibiti wageni wanaoingia nchini kinyume cha sheria. Hadi kufikia mwezi Mei, 2023 jumla ya watuhumiwa 22,882 wa makosa ya kiuhamiaji walikamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto ya wahamiaji haramu, hususan kutoka nchi ya Ethiopia, Serikali imefanya mapitio ya Kanuni ya Uhamiaji ya mwaka 2016 eneo la Visa kwenye Jedwali Na. 4 la nchi zinazohitaji viza rejea. Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa nchi ya Ethiopia sasa imeondolewa kwenye Jedwali Na. 4 la Orodha ya nchi zinazopata viza rejea kupitia Gazeti la Serikali la tarehe 27 Januari, 2023, *GN*. 37/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa raia wa Ethiopia wanaruhusiwa kuingia nchini kwa sharti la kuwa na Pasipoti ya Taifa lao na viza na kuendelea na safari nje ya Tanzania. Hatua hii ni katika kupata ufumbuzi wa changamoto ya muda mrefu ya wahamiaji haramu kutoka nchini humo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2023/2024 Wizara itaendelea kudhibiti wahamiaji haramu kwa kuhakikisha watu wote wanaoingia nchini wanazingatia sheria. Aidha, elimu itaendelea kutolewa kuhusu Sheria za Uhamiaji pamoja na kuanzisha kauli mbiu isemayo "Mjue Jirani Yako." Lengo ni kuwashirikisha wananchi katika kuwabaini wahamiaji haramu na kuwapa elimu juu ya madhara ya kuwahifadhi wageni wasiostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Idara ya Uhamiaji itaanza ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Songwe, Ofisi ya Wilaya Mufindi, Iringa, Kituo cha Uhamiaji Kirongwe, Mara, vilevile ujenzi wa nyumba 12 zitajengwa kwa ajili ya makazi ya wakufunzi katika Chuo cha Raphael Kubaga, Tanga. Aidha, ukarabati utafanyika katika nyumba 12 za watumishi Mkoani Tabora na Ofisi za Uhamiaji za Wilaya ya Kahama, Shinyanga na Ifakara, Morogoro. Jumla ya shilingi bilioni 4.34 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)*. Kazi ya usajili na utambuzi wa watu inaendelea kufanyika, katika kipindi cha mwezi Julai, 2022 hadi Mei, 2023, wananchi

774,594 walisajiliwa kati ya hao 733,238 walisajiliwa Tanzania Bara na 41,356 walisajiliwa Zanzibar. Hivyo, kufanya idadi ya wananchi waliosajiliwa tangu kuanza kwa usajili wa watu nchini mwaka 2012 kufikia watu 23,960,323.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza kasi ya usajili, napenda kulitangazia Bunge hili kuwa mwezi Desemba, 2022 *NIDA* imeanza kupokea maombi ya usajili kwa njia ya mtandao. Huduma hiyo itapunguza gharama na foleni kwa watu katika ofisi za usajili za *NIDA*, hususan maeneo ya mijini. Hadi kufikia mwezi Mei, 2023 maombi 17,248 yalipokelewa kupitia njia ya mtandao. Katika mwaka 2023/2024 Serikali itaendelea na zoezi la usajili na utambuzi wa watu katika Wilaya na Mikoa yote, ambapo jumla ya watu 1,597,827 wanatarajiwa kusajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kufanya jitihada za kuhakikisha watu wote wenye namba za utambulisho wanapata vitambulisho vyao. Hadi kufikia Mei, 2023 *NIDA* imepokea shilingi bilioni 28. Aidha, *NIDA* imeshafungua barua za malipo *(Letter of Credit)* ya shilingi bilioni 42.5 kwa ajili ya ununuzi wa kadighafi 11,242,353 na taratibu za ununuzi zinaendelea. Upatikanaji wa kadighafi hizo utawezesha wananchi wote waliosajiliwa nchi nzima kupata vitambulisho vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imefanya marekebisho ya Kanuni za Usajili na Utambuzi wa Watu za mwaka 2014. Marekebisho hayo yamefanyika katika maeneo ya ukomo wa muda wa Vitambulisho vya Taifa kwa Watanzania, huduma ya ushirikishanaji wa taarifa na usajili wa walowezi na Watanzania wanaoishi nje ya nchi. Matokeo tarajiwa ni kuimarika kwa usalama kwa kuwatambua watu wote, kuboresha utolewaji wa huduma na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Naomba nitoe maagizo kwa watoa huduma wote kuendelea kuvitambua Vitambulisho vya Taifa bila kuzingatia tarehe ya muda wa ukomo wa matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 27 Oktoba, 2022 Serikali ilisaini Mkataba wa Mkopo wa Masharti Nafuu na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Korea kwa ajili ya kuanza awamu ya pili ya mradi wa ujenzi wa ofisi za *NIDA*. Mradi unahusisha ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu, Dodoma, ofisi 31 za usajili za Wilaya na ghala la kuhifadhia

vifaa vya TEHAMA. Kwa sasa *NIDA* ipo katika taratibu za mwisho za ununuzi za kumpata mshauri elekezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaangalia uwezekano wa kuunganisha vitambulisho vinavyotumika kwa huduma mbalimbali ikiwemo leseni ya udereva, kadi za bima za afya na vitambulisho vya mpiga kura ili kuwa na kitambulisho Kitambulisho Kimoja cha Taifa *(Universal National Identification Card)*. Katika kufanikisha hilo, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi mwezi Mei, 2023 imefanya majadiliano ya awali na Maafisa Waandamizi wa *Bill & Melinda Gates Foundation* ya Marekani ambayo imeonesha nia ya kusaidia mpango huo. Mpango huo utapunguza gharama za Serikali katika ununuzi wa kadi ghafi na kuchapisha vitambulisho, kuwezesha upatikanaji wa huduma za kiuchumi na kijamii kwa wananchi na kurahisisha upatikanaji wa kadi hizo kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha mpango huo, katika mwaka 2023/2024 Serikali itaanza kufanya yafuatayo:-

(i) Kushirikisha wadau wote muhimu kupata maoni;

(ii) Kurekebisha Sheria ya Utambuzi na Usajili ili kuwezesha mtu kusajiliwa tangu anapozaliwa hadi anapofariki;

(iii) Kutumia teknolojia ya kisasa kwa kushirikiana na nchi zenye uzoefu na zinazotumia kitambulisho kimoja cha Taifa na kuwekeza katika mifumo ya kisasa ya utambuzi na usajili wa watu pamoja na utoaji wa vitambulisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma kwa wakimbizi; hadi kufikia Mei, 2023, Tanzania inahifadhi jumla ya wakimbizi 269,749. Serikali kwa kushirikiana na *UNHCR* imefanikiwa kutafuta suluhisho la kudumu kwa ajili ya wakimbizi 10,335 kati ya hao wakimbizi 5,324 walirejeshwa kwa hiyari yao katika nchi ya Burundi na wakimbizi 5,011 walihamishiwa katika Mataifa ya Marekani, Canada, Ufaransa na Australia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2023/2024 Wizara ya itaendelea kusimamia hali ya ulinzi na usalama katika makazi ya kambi za wakimbizi na maeneo yanayozunguka kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama. Kuwatafutia suluhisho la

kudumu wakimbizi waliopo nchini, kusimamia na kufuatilia utunzaji wa mazingira katika maeneo ya kambi za wakimbizi. Jumla ya shilingi bilioni 1.73 zimetengwa katika mwaka 2023/2024 kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usajili wa jumuiya za kidini na zisizo za Kidini. Wizara inaendelea kusajili na kusimamia Jumuiya za Kidini na zisizo za Kidini kwa kuzingatia Sheria. Hadi mwezi Mei, 2023 jumla ya maombi ya usajili wa jumuiya 429 yalipokelewa. Jumla ya Jumuiya 375 zilisajiliwa na maombi 54 yanaendelea kufanyiwa kazi. Usajili huu unafanya idadi ya jumuiya za kidini na zisizo za kidini zilizosajiliwa kufikia 10,108. Aidha, Ofisi ya Msajili wa Jumuiya ilifanya zoezi la uhakiki wa Taasisi za Kidini 672 na kuhuisha vyeti husika vya usajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kudhibiti na kupambana na katika kudhibiti na kupambana na vitendo vya mmomonyoko wa maadili kwenye Jumuiya za Kidini na zisizo za Kidini, Ofisi ya Msajili wa Jumuiya imefanya yafuatayo:-

(i) Imesitisha shughuli za Jumuiya ya kidini iitwayo *Spirit Word Ministry* iliyoko Jijini Dar es Salaam. Jumuiya hiyo imefutiwa usajili kwa sababu ya kutoa mahubiri na mafundisho yenye mwelekeo wa kuhamasisha vitendo vya mapenzi ya jinsia moja na kutoa ujumbe kwenye mitandao ya ushoga.

(ii) Vilevile taarifa zimekusanywa zinazohusu idadi ya vituo vya kulea watoto na shule zinazotoa mafunzo ya kidini kwa watoto wadogo ili kuzifanyia kazi.

(iii) Pia elimu imetolewa kwa Viongozi wa Jumuiya za Kidini ili waendelee kutoa mafundisho kwa waumini yanayoendana na mila, desturi na maadili ya Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2020/2023 Wizara imepanga kuandaa mwongozo wa taratibu za kuabudu na ithibati ya taasisi zinazotoa elimu ya dini. Kuimarisha ufuatiliaji na utendaji wa Jumuiya za Kidini na zisizokuwa za Kidini na kutoa mafunzo kwa Viongozi wa Jumuiya yatakayochangia kudumisha amani na utulivu nchini. Aidha. Wizara itaanzisha Ofisi ya Kanda ya Msajili,

Kanda ya Ziwa na Ofisi ya Kanda Nyanda za Juu Kusini pamoja na kuifanyia marekebisho Sheria ya Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani. Naomba nimshukuru Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mussa Hassan Zungu. Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge ukiwemo wewe mwenyewe Mheshimiwa Baran Sillo na Wenyeviti wengine. Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge ikiwemo Kamati ya Kudumu ya NUU kwa kusimamia vizuri shughuli za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa umoja wenu mmewezesha shughuli za Bunge kuendelea vema na kutoa ushauri unaosaidia kuimarisha utendaji wa Wizara na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile natoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mbunge wa Jimbo la Butiama kwa kunisaidia kusimamia majukumu ya Wizara. Aidha, ninawashukuru Katibu Mkuu Ndugu Kaspar Mmuya na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Maduhu Kazi, kwa kusimamia vema utekelezaji wa kazi za Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawashukuru Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama vilivyopo chini ya Wizara kwa kuhakikisha uwepo wa amani na utulivu nchini na kuwezesha kupatikana kwa mafanikio mbalimbali. Viongozi hao ni Inspekta Jenerali wa Jeshi la Polisi, *IGP* Camillus Wambura, Kamishna Jenerali wa Magereza, Mzee Ramadhan Nyamka, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, John Masunga, Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dkt. Anna Makakala. Pia namshukuru Mkurugenzi Mkuu wa *NIDA,* Ndugu Ismail Rumatila. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani nyingine nazitoa kwa Wenyeviti wa Bodi za Mashirika yaliyopo chini ya Wizara ambao ni Prof. Suffian Bukurura, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi, Inspekta Jenerali wa Polisi Mstaafu Saidi Mwema, Mwenyekiti wa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Magereza. Wenyeviti hao kwa kushirikiana na Wajumbe wa Bodi wamekuwa wakitoa ushauri na kuboresha utendaji na usimamizi wa mashirika hayo ambayo yanaendelea kuimarika. Aidha,

namshukuru Mheshimiwa Balozi Khamis Kagasheki Mwenyekiti wa Bodi ya Parole kwa kusimamia vema majukumu ya Bodi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawashukuru Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Makamishna, Makamishna Wasaidizi, Wakuu wa Vitengo, Maafisa, Askari na watumishi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kuendelea kutekeleza majukumu ya Wizara hii kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, naomba nitoe shukrani pia kwa wadau mbalimbali wa maendeleo zikiwemo Nchi za Austria, Marekani, Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu, Umoja wa Ulaya, Jamhuri ya Korea Kusini pamoja na Kampuni na Mashirika ya *IOM, UNDP, UNHCR, UNICEF, UNFPA, UN – Women, WFP, TIRA, Buzwagi Gold Mine, North Mara Gold Mine,* taasisi za kidini na zisizokuwa za kidini, vyombo vya habari na wananchi kwa ujumla kwa kuendelea kushirikiana na Wizara katika nyanja mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, shukrani za kipekee nizitoe kwa familia yangu, akiwemo mke wangu, Ndg. Thaniya Abdallah, baba yangu mzazi, ndugu na jamaa, kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Kwa dhati kabisa ninawashukuru na kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Kikwajuni kwa kushirikiana nami katika kuwezesha maendeleo ya jimbo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hapa nina ujumbe mzito kutoka Jimbo la Kikwajuni, viongozi wa Chama cha Mapinduzi, ngazi za wilaya, jimbo, wadi na matawi, wote wapo. Ni miongoni mwa orodha ambazo ziliwasilishwa, na ninadhani ikikupendeza vilevile utaweza kuwatambulisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kuhusu makadirio ya ukusanyaji wa mapato kwa mwaka 2023/2024; katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara imewekewa lengo la kukusanya jumla ya shilingi bilioni 393.50 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, naomba sasa Bunge lako liidhinishe Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya

Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 yenye jumla ya shilingi 1,293,820,903,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 510,135,630,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, shilingi 678,657,324,000 ni mishahara na shilingi 105,027,949,000 ni fedha za miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo, shilingi 100,233,364,000 ni fedha za ndani na shilingi 4,794,555,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI MHE. MHANDISI HAMAD M. Y. MASAUNI (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2023/2024 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZNAI**

**A. UTANGULIZI**

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2022/23 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2023/24.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na akuweza kusimama katika Bunge hili kuwasilisha Hotuba hii. Kipekee namshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini kuendelea kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Nampongeza Mhe. Rais kwa kuendelea kuingoza vema nchi yetu chini ya Chama cha Mapinduzi Mapinduzi (CCM). Wote tunashuhudia hali ya amani, utulivu na usalama ikiendelea kuwepo nchini, ikiwa ni miongoni mwa misingi ya maendeleo ya Taifa letu.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** pongezi zangu pia nazitoa kwa Viongozi wote wa Kitaifa akiwemo Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.) na Naibu Spika Mhe. Mussa Azan Zungu (Mb.).

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** Viongozi wote hawa kwa pamoja wameonesha uwezo mkubwa katika kumsaidia Mhe. Rais kuliongoza Taifa letu. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itaendelea kupokea na kutekeleza maelekezo ya Viongozi hawa yenye lengo la kuimarisha utendaji wa Wizara ili kuongeza ufanisi katika kuhudumia wananchi.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mara nyingine namshukuru Mhe. Rais kwa kufanya uteuzi wa baadhi ya Viongozi wa Wizara hii. Tarehe 09 Desemba, 2022 Mhe. Rais alimteua Bw. Kaspar K. Mmuya kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kufuatia kustaafu kwa aliyekuwa Katibu Mkuu ndugu Christopher Kadio. Tarehe 20 Agosti, 2022 alimteua Kamishna wa Polisi Camillus M. Wambura kuwa Inspekta Jenerali wa Jeshi la Polisi.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, tarehe 24 Agosti, 2022 Mhe. Rais alimpandisha cheo na kumteua Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Magereza Mzee Ramadhani Nyamka kuwa Kamishna Jenerali wa Magereza. Kwa niaba ya watumishi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi nawapongeza kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mhe. Rais. **HONGERENI SANA**. Pia, tarehe 18 Aprili, 2023 Mhe. Rais alimteua Mhe. Balozi Khamis Sued Kagasheki kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Parole, nampongeza kwa uteuzi huo.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** natumia nafasi hii pia kuwapongeza na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ikijumuisha Wajumbe Mahiri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama (NUU) chini ya uongozi wa Mhe. Vita Rashid Kawawa Mbunge wa Jimbo la Namtumbo na Makamu Mwenyekiti Mhe. Vincent Paul Mbogo Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kusini. Kamati hii imekuwa na mchango muhimu katika kutoa maoni, ushauri na maelekezo yanayosaidia kutatua changamoto za Wizara. Aidha, Kamati imetoa ushirikiano mkubwa uliosaidia kuboresha bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka 2023/24.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** tarehe 13 Oktoba, 2022 tulimpoteza Mbunge mwenzetu Mhe. Mussa Hassan, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Amani, Zanzibar kupitia CCM. Tarehe 12 Mei, 2023 Taifa lilimpoteza mwana Diplomasia mahiri na aliyewahi kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Bw. Bernad Membe. Pia, tarehe 30 Novemba, 2022 tulimpoteza Bw. Mbarak Abdulwakil

Katibu Mkuu Mstaafu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Naomba nitumie fursa hii kutoa pole kwako Mhe. Spika, Waheshimiwa Wabunge na familia yake, kwa kuondokewa na mpendwa wetu. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, ***Amina***. Natoa pole pia kwa ndugu, familia na marafiki waliopoteza ndugu zao kutokana na sababu mbalimbali.

**Mapitio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2022/23**

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya Shilingi 1,211,881,077,000. Kati ya fedha hizo Shilingi 600,219,122,000 ni kwa ajili ya Mishahara, Shilingi 471,249,055,000 ni za Matumizi Mengineyo na Shilingi 140,412,900,000 ni za Miradi ya Maendeleo.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Mei, 2023 jumla ya Shilingi 976,877,690,655.38 zilipokelewa na Wizara. Kati ya fedha hizo, Shilingi 504,645,025,215.43 zilikuwa ni za Mishahara, Shilingi 386,567,104,386.27 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi 85,665,561,054 ni za Miradi ya Maendeleo. Fedha zilizopokelewa ni sawa na **asilimia 80.61** ya bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia ilipokea jumla ya Shilingi 82,521,836,419.70 kwa ajili ya kulipa madeni ya watumishi, wakandarasi, wazabuni na watoa huduma. Kati ya fedha hizo, Shilingi 280,008,599.3 ni za Makao Makuu ya Wizara, Shilingi 53,910,466,616.18 ni kwa Jeshi la Polisi, Shilingi 8,116,884,045.61 ni za Jeshi la Magereza, Shilingi 2,408,599,070.77 za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Shilingi 4,068,825.06 ni kwa Idara ya Uhamiaji na Shilingi 17,801,809,262.78 kwa ajili ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa.

**Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali**

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** malengo ya ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali yaliyowekwa kwa mwaka 2022/23 ni jumla ya Shilingi 367,600,000,000. Kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 jumla ya Shilingi 264,662,604,640.27 zilikusanywa sawa na asilimia 72 ya lengo.

## B. MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA MWAKA 2022/23

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2022/23 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imefanikiwa kukamilisha jumla ya miradi 23 ambayo ni: ujenzi wa majengo mawili (2) ya makazi ya familia 24 za askari Polisi eneo la Mabatini – Mwanza; nyumba nne (4) za kuishi familia nane (8) za askari Polisi Kusini Pemba; jengo moja (1) la kuishi familia nne (4) za askari Kaskazini Pemba; Ofisi tatu (3) za Makamanda wa Polisi wa Mikoa ya Kusini Unguja, Kaskazini Unguja, na Mkoa wa Kipolisi Tarime – Rorya; ujenzi wa nyumba tatu (3) za kuishi Makamishna wa Jeshi la Polisi – Jijini Dodoma; ujenzi wa vituo vitatu (3) vya Polisi Daraja "A'' vilivyopo Lushoto – Tanga, Wanging'ombe – Njombe na Kigamboni – Dar es Salaam; na ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja "B'' Ruangwa – Lindi.

**14.** ***Mheshimiwa Spika***, miradi mingine iliyokamilika ni ujenzi wa Vituo viwili (2) vya Polisi Daraja "C'' Kizimkazi – Kusini Unguja na Kirongwe Mkoa wa Kipolisi Tarime – Rorya; ujenzi wa Wodi ya wazazi na chumba cha upasuaji katika Zahanati ya FFU Ukonga – Dar es Salaam; ujenzi wa Vituo vitatu (3) vya Zimamoto na Uokoaji vilivyopo Nzuguni na Chamwino – Dodoma na Kituo Kikuu cha Zimamoto na Uokoaji TAZARA – Dar es Salaam; ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji Mikoa ya Geita, Lindi na Manyara; na ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji za Wilaya za Masasi, Nanyumbu, Newala na Tandahimba.

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** kukamilika kwa miradi 23 ambayo mingi ilikuwa haijakamilika kwa muda mrefu, kumeweka historia ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Historia hii ni matokeo ya dhamira ya dhati aliyonayo Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu ya kuleta mageuzi katika Wizara hii kwa kuviwezesha na kuviimarisha vyombo vyake vya usalama ili viweze kuhudumia wananchi kwa weledi na ufanisi zaidi.

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanikiwa kupokea jumla ya magari 162, kati ya hayo, magari mawili (2) ni ya Makao Makuu ya Wizara; 156 ya Jeshi la Polisi; na manne (4) ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Mafanikio mengine ni kuanza kutoa huduma za Polisi katika Kata 3,956 za Tanzania Bara na Shehia 388 za Zanzibar; kuokolewa na kutoa misaada kwa wahanga 156 wa usafirishaji

haramu wa binadamu; wakimbizi 10,335 walipatiwa suluhisho la kudumu, ambapo wakimbizi 5,324 walirejeshwa kwa hiari yao nchini Burundi na wakimbizi 5,011 walihamishiwa katika mataifa ya Marekani, Canada, Ufaransa na Australia; na kuanza kutumika kwa mfumo wa NIDA wa kielektroniki katika kuwasilisha maombi ya usajili na utambuzi wa watu.

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio hayo yanaonesha dhamira ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na CCM chini ya uenyekiti wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuleta mageuzi katika Wizara hii. Pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais, Viongozi wote wa kitaifa wa chama na Serikali, Viongozi na watumishi wote wa Wizara kwa ujumla.

## C. MAENEO YA KIPAUMBELE KATIKA BAJETI YA MWAKA 2023/24

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2023/24 imeweka kipaumbele katika maeneo yafuatayo: kuendelea kudumisha amani na usalama wa raia na mali zao kwa kufanya doria, misako na operesheni maalum; kuendeleza ushirikishwaji jamii kwenye ulinzi wa umma; kukamilisha miradi ya maendeleo inayoendelea kutekelezwa; kuimarisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utoaji wa huduma na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali; kuboresha mazingira ya kazi na makazi kwa watumishi na askari; na kuongeza vitendea kazi vya kisasa katika kutoa huduma ikiwemo magari, boti, helkopta, pikipiki pamoja na mitambo na dhana za kisasa.

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** maeneo mengine ya kipaumbele ni: kuimarisha ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo; kuimarisha usimamizi wa Sheria ya Usalama Barabarani ili kupunguza matukio ya ajali na kufanya mapitio ya Sheria nyingine zinazohusu Wizara na kuandaa Kanuni; kuboresha huduma za urekebu wa wafungwa; kuimarisha uzalishaji katika mashamba ya magereza kwa ajili ya mahitaji ya chakula cha wafungwa na mahabusu; kuimarisha mashirika yaliyopo chini ya Wizara; kuboresha usimamizi wa watumishi na stahiki zao; kutoa mafunzo kwa watumishi raia na askari ndani na nje ya nchi; kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala yanayohusu Wizara; na kuimarisha utunzaji wa mazingira kwa kupanda miti, kupunguza matumizi ya kuni kwa kutumia nishati

mbadala kwenye Magereza, Makambi ya Wakimbizi na vyuo vilivyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa ujumla Wizara itaendelea kusimamia maboresho yanayoendelea kwenye vyombo vyake vya usalama pamoja na kuendelea kufanyia kazi maelekezo ya Mhe. Rais anayoyatoa na yatakayotolewa kupitia Tume ya Uboreshaji wa Haki Jinai, inayohusisha masuala ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

## D. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2022/23 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2023/24

### Upandishaji Vyeo

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya watumishi 1,696 wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi walipandishwa vyeo. Idadi hiyo inajumuisha maafisa, wakaguzi na askari 622 wa Jeshi la Polisi, 130 wa Jeshi la Magereza, 762 wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na 182 wa Idara ya Uhamiaji. Katika mwaka 2023/24 Wizara itaendelea kuwapandisha vyeo maafisa, wakaguzi, askari na watumishi raia katika ngazi mbalimbali.

### Ajira kwa Askari na Watumishi Raia

**22.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/23 Serikali imetoa kibali cha kuajiri jumla ya askari 6,608 kwa majeshi yaliyopo chini ya Wizara. Jeshi la Polisi limepata kibali cha kuajiri askari wapya 3,158 na watumishi raia 57. Askari hawa wameanza mafunzo ya awali ya Jeshi la Polisi katika Shule ya Polisi Moshi mwezi Aprili, 2023.

**23.** ***Mheshimiwa Spika***, pia, Jeshi la Magereza limepata kibali cha kuajiri askari wapya 1,975. Kati ya hao, askari wapya 1,241 wamemaliza mafunzo na wamepangiwa vituo vya kazi. Usaili wa kuwapata askari wengine 734 wenye sifa za kujiunga na Jeshi la Magereza umekamilika na mafunzo yataanza mwezi Juni, 2023 na kukamilika mwezi Desemba, 2023.

**24.** ***Mheshimiwa Spika***, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limepatiwa kibali cha kuajiri askari wapya 79 ili kuendelea kuboresha utendaji kazi. Askari hao wanaendelea na mafunzo ya awali katika Chuo cha Zimamoto na Uokoaji kilichopo Chogo katika Wilaya ya Handeni – Tanga. Baada ya kumaliza mafunzo hayo, Askari hao watapelekwa katika Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo – Zanzibar (KMKM) kwa ajili ya kupata mafunzo ya uogeleaji na uokoaji.

**25.** ***Mheshimiwa Spika***, Idara ya Uhamiaji imeajiri Askari 818 ambao wameanza kazi mwezi Septemba, 2022. Idara hiyo pia imepata kibali cha kuajiri Askari wapya 521 ambao wameanza mafunzo ya awali ya uhamiaji mwezi Machi, 2023 katika Chuo cha Raphel Kubaga kilichopo Wilaya ya Mkinga – Tanga. Kuajiriwa kwa askari hao kutawezesha kuimarisha utendaji kazi katika majeshi hayo na kuendelea kutoa huduma bora kwa jamii.

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Wizara inatarajia kuajiri jumla ya askari 3,117 kwa lengo la kuboresha utendaji kazi. Kati ya hao, askari 2,000 ni wa Jeshi la Polisi, 517 wa Jeshi la Magereza, 200 wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na 400 wa Idara ya Uhamiaji.

**Mafunzo kwa Watumishi**

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya maafisa, wakaguzi, askari na watumishi raia 7,282 wameendelea kupatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo. Kati ya hao, 69 ni wa Makao Makuu ya Wizara, 5,041 Jeshi la Polisi, 662 Jeshi la Magereza, 764 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na 751 Idara ya Uhamiaji. Mafunzo hayo yamegharamiwa na Serikali kwa asilimia 100 bila kuwa na makato yoyote kutoka kwenye posho za askari. Lengo la mafunzo hayo ni kuimarisha utendaji na kuwaendeleza watumishi kitaaluma ili kuwaongezea ujuzi, maarifa na stadi katika utekelezaji wa majukumu yao.

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Wizara itaendelea kuwapatia mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kiutendaji askari, maafisa na watumishi raia. Jumla ya Shilingi 29,930,465,106 zimetengwa ili kuwezesha mafunzo hayo. Kati ya fedha hizo, Shilingi 546,833,100 ni kwa ajili ya Makao Makuu ya Wizara, Shilingi 20,745,066,706 ni za Jeshi la Polisi, Shilingi 4,014,610,000 ni za Jeshi la

Magereza, Shilingi 570,000,000 ni za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Shilingi 3,203,994,000 ni za Idara ya Uhamiaji. Hivyo, napenda kusisitiza kuwa Askari wote wa Vyombo vya Usalama chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi wataendelea kupata mafunzo bila kukatwa posho zao kama nilivyoeleza katika Hotuba yangu ya mwaka 2022/23.

**Ununuzi wa Sare za Maafisa na Askari**

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23 imetoa jumla ya Shilingi bilioni 10,256,793,289.10 kwa ajili ya ununuzi wa sare za maafisa na askari wa Vyombo vya Usalama vilivyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Zabuni za ununuzi wa Sare hizo zimetolewa kwa Shirika la Jeshi la Polisi na Shirika la Magereza (SHIMA). Aidha, jumla ya Shilingi bilioni 2,872,768,000 zimetolewa kwa ajili ya kununua jozi za viatu vya maafisa na askari. Viatu hivyo vitanunuliwa kutoka Kampuni ya kutengeneza Bidhaa za Ngozi Kilimanjaro International Leather Company.

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Serikali imetenga jumla ya bilioni 16,027,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa sare za maafisa na askari. Aidha, ninahamasisha mashirika yaliyopo chini ya Wizara yaendelee kushiriki katika zabuni za ununuzi wa sare za Vyombo vya Usalama chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa lengo la kupata sare zenye ubora na bei nafuu pamoja na kuwezesha mashirika kujiimarisha kwa kuzingatia fursa zilizopo kwenye vyombo hivyo.

**Upimaji, Uthamini na Ulipaji wa Fidia katika Maeneo ya Majeshi yaliyopo Chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kupima na kupata hati za maeneo yake. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Shilingi 499,995,500 zimepokelewa kwa ajili ya kufanya upimaji na uthamini katika maeneo 55 yanayomilikiwa na Jeshi la Magereza. Pia, maeneo 35 ya Jeshi la Zimamoto na uokoaji yamepatiwa hati miliki na maeneo 47 yamelipiwa gharama za upimaji kati ya maeneo 163 inayomiliki. Upimaji huo utasaidia kuondoa mwingiliano na migogoro katika maeneo ya majeshi hayo.

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Jeshi la Polisi litalipa fidia ya maeneo manne (4) kwa gharama ya Shilingi 312,441,377. Maeneo hayo yapo katika Wilaya ya Kilolo – Iringa (2), Chalinze – Pwani (1) na Njombe – Njombe (1). Maeneo husika ni kwa ajili ya ujenzi wa Vituo na Kambi za Polisi. Pia, Shilingi 53,645,845 zitatumika kugharamia upimaji na umilikishwaji wa maeneo matano (5) kwa matumizi ya Jeshi la Polisi katika Wilaya za Kilindi – Tanga (1), Loliondo – Arusha (1) na Tanganyika – Katavi (3).

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Shilingi 242,747,421 zitatumika kupima ardhi ya maeneo mbalimbali ya Jeshi la Polisi ili kuwezesha upatikanaji wa hati miliki. Upimaji huo unajumuisha kuchora ramani za maeneo hayo kulingana na mipango miji ya mji husika. Shilingi 200,000,000 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na upimaji na uthamini wa ardhi katika maeneo 14 ya Jeshi la Magereza ambayo ni Chuo Kiwira – Mbeya, Chalinze – Pwani, Namtumbo – Ruvuma, Nanyumbu – Mtwara, Hanan'g – Manyara, Muleba – Kagera, Liwale – Lindi, Kalambo – Rukwa, Mlele – Katavi, Ikungi – Singida, Bahi – Dodoma, Wazo Hill na Kambi Kimbiji na Mvuti – Dar es Salaam.

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shilingi 550,000,000 zitatumika kulipa fidia ya ardhi iliyotwaliwa na Jeshi la Magereza katika Wilaya za Chamwino – Dodoma na Kaliua – Tabora. Aidha, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limetenga Shilingi 210,000,000 kwa ajili ya kulipa fidia na kugharamia upatikanaji wa hati katika maeneo yake. Pia, kiasi cha Shilingi 120,000,000 kimetengwa kwa ajili ya ulipaji wa fidia, upimaji na upatikanaji wa hati miliki ya viwanja 46 vya Idara ya Uhamiaji.

**Mapitio ya Sheria, Kanuni na Itifaki**

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwezi Julai, 2022 hadi Mei, 2023 mapitio yamefanyika katika kanuni zifuatazo: Kanuni za Kuzuia Ugaidi za Mwaka 2022; Kanuni za Usajili na Utambuzi wa Watu za Mwaka 2014; Kanuni za Viza za Uhamiaji za mwaka 2016; na Marekebisho ya Amri ya uanzishaji wa Bodi ya Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza ya Mwaka 2006. Aidha, Kanuni za Kudumu za Idara ya Uhamiaji – Immigration General Orders (IGO), 2023 zimetungwa.

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali iliridhia Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi ya Mwaka 2004 (Protocol to the (OAU) Convention on the Prevention of Terrorism, 2004). Azimio la Itifaki hiyo liliridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Septemba, 2022. Pia, Serikali ililiridhia Itifaki ya Uwezeshaji wa Uingiaji na Utokaji wa Watu ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika ya Mwaka 2005 (SADC Protocol on the Facilitation of Movement of Persons, 2005). Azimio la Itifaki hii litawasilishwa Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa kwa mujibu wa Ibara 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Wizara itafanya mapitio ya baadhi ya Sheria ili kuimarisha usimamizi. Miongoni mwa Sheria hizo ni: Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54; Sheria ya Parole, Sura ya 400; Sheria ya Magereza, Sura ya 58; Sheria ya Huduma kwa Jamii, Sura ya 291; Sheria ya Uangalizi wa Wafungwa, Sura ya 247; Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432; Sheria ya Jumuiya, Sura ya 337; Sheria ya Tume ya Utumishi ya Jeshi la Polisi, Magereza, Zimamoto na Uokoaji na Uhamiaji, Sura ya 241; Sheria ya Wakimbizi Na. 9 ya mwaka 1998; na Sheria ya Usajili na Utambuzi wa Watu ya mwaka 1986, Rejeo la mwaka 2012. Mabadiliko hayo ya sheria yataenda sambamba na marekebisho ya kanuni za sheria husika na utekelezaji wa program ya maboresho yanayoendelea ndani ya Wizara.

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Shilingi 480,041,500 zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha mapitio ya sheria, kanuni na kazi nyingine za kisheria. Mabadiliko hayo yataenda sambamba na utekelezaji wa program ya maboresho yanayoendelea ndani ya Wizara.

## JESHI LA POLISI

### Hali ya Usalama Nchini

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** wajibu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni kuhakikisha usalama wa watu na mali zao na kuendelea kuwepo kwa amani na utulivu nchini. Hali hii inawezesha shughuli za kiuchumi na kijamii kufanyika na kuchangia katika maendeleo ya Taifa letu. Katika kutekeleza wajibu huo, Wizara hushirikiana na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama, jamii na wadau wengine ili kuhakikisha uhalifu wa aina zote unadhibitiwa.

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kuwepo kwa hali ya amani na utulivu nchini, uhalifu wa makosa dhidi ya binadamu, maadili ya jamii na kuwania mali umeendelea kuwepo. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 makosa makubwa ya jinai yaliyotolewa taarifa katika Vituo vya Polisi yalikuwa 45,455 ikilinganishwa na makosa 43,771 yaliyotolewa taarifa katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Hili ni ongezeko la makosa 1,684 sawa na asilimia 3.8.

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** ongezeko la makosa haya makubwa linatokana na watu kujichukulia sheria mkononi, wivu wa mapenzi, imani za kishirikina, migogoro ya ardhi na mirathi, mmomonyoko wa maadili na tamaa ya mapenzi. Hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ni kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu kuzingatia sheria, kuhamasisha jamii kutoa taarifa za makosa hayo kwa wakati kwa kushirikisha Viongozi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji na kushirikisha Viongozi wa Dini katika kutoa elimu ya maadili mema kwa jamii.

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023, jumla ya mashauri ya Jinai 45,455 yameshughulikiwa. Mashauri 19,671 yalifikishwa mahakamani, ambapo 4,400 yameshinda, 545 yalishindwa, mashauri 41 yaliondolewa mahakamani na 14,685 yanaendelea kusikilizwa mahakamani. Aidha, mashauri 2,334 yalifungwa katika vituo vya polisi, 136 yalipelekwa Idara ya Uhamiaji na 23,314 yapo chini ya upelelezi.

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa upelelezi unafanyika kwa weledi na kuzingatia *Police General Order,* Jeshi la Polisi linaendelea kuwapatia mafunzo ndani na nje ya nchi maafisa, wakaguzi na askari. Mafunzo hayo yanahusisha upelelezi wa makosa ya Jinai kwa kutumia vifaa vya kisasa yakiwemo makosa ya mtandao, uhalifu wa kifedha na yanayovuka mipaka. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 jumla ya askari 240 walipatiwa mafunzo. Kwa kuwa upelelezi wa mashauri ya makosa ya Jinai ni suala mtambuka, Jeshi la Polisi limeimarisha ushirikiano na taasisi mbalimbali ili kuhakikisha upelelezi wa mashauri unakamilika kwa wakati.

**Hali ya Usalama Barabarani**

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama barabarani imeendelea kuimarika kutokana na Jeshi la Polisi kuendelea kusimamia Sheria za Usalama Barabarani kwa kushirikiana na wadau. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 jumla ya matukio ya ajali 1,283 yaliyotolewa taarifa ikilinganishwa na matukio 1,731 yaliyotolewa taarifa katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22 ikiwa ni kupungua kwa matukio 448 sawa na asilimia 25.9.

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupungua kwa matukio ya ajali kunatokana na kuimarisha usimamizi wa sheria, kufanyika kwa operesheni maalum, doria na misako nchi nzima. Aidha, elimu ya usalama barabarani imeendelea kutolewa kwa makundi yote yanayotumia barabara.

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** matukio ya ajali za barabarani, yalisababisha watu 1,893 kujeruhiwa katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 ikilinganishwa na watu 2,323 waliojeruhiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Idadi ya majeruhi imepungua kwa watu 430, sawa na asilimia 18.5. Aidha, matukio hayo yalisababisha vifo 842 katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 ikilinganishwa na vifo 946 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Idadi ya vifo imepungua kwa watu 104, sawa na asilimia 11.

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** itakumbukwa kuwa mwishoni mwa miaka ya 1990 Serikali ilizuia mabasi ya abiria kusafiri nyakati za usiku. Zuio hilo lilitokana na ongezeko la utekaji wa magari uliohusisha uporaji na udhalilishaji wa abiria, ongezeko la ajali mbaya za mabasi zilizogharimu maisha ya watu na wengine kupata ulemavu wa maisha na uharibifu wa mali na miundombinu ya barabara. Aidha, maeneo mengi ambayo mabasi yalikuwa yanatekwa ni yale yaliyokuwa na barabara mbovu na yasiyokuwa na mawasiliano ya simu.

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** wote ni mashahidi kuwa changamoto za usalama na miundombinu zilizokuwepo wakati huo zimepungua kwa kiasi kikubwa au kuondolewa kabisa. Hii imetokana na Serikali kuendelea kuimarisha miundombinu ya barabara na mawasiliano ya simu. Aidha, juhudi za Jeshi la Polisi katika kupambana na

kudhibiti uhalifu zimesaidia kupunguza matukio makubwa ya ajali za barabarani.

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia mabadiliko hayo chanya na maoni ya wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, utayari wa wamiliki na madereva wa mabasi kuzingatia sheria na kanuni za usalama barabarani, utimamu wa Jeshi la Polisi na Vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama, Baraza la Usalama Barabarani limefanyia kazi suala la mabasi ya abiria kusafiri masaa 24 na kutoa mapendekezo yake. Serikali inayafanyia kazi mapendekezo hayo na itatoa uamuzi.

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kudhibiti ajali za barabarani katika mwaka 2023/24, Wizara kupitia Jeshi la Polisi litaangalia mfumo mzima wa utoaji wa leseni kwa kushirikiana na taasisi nyingine zinazohusika katika utoaji wa leseni, hususan za shule za udereva na zinazotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Hatua nyingine ni pamoja na kufanya uhakiki wa leseni za madereva nchini zikiwemo za mabasi na malori na kuwaelekeza kujisajili katika mfumo wa LATRA pamoja na kuhakikisha madereva wa mabasi ya abiria wana sifa za udereva kwa mujibu wa sheria.

**51.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Serikali itaharakisha taratibu za kuweka kamera za barabarani ambazo zitasaidia kubaini matukio ya uvunjifu wa sheria katika barabara kuu kwa maeneo ambayo hayana askari polisi. Pia, operesheni maalum zitafanyika usiku na mchana katika barabara kuu kwa lengo la kufuatilia nyendo za madereva wanaovunja sheria za usalama barabarani na kuchukua hatua stahiki. Aidha, Wizara itaendelea kuchukua hatua za kinidhamu kwa askari yoyote atakayejihusisha na vitendo vya ukiukwaji wa maadili na rushwa. Pia, Wizara itaendelea kutambua kazi zinazofanywa na askari waadilifu kama Koplo Hamisi R. Masana ambaye alikataa rushwa wakati akitekeleza majukumu yake.

**Operesheni za Kupambana na Uhalifu**

**52.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 Jeshi la Polisi limeendelea kutekeleza **Ibara Na.105 (a) ya Ilani ya CCM ya mwaka 2020 – 2025** inayoelekeza kuimarishwa kwa usalama wa raia na mali zao. Misako, doria na operesheni

zimefanyika kwa ajili ya kupambana na uhalifu wa aina zote. Matokeo ya operesheni hizo ni kukamatwa kwa risasi 442 na silaha 198 zikiwemo Mark IV mbili (2), AK 47 moja (1), G.3 mbili (2), Air Gun moja (1), Rifle sita (6), Shortgun (32), Bastola (18) na magobore (130). Jumla ya watuhumiwa 169 walikamatwa na kufikishwa mahakamani kwa makosa ya kupatikana na risasi pamoja na silaha kinyume cha Sheria na kesi zao zinaendelea. Aidha, wamiliki 20 waliopatikana na makosa ya matumizi mabaya ya silaha walifutiwa vibali na kunyang'anywa silaha.

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Jeshi la Polisi iliratibu kampeni za usalimishaji wa silaha haramu kwa hiari ikiwa ni utekelezaji wa Makubaliano ya Umoja wa Afrika ya Mwaka 2017 ambapo jumla ya silaha 1,220 zilisalimishwa. Kati ya silaha hizo, Bastola zilikuwa ni 18, Shotgun – 122, Rifle – 30, Magobore – 1,049 na AK 47 – 1. Aidha, Jeshi la Polisi liliteketeza jumla ya silaha 6,208 ambazo ni matokeo ya kampeni hiyo pamoja na operesheni za kupambana na uhalifu. Mchanganuo wa silaha zilizoteketezwa ni pamoja na: Bastola – 37, FN – 5, Shotgun – 259, Rifle – 209, Magobore – 5,562, AK 47 – 119, SAR – 11, G3 – 1, Uzigun – 2, Shegun – 1 na Sterling gun – 2. Katika kipindi husika Jeshi la Polisi limeweka alama ya utambuzi silaha 980 zikiwemo Bastola – 75, Shotgun – 10, Rifle – 8 na AK 47 – 557.

**54.** ***Mheshimiwa Spika***, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine za Serikali limefanya operesheni za kupambana na uhalifu wa Nyara za Serikali. Ushirikiano huo ulifanikisha kukamata Nyara za Serikali 2,201 zenye uzito wa kilo 17,211 na gramu 913 zikiwa na thamani ya Shilingi 9,551,632,436.75. Jumla ya watuhumiwa 917 walikamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.

**55.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza majukumu ya Jeshi, wapo askari wanaoumia na wengine kupoteza maisha. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 Jeshi la Polisi kupitia mfuko wake wa Tuzo na Tozo limelipa fidia ya Shilingi 1,200,335,400 kwa askari walioumia na kwa familia za askari waliopoteza maisha wakati wakitekeleza majukumu yao. Kati ya fedha hizo, Shilingi 948,335,400 zimelipwa kwa askari 217 walioumia na Shilingi 252,000,000 kwa wasimamizi wa mirathi kwa familia za askari 16 waliopoteza maisha. ***Mwenyezi Mungu azipumzishe roho za mashujaa wetu mahali pema peponi, Amina.***

## Uboreshaji wa Huduma ya Polisi Jamii

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Polisi linaboresha huduma zake kwa kuhakikisha kuwa askari polisi wanapatikana muda wote na kuwa karibu zaidi na wananchi. Ili kufanikisha azma hiyo, kuanzia mwezi Julai, 2022 Jeshi la Polisi limepeleka askari katika Kata 3,956 na Shehia 388. Hatua hiyo inalenga kuimarisha ushirikiano na mawasiliano kati ya askari polisi, Maafisa Watendaji wa Kata na wananchi katika masuala ya ulinzi na usalama na kupambana na uhalifu. Askari waliopo kwenye Kata na Shehia hushirikiana na Watendaji kuanzisha vikundi vya ulinzi shirikishi katika maeneo hayo. Hatua hii ni utekelezaji wa Ibara Na.104(c) na 105(f) za Ilani ya CCM ya mwaka 2020 – 2025. ***Naomba kutoa wito kwa Kamati za Usalama za Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji kuwatambua askari Kata na Shehia na kuwapa ushirikiano stahiki.***

**57.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza **Ibara Na. 105(e) ya Ilani ya CCM ya mwaka 2020 – 2025**, elimu ya uhamasishaji juu ya masuala ya Ulinzi, Uzalendo kwa Taifa na usalama wa nchi yetu imeendelea kutolewa kwa jamii. Elimu hiyo imetolewa kwa kutumia vyombo vya habari vilivyopo mikoani, mikutano ya hadhara, mashuleni na nyumba za ibada kupitia Maafisa wa Polisi Jamii, Wakaguzi na Askari waliopo kwenye Kata na Shehia. ***Naomba nitumie nafasi hii kuwapongeza Askari Kata na Askari Shehia ambao wanatekeleza majukumu yao kwa kujituma na ubunifu wa hali ya juu. Miongoni mwao ni Wakaguzi Wasaidizi wa Polisi ambao ni Dkt. M. Lwena, Khalfani A. Ussi, Daniel N. Mbebela, Msike F. Banda, Fransis S. Msuku ambao nimewatambulisha hapa Bungeni leo.***

## Dawati la Jinsia na Watoto

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** Dawati la Jinsia na Watoto ndani ya Jeshi la Polisi linashughulikia kesi na matukio ya ukatili wa kijinsia na watoto. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 jumla ya mashauri 14,184 ya matukio ya ukatili wa kijinsia na watoto yalitolewa taarifa katika vituo vya polisi ikilinganishwa na matukio 12,642 yaliyotokea kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Hii ni ongezeko la matukio 1,542 sawa na asilimia 12.2. Kati ya mashauri

hayo 4,120 yalipelekwa mahakamani 2,144 yalishinda na 988 yalishindwa.

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Jeshi la Polisi limezindua majengo matatu (3) ya ofisi za Dawati la Jinsia na Watoto katika Wilaya ya Simanjiro, Kiteto na Mbulu Mkoani Manyara yaliyojengwa kwa ufadhili wa (United Nations Population Fund – UNFPA. Ujenzi wa ofisi za madawati hayo ulifanyika kupitia Shirika lisilokuwa na Kiserikali la Children Dignity Forum kwa gharama ya Shilingi 275,000,000. Sambamba na uzinduzi wa ofisi hizo, elimu ya kuzuia na kupambana na ukatili wa kijinsia ilitolewa kwa jamii.

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa Ofisi ya Dawati la Jinsia na Watoto katika Kituo cha Polisi Bugarama Wilaya ya Msalala – Shinyanga umekamilika kwa gharama ya Shilingi 100,000,000 na kuzinduliwa rasmi tarehe 24 Mei, 2023. Ofisi hiyo imejengwa kwa ufadhili wa UNFPA kupitia shirika lisilo la kiserikali la KIWOHEDE. Aidha, ujenzi wa ofisi mbili (2) za Dawati la Jinsia na Watoto umeanza kwa ufadhili wa UN – WOMEN. Ofisi hizo zinajengwa katika Wilaya za Ikungi na Mkalama Mkoani Singida.

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** mapitio na uhuishaji wa mitaala ya Jeshi la Polisi ulifanyika kwa kuingiza somo linalojitegemea la *"Gender & Child Protection''*. Mitaala hiyo imepitishwa na NACTE kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa kada zote katika Vyuo vya Polisi. Mafunzo hayo yanahusu kushughulikia unyanyasaji wa kingono kwa watoto mitandaoni, ukatili na unyanyasaji wa kijinsia katika jamii ambayo yatatolewa wakati wa mafunzo ya awali, upandishwaji vyeo na mafunzo ya utayari.

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafunzo ya kushughulikia makosa ya ukatili wa kijinsia na unyanyasaji dhidi ya watoto yametolewa kwa watendaji wa Dawati na Viongozi wa Jeshi la Polisi 155. Viongozi hao ni Makamanda wa Polisi na Maafisa Upelelezi wa Wilaya na Mikoa ya Kigoma, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Dar es Salaam, Pwani na Tanga. Aidha, elimu ya kuzuia na kutoa taarifa juu ya masuala ya ukatili na unyanyasaji katika jamii imeendelea kutolewa katika Shule za Msingi na Sekondari, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu, Nyumba za Ibada, mikusanyiko ya watu na kupitia vipindi vinavyorushwa kwenye vyombo vya habari.

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Jeshi litaanzisha maabara maalum kwa ajili ya kushughulikia makosa ya kimtandao juu ya unyanyasaji wa watoto. Jumla ya Shilingi 361,930,000 zimepangwa kutumika kununua vifaa kwa ufadhili wa UNICEF. Aidha, mafunzo ya kushughulikia makosa ya ukatili wa kijinsia na unyanyasaji dhidi ya watoto yataendelea kutolewa kwa maafisa, wakaguzi na askari. Vilevile, elimu itaendelea kutolewa kwa jamii katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar kuhusu kuzuia na kutoa taarifa juu ya masuala ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia.

**Kushiriki katika Kuimarisha Ulinzi wa Amani Kikanda na Kimataifa**

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Jeshi la Polisi imeendelea kutekeleza kwa vitendo **Ibara Na.104 (g) ya Ilani ya CCM ya Mwaka 2020 – 2025**. Ibara hiyo inaelekeza kuwapeleka Askari kushiriki katika operesheni za Ulinzi wa Amani katika nchi mbalimbali kikanda na kimataifa ili kupata uzoefu na mbinu za kisasa za ulinzi wa amani. Katika kipindi husika, jumla ya Maafisa na Askari 23 wanaendelea kushiriki Ulinzi wa Amani katika nchi zifuatazo: Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo 14 – United Nations Organization Stabilization Mission in the Democratic Republic of Congo (MONUSCO), Sudan Kusini wanne (4) – United Nations Mission in South Sudan (UNMISS), Sudan Abyei wawili (2) – United Nations Interim Security Force for Abyei (UNISFA) na Sudan mmoja (1) – United Nations Integrated Transition Support Mission in Sudan (UNITAMS). Aidha, Maafisa wa Polisi wawili (2) wanafanya kazi kwa muda maalum (Secondment) kwenye Umoja wa Afrika (AU) mmoja (1) na UNISFA mmoja (1).

**65.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/24 Jeshi la Polisi litaendelea kuwapeleka maafisa na askari katika nchi, jumuiya za kimataifa na kikanda ili kuwawezesha kupata uzoefu zaidi. Aidha, ushirikiano utaendelea kuimarishwa katika nyanja mbalimbali kwa Jumuiya ambazo Jeshi la Polisi ni mwanachama zikiwemo: Jumuiya ya Wakuu wa Polisi Kanda ya Afrika Mashariki (Eastern Africa Regional Police Chiefs Cooperation – EARPCCO) na Jumuiya ya Wakuu wa Polisi Kanda ya Kusini mwa Afrika (Southern Africa Regional Police Chiefs Cooperation Organisation – SARPCCO). Ushirikiano huo utaongeza wigo wa kuzuia, kudhibiti na kupambana na makosa yanayovuka mipaka.

**Upatikanaji wa Vitendea Kazi kwa Jeshi la Polisi**

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili Jeshi la Polisi liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi linahitaji vitendea kazi vya kisasa na vya kutosha. Kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 Serikali imenunua magari sita (6) ya kusindikiza misafara ya Viongozi Wakuu wa Serikali na Viongozi Wakuu Waandamizi. Aidha, magari 150 yamepokelewa kati ya magari 369 yaliyotarajiwa kupokelewa ikiwa ni utekelezaji wa Mkataba kati ya Serikali na Kampuni ya Ashok Leyland ya nchini India. Magari yaliyopokelewa yamepelekwa katika Vituo vya Polisi vyenye uhitaji mkubwa. Magari 219 yaliyobaki yatapokelewa kabla ya Septemba, 2023.

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Jeshi la Polisi limepata msaada wa magari 13 na pikipiki 14 kutoka kwa wadau. Magari mawili (2) yametolewa na Wizara ya Fedha na Mipango na 11 yametolewa na Kamati za Usalama Barabarani katika Mikoa ya Dodoma (1), Lindi (1), Morogoro (1), mwanza (1), Njombe (1) na Mikoa ya Kipolisi ya Ilala (1), Kinondoni (1) na Temeke (4). Pikipiki zote 14 zimetolewa na Kamati ya Usalama Barabarani ya Mkoa wa Dar es Salaam na kugawanywa katika Mikoa ya Kipolisi ya Ilala (5), Kinondoni (4) na Temeke (5). ***Natumia nafasi hii kuwashukuru wadau wote waliohusika kulipatia Jeshi la Polisi vitendea kazi.***

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2022/23 Serikali ilitenga Shilingi 15,000,000,000 kwa ajili ya Jeshi la Polisi kununua magari 101 na pikipiki 336. Hadi kufikia mwezi Mei, 2023 Shilingi 7,500,000,000 zimepokelewa kwa ajili ya ununuzi wa magari 53 na pikipiki 56, ambapo taratibu za ununuzi zinaendelea. Katika kutekeleza maagizo ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, magari hayo yatasambazwa kwenye wilaya zote nchini na pikipiki zitasambazwa kwenye kata zote.

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Jeshi limepanga kununua magari 24 kwa gharama ya Shilingi 7,680,000,000. Kati ya magari hayo, nane (8) ni kwa ajili ya Makamishna na 16 ya Manaibu Kamishna wa Jeshi la Polisi. Pia, Shilingi 2,100,000,000 zitatumika kununua pikipiki 21 kwa ajili ya kuongoza misafara ya Viongozi Wakuu wa Serikali. Shilingi 4,500,000,000 zitatumika kununua boti 10 kwa ajili ya doria katika Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23 Serikali ilitenga jumla Shiingi 3,333,573,725 kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ili kuwezesha huduma za polisi katika ngazi ya wilaya, ambayo hupelekwa hadi katika ngazi ya kata. Serikali inaendelea kuongeza fedha hizo, ambapo katika mwaka 2023/24 jumla ya Shilingi 12,573,598,575 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya magari na pikipiki ili kuwezesha huduma za polisi katika ngazi ya wilaya. Aidha, jumla ya Shilingi 4,191,199,525 zimetengwa kwa ajili ya kutumika katika ngazi ya mikoa. Lengo la Serikali ni kuongeza huduma za polisi na kuwafikia wananchi kwa harala katika ngazi zote ikiwemo kata, vijiji na shehia.

**Miradi ya Jeshi la Polisi iliyokamilika**

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23 Jeshi la Polisi limetumia Shilingi 590,000,000 kukamilisha ujenzi wa majengo mawili (2) yaliyopo eneo la Mabatini – Mwanza. Majengo hayo yenye ghorofa tatu (3) yana uwezo wa kuishi familia 24 za askari. Aidha, Shilingi 200,000,000 zimetumika kukamilisha nyumba nne (4) za kuishi familia nane (8) za askari Kusini Pemba na Shilingi 150,000,000 zimetumika kukamilisha jengo moja (1) la kuishi familia nne (4) za askari Kaskazini Pemba.

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** miradi mingine iliyokamilika ni: Ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kusini Unguja kwa Shilingi 1,501,081,700; Ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa Shilingi 1,559,724,400; Ofisi ya Mkoa wa Kipolisi Tarime Rorya kwa gharama ya Shilingi 1,560,953,000; na kuunganisha mtandao katika jengo la ofisi ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai kwa gharama ya Shilingi 50,000,000. Aidha, ukarabati wa hanga la ndege katika Kikosi cha Polisi Anga – Dar es Salaam umefanyika kwa gharama ya Shilingi 220,000,000.

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shilingi 700,000,000 zimepokelewa kwa ajili ya umaliziaji wa ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja "A'' kilichopo Wilaya ya Ikungi. Shilingi 300,000,000 zimepokelewa kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja "A'' Wilaya ya Mkalama. Ujenzi wa vituo hivyo vilivyopo Mkoa wa Singida utakamilika mwezi Juni, 2023.

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** vituo vingine vitakavyokamilishwa katika kipindi hiki ni: Kituo cha Polisi Daraja "B'' Wilayani Namtumbo – Ruvuma kitakachogharimu Shilingi 400,000,000 na Makunduchi Zanzibar Shilingi 110,000,000; Kituo cha Polisi Daraja "C'' Dunga Mitini Kusini Unguja Shilingi 48,000,000 na Shilingi 40,000,000 zitatumika kukamilisha ujenzi wa ukumbi wa Chuo cha Polisi Zanzibar.

**75.** ***Mheshimiwa Spika***, miradi mingine imekamilishwa kwa ushirikiano kati ya Jeshi la Polisi na wananchi. Miradi hiyo ni ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja "C'' Kizimkazi – Kusini Unguja pamoja na nyumba ya makazi ya familia mbili (2) kwa gharama ya Shilingi 198,934,750, ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja 'C' Kirongwe Mkoa wa Kipolisi Tarime Rorya kwa Shilingi 120,368,758 na ujenzi wa Wodi ya Wazazi na chumba cha upasuaji katika Zahanati ya FFU Ukonga – Dar es Salaam uliogharimu Shilingi 131,378,330, na ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja C Galapo, Babati – Manyara kilichochangiwa kwa nguvu za wananchi na ujenzi wa Kituo cha Polisi Wilaya ya Bukoba.

**Miradi inayoendelea**

**Ujenzi wa Nyumba za Makazi, Ofisi na Vituo vya Polisi**

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** miradi inayoendelea ni: ujenzi wa Ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mara utakaogharimu Shilingi 1,448,675,000 ambao umefikia asilimia 95 na utakamilika kabla ya tarehe 30 Juni, 2023; ujenzi wa Ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi utakaogharimu Shilingi 1,494,919,400 umefikia asilimia 75; na Ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe utakaogharimu Shilingi 800,000,000 ambao umefikia asilimia 60. Miradi hii miwili (2) itakamilika mwezi Oktoba, 2023.

**77.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23 Serikali ilitenga fedha za bajeti ya maendeleo jumla ya Shilingi 32,500,000,000. Hadi kufikia mwezi Machi, 2023 Jeshi la Polisi limepokea fedha kwa ajili ya shughuli zifuatazo: Shilingi 5,580,132,700 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa maalum vya Jeshi ambapo mzabuni ameshapatikana; Shilingi 528,625,118 kwa ajili ya mradi wa kuimarisha na kuendeleza maabara tano (5) za uchunguzi wa sayansi ya jinai ambapo taratibu za manunuzi zinakamilishwa; Shilingi 7,500,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa magari 53 na pikipiki 56 na fedha hizo zimeshalipwa GPSA kwa ajili ya ununuzi wa magari na pikipiki; na Shilingi

3,281,129,000 ni kwa ajili ya kugharamia matengenezo ya Helkopta ambapo mzabuni anaendelea na matengenezo.

**78.** ***Mheshimiwa Spika***, taratibu za ununuzi zimekamilika kwa ajili ya kumpata mzabuni wa ununuzi wa vifaa vya TEHAMA na kuunganisha vituo ambavyo havijaunganishwa na Mkongo wa Taifa vya Kidatu, Makao Makuu ya Mkoa wa Kipolisi Rufiji na Vikosi vya Polisi vilivyoko Dar es Salaam. Fedha zilizopokelewa kwa kazi hizo ni Shilingi 178,950,000. Aidha, taratibu za ununuzi wa vifaa zinakamilishwa kwa ajili ya kuanzisha mifumo ya *Clearance Certificate Information System*, *Online Police Gazzette Information System* na *Tanzania Police Portal.* Kazi hizi zitagharimu Shilingi 160,000,000 na zitakamilika mwezi Juni, 2023.

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafunzo yamefanyika ya kuwajengea uwezo wakufunzi wa Vyuo vya Polisi na Wakaguzi wa Polisi ngazi ya Kata na Shehia. Mafunzo hayo yamefanyika kwa mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar, ambapo Shilingi 67,660,000 zimetumika. Shilingi 28,000,000 zimetumika kwa ajili ya kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo Maafisa Polisi wa Kitengo cha Habari wa Makao Makuu na waliopo katika ofisi za Makamanda wa Polisi wa Mikoa ili kuboresha utoaji wa taarifa za kazi za Polisi.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Machi, 2023 Jeshi la Polisi limepokea jumla ya Shilingi 402,000,000 kwa ajili ya ukarabati wa majengo yafuatayo: Kituo cha Polisi Malindi kilichopo Mji Mkongwe Mjini Magharibi Shilingi 126,887,750; jengo la Makao Makuu ya Polisi Zanzibar Shilingi 40,753,800; jengo la ofisi ya Kamanda wa Polisi Kaskazini Pemba Shilingi 50,000,000; nyumba za askari kambi ya Ziwani na Mwera Zanzibar Shilingi 165,000,000; na Bwalo la Askari Bububu Zanzibar Shilingi 19,358,450. Taratibu za ununuzi zinakamilishwa kwa ajili ya kuanza ukarabati.

**Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa kutoka Vyanzo Vingine**

**81.** ***Mheshimiwa Spika***, ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja "A'' Gezaulole Kigamboni – Dar es Salaam umekamilika na ulizinduliwa rasmi na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango (Mb.) tarehe 28 Aprili, 2023. Gharama zilizotumika kukamilisha mradi huu ni 'Shilingi 899,481,533. Aidha, ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja "A'' katika Mji wa Serikali Mtumba

– Dodoma kwa gharama ya Shilingi 948,384,951 umefikia asilimia 80. Fedha za mradi huo zinaratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Mfuko wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Jiji la Dodoma.

**82.** ***Mheshimiwa Spika***, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wananchi pamoja na wadau linaendelea na umaliziaji wa ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja C Mbande Mkoa wa Kipolisi Temeke. Mradi umefikia asilimia 80 ambapo Shilingi 120,368,758 zimetumika. Aidha, ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja "C'' Chang'ombe – Dodoma, umefikia asilimia 50 na hadi sasa Shilingi 50,000,000 zimetumika.

**Miradi ya Kipaumbele ya Jeshi la Polisi katika Mwaka 2023/24**

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imedhamiria kuendelea kuboresha utendaji wa Jeshi la Polisi kwa kuongeza kasi ya ujenzi wa makazi ya Askari, majengo ya ofisi, Vituo vya Polisi na ununuzi wa Vitendea kazi. Katika mwaka 2023/24 Serikali imetenga jumla ya Shilingi 27,193,239,000 kutekeleza miradi ya kipaumbele ifuatayo: kukamilisha ujenzi wa jengo la ghorofa tatu la kuishi familia 12 za Askari eneo la Buyekera – Kagera kwa gharama ya Shilingi 1,000,000,000; kumalizia ujenzi wa nyumba 3 za kuishi familia 6 za Askari eneo la Tunguu, Kusini Unguja – Zanzibar kwa gharama ya Shilingi 291,480,700; na kukamilisha ujenzi wa Ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara kwa Shilingi 1,383,849,000.

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** miradi mingine ni kumalizia ujenzi wa Vituo (2) vya Polisi Daraja "B'' vya Bariadi – Simiyu kwa Shilingi 220,000,000 na Mkuranga – Pwani kwa Shilingi 300,000,000; kumalizia ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja "C'' Igoma – Mbeya kwa Shilingi 100,000,000; ujenzi wa jengo la ghorofa la kuishi familia za Askari 12 kambi ya Polisi FFU Dodoma kwa Shilingi 302,249,004; *Rest House* ya Polisi Mkoa wa Arusha kwa Shilingi 139,000,000; jengo la Maktaba Chuo cha Polisi Zanzibar kwa Shilingi 178,803,839; jengo la wagonjwa wa nje (OPD) awamu ya pili katika Hospitali ya Polisi Kilwa Road – Dar es Salaam kwa Shilingi 528,000,000; na kukamilisha ujenzi wa ukuta wa nyumba za Makamishna awamu ya kwanza – Dodoma kwa Shilingi 344,213,080.

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** ukarabati wa makazi ya Askari, Vituo na Ofisi utafanyika kama ifuatavyo: majengo mawili (2) ya ghorofa moja (1) la kuishi askari familia sita (6) na nyumba mbili (2) za kuishi

familia za Askari 12 Makunduchi, Kusini Unguja – Zanzibar kwa gharama ya Shilingi 214,921,000; majengo matatu (3) yenye ghorofa moja (1) ya kuishi familia za Askari 12 Wete Kaskazini Pemba – Zanzibar kwa Shilingi 178,086,000; majengo 10 ya kuishi askari familia 40 kwa Shilingi 376,591,778; na jengo la ghorofa mbili (2) za kuishi familia za Askari 8 Kambi ya Polisi Ziwani, Mjini Magharibi – Zanzibar kwa gharama ya Shilingi 182,679,000.

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** ukarabati utafanyika katika maghorofa 90 ya kuishi familia za Askari 360 katika Kambi ya Polisi Kilwa Road – Dar es Salaam kwa Shilingi 126,457,320; Ofisi ya FFU Kambi ya Polisi Ziwani, Mjini Magharibi – Zanzibar kwa Shilingi 113,141,925; na Kituo cha Polisi Daraja B Malindi, Mjini Magharibi – Zanzibar kwa Shilingi 149,958,250.

**87.** ***Mheshimiwa Spika***, pia matengenezo ya magari 40 ya kuzuia ghasia yatafanyika kwa gharama ya Shilingi 432,880,000; minara 15 ya mawasiliano ya redio za masafa mafupi (VHF) itasimikwa katika mikoa tisa (9) kwa Shilingi 686,000,000. Mikoa hiyo ni Kagera (1), Kilimanjaro (2), Dar es Salaam (2), Dodoma (1), Mtwara (2), Mwanza (2), Mara (2), Mbeya (2) na Mjini Magharibi – Zanzibar (1). Kununua redio 150 za masafa mafupi na kuzifunga katika magari ya Polisi ya operesheni kwa gharama ya Shilingi 600,000,000; na kununua vifaa vya kijeshi kwa gharama ya Shilingi 3,865,910,256.

**88.** ***Mheshimiwa Spika***, kazi nyingine zitakazotekelezwa kwa mwaka 2023/24 ni kununua vifaa vya uchunguzi kwa ajili ya maabara ya Uchunguzi wa Sayansi ya Jinai kwa gharama ya Shilingi 442,183,839 pamoja na vifaa vingine vya kijeshi.

**Maboresho katika Mfuko wa Tuzo na Tozo**

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Tuzo na Tozo ulianzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 66(1) cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi, Sura ya 322. Kwa mujibu wa Kifungu cha 66(4) cha Sheria hiyo malengo ya Mfuko huo ni pamoja na: kutoa msaada kwa familia za askari waliofariki wakiwa wanatekeleza majukumu yao ya kazi; kutoa tuzo kwa matendo ya kishujaa kwa askari; ujenzi wa miundombinu ikiwemo makazi ya askari, ofisi na vituo vya Polisi; na kufanya maadhimisho ya matamasha ya michezo yanayoandaliwa na Jeshi la Polisi.

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliunda Timu ya Watalamu kwa ajili ya kufanya uchambuzi wa Mfuko wa Tuzo na Tozo uliopo chini ya Jeshi ya Polisi na kutoa mapendekezo. Timu hiyo iliundwa na wataalam kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Jeshi la Polisi na ilipewa Hadidu za Rejea zifuatazo: kufanya uchambuzi na maboresho ya Muundo wa Mfuko; kuangalia uwezekano wa Mfuko huo kutumika na Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi kama dhamana ya mikopo; matumizi ya mkopo kuwezesha utekelezaji wa miradi ya Jeshi la Polisi; kubainisha uendelevu (Sustainability) wa Mfuko na vihatarishi (risks) vya mapato; kuboresha huduma za ustawi wa askari; kubainisha maeneo yatakayo liwezesha Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi kutekeleza majukumu kwa ufanisi; na mapendekezo mengine yatakayosaidia kuimarisha utendaji wa Mfuko.

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** tathmini iliyofanyika kupitia Timu husika ilionesha kuwa chanzo kikuu cha mapato ya Mfuko huo ni huduma za ulinzi kwa taasisi za umma. Katika kipindi cha mwaka 2019/20 fedha zilizokusanywa kupitia Mfuko husika ni jumla ya Shilingi 8,908,416,947.40, katika mwaka 2020/21 zilikusanywa Shilingi 12,952,103,210 na mwaka 2021/22 Shilingi 10,845,672,146 zilikusanywa. Pamoja na masuala yaliyopendekezwa na Timu, Wizara imepanga kufanya mambo yafuatayo: kugawanya mapato ya mfuko na kulindwa (reinfenced) kwa mgawanyo wa asilimia 40 kwa matumizi ya ustawi wa askari na asilimia 60 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya Jeshi la Polisi.

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** mambo mengine yatakayotekelezwa na Wizara kupitia mapendekezo hayo ni: Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi litafute mkopo katika taasisi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya miundombinu na marejesho ya mkopo yafanyike kupitia fedha za Mfuko wa Tuzo na Tozo; na kuweka mikakati thabiti ya kulinda vyanzo vya mapato vya Mfuko.

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** maboresho hayo pia yanahusisha: mapitio ya Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi, Sura 322 ili kurekebisha Kifungu cha 66(3) na 66(4) cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi, Sura 322 kinachohusu uanzishwaji wa Mfuko wa Tuzo na Tozo; mapitio ya kurekebisha Amri ya Uanzishwaji wa Bodi ya Shirika la Polisi (The Police Force Corporation Sole Board (Establishment),

Order 2013) iliyotangazwa kupitia Gazeti la Serikali Na. 66 la tarehe 29 Machi, 2013; na kutunga Kanuni za Mfuko wa Tuzo na Tozo, ambapo Rasimu ya Kanuni hizo imeandaliwa.

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hilo, Wizara itafanya maboresho ya menejimenti na uendeshaji wa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi kwa ujumla. Lengo la maboresho hayo ni kuimarisha utendaji kazi wa Shirika la Uzalishaji Mali la Polisi na kuliwezesha Jeshi la Polisi kubaki na jukumu la msingi la ulinzi na usalama wa raia na mali zao. Aidha, maboresho hayo yatawezesha kuongeza kasi ya ujenzi wa miundombinu ya Jeshi la Polisi kipaumbele kikiwa ni kwenye ujenzi wa vituo vya polisi katika ngazi ya kata na shehia. ***Hivyo, natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kuwahamasha wananchi kuanza maandalizi ya kutafuta maeneo na kuanza hatua za awali za ujenzi na baada ya taratibu zote za kisheria kukamilika kipaumbele kitatolewa katika kata zilizoonesha mwamko wa wito huu.***

**Miradi inayotekelezwa kupitia Mfuko wa Tuzo na Tozo**

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Polisi limekamilisha miradi sita (6) kwa kutumia fedha za Mfuko wa Tuzo na Tozo ambayo ni: ujenzi wa nyumba tatu (3) za kuishi Makamishna wa Jeshi la Polisi – Dodoma uliogharimu Shilingi 1,050,000,000; ukarabati wa majengo saba (7) ya ghorofa ya kuishi familia 28 za Askari katika Kambi ya Ziwani – Zanzibar kwa gharama ya Shilingi 250,000,000; ukarabati wa Rest House ya Mkoa wa Shinyanga uliogharimu Shilingi 86,810,000; ujenzi wa Vituo viwili (2) vya Polisi Daraja "A'' Lushoto - Tanga kwa gharama ya Shilingi 417,040,450 na Wanging'ombe – Njombe kwa Shilingi 948,384,951; na ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja "B'' Ruangwa – Lindi uliogharimu Shilingi 768,024,626.

**96.** ***Mheshimiwa Spika,*** taratibu za ununuzi zinakamilishwa kwa ajili ya kazi zifuatazo: kuanza ujenzi wa kituo cha ufumbuzi wa dijitali ya intelijensia ya jinai Shilingi 122,500,000; na kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa malipo ya Mfuko wa Tuzo na Tozo Shilingi 63,300,000.

**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** miradi inayoendelea kutekelezwa kupitia Mfuko wa Tuzo na Tozo ni ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Kikosi cha Kutuliza Ghasia Madengi Hill – Dodoma kwa gharama ya Shilingi 391,873,963 umefikia asilimia 80 na ujenzi wa ghorofa mbili

(2) ikiwa ni awamu ya kwanza ya ujenzi wa jengo la ghorofa (4) la Polisi Afya Kuu – Dar es Salaam kwa gharama ya Shilingi 800,000,000 ambao umefikia asilimia 50.

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Mei, 2023 Jeshi la Polisi limepokea Shilingi 8,462,526,783 kupitia Mfuko wa Tuzo na Tozo kwa ajili ya miradi ya inayoendelea ya Jeshi la Polisi. Kati ya fedha zilizopokelewa, jumla ya Shilingi 3,410,741,000 zitatumika kwa ujenzi wa majengo ya Ofisi tano (5) za Makamanda wa Polisi wa Mikoa ya Geita Shilingi 800,000,000, Manyara Shilingi 800,000,000, Mtwara Shilingi 600,000,000; Njombe Shilingi 610,741,000 na Mkoa wa Kipolisi Rufiji Shilingi 600,000,000.

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Shilingi 2,050,000,000 zilizopokelewa zinaendeleza ujenzi wa vituo vitano (5) vya Polisi Daraja "B''. Vituo hivyo ni Kilolo – Iringa Shilingi 400,000,000, Kituo cha Mkoani – Kusini Pemba Shilingi 700,000,000, Butiama – Mara Shilingi 500,000,000, Chemba – Dodoma Shilingi 350,000,000 na Siha – Kilimanjaro Shilingi 100,000,000.

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Shilingi 524,167,899 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi unaoendelea wa vituo vinne (4) vya Polisi Daraja "C'' kwa mchanganuo ufuatao: Shilingi 115,809,000 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi Mapasa kilichopo Wilaya ya Nkasi – Rukwa; Shilingi 50,000,000 Kituo cha Polisi Songambele Wilaya ya Urambo – Tabora; Shilingi 80,000,000 Kito cha Polisi Nyakanazi – Kagera; na Shilingi 278,358,899 Kituo cha Polisi Tumbatu pamoja na nyumba tano (5) za kuishi familia 10 za Askari katika Mkoa wa Kaskazini – Unguja.

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Shilingi 2,564,210,205 zilipokelewa mwezi Aprili, 2023 ili kuanza utekelezaji wa miradi ifuatayo: ujenzi wa nyumba nyingine tatu (3) za Makamishna wa Polisi Jijini Dodoma, Shilingi 1,050,000.000; ujenzi wa nyumba ya kuishi Kamishna wa Polisi Zanzibar, Shilingi 350,000,000; ujenzi wa uzio wa nyumba tatu (3) za Makamishna wa Polisi zilizokamilika Jijini Dodoma Shilingi 344,213,080; ujenzi wa Bweni la kulala Askari Chuo cha Polisi Kidatu Shilingi 500,000,000; ujenzi wa nyumba ya makazi ya Askari familia mbili (2) Mtwara Shilingi 33,350,000; ukarabati wa Bwalo la Maafisa wa Polisi Mkoa wa Kagera Shilingi 93,647,125; na ukarabati wa jengo la Ofisi ya Makao Makuu Ndogo Dar es Salaam Shilingi

80,000,000. Aidha, Shilingi 113,000,000 zitatumika kumalizia ujenzi wa jengo la Zahanati ya Polisi Njombe.

**102. *Mheshimiwa Spika,*** miradi ambayo Serikali imepanga kuikamilisha kupitia Mfuko wa Tuzo na Tozo katika mwaka 2023/24 kwa jumla ya Shilingi 4,248,026,084 ni kama ifuatayo: ujenzi wa jengo la Kamanda wa Polisi Mtwara Shilingi 800,000,000; ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja B Namtumbo – Ruvuma Shilingi 398,000,000; ujenzi wa jengo la RPC Rufiji Shilingi 800,000,000; ujenzi wa bweni la wanafunzi Kidatu Shilingi 290,000,000; kujenga Kituo cha Polisi Daraja C Kitangari, Newala – Mtwara Shilingi 173,349,367; na ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja B Misungwi – Mwanza Shilingi 484,949,817.

**103. *Mheshimiwa Spika,*** miradi mingine itakayokamilishwa katika mwaka 2023/24 kupitia fedha za mfuko huo ni: ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja B Chang'ombe – Dodoma Shilingi 261,000,000; kukarabati Kituo cha Polisi Micheweni – Zanzibar Shilingi 65,000,000; ukarabati wa Makao Makuu ya Polisi Zanzibar Shilingi 25,726,900; ukarabati wa jengo la Maabara ya Uchunguzi wa Kisayansi – Dar es Salaam Shilingi 200,000,000; kukamilisha nyumba tano (5) za makazi ya familia 20 za Askari Polisi eneo la Mfikiwa – Kaskazini Pemba Shilingi 150,000,000; kukamilisha nyumba saba (7) za makazi ya familia 14 za Askari Polisi eneo la Finya – Kusini Pemba Shilingi 200,000,000; ukarabati wa Shule ya Polisi Moshi – Kilimanjaro Shilingi 200,000,000; na kuendelea na upimaji wa viwanja vya Jeshi la Polisi Shilingi 200,000,000.

**SHIRIKA LA UZALISHAJI MALI LA JESHI LA POLISI**

**104. *Mheshimiwa Spika,*** Shirika linaendelea na utekelezaji wa miradi ya kimkakati iliyopo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo:

**Mradi wa Usindikizaji Fedha (Cash In Transit)**

**105. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2022/23 utekelezaji wa mradi wa usindikizaji fedha umeanza kwa Benki ya NMB. Naipongeza Benki ya NMB kwa kushirikiana na Shirika hilo katika kazi hiyo. ***Nitumie fursa hii kuzihamasisha Taasisi nyingine za fedha na za umma, kampuni binafsi, vituo vya mafuta, Taasisi za***

***Dini na watu binafsi kutumia huduma za Shirika katika usafirishaji wa fedha kwa njia salama na ya uhakika***.

**Mradi wa Ukaguzi wa Vyombo vya Moto**

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23 Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi limekamilisha andiko la Mradi wa Ukaguzi wa Vyombo vya Moto. Mradi husika umepangwa kutekelezwa kwa ubia na sekta binafsi kuanzia mwaka 2023/24 na vituo vya ukaguzi 40 vitatumika katika mikoa yote vikiwemo vituo hamishika (Mobile Centers). Lengo ni kutumia teknolojia ya kisasa bila mwingiliano mkubwa wa kibinadamu katika kukagua vyombo vya moto. Mfumo huu utasaidia kupunguza udhaifu wa kibinadamu katika ukaguzi wa magari, hivyo vyombo vya moto vitakavyokidhi viwango vya ubora na usalama ndivyo vitaruhusiwa kuingia barabarani ili kutoa huduma ya usafiri na usafirishaji wa watu na mizigo.

**Mradi wa Miji Salama (Safer Cities)**

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23 Shirika limekamilisha andiko la Mradi wa Miji Salama utakaotumia kamera zenye mifumo ya utambuzi ya sura (Facial Recognition). Lengo ni kusaidia ulinzi wa maeneo mbalimbali kupunguza matukio ya uhalifu na kuongeza mapato ya Serikali. Katika awamu ya kwanza kamera hizo zitafungwa Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Dodoma kwenye barabara, maduka, majengo na mitaa ili kubaini, kudhibiti na kukabiliana na matishio na mianya ya uhalifu. Aidha, Serikali ipo katika hatua za kukamilisha majadiliano na Serikali ya Falme za Kiarabu kwa ajili ya upatikanaji wa mkopo wa Dola za Marekani milioni 105 za kutekeleza mradi huo. ***Naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa msukumo wake katika upatikanaji wa nyenzo na vifaa vya kisasa vya kubaini, kushughulikia na kuzuia uhalifu nchini.***

**Mafunzo ya Umahiri wa Matumizi ya Silaha za Moto**

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 Shirika limetoa mafunzo ya umahiri kwa wamiliki 7,250 wa silaha za moto. Ili kuhakikisha wamiliki wa silaha za moto wanapata

mafunzo hayo, kuanzia mwaka 2023/24 watatakiwa kuwasilisha hati ya umahiri kama sharti la kuhuisha vibali vya umiliki wa silaha. Vilevile, Makampuni ya Ulinzi yatatakiwa kuwasilisha hati za umahiri za askari wao wakati wa kuhuisha vibali vya usajili wa kampuni na umiliki wa silaha. ***Natoa rai kwa wamiliki wote wa silaha za moto kuendelea kujitokeza katika Ofisi za Makamanda wa Polisi wa Mikoa ili kupata mafunzo stahiki.***

**Mradi wa Dar City na Bwalo la Maafisa wa Polisi Dar es Salaam – Oysterbay**

**109.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inatafuta njia sahihi ya kuendeleza miradi hiyo kwa njia ya ubia. Shirika linashirikiana na Mshauri Elekezi ambaye ni Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) katika hatua za kutafuta mbia wa kuwekeza kwenye eneo la Bwalo la Maafisa wa Polisi lililopo eneo la Oysterbay, Dar es Salaam.

**JESHI LA MAGEREZA**
**Hali ya Ulinzi na Usalama Magerezani**

**110.** ***Mheshimiwa Spika***, Jeshi la Magereza lina wajibu wa kuwapokea, kuwahifadhi na kuwapatia huduma muhimu wahalifu wanaopelekwa magerezani kwa mujibu wa Sheria. Hadi kufikia mwezi Mei, 2023 jumla ya wahalifu 30,901 walikuwepo katika magereza yote nchini ambapo wafungwa ni 18,857 na mahabusu ni 12,044. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 3.3 zaidi ya uwezo wa magereza wa kuwahifadhi wafungwa na mahabusu 29,902. Katika kipindi hicho, hali ya ulinzi na usalama kwa magereza yote nchini ni salama na tulivu.

**Kupunguza Msongamano Magerezani**

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya msongamano magerezani imeendelea kudhibitiwa kwa kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo utekelezaji wa adhabu mbadala kama vile Mpango wa Parole, kifungo cha nje na huduma kwa jamii. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 jumla ya wafungwa 780 walitolewa magerezani kupitia utaratibu wa Kifungo cha Nje (Extra Mural Labour – EML). Pia, Jeshi la Magereza limeendelea kudhibiti msongamano katika magereza yaliyopo katika miji mikuu kwa kuhamisha wafungwa na mahabusu 2,027 kwenda katika magereza yenye nafasi.

**112.** ***Mheshimiwa Spika,*** tunamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa msamaha uliowanufaisha wafungwa 1,637 waliokuwepo magerezani. Mhe. Rais alitoa msamaha huo katika siku ya Maadhimisho ya Sherehe za miaka 61 ya Uhuru wa Tanzania Bara zilizofanyika tarehe 9 Desemba, 2022 na Sherehe za Maadhimisho ya miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar tarehe 26 Aprili, 2023.

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** hatua hizi zimewezesha kupungua kwa idadi ya wafungwa magerezani kutoka 32,671 katika kipindi cha mwezi Julai, 2021 hadi Mei, 2022 na kufikia wafungwa 30,901 katika kipindi kinachoishia Mei, 2023. Hivyo, kuwezesha kupungua kwa msongamano wa wafungwa kutoka asilimia 9.2 hadi 6.2 ikilinganishwa na uwezo wa kuhifadhi wafungwa 29,902.

**Kuimarisha Ulinzi na Usalama Magerezani**

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** ulinzi na usalama magerezani unaendelea kuimarishwa kwa kutumia vifaa vya usalama vya kielektroniki. Mwezi Septemba, 2022 vifaa hivyo vimefungwa katika Gereza Butimba – Mwanza. Aidha, Shilingi 1,598,640,738.66 zimepokelewa kwa ajili ya ununuzi na usimikaji wa vifaa vya kielektroniki katika Magereza ya Ruanda – Mbeya, Maweni – Tanga, Uyui – Tabora, Karanga – Kilimanjaro na Gereza Arusha. Pia, mkataba wa ununuzi wa vifaa vya upekuzi vyenye thamani ya Shilingi 990,950,000 umesainiwa mwezi Machi, 2023.

**115.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Magereza litaendelea kuimarisha ulinzi magerezani kwa kutumia vifaa vya usalama vya kielektroniki. Katika mwaka 2023/24 Shilingi 600,000,000 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya usalama vya kielektroniki na usimikaji wa mifumo ya ulinzi na usalama katika Gereza Lilungu – Mtwara, Gereza Lindi na Gereza Bukoba – Kagera. Utumiaji wa vifaa na mifumo ya usalama ya kielektroniki utendelea kufanyika katika magereza mengine kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha.

**Huduma za Urekebu**

**116.** ***Mheshimiwa Spika,*** huduma ya urekebu inatolewa kwa wafungwa wote waliopo magerezani kwa kuwapatia stadi za kazi, huduma za kiroho, ushauri wa kisaikolojia na michezo. Elimu ya ufundi stadi hutolewa kupitia Vyuo vya Ufundi vya Magereza vilivyosajiliwa na Serikali. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023, jumla ya wafungwa 196 walipatiwa mafunzo ya ufundi stadi katika Chuo cha Ufundi Ruanda – Mbeya na Wami Vijana – Morogoro. Kati ya hao, 128 wamehitimu na 68 wanaendelea na mafunzo. Wafungwa 3,000 wanaendelea kupatiwa stadi za kazi kupitia shughuli za viwanda vya magereza.

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 huduma za urekebu zitaendelea kuimarishwa katika magereza yote nchini. Programu maalumu zitatolewa kupitia mashamba darasa katika magereza ya Isanga na Msalato – Dodoma, Wami Kuu na Wami Vijana – Morogoro na Ukonga – Dar es Salaam. Aidha, mafunzo ya ufundi stadi yatatolewa kwa wafungwa 230 kupitia Vyuo vya Magereza. Mafunzo hayo yanalenga kuwajengea uwezo wafungwa katika eneo la uzalishaji na ujasiriamali ili wamalizapo kutumikia vifungo vyao waweze kujitegemea kiuchumi.

**118.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Magereza litafanya maboresho katika mitaala ya mafunzo ya urekebu kuanzia mafunzo ya awali hadi mafunzo ya uongozi kwa ngazi zote. Lengo ni kuimarisha shughuli za urekebu na usalama magerezani. Shilingi 300,000,000 zimetengwa kwa ajili ya kuboresha mitaala hiyo na Shilingi 67,000,000 zitatumika kuandaa mpango wa mafunzo wa Jeshi la Magereza.

**Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Magereza**

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** miundombinu ya magereza inaendelea kukarabatiwa na kujenga majengo mapya. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Jeshi la Magereza limefanya ukarabati wa mabweni ya wafungwa katika Gereza la Wanawake Kingolwira na Gereza Mbigiri – Morogoro, Gereza Shinyanga, Gereza Kongwa – Dodoma, Gereza la Wanawake Ruvuma, Gereza Lindi na Gereza Lilungu – Mtwara. Ukarabati mwingine umefanyika kwa kujenga

ukuta wa ngome katika Gereza Ileje – Songwe, Idete na Mbigiri – Morogoro na Kalilankulukulu – Katavi.

**120.** ***Mheshimiwa Spika,*** uboreshaji wa majengo ya ofisi umefanyika katika Gereza Mng'aro na Korogwe – Tanga, Gereza Babati – Manyara, Kongwa – Dodoma, Mkuza – Pwani na Gereza Shinyanga. Hii ni hatua ya kuboresha mazingira ya kufanyia kazi katika vituo vya magereza.

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Aprili, 2023 Shilingi 2,033,270,000 zimepokelewa kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa magereza katika Wilaya ya Karatu – Arusha, Msalato – Dodoma na Kilosa – Morogoro. Fedha hizo pia zitatumika kuanza ujenzi wa magereza matatu (3) katika Wilaya ya Gairo – Morogoro, Kakonko – Kigoma na Kaliua – Tabora. Hatua hii ina lengo la kuwa na majengo yatakayozingatia utoaji wa huduma bora na kuwa na mahali salama pa kuhifadhi wafungwa na mahabusu.

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Shilingi 2,769,600,000 zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Magereza ya Gairo na Kilosa – Morogoro, Kakonko – Kigoma, Kaliua – Tabora, Karatu – Arusha na Msalato na Isanga – Dodoma, Igunga – Tabora, Kwa Mturuki (Bagamoyo) – Pwani pamoja na kuanza ujenzi wa magereza mapya ya Kiabakari – Mara, Mpimbwe – Katavi, Sengerema – Mwanza, Kyerwa – Kagera, Kingurungundwa – Lindi na Mlolo – Iringa. Shilingi 800,000,000 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Ofisi za Magereza katika Mikoa mitano (5) ya Geita, Kigoma, Lindi, Songwe na Tanga. Jeshi litaendelea kujenga miundombinu ya magereza na majengo ya ofisi kwa kuzingatia mahitaji na upatikanaji wa fedha.

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Shilingi 285,000,000 zimetengwa kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa maji safi na salama katika magereza matano (5). Magereza hayo ni Ilagala – Kigoma, Mbarali – Mbeya, Kiteto – Manyara, Kingurungundwa – Lindi na Kongwa – Dodoma.

**Vitendea Kazi kwa Jeshi la Magereza**

**124.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kulipatia Jeshi la Magereza vitendea kazi

ikiwemo magari ya utawala na usafirishaji wa mahabusu. Hadi kufikia tarehe 22 Mei, 2023 jumla ya Shilingi 4,459,410,727.35 zimelipwa kwa mtoa huduma kwa ajili ya ununuzi wa magari 23, kati ya hayo 18 ni ya utawala na matano (5) ya mahabusu. Aidha, katika mwaka 2023/24 Jeshi la Magereza limetenga Shilingi 6,691,416,000 kwa ajili ya ununuzi wa magari 28 yatakayotumika kwa shughuli za utawala na 14 kwa utekelezaji wa jukumu la usafirishaji wa mahabusu.

**Uboreshaji wa Makazi ya Watumishi**

**125.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Magereza linaendelea kuboresha makazi ya watumishi kwa njia ya ubunifu ikiwemo kutumia nguvu kazi ya wafungwa. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 nyumba 34 za makazi kwa ajili ya watumishi zinaendelea kujengwa katika vituo mbalimbali nchini. Nyumba hizo zitakapokamilika zitakuwa na uwezo wa kuhudumia familia 68 za askari. Matumizi ya nguvu kazi ya wafungwa yameanza kuokoa fedha kwa kiasi cha Shilingi 484,500,000.

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Shilingi 225,000,000 zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa nyumba tano (5) za maafisa na askari wa Kikosi Maalum cha Kutuliza Ghasia Magerezani zilizopo Msalato – Dodoma. Nyumba hizo zitakuwa na uwezo wa kuishi familia 10 za maafisa na askari.

**Huduma za Afya Magerezani**

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** maboresho ya huduma za afya magerezani yanahusisha ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023, Jeshi limefanya ukarabati wa jengo la Zahanati ya Gereza Mollo – Rukwa ili kuwezesha utoaji wa huduma bora za afya. Ukarabati huo umegharimu Shilingi 62,000,000. Vilevile, Shilingi 600,000,000 zimetolewa na Serikali mwezi Aprili, 2023 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa jengo la mama na mtoto, jengo la OPD, maabara na *power house* katika Hospitali ya Makao Makuu iliyopo Msalato – Dodoma. Taratibu za ununuzi zinakamilishwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa majengo hayo. Katika mwaka 2023/24 Shilingi 500,000,000 zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa hospitali hiyo.

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Magereza kwa kushirikiana na Shirika lisilokuwa la Serikali la Tanzania Health Promotion Support (THPS) limesambaza vifaa vya kutunzia takwimu za afya katika vituo 36 vya Magereza. Shirika hilo pia limetoa mafunzo kwa watumishi 29 wa huduma za afya magerezani. Aidha, lishe ya wafungwa na mahabusu imeendelea kuboreshwa na magonjwa ya milipuko yanadhibitiwa kupitia uzingatiaji miongozo ya kinga na tiba inayotolewa na Wizara ya Afya.

**Kuboresha Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo katika Mashamba ya Magereza**

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Magereza linaendeleza ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji katika Mradi wa Umwagiliaji Idete – Morogoro. Mradi huo unamilikiwa na Shirika la Magereza ili kuwezesha umwagiliaji katika shamba la hekta 1,000. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 Shilingi 785,265,600 zimepokelewa na kwa sasa ununuzi wa vifaa unaendelea ili kuanza ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika shamba hilo.

**130.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, Jeshi limefanya upembuzi yakinifu wa awali (Pre – Feasibility Study) kwa ajili ya kuboresha uzalishaji wa mazao kwa njia ya umwagiliaji katika magereza matatu (3) ya Ushora – Singida (Zao la alizeti), Kitete Nkasi – Rukwa (maharage) na Kalilankulunkulu – Katavi (Mpunga). Matokeo ya Upembuzi huo yameonesha kuwa kilimo cha umwagiliaji kinaweza kufanyika kwa kutumia mabwawa na maji ya mito ya msimu katika maeneo husika. Katika mwaka 2023/24 ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji utafanyika katika magereza hayo pamoja na magereza ya Ilagala – Kigoma na Kilindi – Tanga.

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika msimu wa mwaka 2022/23 Jeshi limelima jumla ya ekari 7,687 za mazao. Kati ya hizo, ekari 3,920 za mahindi, 1,340.5 za mpunga, 1,936 za alizeti na 490.5 za maharage. Matarajio ni kuvuna tani 3,279.42 za mahindi, 1,108.35 za Mpunga, 805 za alizeti na 192 za maharage. Mavuno hayo yatasaidia kujitosheleza kwa chakula cha wafungwa kama ifuatavyo: mahindi – asilimia 48.06, mpunga – asilimia 86.59, alizeti – asilimia 76.67 na maharage – asilimia 14.66.

**132.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa uzalishaji wa mbegu bora za mazao, jumla ya ekari 300 zimelimwa kama ifuatavyo: mahindi ekari 100 na alizeti ekari 100 – Gereza Wami Kuu – Morogoro, ufuta ekari 50 – Gereza Nachingwea – Lindi na maharage ekari 50 – Gereza Ilagala - Kigoma. Mavuno yanayotarajiwa ni tani 72 za mahindi, 30 za alizeti, 17.5 za ufuta na 25 za maharage. Mavuno ya mbegu hizo yamesaidia kuokoa Shilingi 667,500,000 ambazo zingetumika katika ununuzi wa mbegu.

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Jeshi la Magereza limeweka lengo la kulima mazao katika jumla ya ekari 15,000. Kati ya hizo, ekari 5,245 zitalimwa mahindi, 1,434 mpunga, 2,533 alizeti, 790 maharage na 4,998 mazao mengine. Mavuno yanayotarajiwa ni tani 4,420 za mahindi, 1,186 za Mpunga, 975 za alizeti na 245 za maharage. Aidha, Jeshi litazalisha mbegu bora za mazao katika jumla ya ekari 500 ambapo mahindi ni ekari 200, Mpunga ekari 50, alizeti ekari 100, maharage ekari 100 na ufuta ekari 50. Matarajio ni kuvuna jumla ya tani 268.9 ambapo mahindi ni tani 144, Mpunga tani 27.4, alizeti tani 30, maharage tani 50 na ufuta tani 17.5.

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuunga mkono juhudi za Serikali za kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula nchini, Jeshi la Magereza limeendelea kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Mazao ya Kilimo (TARI Kihinga) katika uzalishaji wa zao la chikichi Gereza Kwitanga – Kigoma. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023, Jeshi limehudumia jumla ya ekari 1,908 zilizopandwa zao la chikichi.

**135.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi husika jumla ya miche 85,053 ya mbegu bora za michikichi imezalishwa. Kati ya miche hiyo, 25,015 imesambazwa kwa wananchi na wadau, 51,688 ipo kwenye vitalu na itasambazwa kwenye mashamba ya magereza ikiwemo Gereza Lilungu – Mtwara, Gereza Ruangwa – Lindi, Kambi Mvuti – Dar es Salaam, Gereza Kibiti na Kigongoni – Pwani na Gereza Kalilankulukulu – Katavi na 8,350 imepandwa katika ekari 167. Katika mwaka 2023/24, Shilingi 4,760,000,000 zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza Kilimo katika mashamba ya magereza pamoja na ununuzi wa mitambo na zana za kilimo.

**Matumizi ya Nishati Safi na Utunzaji wa Mazingira**

**136.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Magereza limeanza kutekeleza agizo la Mhe. Rais la kutumia nishati safi ya kupikia chakula cha wafungwa badala ya kutumia kuni. Kwa sasa gesi (LPG) inatumika katika Gereza Keko na Chuo cha Taaluma ya Urekebishaji Tanzania – Dar es Salaam. Katika mwaka 2022/23 mifumo ya gesi asilia imeanza kufungwa katika Gereza Ukonga – Dar es Salaam kwa ajili ya kupikia chakula cha wafungwa.

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Jeshi limetenga Shilingi 1,000,000,000 kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa agizo hilo katika Magereza 19 ambayo ni Arusha, Karanga – Kilimanjaro, Maweni – Tanga, Isanga, King'ang'a na Msalato – Dodoma, Uyui – Tabora, Butimba – Mwanza, Lilungu – Mtwara, Ruanda – Mbeya, Ukonga, Segerea, Keko, Wazo Hill na Kambi Kimbiji – Dar es Salaam, Lindi, Mbigiri – Morogoro, Ubena – Pwani na Ngara – Kagera. Pamoja na kutumia nishati safi kupikia katika magereza yetu, napenda kutumia nafasi hii kulielekeza Jeshi la Magereza kuendeleza kwa kasi upandaji wa miti kama njia ya kuhifadhi mazingira na kudhibiti mabadiliko ya tabia nchi.

**Kuboresha Uzalishaji wa Samani katika Kiwanda cha Msalato**

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Magereza limeendelea kufanya urekebishaji wa wafungwa na kutoa huduma bora kwa jamii kupitia uzalishaji wa bidhaa katika viwanda vya magereza. Katika mwaka 2023/24, Shilingi 500,000,000 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa malighafi ili kuanza uzalishaji wa bidhaa za samani kwenye Kiwanda cha Samani Msalato – Dodoma. Hatua hii itawezesha kuongeza huduma za urekebu, mapato ya Serikali na upatikanaji wa bidhaa bora za samani kwa matumizi ya ofisi na majumbani. ***Naomba kutoa wito kwa wananchi, taasisi binafsi na za umma kununua bidhaa za samani kutoka Kiwanda cha Samani Msalato.***

**Kuimarisha Masuala ya Jinsia Magerezani**

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Magereza linazingatia ujumuishaji wa masuala ya kijinsia katika utekelezaji wa majukumu yake. Shughuli zilizofanyika katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 ni: kuwapatia maafisa, askari na watumishi raia 170 elimu kuhusu

ujumuishaji wa masuala ya kijinsia; kuanzisha madawati ya jinsia na watoto katika vituo vyote vya magereza; na kuandaa na kusambaza Mwongozo wa kushughulikia ukatili wa kijinsia na watoto magerezani kwenye mikoa yote. Shughuli hizo zitaendelea kutekelezwa katika mwaka 2023/24 ikiwa ni pamoja na kuandaa Mpango Mkakati wa Masuala ya Jinsia na Watoto wa Jeshi la Magereza wa mwaka 2023/24 – 2027/28. Jumla ya Shilingi 71,940,000 zimetengwa kwa ajili ya shughuli hizo.

**HUDUMA ZA UANGALIZI WA WAFUNGWA WA VIFUNGO VYA NJE**

**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inaendelea kusimamia huduma za uangalizi wa wafungwa wa vifungo vya nje. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2022 hadi Mei, 2023 jumla ya Taarifa za Uchunguzi wa Kijamii 4,808 ziliwasilishwa Mahakamani. Taarifa hizo zimewezesha Mahakama kutoa maamuzi ya kuwaweka wafungwa chini ya Amri ya Huduma kwa Jamii na Amri ya Uangalizi. Kupitia Taarifa hizo jumla ya wafungwa 3,719 walihukumiwa kutumikia adhabu zao kwenye jamii, kati ya hao wanaume 3,008 na wanawake 711. Wafungwa 3,762 walimaliza kutumikia vifungo vyao na kurudishwa kwenye jamii kuungana na familia zao. Kati ya hao Wanaume 3,018 na Wanawake 744.

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na wafungwa hao kutekeleza adhabu zao nje ya Magereza, Serikali imeweza kuokoa Shilingi 5,764,450,000 ambazo zingetumika kuwalisha kama wangeendelea kukaa magerezani. Gharama hizo ni za kumlisha mfungwa mmoja kwa wastani wa Shilingi 5,000 kwa siku.

**142.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeweza kuokoa jumla ya Shilingi 3,049,580,000 ambazo zingetumika kuwalipa vibarua kwa kufanya kazi kwenye Taasisi za Umma baada ya kazi hizo kufanywa na wafungwa wa vifungo vya nje. Hii ikiwa ni wastani wa malipo ya Shilingi 4,000 kwa kibarua kwa masaa manne kwa siku. Hatua hii ni utekelezaji wa Ibara Na. 120(J) ya Ilani ya CCM ya mwaka 2020 – 2025 inayohimiza uzingatiaji wa matumizi ya adhabu mbadala ili kupunguza mlundikano wa mahabusu na wafungwa magerezani na kupunguza gharama za uendeshaji wa kesi mahakamani.

**143.** ***Mheshimiwa Spika,*** programu za urekebishaji wa tabia kwa wafungwa waliowekwa chini ya Amri ya Huduma kwa Jamii na Amri ya Uangalizi zilifanyika kwa kuzingatia mahitaji ya kila mfungwa. Wafungwa 382 walifundishwa stadi za kazi na maisha, 20 wameunganishwa na Mfuko wa TASAF, 552 walipewa ushauri wa kisaikolojia na kufundishwa maadili ya jamii, 167 walifundishwa ujasiriamali ili kupata kazi mbadala, wawili (2) walipelekwa kwenye vituo vya afya kupata huduma za ARV na kifua kikuu, 62 waliokuwa wanatumia dawa za kulevya walipewa ushauri nasaha na matibabu na 2,263 walipewa ushauri nasaha kuwasaidia kuishi maisha yasiyotegemea uhalifu.

**144.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na wafungwa hao kushiriki katika programu za urekebishaji, pia walifanya kazi za usafi wa mazingira kwenye Taasisi za Umma, upandaji na utunzaji wa miti, utunzaji wa bustani, kushiriki shughuli za ujenzi wa majengo ya Serikali, mfano ujenzi wa Kituo cha Afya Uvinza mkoani Kigoma, kuboresha miundombinu katika Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma na jengo la Mkuu wa Magereza (RPO) mkoani Songwe.

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilitoa elimu ya uhamasishaji kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Huduma kwa Jamii, Sura ya 291 na Sheria ya Uangalizi wa Wafungwa, Sura ya 247 kwa wadau wa Haki Jinai. Elimu hiyo ilitolewa katika Mikoa ya Dodoma, Kigoma, Iringa, Morogoro na Tanga. Vilevile, elimu ilitolewa kwa jamii kupitia vyombo vya habari vikiwemo redio, runinga, mitandao ya kijamii na magazeti.

**146.** ***Mheshimiwa Spika,*** elimu pia ilitolewa katika shule za msingi na sekondari, vyuo vya elimu ya kati na juu na kwa wafungwa na mahabusu waliopo magerezani. Zoezi hilo la uelimishaji lilitolewa katika Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara kupitia ushiriki wa Wizara katika Maadhimisho ya wiki ya Sheria.

**147.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) iliendesha semina ya mafunzo mkoani Kigoma kuhusu utekelezaji wa Amri za Huduma kwa Jamii na Uangalizi wa wafungwa.

**148.** ***Mheshimiwa Spika,*** semina hiyo ilitolewa kwa wadau wa Haki Jinai na maafisa wa Idara ya Wakimbizi ili kuwezesha wakimbizi

waliopo katika makambi wenye makosa ya jinai na kukidhi vigezo kutumikia vifungo vya nje ya gereza. Hadi kufikia tarehe 10 Mei, 2023 wakimbizi 19 wamewekwa chini ya programu ya Huduma kwa Jamii na kuamriwa kufanya kazi za utunzaji wa mazingira bila malipo katika makambi yao.

**149.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Idara ya Huduma za Uangalizi itawasimamia na kuwafuatilia wafungwa 5,500 wanaolengwa kuwekwa chini ya Amri za Huduma kwa Jamii na Uangalizi. Ili kufikia azma hii kazi zitakazofanyika ni: kutoa elimu ya utekelezaji wa Sheria ya Huduma kwa jamii na Uangalizi wa wafungwa kwa wadau wa Haki Jinai na walio nje ya mfumo wa Haki Jinai; kufanya Uchunguzi wa Kijamii; kutekeleza Programu za Urekebishaji wa tabia za wafungwa; kukagua taasisi za Serikali zinazotoa kazi kwa wafungwa ili kubaini kama zimetimiza vigezo vya kupewa wafungwa; na kusimamia na kufuatilia wafungwa wanaotekeleza adhabu kwenye mikoa na wilaya ili kuhakikisha amri zilizotolewa na Mahakama dhidi yao zinatekelezwa ipasavyo.

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zitakazofanyika ni: kutoa elimu ya utangamano wa wafungwa kwa taasisi za Haki Jinai, mashirika ya kijamii na dini; kutoa huduma za utangamano (Re-intergration) kwa wafungwa wanaoachiwa baada ya kumaliza kutumikia adhabu zao; na kuanzisha kanzidata ya wafungwa wa vifungo vya nje (Non-Custodial Offenders' Database Information System). Katika kutekeleza na kufanikisha kazi hizo, Shilingi 1,900,339,000 zimetengwa katika mwaka 2023/24.

**SHIRIKA LA MAGEREZA (SHIMA)**

**151.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imefanya mabadiliko ya Kanuni za Shirika la Magereza ili kuhakikisha linajiendesha kibiashara. Aidha, uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi Inspekta Jenerali wa Polisi Mstaafu Said Ally Mwema, Bodi mpya ya Wakurugenzi na Afisa Mtendaji Mkuu Bw. Moremi Marwa umefanyika. Bodi ilizinduliwa rasmi tarehe 01 Novemba, 2022. Kufanyika kwa mabadiliko haya kunachochea ufanisi katika utendaji wa Shirika na kuwezesha kufikia malengo ya uanzishwaji wake.

**152.** ***Mheshimiwa Spika,*** mabadiliko hayo yamewezesha kupatikana na mafanikio kwa Shirika ikiwemo: kuandaliwa kwa Mpango wa Biashara (Business Plan) wa miaka mitatu 2023/24 – 2025/26. Mpango huo unatoa dira ya ukuaji wa biashara ya SHIMA kwa kuzingatia utatuzi wa changamoto za kiutendaji kwa miradi inayohusu shughuli za msingi za shirika; kufanya marekebisho ya miongozo ya uendeshaji wa miradi; na kuboresha matumizi ya rasilimali zilizopo ili zilete tija.

**153.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine ni kuboreshwa kwa utunzaji wa kumbukumbu za hesabu na matumizi ya mifumo ya teknolojia katika makusanyo ya mapato, ambapo katika kipindi cha Novemba, 2022 hadi Machi, 2023 mizania ya hesabu, mali na mtaji wa Shirika imeongezeka kutoka Shilingi 29,000,000,000 hadi kufikia Shilingi 49,440,000,000 sawa na ongezeko la takriban Shilingi 20,000,000,000. Hii inawezesha Shirika kuongeza mtaji na kuwezesha ushirikiano wa kibiashara na sekta ya kifedha na sekta binafsi.

**154.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Shirika limeandaa sera mahsusi kwa ajili ya kusimamia masuala ya Uwekezaji, Utawala bora, Udhibiti wa vihatarishi na Usimamizi wa miradi. Sera hizo zitasaidia kuongoza Shirika kwenye masuala ya uwekezaji na usimamiaji bora wa rasilimali zilizopo kwa manufaa ya Jeshi la Magereza na Taifa kwa ujumla.

**155.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha shughuli za kilimo msimu wa mwaka 2022/23, Shirika limeongeza ufanisi katika kilimo kwa kutumia mbegu bora za mazao ya kilimo, kuzingatia upandaji na utumiaji wa viuatilifu kwa wakati, kuimarisha huduma za ugani na usimamizi na ufuatiliaji wa mashamba. Jumla ya ekari 5,385 zimelimwa, ambapo ekari 3,925 zimelimwa mahindi, 865 mpunga,197 maharage, 230 alizeti na 89 miwa. Matarajio ni kuvuna tani 5,298 za mahindi, 973 mpunga, 99 maharage, 138 alizeti na 2,670 miwa.

**156.** ***Mheshimiwa Spika,*** mavuno hayo yatasaidia kuongeza chakula cha wafungwa kinachozalishwa na Shirika kutoka wastani wa tani 2,900 za mahindi na tani 973 za mpunga mwaka 2022/23 hadi kufikia tani 4,800 za mahindi na tani 1,486 za mpunga mwaka 2023/24. Pia, itasaidia Serikali kupunguza gharama zinazotumika kununua chakula kwa wazabuni wa nje kupitia Jeshi la Magereza.

Mpango wa Shirika ni kuwezesha kufikia zaidi ya asilimia 70 ya kujitosheleza kwa chakula cha wafungwa kwa mazao ya mahindi, mpunga na maharage ifikapo mwaka 2025.

**157.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 miundombinu ya umwagiliaji katika Gereza Idete kwenda mashambani itaendelea kujengwa. Shughuli nyingine zilizopangwa kufanyika ni uchimbaji wa visima vinne (4) ambapo, kimoja kitachimbwa Gereza Arusha na vitatu (3) Gereza Mang'ola – Manyara na ukarabati wa mifereji ya umwagiliaji ili kupunguza upotevu wa maji. Hatua hii itapunguza utegemezi wa mvua kwenye kilimo. Ili kutekeleza kazi hizo Shilingi 100,000,000 zimetengwa kwa ajili ya uchimbaji wa visima hivyo na ukarabati wa miundombinu husika. Aidha, Shilingi 100,000,000 zimetengwa ili kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha kusindika mazao ya kilimo kilichopo Kitai – Ruvuma.

**158.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika bajeti ya mwaka 2023/24 jumla ya Shilingi 700,000,000 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa matrekta matano (5) na vitendea kazi vingine. Vitendea kazi hivyo vitasaidia Shirika kuongeza matumizi bora ya ardhi katika kilimo kwa mazao mbalimbali kutoka wastani wa ekari 5,385 zilizolimwa mwaka 2022/23 hadi kufikia ekari 7,250 mwaka 2023/24. Ukubwa wa maeneo ya kilimo utaendelea kuongezwa kulingana na upatikanaji wa vitendea kazi vya kisasa pamoja na fedha.

**159.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limepanga kufanya maboresho ya viwanda vya samani na ushonaji Ukonga na Kiwanda cha samani Uyui. Maboresho hayo yatafanyika kwa kufanya matengenezo na ununuzi wa mashine mpya. Lengo ni kuongeza ufanisi wa shughuli zinazotekelezwa kwenye viwanda hivyo katika utengenezaji wa bidhaa. Ili kufanikisha shughuli hizo, kiasi cha Shilingi 165,000,000 kimepangwa kutumika katika mwaka 2023/24.

**Kampuni Tanzu ya SHIMA Guard Security Company**

**160.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika kupitia kampuni yake tanzu ya SHIMA Guard Security Company Limited imeendelea kutoa huduma za ulinzi wa watu na mali kwa taasisi za umma na binafsi. Hadi kufikia mwezi Mei, 2023 jumla ya malindo 40 yamepatikana, ambapo vijana wa kitanzania zaidi ya 650 wamepatiwa mafunzo na kuajiriwa, ambapo wamepangiwa kazi katika maeneo

mbalimbali. Kuanzishwa kwa Kampuni hii kumewezesha SHIMA kupata mapato ya wastani wa Shilingi 2,600,000,000 kwa kipindi cha kuanzia Novemba, 2022 hadi Mei, 2023. Katika mwaka 2023/24 SHIMA itaendelea kutoa huduma za ulinzi na hivyo kuchangia katika mapato ya Shirika na kutoa ajira kwa Watanzania.

**161.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba ***nitoe rai kwa Taasisi za Serikali, mashirika ya umma na binafsi pamoja na watu binafsi kutumia huduma za ulinzi kupitia kampuni hii ya kizalendo kwa gharama nafuu.*** Kampuni ya SHIMA Guard Co. Ltd itaendelea kutoa huduma bora na zenye viwango stahili sehemu zote itakazoaminiwa na kupewa nafasi kwani huduma za kampuni hii zinapatikana nchini kote.

**Maendeleo katika Kampuni zilizoingia Ubia na SHIMA**

**162.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika ushirikishwaji wa Sekta Binafsi, Shirika linaendelea na ubia na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii nchini ya NSSF na PSSSF. Katika ubia na NSSF Shirika chini ya Kampuni ya Ubia ya Mkulazi Holding Company Limited, usimikaji wa mitambo kwa ajili ya uzalishaji wa sukari unaendelea. Matarajio ni kuanza kuzalisha sukari mwaka 2023/24. Aidha, kiwanda hicho kitakuwa na uwezo wa kuzalisha metriki tani 50,000 za sukari kwa mwaka.

**163.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ubia kati ya SHIMA na PSSSF unaendelea kwenye Kiwanda cha Kuzalisha Bidhaa za Ngozi chini ya Kampuni ya Ubia ya Kilimanjaro International Leather Industries Company Limited. Shughuli za ujenzi wa mifumo ya majitaka na ujenzi wa uzio zinaendelea. Kwa sasa kiwanda kinaendelea kuzalisha bidhaa za ngozi kama vile viatu, mabegi, mikanda.

**164.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia maelekezo ya Serikali, ubora wa bidhaa zinazozalishwa na Kampuni ya Kilimanjaro International Leather Industries Company Limited umeimarishwa na bei zimepunguzwa ili kuweza kukidhi mahitaji ya watumiaji ikiwemo viatu vinavyohitajika katika majeshi yetu. Aidha, naendelea kuwahamasisha Watanzania kununua bidhaa zinazozalishwa na Kampuni hiyo kwa kuwa viwanda hivi vinarahisisha upatikanaji kwa bidhaa hizo ndani ya nchi. Pia, niwaombe Wafanyabiashara watumie fursa ya uwepo wa viwanda hivi katika kuongeza

mnyororo wa thamani kwa kuwa mawakala na kurahisisha kusambaza bidhaa hizo nchini kote.

**JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI**

**165. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limezima moto na kufanya uokoaji katika matukio 2,405. Baadhi ya matukio hayo ni: moto wa Mlima Kilimanjaro karibu na Kambi ya Karanga; ajali ya basi la abiria Kampuni ya Frester na lori Kampuni ya Texas iliyotokea Kijiji cha Silwa, Kata ya Pandambili Wilaya ya Kongwa – Dodoma; ajali ya gari iliyohusisha basi dogo la abiria (Toyota Coaster) na lori dogo (Mitsubish Fuso) iliyotokea katika eneo la Magira Wilaya ya Korogwe – Tanga; uokoaji kwenye shughuli za uchimbaji wa madini katika Kijiji cha Ipalamasa Mkoani – Geita; na ajali ya gari la shule iliyotokea eneo la Mjimwema Kata ya Mikindani – Mtwara.

**166. *Mheshimiwa Spika,*** matukio hayo yote yalisababisha vifo vya watu 64 na uharibifu wa nyumba 15 za watalii na kuteketea kwa kilomita za mraba 34.2 za uoto wa asili. Katika matukio hayo, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama na wadau wengine wameweza kuokoa majeruhi 71 na kilometa za mraba 719.33 za uoto wa asili wa Mlima Kilimanjaro.

**167. *Mheshimiwa Spika,*** ukaguzi wa kinga na tahadhari ya moto umefanyika kwenye maeneo 64,838 ikilinganishwa na lengo la mwaka 2022/23 la kukagua maeneo 64,167 ikiwa ni ongezeko la maeneo 671, sawa na asilimia 1.5. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 jumla ya Shilingi 9,458,104,532.46 zilikusanywa kutokana na ukaguzi huo ikilinganishwa na Shilingi 7,381,000,000 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Vilevile, ramani za majengo 1,361 zimesomwa na kupitishwa baada ya kujiridhisha kuwa zimezingatia vigezo vya kinga na tahadhari ya moto na majanga mengine.

**168. *Mheshimiwa Spika,*** Mfumo wa Usimamizi wa Ukaguzi wa Kinga na Tahadhari ya Moto umeboreshwa ili kuwezesha wananchi kufanya maombi ya Ukaguzi wa Kinga na Tahadhari ya Moto. Mfumo huo una faida zifuatazo: kuongeza mapato yasiyo ya kodi; kuongeza ufanisi kwa kupunguza muda wa kuwatambua na

kuwahudumia wateja na wananchi; na kuongeza uwazi katika ukaguzi wa kinga na tahadhari ya moto kwa kupata makadirio ya tozo katika hatua za awali bila kuhusika kwa Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Mfumo huu unapatikana kwa kupitia https://portal.zimamoto.go.tz. Kwa sasa mfumo upo katika majaribio kwenye Mikoa ya Dodoma na Pwani.

**169.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na madhara makubwa yanayosababishwa na majanga ya moto, Serikali imedhamiria kuongeza vitendea kazi vya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Katika mwaka 2022/23 ununuzi wa boti mbili (2) za uokoaji na magari matatu (3) ya kuzima moto umekamilika. Boti moja (1) inafanya kazi katika Mkoa wa Dar es Salaam na nyingine Mkoa wa Mwanza. Aidha, magari mawili (2) yapo Mkoa wa Dar es Salaam na moja lipo Mkoa wa Dodoma. Katika mwaka 2023/24 Jeshi limetenga Shilingi 3,000,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa magari mengine matano (5) ya kuzima moto.

**170.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imepata mkopo wa masharti nafuu wa Euro milioni 4.9, sawa na takribani Shilingi 12,798,831,884 kutoka Serikali ya Austria kwa ajili ya ununuzi wa magari 12 ya kuzima moto ikiwemo magari mawili (2) ya ngazi yenye uwezo wa kuzima moto kwenye majengo yenye zaidi ya ghorofa 20. Magari hayo yanatarajiwa kupokelewa nchini mwezi Desemba, 2023.

**171.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada nyingine, Serikali inakamilisha taratibu zitakazowezesha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kupata vitendea kazi vya kisasa kwa mkopo wa Dola za Marekani 100,000,000 sawa na takribani Shilingi 232,610,000,000. Mkopo huo wa masharti nafuu unatarajiwa kutolewa na Abu Dhabi Export Credit Agency (ADEX) kutoka Serikali ya Falme za Kiarabu (UAE). Mkopo husika ukipatikana utalifanya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kupata kwa mara ya kwanza fedha nyingi za maendeleo kwa ajili ya kugharamia ununuzi wa vifaa na vitendea kazi vya kisasa katika kukabiliana na majanga mbalimbali katika mikoa yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa sasa Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango ipo katika hatua za juu za majadiliano na Serikali ya Falme za Kiarabu (UAE) kupitia ADEX kuhusu upatikanaji wa mkopo huo. ***Kwa mara nyingine tena nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa azma ya kutaka kuweka uwekezaji***

***mkubwa wa kihistoria katika Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ambao haujawahi kutokea tangu dunia hii ilipoumbwa.***

**172.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23 Serikali imetenga Shilingi 1,960,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa magari 15 ya utawala na shughuli za ukaguzi wa kinga na tahadhari dhidi ya moto. Hadi kufikia mwezi Mei, 2023 Shilingi 1,887,217,000 zimepokelewa kwa ajili ya ununuzi wa magari hayo na malipo yamefanyika kwa mtoa huduma. Katika mwaka 2023/24 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limetenga Shilingi 1,960,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa magari 12 ya utawala na ukaguzi.

**Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

**173.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ujenzi wa Kituo Kikuu cha Zimamoto na Uokoaji TAZARA – Dar es Salaam umekamilika na ulizinduliwa rasmi na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango tarehe 28 Aprili, 2023. Miradi mingine iliyokamilika ni ujenzi wa Vituo vya Zimamoto na Uokoaji Nzuguni na Chamwino - Dodoma. Miradi hiyo ilizinduliwa rasmi na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) tarehe 26 Aprili, 2023. Aidha, ukarabati wa Kituo cha Zimamoto na Uokoaji Ilala - Dar es Salaam unaendelea na umefikia asilimia 74.

**174.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Mei, 2023 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limepokea Shilingi 6,405,009,800 za bajeti ya maendeleo ya mwaka 2022/23. Fedha hizo zinaendelea kutumika katika: kukamilisha majengo sita (6) ya makazi ya askari eneo la Kikombo - Dodoma Shilingi 3,038,634,800; ujenzi wa vituo vitatu (3) katika Mikoa ya Songwe, Simiyu na Manyara Shilingi 2,300,000,000; na ukarabati wa Kituo cha Zimamoto na Uokoaji katika Mkoa wa Ruvuma Shilingi 110,000,000; na ujenzi wa vyumba maalum vinne (4) katika Mikoa ya Arusha, Dodoma, Tanga na Kituo cha Zimamoto na Uokoaji Ilala Shilingi 212,000,000.

**175.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha usalama katika miradi ya kitaifa ya kimkakati, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaendelea kufuatilia uzingatiaji wa ushauri wa kiusalama katika hatua za utekelezaji. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa Uwanja wa Ndege

Msalato – Dodoma, Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere, Reli ya Kiwango cha Kimataifa (*Standard Gauge Railway – SGR)* na Mradi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima – Uganda hadi Tanga – Tanzania. Ushauri huo ni pamoja na ufungaji wa mifumo ya kisasa ya kung'amua na kuzima moto na ujenzi wa vituo vidogo vya zimamoto na uokoaji katika miradi hiyo.

**Miradi iliyopangwa kutekelezwa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa Mwaka 2023/24**

**176.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika bajeti ya maendeleo ya mwaka 2023/24 Jeshi litafanya yafuatayo: ununuzi wa vifaa vya zimamoto na uokoaji Shilingi 500,000,000; ujenzi wa majengo mawili (2) ya ghorofa Kikombo – Dodoma Shilingi 2,500,000,000; ukarabati wa nyumba 10 za makazi ya askari katika Mikoa ya Arusha, Iringa na Morogoro Shilingi 400,000,000; na uendelezaji wa ujenzi wa Chuo cha Zimamoto na Uokoaji Chogo – Tanga Shilingi 1,100,000,000.

**177.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shilingi 2,010,000,000 zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa vituo vinne (4) vya zimamoto na uokoaji katika Mikoa ya Kagera, Katavi, Geita na Njombe na Shilingi 300,000,000 zitatumika kujenga vyumba vitano (5) vya kuhifadhi vifaa vya usalama katika Mikoa ya Kilimanjaro, Rukwa, Mtwara, Kigoma na Shinyanga.

**178.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kushirikiana na Mamlaka za Maji za Mikoa linaendelea na zoezi la kubaini vituo vya maji ya kuzima moto (*fire hydrants)* zote zinazohitaji matengenezo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2023 jumla ya *fire hydrants* 702 zimekaguliwa katika mikoa 11 kati ya hizo 315 zinahitaji matengenezo. Aidha, matengenezo ya *fire hydrants* hizo yatafanyika kwa awamu kuanzia mwaka 2023/24 kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika mwaka 2023/24 Shilingi 120,000,000 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya *fire hydrants* 98 katika Mikoa ya Dodoma, Ilala, Iringa, Kagera, Katavi, Kilimanjaro, Morogoro, Mtwara, Njombe, Pwani na Songwe.

**Elimu kwa Umma kuhusu Kinga na Tahadhari dhidi ya Majanga ya Moto**

**179.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaendelea kutoa elimu ya kinga na tahadhari dhidi ya moto na majanga

mengine ili kuzuia na kupunguza madhara yanayotokana na majanga hayo. Hadi kufikia mwezi Mei, 2023 elimu kwa umma imetolewa kupitia vyombo vya habari ikiwemo vipindi vya runinga 107 na vipindi vya redio 420. Elimu hiyo pia imekuwa ikitolewa katika maeneo yenye mkusanyiko mkubwa wa watu ikiwemo masoko, shule, vivuko, vituo vya mabasi, nyumba za ibada na taasisi mbalimbali.

**180.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kudhibiti matukio ya moto kwenye shule, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limefungua klabu 55 za zimamoto katika shule za msingi 35 na shule za sekondari 20 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Geita, Iringa, Katavi, Kinondoni, Morogoro, Njombe, Pwani, Shinyanga na Tanga. Klabu hizo zina jumla ya wanachama 3,941 na hivyo kufanya jumla ya klabu hizo kufikia 705 na wanachama 54,909 nchi nzima. Vilevile, Skauti 769 waliopo mashuleni wamepewa elimu ya kinga, tahadhari ya moto na majanga mengine.

**181.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/24 elimu kwa umma itaendelea kutolewa kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Aidha, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji litaanzisha vikundi vya Zimamoto na Uokoaji Jamii kwa lengo la kuimarisha utoaji wa elimu na ushiriki wa jamii katika uokoaji wakati wa majanga ikiwemo moto, mafuriko, ajali za barabarani na dharura zote zisizo za jinai. Shilingi 285,560,000 zimetengwa kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma.

## IDARA YA UHAMIAJI

### Udhibiti wa Uingiaji na Utokaji wa Wageni na Raia Nchini

**182.** ***Mheshimiwa Spika,*** Idara ya Uhamiaji inatekeleza majukumu yake ya msingi ya utoaji wa huduma za kiuhamiaji kwa wageni na raia. Majukumu hayo hutekelezwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za nchi ili kulinda Usalama wa Taifa na kukuza maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2022 hadi Mei, 2023 jumla ya wageni 1,412,404 waliingia nchini ikilinganishwa na wageni 1,129,844 waliongia katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Aidha, jumla ya wageni 1,292,962 walitoka nchini ikilinganishwa na wageni 955,453 waliotoka mwaka 2021/22.

**183.** ***Mheshimiwa Spika,*** ongezeko la wageni walioingia na kutoka nchini linatokana na sera ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuwavutia wageni kutembelea Tanzania kwa shughuli za uwekezaji, utalii, biashara na shughuli za kijamii. ***Nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake za kuvutia wageni kuingia nchini kwa shughuli za kiuchumi na kijamii kupitia filamu yake ya Royal Tour.***

**184.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na Wizara kupitia Idara ya Uhamiaji kuwezesha uingiaji na utokaji wa watu, hatua zimechukuliwa kwa waliokiuka sheria. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2022 hadi Mei, 2023 jumla ya wageni 390 walizuiliwa kuingia nchini kwa kutokidhi vigezo vya kiuhamiaji. Pia, Watanzania 797 waliokwenda nje ya nchi kinyume cha sheria walirudishwa nchini. Katika mwaka 2023/24 Idara ya Uhamiaji itaendelea kusimamia uingiaji na utokaji wa wageni kwa mujibu wa sheria na kutoa elimu stahiki kwa Watanzania na wageni wenye nia ya kutoka nje au kuingia nchini.

**Vibali vya Ukaazi kwa Wageni**

**185.** ***Mheshimiwa Spika***, vibali vya ukaazi kwa wageni wanaoingia, kuishi na kufanya kazi hapa nchini vinaendelea kutolewa. Kwa kipindi cha mwezi Julai, 2022 hadi Mei, 2023, jumla ya vibali vya ukaazi 15,211 (Daraja A – 2,295; Daraja B – 9,361; na Daraja C – 3,555) vilitolewa ikilinganishwa na vibali 17,910 (Daraja A – 2,202; Daraja B – 12,402; na Daraja C – 3,306) vilivyotolewa kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Vibali vya Daraja A hutolewa kwa wawekezaji wakubwa, Daraja B hutolewa kwa wageni walioajiriwa katika kampuni mbalimbali hapa nchini na Daraja C walioajiriwa katika mashirika (NGOs), kujitolea na wanafunzi wanaokuja kusoma hapa nchini.

**186.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Hati za Mfuasi 4,327 na Hati za Msamaha 590 zilitolewa ikilinganishwa na Hati za Mfuasi 3,035 na Hati za Msamaha 905 zilizotolewa katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Aidha, visa 864,968 zilitolewa kwa wageni walioomba kuingia nchini kwa shughuli mbalimbali ikilinganishwa na viza 386,728 kwa kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Katika mwaka 2023/24 Idara ya Uhamiaji itaendelea kutoa vibali vya ukaazi na

Hati nyingine za kuingia nchini kwa wageni watakaokidhi vigezo vya kiuhamiaji.

***Pasipoti na Hati Nyingine za Safari***

**187.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwezi Julai, 2022 hadi Mei, 2023 jumla ya Pasipoti 107,751 zimetolewa kwa Watanzania ikilinganishwa na Pasipoti 73,557 zilizotolewa katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Kati ya hizo, Pasipoti 492 zilikuwa za Kibalozi, 173 za Kiutumishi na 107,086 za Kawaida. Aidha, Hati za Safari za Dharura 289,628 zimetolewa ikilinganishwa na Hati 260,540 zilizotolewa kwa kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Kwa mwaka 2023/24, Idara ya Uhamiaji itaendelea kutoa Pasipoti na hati nyingine za safari kwa Raia wa Tanzania ili kuwawezesha kusafiri nje ya nchi kulingana na mahitaji yao.

**Operesheni, Misako, Doria na Ukaguzi**

**188.** ***Mheshimiwa Spika***, operesheni, misako, doria na ukaguzi zimefanyika ili kuwadhibiti wageni wanaoingia nchini kinyume cha sheria. Hadi kufikia mwezi Mei, 2023 jumla ya watuhumiwa 22,882 wa makosa ya kiuhamiaji walikamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.

**189.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na changamoto ya wahamiaji haramu, hususan kutoka nchi ya Ethiopia, Serikali imefanya mapitio ya Kanuni za Uhamiaji za mwaka 2016 eneo la Visa kwenye Jedwali Na. 4 la nchi zinazohitaji Viza Rejea. ***Napenda kulitaarifu Bunge lako kuwa nchi ya Ethiopia imeondolewa kwenye Jedwali Na. 4 la Orodha ya nchi zinazopata Viza Rejea kupitia Gazeti la Serikali la tarehe 27 Januari, 2023 (GN 37/2023).***

**190.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa sasa raia wa nchi ya Ethiopia wanaruhusiwa kuingia nchini kwa sharti la kuwa na Pasipoti ya Taifa lao na visa ya kuendelea na safari nje ya Tanzania. Hatua hii imesaidia kupata ufumbuzi wa changamoto ya muda mrefu ya wahamiaji haramu kutoka nchi hiyo.

**191.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/24 Wizara itaendelea kudhibiti wahamiaji haramu kwa kuhakikisha watu wote wanaoingia nchini wanazingatia sheria. Aidha, elimu itaendelea

kutolewa kuhusu Sheria za Uhamiaji pamoja na kuanzisha kauli mbiu isemayo **"Mjue Jirani Yako"**. Lengo ni kuwashirikisha wananchi katika kuwabaini wahamiaji haramu na kuwapa elimu juu ya madhara ya kuwahifadhi wageni wasiostahili.

***Wageni Waliopewa Uraia wa Tanzania***

**192.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia mwezi Mei, 2023 jumla ya wageni 204 walipewa uraia wa Tanzania ikilinganishwa na wageni 112 ambao walipewa uraia katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Wageni hao ni kutoka mataifa yafuatayo: Afrika Kusini (3), Cameroon (1), China (2), Cuba (1), DRC (11), India (75), Japan (1), Kenya (12), Lebanon (10), Lithuania (2), Oman (1), Pakistani (22), Palestina (1), Rwanda (4), Sierra Leone (1), Somalia (4), Ugiriki (2), Uingereza (2), Uswizi (2), Yemeni (43), Zambia (2) na Zimbabwe (2).

***Watanzania Waliopatiwa Uraia wa Mataifa Mengine***

**193.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi mwezi Mei, 2023 Watanzania 66 waliukana uraia wa Tanzania na kupewa uraia wa mataifa mengine yafuatayo: Canada (6), China (1), Hispania (2), India (3), Marekani (11), Namibia (1), Newzealand (2), Oman (12), Ubelgiji (1), Uingereza (2), Ujerumani (23), Uganda (1) na Umoja wa Falme za Kiarabu (1). Hivyo, kwa mujibu wa Sheria ya Uraia Sura ya 357 Rejeo la 2002, wote walioukana Uraia wa Tanzania wanapoteza haki ya kuendelea kuwa Watanzania. Katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22 Watanzania 40 waliukana Uraia wa Tanzania.

**Uboreshaji wa Vitendea Kazi katika Idara ya Uhamiaji**

**194.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Mei, 2023 jumla ya Shilingi 4,894,840,900 zimepokelewa kwa ajili ya ununuzi wa magari 29 na malipo yameshafanyika. Magari hayo yatatumika katika operesheni, misako, doria, ukaguzi pamoja na shughuli za utawala. Katika mwaka 2023/24 Shilingi 3,894,981,000 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa magari mengine 23.

**195.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia ushirikiano na wadau, Shirika la Uhamiaji Duniani (IOM), limewezesha kujenga na kukamilisha Ofisi nne (4) za Uhamiaji. Ofisi hizo zimejengwa katika Wilaya za Masasi, Nanyumbu, Newala na Tandahimba. Shirika hilo pia, limewezesha

ukarabati wa Kituo cha Uhamiaji kilichopo Kilambo – Mtwara. Miradi hiyo imegharimu jumla ya Shilingi 988,215,316.26 ikiwa ni fedha za nje.

**196.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwezi Julai, 2022 hadi Mei, 2023 Idara ya Uhamiaji imekamilisha miradi ya Ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji Mikoa ya Geita, Lindi na Manyara. Miradi hiyo imegharimu jumla ya Shilingi 3,555,149,361.13 kati ya fedha hizo, Shilingi 1,545,084,378.78 zimetumika kukamilisha jengo la Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Geita, Shilingi 1,243,509,542.73 jengo la Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Lindi na Shilingi 766,555,439.62 kukamilisha jengo la Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Manyara. Aidha, mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mtwara unaendelea na umefikia asilimia 75.

**197.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Idara ya Uhamiaji itaanza ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Songwe, Ofisi ya Wilaya ya Mufindi – Iringa na Kituo cha Uhamiaji Kirongwe – Mara. Vilevile, nyumba 12 zitajengwa kwa ajili ya Makazi ya Wakufunzi katika Chuo cha Raphael Kubaga – Tanga. Aidha, ukarabati utafanyika katika nyumba 12 za watumishi mkoani Tabora na ofisi za Uhamiaji za Wilaya za Kahama – Shinyanga na Ifakara – Morogoro. Jumla ya Shilingi 4,345,544,000 zimetengwa katika mwaka 2023/24 kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo.

## TUME YA UTUMISHI YA JESHI LA POLISI, MAGEREZA, JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI NA UHAMIAJI

**198.** ***Mheshimiwa Spika,*** **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Jeshi la Polisi, Magereza, Zimamoto na Uokoaji na Uhamiaji imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Jeshi la Polisi, Magereza, Zimamoto na Uokoaji na Uhamiaji Sura 241. Tume hii imetambuliwa rasmi katika Muundo wa Wizara uliohuishwa na kuidhinishwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 29 Januari, 2022 ambapo imepewa Mamlaka ya kuajiri, kusitisha, kupandisha cheo, kuthibitisha kazini na kushughulikia masuala ya nidhamu kwa Askari mwenye cheo kuanzia Mkaguzi Msaidizi hadi Kamishna Msaidizi. Aidha, pamoja na majukumu mengine Tume imepewa jukumu la Kumshauri Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutekeleza mamlaka yake ya Ibara ya 36 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**199. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Mei, 2023 Tume iliwapandisha vyeo Maafisa, Wakaguzi na Askari 9,722. Vilevile, katika kipindi hicho Tume ilipokea na kutolea maamuzi mashauri ya kinidhamu na rufaa 131 ambapo Maafisa na Wakaguzi 33 walifukuzwa kazi, watatu (3) waliachishwa kazi, sita (6) walirudishwa kazini, 33 walishushwa cheo na 56 walipewa adhabu ya onyo.

**200. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2023/24 Tume imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo: kuwapandisha vyeo Maafisa, Wakaguzi na Askari wenye sifa na vigezo vilivyoainishwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Miongozo ya Vyombo husika; kupokea na kushughulikia mashauri ya nidhamu na rufaa za Maafisa na Wakaguzi kutoka Vyombo vya Usalama vilivyo chini ya Wizara; kuimarisha uwezo wa Tume kutekeleza majukumu yake kwa kuongeza rasilimaliwatu na kuwajengea uwezo kwa kuwapatia mafunzo; na kununua vitendea kazi muhimu kama samani na magari. Jumla ya Shilingi 802,806,800 zimetengwa katika bajeti ya mwaka 2023/24 ili kutekeleza majukumu hayo.

**MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA (NIDA)**
**Hali ya Usajili na Utambuzi wa Watu Nchini**

**201.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi ya usajili na utambuzi wa watu inaendelea. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2022 hadi Mei, 2023, wananchi 774,594 walisajiliwa kati ya hao 733,238 walisajiliwa Tanzania Bara na 41,356 Zanzibar. Hivyo kufanya idadi ya wananchi waliosajiliwa tangu kuanza kwa usajili wa watu nchini mwaka 2012 kufikia 23,960,323. Miongoni mwa idadi hiyo, watu 223,058 wamesajiliwa kutoka Kaya Masikini kwa ushirikiano na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF). Lengo ni kuwatambua wanaokidhi vigezo vya kupata ruzuku ya Serikali kupitia mfuko huo.

**202.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza kasi ya usajili, ***napenda kulitangazia Bunge hili kuwa mwezi Desemba, 2022 NIDA imeanza kupokea maombi ya usajili kwa njia ya mtandao.*** Huduma hiyo itapunguza gharama na foleni za watu katika ofisi za usajili za NIDA, hususan maeneo ya mijini. Hadi kufikia mwezi Mei, 2023 maombi 17,248 yalipokelewa kupitia njia hiyo. Vilevile, NIDA imefanya usajili wa majaribio kwa Watanzania waishio nje ya nchi, ambapo 154

walisajiliwa katika ubalozi wa Tanzania nchini Marekani. Katika mwaka 2023/24 Serikali itaendelea na zoezi la usajili na utambuzi wa watu katika wilaya na mikoa yote, ambapo jumla ya watu 1,597,827 wanatarajiwa kusajiliwa.

**203. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi husika NIDA imezalisha Namba za Utambulisho 623,247 na vitambulisho 1,059,716. Idadi hii inafanya jumla ya Namba za Utambulisho zilizozalishwa kuwa 20,126,693 na vitambulisho kuwa 12,097,933 tangu kuanza kwa zoezi la usajili. Kati ya vitambulisho vilivyozalishwa, 584,171 vimegawiwa kwa wananchi na kufanya jumla ya vitambulisho vilivyogawiwa kufikia 10,738,070.

**204. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kufanya jitihada za kuhakikisha watu wote wenye Namba za Utambulisho wanapata vitambulisho vyao. Hadi kufikia Mei, 2023 NIDA imepokea Shilingi 28,000,000,000. Aidha, NIDA imeshafungua barua za malipo (Letter of Credit – LC) ya Shilingi 42,500,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa kadighafi 11,242,353 na taratibu za ununuzi zinaendelea. Upatikanaji wa kadighafi hizo utawezesha wananchi wote waliosajiliwa kupata vitambulisho vyao. ***Napenda kuishukuru Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kulipa deni la muda mrefu la Shilingi 17,578,313,987.78 na hivyo kurejesha uhusiano wa kimkataba baina ya NIDA na mzabuni.***

**205. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya marekebisho ya Kanuni za Usajili na Utambuzi wa Watu za mwaka 2014. Marekebisho hayo yamefanyika katika maeneo ya ukomo wa muda wa Vitambulisho vya Taifa kwa Watanzania, huduma ya ushirikishanaji wa taarifa, usajili wa walowezi na Watanzania wanaoishi nje ya nchi. Matokeo tarajiwa ni kuimarika kwa usalama kwa kuwatambua watu wote, kuboresha utolewaji wa huduma na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali. ***Naomba nitoe maagizo kwa watoa huduma kuendelea kuvitambua Vitambulisho vya Taifa bila kuzingatia tarehe ya muda wa ukomo wa matumizi.***

**206. *Mheshimiwa Spika,*** tarehe 27 Oktoba, 2022 Serikali ilisaini Mkataba wa Mkopo wa Masharti Nafuu na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Korea Kusini kwa ajili ya kuanza awamu ya pili ya mradi wa ujenzi wa ofisi za NIDA. Mradi unahusisha ujenzi wa Ofisi ya

Makao Makuu – Dodoma, ofisi 31 za usajili za Wilaya na ghala la kuhifadhia vifaa vya TEHAMA. Kwa sasa NIDA ipo katika taratibu za mwisho za ununuzi za kumpata mshauri elekezi.

**Uunganishaji wa Mfumo wa NIDA na Mifumo ya Taasisi Nyingine**

**207.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwezi Julai, 2022 hadi Mei, 2023 NIDA imeunganisha taasisi 14 katika Mfumo wa Usajili na Utambuzi. Kuunganishwa kwa taasisi hizo, kunafanya jumla ya taasisi zilizounganishwa katika mfumo huo kufikia 75. Katika mwaka 2023/24 jumla ya taasisi 15 za umma na binafsi zitaunganishwa kwenye mfumo wa NIDA. ***Nitoe wito kwa taasisi za umma na binafsi kujiunga na Mfumo wa NIDA ili kuungana na Serikali katika kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi.***

**208.** ***Mheshimiwa Spika,*** NIDA imefanikiwa kuunganisha mtandao wa mawasiliano katika ofisi za usajili nne (4) ambazo ni Malinyi, Gairo, Ulanga – Morogoro na Mbogwe – Geita. Hivyo, kufanya jumla ya ofisi za usajili zilizounganishwa na mtandao huo kuwa 143 kati ya 153. Uunganishaji mtandao wa mawasiliano unawezesha usafirishaji wa taarifa za usajili na utambuzi kutoka ofisi za usajili kwenda kituo cha uchakataji na uzalishaji wa vitambulisho.

**209.** ***Mheshimiwa Spika,*** NIDA inaendelea na utaratibu wa kuunganisha ofisi za usajili nane (8) ambazo ni Ngorongoro – Arusha, Buhigwe – Kigoma, Uyui – Tabora, Magharibi B, Kaskazini A, Kaskazini B, Kusini Unguja na Micheweni – Zanzibar. Kazi hiyo itakamilika ifikapo mwezi Juni, 2023. Katika mwaka 2023/24 NIDA itaunganisha ofisi mbili (2) za usajili zilizopo Chalinze – Pwani na Itigi – Singida kwenye kituo cha uchakataji na uzalishaji wa vitambulisho.

**210.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaangalia uwezekano wa kupunguza vitambulisho vinavyotumika kwa huduma mbalimbali ili kuwa na kitambulisho kimoja cha taifa (Universal National Identification Card). Katika kufanikisha hilo, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imefanya majadiliano ya awali na maafisa waandamizi wa Bill & Melinda Gates Foundation ya Marekani mwezi Mei, 2023. Ili kuwezesha mpango huo, katika mwaka 2023/24 Serikali itaanza kufanya yafuatayo: kushirikisha wadau wote muhimu kupata maoni; kurekebisha Sheria ya Utambuzi na Usajili ili

kuwezesha mtu kusajiliwa tangu anapozaliwa hadi anapofariki; kutumia teknolojia ya kisasa kwa kushirikiana na nchi zenye uzoefu na zinazotumia kitambulisho kimoja cha taifa; na kuwekeza katika mifumo ya kisasa ya utambuzi na usajili wa watu pamoja na utoaji wa vitambulisho.

**211.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufanikiwa kwa utekelezaji wa mpango huo kutawezesha kuunganisha Kitambulisho cha Taifa na vitambulisho vingine kama vile leseni ya udereva, kadi ya bima ya afya na kitambulisho cha mpiga kura. Aidha, kutapunguza gharama za Serikali katika ununuzi wa kadi ghafi za kuchapisha vitambulisho, kuwezesha upatikanaji wa huduma za kiuchumi na kijamii kwa wananchi na kurahisisha upatikanaji wa kadi hizo kwa wananchi.

**HUDUMA KWA WAKIMBIZI**

**212.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Mei, 2023, Tanzania inahifadhi jumla ya wakimbizi 269,749. Katika kuwatafutia suluhisho la kudumu wakimbizi waliopo nchini, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Wakimbizi Duniani (UNHCR) imefanikiwa kuwarudisha wakimbizi katika nchi zao za asili kwa hiari na kuwahamishia nchi ya tatu. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023, jumla ya wakimbizi 5,324 wenye asili ya Burundi walirejea nchini kwao. Pia, wakimbizi 5,011 walihamishiwa katika mataifa manne (4), ambapo 4,479 walipelekwa Marekani, 511 Canada, 14 Ufaransa na 7 Australia.

**213.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu upokeaji wa waomba hifadhi kutoka nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), hadi kufikia tarehe 16 Mei, 2023 jumla ya waomba hifadhi 10,623 walikuwa wamepokelewa. Aidha, 9,624 tayari wamehojiwa na kuhamishiwa katika Kambi ya Wakimbizi ya Nyarugusu. Waomba hifadhi 2,838 wamesajiliwa katika mfumo wa NIDA na 437 wamebainika kutokuwa na sifa hivyo wamekabidhiwa kwa Idara ya Uhamiaji kwa ajili ya kuchukuliwa hatua za kisheria.

**214.** ***Mheshimiwa Spika,*** udhibiti wa uingiaji wa watu kutoka DRC umeendelea kudhibitiwa kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama. Udhibiti huo umewezesha idadi ya wanaoingia

nchini kupungua kutoka zaidi ya watu 400 – 600 kwa siku hapo awali na kufikia wastani wa watu 33.

**215.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na uharibifu mkubwa wa mazingira, Wizara inafanya ufuatiliaji wa shughuli za mazingira zinazofanywa na mashirika ndani ya kambi na kwenye vijiji jirani ili kuongeza uwajibikaji. Aidha, jumla ya miche 267,526 imeoteshwa katika kambi ili kusaidia urejeshaji wa uoto wa asili.

**216.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itaendelea: kusimamia hali ya ulinzi na usalama katika makazi, kambi za wakimbizi na maeneo yanayozunguka kwa kushirikiana na vyombo vingine vya usalama; kuwatafutia suluhisho la kudumu wakimbizi waliopo nchini; kupitia Mkataba wa Makubaliano (MoU) wa mwaka 1991 kati ya Serikali na UNHCR; kupokea na kufanya uchambuzi wa maombi ya waomba hifadhi; na kusimamia na kufuatailia utunzaji wa mazingira katika maeneo ya kambi za wakimbizi. Jumla ya Shilingi 1,731,219,000 zimetengwa katika mwaka 2023/24 kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo.

**USAJILI WA JUMUIYA ZA KIDINI NA ZISIZO ZA KIDINI**

**217.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kusajili na kusimamia Jumuiya za Kidini na zisizo za Kidini kwa kuzingatia Sheria ya Jumuiya, Sura ya 337. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2022 hadi Mei, 2023 jumla ya maombi ya usajili wa Jumuiya 429 yalipokelewa. Jumla ya Jumuiya 375 zilisajiliwa, ambapo 279 ni Jumuiya za Kidini na 96 ni Jumuiya zisizo za Kidini na maombi ya usajili 54 yanaendelea kufanyiwa kazi. Usajili huu unafanya idadi ya Jumuiya za Kidini na zisizo za Kidini zilizosajiliwa kufikia 10,108 mwezi Mei, 2023. Aidha, Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Usimamizi wa Jumuiya (RSMIS) ulizinduliwa rasmi tarehe 08 Novemba, 2022 na umeanza kutumika.

**218.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza jitihada za kuhakikisha kuwa Jumuiya za Kiraia zinaendesha shughuli zake kwa kuzingatia sheria na malengo ya kuanzishwa kwake bila kuathiri amani na utulivu nchini, Ofisi ya Msajili wa Jumuiya ilifanya uhakiki na kuhuisha vyeti vya usajili wa Taasisi za Kidini katika Kanda ya Mashariki, Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Ziwa, Kanda ya Magharibi, Kanda ya Kati, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Kusini. Katika

zoezi hilo, jumla ya Taasisi za Kidini 672 zilihakikiwa na vyeti vya usajili 672 vilihuishwa.

**219.** ***Mheshimiwa Spika,*** zoezi hili ambalo linaendeshwa nchi nzima, litaendelea hadi tarehe 31 Mei, 2023 na taasisi ambazo hazitoshiriki na kuhuisha vyeti vyao vya usajili, zitatafsirika kuwa haziko hai na hivyo kuondolewa kwenye daftari la usajili. Aidha, katika kipindi husika ukaguzi umefanyika kwenye Jumuiya za Kidini zilizosajiliwa 17 zilizopo katika Mikoa ya Lindi na Mtwara kwa kushirikiana na Vyombo vya Ulinzi na Usalama na kuchukua hatua stahiki kwa zilizobainika kukiuka sheria za nchi.

**220.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na uhakiki na ukaguzi uliofanyika, elimu ilitolewa kwa jamii kuhusu taratibu za usajili kwa Jumuiya za Kidini na zisizo za Kidini. Aidha, vikundi vyenye sifa ambavyo havijasajiliwa vimetakiwa kujisajili kwa mujibu wa Sheria. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 jumla ya vikundi 38 vilisajiliwa.

**221.** ***Mheshimiwa Spika,*** usajili huwezesha vikundi kutambulika katika mfumo rasmi utakaorahisisha vikundi hivyo kufikiwa na programu za maendeleo na kupatiwa mafunzo. Katika kusogeza huduma hizo karibu na wananchi Wizara imefungua Ofisi Ndogo ya Msajili Kanda ya Mashariki Jijini Dar es Salaam inayohudumia Mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Morogoro, Mtwara na Pwani. Huduma hizo ni utekelezaji wa Ibara ya 127 ya Ilani ya CCM ya mwaka 2020 – 2025.

**222.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kudhibiti na kupambana na vitendo vya mmomonyoko wa maadili kwenye Jumuiya za Kidini na zisizo za Kidini, Ofisi ya Msajili wa Jumuiya imefanya yafuatayo: imesitisha shughuli za Jumuiya ya kidini iitwayo Spirit Word Ministry iliyopo eneo la Stakishari Wilaya ya Ilala Jijini Dar es Salaam. Jumuiya hiyo imefutiwa usajili kwa sababu ya kutoa mahubiri na mafundisho yenye mwelekeo wa kuhamasisha vitendo vya mapenzi ya jinsia moja na kutoa ujumbe wenye kuhafifisha jitihada za kupambana na vitendo vya ushoga nchini.

**223.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, taarifa zimekusanywa zinazohusu idadi ya vituo vya kulea watoto na shule zinazotoa mafundisho ya dini kwa watoto wadogo. Lengo ni kutambua idadi ya vituo au

shule za bweni zinazotoa mafunzo yenye mwelekeo unaokinzana na maadili ya nchi yetu ikiwemo vitendo vya mapenzi ya jinsia moja. Pia, elimu imetolewa kwa Viongozi wa Jumuiya za Kidini ili waendelee kutoa mafundisho yanayoendana na mila, desturi na maadili ya Kitanzania kwa waumini wao na kujiepusha na vitendo vya uvunjifu wa maadili. Aidha, kazi ya kuboresha vigezo vya usajili inaendelea kwa lengo la kuhakikisha kuwa Jumuiya zinazosajiliwa ni zile zenye kuleta tija na zisizokinzana na mila, desturi na utamaduni wa Kitanzania. Serikali inaendelea kufuatilia kwa karibu mienendo ya jumuiya zote na kuchukua hatua kali kwa watu au jumuiya zitakazo hamasisha vitendo vya ukiukwaji wa maadili.

**224.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Wizara imepanga: kuandaa mwongozo wa taratibu za kuabudu na ithibati ya taasisi zinazotoa elimu ya dini; kuimarisha ufuatiliaji na utendaji wa Jumuiya za Kidini na zisizokuwa za Kidini; kufanya ukaguzi na tathmini ya vihatarishi vya kiusalama kwa kushirikiana na Vyombo vya Ulinzi na Usalama; na kutoa mafunzo kwa Viongozi wa Jumuiya yatakayochangia kudumisha amani na utulivu nchini.

**225.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine itakayofanyika ni kuanzisha Ofisi za Kanda za Msajili katika Kanda ya Ziwa itakayohudumia Mikoa ya Mwanza, Mara, Geita, Simiyu, Shinyanga na Kagera na Ofisi ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini itakayohudumia Mikoa ya Mbeya, Songwe, Iringa na Njombe.

## UDHIBITI WA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU

**226.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 Wizara kwa kushirikiana na wadau imeokoa na kusaidia wahanga 190 wa usafirishaji haramu wa binadamu. Kati ya hao, wahanga 184 walikuwa ni Watanzania na sita (6) ni raia wa Burundi. Wahanga hao walikuwa wakitumikishwa kufanya kazi majumbani, kwenye mashamba na migodi midogo, kuomba mitaani na kutumikishwa kingono. Aidha, jumla ya kesi 13 za usafirishaji haramu wa binadamu zinazohusisha wahalifu 23 zilifunguliwa kwa hatua za kisheria.

**227.** ***Mheshimiwa Spika,*** takwimu zinaonesha wahanga wakubwa wa usafirishaji haramu wa binadamu ni watoto na wanawake. Kati ya idadi ya wahanga 190 waliookolewa, wahanga 148 walikuwa ni

wanawake na 42 ni wanaume. Vilevile, wahanga 138 walikuwa ni watoto na wahanga 52 walikuwa ni watu wazima. Wahanga wote walipewa hifadhi ya muda na huduma muhimu kama vile chakula, matibabu, msaada wa kisheria, ushauri nasaha, msaada wa kisaikolojia na elimu. Pia, Wizara iliratibu zoezi la kutambua familia za wahanga hao na kuwaunganisha na familia zao.

**228.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilitoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wadau 221 wanaohusika na utekelezaji wa Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432. Idadi hii inafanya wadau waliopewa mafunzo kufikia 2,292 tangu mafunzo hayo yalipoanza kutolewa mwaka 2017. Lengo la mafunzo hayo ni kuboresha mbinu za utambuzi na usimamizi wa wahanga, upelelezi na uendeshaji wa mashtaka yanayohusiana na makosa ya usafirishaji haramu wa binadamu. Mikoa iliyonufaika na mafunzo hayo ni Mbeya, Singida, Geita, Tabora, Kagera, Katavi, Shinyanga, Mtwara, Kigoma, Morogoro, Kaskazini Pemba na Kusini Pemba.

**229.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, elimu ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu imetolewa kwa jamii katika Mikoa ya Kigoma, Shinyanga, Mwanza, Dar es Salaam, Dodoma na Mkoa wa Mjini Magharibi. Aidha, elimu hiyo ilihusisha Madiwani, Watendaji wa Kata, Shehia na Vijiji, Wenyeviti wa Vijiji, Wajumbe wa Halmashauri za Vijiji, Viongozi wa Dini, Wajumbe wa Kamati za Kupinga Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto, Walimu na Wanafunzi 15,741 wa shule za msingi na sekondari.

**230.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inakamilisha taratibu za kufungua Ofisi ya Sekretarieti itakayokuwa Dunga, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja – Zanzibar kabla ya mwezi Julai, 2023. Sambamba na hilo, Wizara imefanikiwa kufanya marekebisho madogo ya Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura 432 kwa kuongeza adhabu kwenye makosa yaliyoainishwa na sheria hii na kuondoa adhabu ya faini kama mbadala wa kifungo gerezani. Aidha, Wizara imeandaa daftari la watoa huduma kwa wahanga walioko nchi nzima ili kurahisisha utoaji wa rufaa na huduma muhimu kwa wahanga.

**231.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Wizara imepanga kufanya kazi zifuatazo: kuanzisha kanzidata ya usafirishaji haramu wa binadamu; kuimarisha Ofisi ya Sekretarieti ya Kuzuia na

Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu – Zanzibar; na kuimarisha mfuko wa kusaidia wahanga. Fedha zilizotengwa kwa mwaka 2023/24 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo ni Shilingi 563,867,000.

**USHUGHULIKIAJI WA MALALAMIKO YANAYOHUSU VYOMBO VYA USALAMA VILIVYOPO CHINI YA WIZARA**

**232.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kupokea na kuyapatia ufumbuzi malalamiko ya wananchi kuhusu masuala ya usalama wa watu na mali zao yanayosimamiwa na Vyombo vya Usalama vilivyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 jumla ya malalamiko 242 yalipokelewa. Kati ya malalamiko hayo 167 yalitoka kwa wananchi, 31 yalitoka kwa watumishi, 14 kwa watumishi wastaafu na 30 kutoka kwenye asasi za kiraia.

**233.** ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya malalamiko yaliyopokelewa, 154 yalihusu Jeshi la Polisi, 29 Jeshi la Magereza, manne (4) Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, 20 Idara ya Uhamiaji na sita (6) Makao Makuu ya Wizara. Malalamiko 81 yalipatiwa ufumbuzi na 161 yapo katika hatua mbalimbali za kupatiwa ufumbuzi ikiwemo kufanyiwa uchunguzi wa kina. Malalamiko 29 yalihusu Taasisi zilizo nje ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na hivyo yaliwasilishwa kwenye Taasisi husika kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi.

**234.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Wizara itaendelea kupokea, kuchambua na kufanya uchunguzi wa kina wa malalamiko ya wananchi ili kuongeza imani yao kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Vyombo vya Usalama vilivyopo chini yake. Aidha, Wizara itaendelea kutumia mfumo wa e-Mrejesho ili kuongeza kasi ya kushughulikia malalamiko na kuhakikisha kuwa wananchi wanapata mrejesho wa ufumbuzi wa malalamiko yao kwa wakati.

**235.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Wizara imepanga kutumia Shilingi 441,074,000 kwa ajili ya kuendeleza kazi za kushughulikia malalamiko ikiwemo kuongeza vitendea kazi vitakavyowezesha mfumo wa e-Mrejesho kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

## E. SHUKRANI

**236.** ***Mheshimiwa Spika,*** nakushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kusimamia vizuri shughuli za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa umoja wenu mmewezesha shughuli za Bunge kuendelea vema na kutoa ushauri unaosaidia kuimarisha utendaji wa Wizara na Serikali kwa ujumla.

**237.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile natoa shukrani zangu za dhati kwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhe. Jumanne A. Sagini na Mbunge wa Jimbo la Butiama kwa kunisaidia kusimamia majukumu ya Wizara. Aidha, ninawashukuru Katibu Mkuu Ndugu Kaspar K. Mmuya na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Maduhu I. Kazi kwa kusimamia vema utekelezaji wa kazi za Wizara.

**238.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia ninawashukuru Wakuu wa Vyombo vya Usalama vilivyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kuwasimamia watumishi waliopo chini yao katika kuhakikisha uwepo wa amani na utulivu nchini na kuwezesha kupatikana kwa mafanikio katika Wizara. Viongozi hao ni: Inspekta Jenerali wa Jeshi la Polisi, Camillus Wambura; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, Mzee R. Nyamka; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, John W. Masunga; na Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dkt. Anna P. Makakala. Namshukuru pia Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, Ndugu Ismail H. Rumatila.

**239.** ***Mheshimiwa Spika,*** shukrani nyingine nazitoa kwa wenyeviti wa Bodi za Mashirika yaliyopo chini ya Wizara ambao ni Prof. Suffian H. Bukurura Mwenyekiti wa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi na Inspekta Jenerali wa Polisi Mstaafu Saidi A. Mwema Mwenyekiti wa Shirika la Magereza. Wenyeviti hao kwa kushirikiana na wajumbe wa bodi wamekuwa wakitoa ushauri wa kuboresha utendaji na usimamizi wa mashirika hayo ambayo yanaendelea kuimarika. Aidha, namshukuru Mhe. Balozi Khamis Kagasheki Mwenyekiti wa Bodi ya Parole kwa kusimamia vema majukumu ya Bodi hiyo.

**240.** ***Mheshimiwa Spika,*** nawashukuru Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Makamishna, Makamishna Wasaidizi, Wakuu wa Vitengo, Maafisa, Askari na watumishi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani

ya Nchi kwa kuendelea kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi.

**241.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, natoa shukrani kwa nchi za Austria, Marekani, Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu, Umoja wa Ulaya, Jamhuri ya Korea Kusini pamoja na Kampuni na Mashirika ya IOM, UNDP, UNHCR, UNICEF, UNFPA, UN – Women, WFP, TIRA, Buzwagi Gold Mine, North Mara Gold Mine, Taasisi za Kidini na sizizokuwa za Kidini, Vyombo vya Habari na wananchi kwa ujumla kwa kuendelea kushirikiana na Wizara katika nyanja mbalimbali.

**242.** ***Mheshimiwa Spika***, shukrani za kipekee nazitoa kwa familia yangu, ndugu na jamaa kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Kwa dhati kabisa ninawashukuru na kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Kikwajuni kwa kushirikiana nami katika kuwezesha maendeleo ya jimbo letu.

**243.** ***Mheshimiwa Spika***, hotuba hii inapatikana pia kwenye tovuti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambayo ni www.moha.go.tz.

## F. HITIMISHO

**244.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/24 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itatekeleza vipaumbele vyake kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Aidha, Wizara itaendelea kusimamia jukumu lake la msingi la usalama wa raia na mali zao ili kuwawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi na kijamii.

### Makadirio ya Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka 2023/24

**245.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2023/24 Wizara imewekewa lengo la kukusanya jumla ya Shilingi 393,500,000,000 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali. Ili kufikia lengo hilo Wizara itatekeleza mikakati inayohusisha: ununuzi wa vitendea kazi ikiwemo magari na pikipiki; kuunganisha na kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika kutoa huduma na ukusanyaji wa mapato; na kukagua utendaji wa jumuiya zilizosajiliwa chini ya Wizara.

**Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2023/24**

**246.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa heshima na taadhima, naomba sasa Bunge lako liidhinishe Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2023/24 yenye jumla ya **Shilingi 1,293,820,903,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 510,135,630,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, **Shilingi 678,657,324,000** ni Mishahara na **Shilingi 105,027,949,000** ni fedha za Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo, **Shilingi 100,233,364,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 4,794,585,000** ni fedha za nje.

**247.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni.

Kabla sijamwita Mwenyekiti wa Kamati, kuna matangazo machache, wapo wageni waliopo Bungeni muda huu, ni wageni walio Jukwaa la Spika.

Kwanza ni wageni wa Mheshimiwa Mhandisi Hamad Masauni, Mbunge na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni Ndugu Charles Mkumbo ambaye ni Kamishna wa Polisi Intelejensia ya Jinai; yupo Ndugu Liberatus Sabas, Kamishna wa Polisi Fedha na *logistics;* yupo Ndugu Shaban Hiki, Kamishna wa Polisi Uchunguzi wa Sayansi ya Jinai; yupo Ndugu Faustine Shilogile, Kamishna wa Polisi Jamii; na mwingine ni Ndugu Suzan Kaganda, Kamishna wa Polisi wa Utawala na Rasilimali Watu; ahsante sana, karibuni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge.

Yupo Ndugu Jeremia Katungu, Kamishna wa Magereza wa Utawala na Rasilimali Watu; yupo Ndugu Chacha Bina Jackson, Kamishna wa Magereza wa Fedha na Mipango; yupo Ndugu

Charo Magare, Kamishna wa Jeshi la Zimamoto upande wa Oparesheni; yupo Ndugu Maria Kulaya, Kamishna wa Jeshi la Zimamoto upande wa Mipango; yupo Ndugu Gerald Kihinga, Kamishna wa Uhamiaji upande wa *Passport* na Uraia; yupo Ndugu Samweli Mahirane ambaye ni Kamishna wa Uhamiaji wa Mipaka; yupo Ndugu Edmund Mroso, Kamishna wa Uhamiaji wa Sheria; yupo Ndugu Sudi Mwakibasi, Mkurugenzi Idara ya Huduma za Wakimbizi Tanzania; yupo Ndugu Alyoce Musika, Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Uangalizi; na Ndugu Emmanuel Kihampa ambaye ni Msajili wa Jumuiya za Kiraia, ahsanteni na karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Mhandisi Hamad Masauni, ambao ni Wakaguzi Wasaidizi watano ambao watapewa sifa na zawadi. Hawa ni kama ifuatavyo; yupo Mkaguzi Msaidizi Dkt. Mwanaidi Lwena anatoka Mkoa wa Morogoro; yupo Mkaguzi Msaidizi, Khalfani Ussi – Mkoa wa Kaskazini Pemba; yupo Mkaguzi Msaidizi, Daniel Mbebela anatoka Mkoa wa Kilimanjaro; yupo Mkaguzi Msaidizi, Fansisi Msuku anatoka Mkoa wa Simiyu; yupo PC Hamis Masana, huyu anatoka Mkoa wa Kipolisi wa Temeke, nadhani ndio yule aliyekataa rushwa. Ahsante, karibu sana, tunakupongeza sana kwa uzalengo wako. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Mhandisi Hamad Masauni ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa na Viongozi wa Wadi kutoka Jimboni kwake Kikwajuni Zanzibar. *(Makofi)*

Wapo wageni wa Waheshimiwa Wabunge; mgeni wa Mheshimiwa Hamida Abdallah, Diwani kutoka Lindi Manispaa na Katibu wa Madiwani. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji (Mbunge) ambao ni Ndugu Ahsa Kitwana na Mariyam Ismail kutoka Kusini Unguja. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Mariam Ditopile ambaye ni mjasiriamali na mwanachama wa CCM. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Joseph Mkundi (Mbunge) ambao ni wafanyakazi kutoka *Lerai Dry Cleaners* Mkoa wa Dodoma, ahsanteni na karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni wanafunzi 80 na walimu 10 wa Shule ya Sekondari *Mvumi Mission* ya Jijini Dodoma, ahsante, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Rebecca Ezekiel ambaye ni mwanafunzi wa Shule ya Sheria *(Law School of Tanzania),* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Mwanzilishi wa Kampeni ya Kitaifa ya Mazingira inayoitwa *Nitunze Campaign* pamoja na Kampeni ya Kuwalinda Watoto inayoitwa Mtoto Wangu ni Mboni Yangu, ameambatana na wenzake, ahsante, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kwa niaba yake Mheshimiwa Joseph Mkundi, njoo uwasilishe Mapendekezo na Maoni ya Kamati, karibu. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na utangulizi. Awali ya yote, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuvisimamia na kuviimarisha vyombo vyote vya ulinzi na usalama nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2022/2023,

pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa taarifa hii ni majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 6(3) na Kifungu cha 7(1)(a), cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, pamoja na masharti ya Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii imegawanyika katika sehemu sita zifuatazo: Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi; Sehemu ya Pili ni Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo; Sehemu ya Tatu ni Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023; Sehemu ya Nne ni Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024; Sehemu ya Tano ni Maoni na Ushauri wa Kamati; na Sehemu ya Sita ni Hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo; kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua miradi minne ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara hii katika Mikoa ya Morogoro, Tanga na Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu hii ya Taarifa inaeleza mambo makuu mawili ambayo ni Muhtasari wa maelezo ya Miradi iliyotekelezwa katika mwaka wa fedha 2022/2023; na Uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo. Lengo la sehemu hii ni kuliwezesha Bunge kufuatilia hali ya utekelezaji na upatikanaji wa fedha lilizoziidhinisha na kupata mantiki ya uamuzi wake wakati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo kuhusu miradi ya maendeleo iliyokaguliwa, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara hii ilipaswa kutekeleza jumla ya miradi 12 katika mikoa mbalimbali nchini. Hata hivyo, kwa madhumuni ya masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilitembelea miradi minne inayotekelezwa katika Mikoa ya Morogoro, Tanga na Manyara, na miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

Moja, Mradi Na. 6305 – Ujenzi wa Gereza la Wilaya na Ofisi za Magereza, Kilosa unaotekelezwa chini ya Fungu 29 – Jeshi la Magereza.

Pili, Mradi Na. 6582 – Ujenzi wa Chuo cha Zimamoto na Uokoaji Chogo, Handeni, Mkoani Tanga unaotekelezwa chini ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Tatu, Mradi Na. 6582 – Ujenzi wa Ofisi za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoani Manyara unaotekelezwa chini ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Nne, Mradi Na. 6302 – Ujenzi wa nyumba 12 katika Chuo cha Uhamiaji, Boma Kichakamiba, Mkinga unatekelezwa chini ya Jeshi la Uhamiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya muhtasari wa maelezo kuhusu miradi ya maendeleo iliyokaguliwa, naomba kutoa taarifa kuhusu matokeo ya ukaguzi na uchambuzi wake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Ujenzi wa Gereza la Wilaya na Ofisi ya Jeshi la Magereza Kilosa; Kamati ilielezwa kuwa mradi huu ulianza kutekelezwa rasmi Februari, 2022 kwa kutumia utaratibu wa *Force Account*. Hadi kukamilika kwake, mradi huu unatarajiwa kugharimu shilingi bilioni 8.3. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Jeshi lilitengewa shilingi 757,200,108 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa mradi huu, lakini hadi wakati Kamati inatembelea mradi, Jeshi halikuwa limepokea fedha yoyote kwa ajili ya mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa fedha inayotumika katika ujenzi ni sehemu ya fidia ambayo Jeshi limepokea kutokana na eneo lake kutwaliwa kwa ajili ya ujenzi wa Reli ya *SGR*, ambapo Jeshi lilipwa kiasi cha shilingi 461,497,022.16, ambapo hadi wakati Kamati inakagua awamu ya kwanza ilikuwa imekamilika, na kiasi cha shilingi 410,326,554 kilikuwa kimetumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa nyumba 12 Chuo cha Uhamiaji, Boma Kichakamiba – Wilayani Mkinga, mradi huu katika mwaka wa fedha 2022/2023 ulitengewa kiasi cha shilingi 600,000,000. Hadi wakati Kamati inatembelea mradi, tarehe 16 Machi, 2023, ujenzi wake haukuwa umeanza. Kamati ilielezwa

kwamba sababu za kutoanza ujenzi wa mradi ni kutokupokelewa kwa fedha kutoka Hazina. Kamati ilidadisi kujua kama Wizara imekamilisha taratibu zote za kuomba fedha Hazina ambapo ilielezwa kuwa taratibu zote zimekamilika na fedha kuombwa Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa mradi wa ujenzi wa Chuo cha Zimamoto na Uokoaji Chogo, Handeni – Tanga ulipaswa kuanza kutekelezwa tangu tarehe 21 Novemba, 2022 kwa uratatibu wa *Force Account* na ungekamilika tarehe 30 Oktoba, 2023. Aidha, mradi huu hadi kukamilika kwake unatarajiwa kutumia jumla ya shilingi 1,553,000,000. Ujenzi unajumuisha jengo la utawala, jengo la ukumbi wa mihadhara, jengo la maktaba na jengo la amali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi wakati Kamati inatembelea mradi huu tarehe 15 Machi, 2023 ikiwa imebaki miezi mitatu kabla mwaka wa fedha 2022/2023 haujaisha, fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa mradi huu hazikuwa zimepokelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakati wa ziara yake, Kamati ilielezwa kuwa mradi wa Ujenzi wa Ofisi za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoani Manyara ulitarajiwa kuanza Tarehe 21 Novemba, 2022 na kukamilika tarehe 30 Oktoba, 2023. Aidha, hadi kukamilika kwake, mradi unatarajiwa kutumia jumla ya shilingi 600,000,000 na utatekelezwa kwa utaratibu wa *Force Account.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, hadi Kamati inatembelea mradi huu tarehe 19 Machi, 2023 ujenzi haukuwa umeanza kutokana na kutopokelewa fedha za ujenzi kutoka Hazina ilhali Jeshi limekamilisha taratibu zote na kuomba fedha Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipofanya uchambuzi wa mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ilizingatia makusanyo ya maduhuli ikilinganishwa na lengo lililokusudiwa, upatikanaji wa fedha za matumizi kwa shughuli zilizopangwa kutekelezwa hususan fedha kwa ajili ya Matumizi Mengineyo *(OC)* na fedha za miradi ya maendeleo kwa mafungu yote matano ya Wizara. Vilevile, Kamati ilizingatia taarifa muhimu na za ziada zilizopatikana kupitia

mahojiano wakati wa vikao vya Kamati. Uchambuzi huo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ikijumuisha Mafungu yake yote matano ilikadiria kukusanya mapato ya shilingi 356,600,000,000 ikilinganishwa na shilingi 331,591,585,600 zilizokadiriwa kukusanywa katika mwaka wa fedha 2021/2022. Kamati ilielezwa kuwa, hadi kufikia mwezi Februari, 2023, kiasi kilichokusanywa kilikuwa ni shilingi 199,834,373,735 sawa na asilimia 56 ya lengo la mwaka lililopangwa. Kamati ilibaini kuwa makusanyo hayo yameongezeka kwa shilingi 24,794,373,735 sawa na asilimia 14.16 ikilinganishwa na makusanyo yaliyokusanywa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambayo yalikuwa shilingi bilioni 174.04.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kufanya uchambuzi wa kina, Kamati ilibaini kuwa mafungu yote matano ya Wizara yalikusanya mapato kwa kiwango cha kuridhisha ikilinganishwa na makusanyo ya kipindi kama hiki kwa kila fungu katika mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijiridhisha kuhusu mwenendo wa makusanyo kwa kipindi cha miaka mitano na kufanya ulinganisho wa makusanyo hayo kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2018/2019 na kubaini kuwa makusanyo ya mapato yamekuwa yakiongezeka kila mwaka hadi mwaka 2019/2020 na kupungua katika mwaka wa fedha 2020/2021. Aidha, mwenendo huo wa makusanyo unadhihirika katika Jedwali Na. 1 & 2 na Grafu Na. 1 katika taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Kamati ilifanya uchambuzi na kuainisha mchanganuo wa makusanyo kwa kila fungu hadi kufikia mwezi Februari, 2023 ikilinganishwa na lengo la mwaka lililowekwa. Aidha, Kamati ilifanya ulinganisho wa makusanyo yaliyopatikana hadi kufikia mwezi Februari 2023 na makusanyo yaliyopatikana katika kipindi kama hicho, kwa mwaka 2022, kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 2 na Grafu Na. 2 katika taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinganisho huo wa makadirio ya makusanyo kwa kila fungu ikilinganishwa na mapato halisi ya kila fungu, umeisaidia Kamati kubaini kuwa Jeshi la Uhamiaji ndilo

linalochangia kwa asilimia kubwa katika makusanyo yote ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uchambuzi uliofanyika, Kamati ina maoni kuwa mwenendo wa makusanyo kwa mwaka huu wa fedha ni wa kuridhisha kwani kiujumla Wizara kwa mafungu yote imekusanya asilimia 54 ya lengo lililowekwa; ingawa kwa kipindi hicho angalau wangekuwa wamefikia asilimia 65 ya lengo. ni dhahiri kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kufikiwa kwa lengo lilowekwa. Pamoja na kwamba ukusanyaji unaridhisha bado ukusanyaji wa maduhuli unakabiliwa na changamoto mbalimbali kama ilivyoelezwa katika taarifa hii. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali itazingatia changamoto hizo na kupanga makadirio ya makusanyo kwa kuzingatia uhalisia katika Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina; Katika Bunge la Kumi na Moja Kamati iliendelea kuishauri Serikali kupitia Hazina kuona umuhimu wa kutoa fedha hizo kama zinavyoidhinishwa na Bunge. Hata hivyo mtiririko wa upatikanaji wa fedha hizo uliendelea kuwa si wa kuridhisha kwa baadhi ya mafungu hasa Fungu 29 na Fungu 14 na hivyo kuathiri ratiba ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia changamoto hiyo, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kufanya ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na kiasi cha fedha kilichopelekwa hadi kufikia mwezi Februari, 2023. mchanganuo wa upatikanaji wa fedha za mishahara, matumizi mengineyo na maendeleo, umeoneshwa dhahiri katika Jedwali Na. 3 na Grafu Na. 3 katika taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa mtiririko wa fedha kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ni wa kuridhisha kwani imepokea zaidi ya asilimia 50 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya mishahara na mengineyo. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, uchambuzi wa Kamati umebaini

kuwa mtiririko wake si wa kuridhisha kwani Mafungu 14, 28, 29 na 93 yamepata fedha za maendeleo chini ya asilimia 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili idhini ya Bunge kwa bajeti ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo iwe na tija, upatikanaji wa fedha hizo kwa wakati na kwa kadiri inavyostahili ni jambo muhimu kufanikisha utekelezaji huo kwa muda uliopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati; ili kujiridhisha na uzingatiaji wa ushauri uliotolewa na Kamati Bungeni kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara hii. Kamati ilichambau taarifa ya utekelezaji wa ushauri huo. Uchambauzi umeonesha kuwa kwa sehemu kubwa ushauri wa Kamati umezingatiwa. Ufafanuzi wa hali ya uzingatiaji unaoneshwa katika kiambatisho namba moja cha taarifa hii. Hata hivyo ni maoni ya Kamati kwamba bado upo umuhimu wa kuzingatia ipasavyo ushauri uliotolewa na ambao haujafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mafungu yote matano inategemea kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 393,500,000,000. Kiasi kilichotarajiwa kukusanywa ni ongezeko la asilimia 7.04 ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambayo yalikuwa shilingi 367,600,000,000. Ongezeko hili linatarajiwa kuwa katika Fungu 28 ambalo lengo la makusanyo yake limeongezeka kwa asilimia 17 na Fungu 93 lengo la makusanyo yake limeongezeka kwa asilimia nne. aidha lengo la makusanyo kwa Fungu 29 na Fungu 14 ni sawa na lengo lilowekwa katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kuwa zipo sababu zilizochangia kupungua kwa makusanyo katika Fungu 63 na hivyo kusababisha Wizara kutofikisha lengo la makusanyo kwa Mwaka 2022/2023. Pamoja na changamoto hizo bado lengo la makusanyo ya fungu hilo limeongezeka kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Ni maoni ya Kamati kuwa, pamoja na nia njema ya kuongeza makusanyo ya Wizara, ni vyema Serikali izingatie changamoto zilizosababisha makusanyo kuwa chini ya lengo na ikalenga uhalisia katika kupanga makisio hayo. Mchanganuo wa lengo la

makusanyo kwa mafungu yote unaonekana katika Jedwali Na.4 katika taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kutokana na mchanganuo huo, ni dhahiri kuwa Fungu 28 - Jeshi la Polisi na Fungu 93 - Jeshi la Uhamiaji, ndiyo yanayotegemewa katika makusanyo ya Wizara hii kama inavyoonekana katika Grafu Na. 4 ya Taarifa ya Kamati. Kamati imebaini kuwa kwa miaka minne mfululizo mafungu hayo yamekuwa yakikadiriwa na kukusanya asilimia nyingi zaidi ikilinganishwa na mafungu mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inayapongeza mafungu hayo kwa kuendelea kuwa na mchango mkubwa na muhimu katika makusanyo. Hata hivyo, pamoja na pongezi hizi, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Fungu 93 - Jeshi la Uhamiaji bado halijapewa uzito unaostahili katika kupelekewa fedha za maendeleo licha ya kuwa ndilo linalokusanya zaidi ya mafungu mengine ya Wizara. Hadi mwezi Februari, 2023 fungu hilo lilikuwa limepokea asilimia 46.05 tu ya fedha iliyotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. ni rai ya Kamati kuwa Fungu 93 lipewe uzito unaostahili katika kutengewa na kupelekewa fedha za maendeleo kwa wakati ili kutekeleza miradi yake ya maendeleo kama ilivyoidhinishiwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi; maelezo yaliyotolewa na Wizara mbele ya Kamati yalibainisha kuwa katika mwaka wa fedha 2023/2024, Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inayoombwa kwa mafungu yote matano ni shilingi 1,293,820,903,000. Kati ya fedha hizo shilingi 678,657,328,000 sawa na asilimia 52.45, ni kwa ajili ya mishahara, shilingi 510,135,630,000 sawa na asilimia 39.43 ni matumizi mengineyo na shilingi 105,027,949,000 sawa na asilimia 8.12 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, kati ya fedha za maendeleo zinazoombwa, shilingi 100,333,364,000 sawa na asilimia 95.5 ni fedha za ndani na shilingi 4,694, 585,000 sawa na asilimia 4.6 ni fedha za nje.

Mgawanyo wa fedha za matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ni kama inavyoonekana kwenye Chati Namba moja katika taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini kuwa katika mwaka wa fedha 2022/2023 fedha za nje za utekelezaji wa miradi ya maendeleo zilikuwa asilimia 4.7, ambapo hadi kufikia Februari, 2023 fedha hizo hazikuwa zimetolewa. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 fedha za maendeleo kutoka nje ni asilimia 4.5. Kamati inatoa rai kwa serikali isitegemee fedha kutoka nje kwenye miradi ya maendeleo kwani fedha hizo hazina uhakika wa kupatikana na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukidhi masharti ya Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio hayo kwa kupitia kasma, vifungu na mafungu yote ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na kutekelezwa katika mwaka wa fedha unaoishia Juni, 2023. Uchambuzi huu umeainishwa katika ukurasa wa 32 na 33 katika taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo yaliyoainishwa hapo juu yanatokana na uchambuzi wa Kamati baada ya kupitia na kujadili randama za mafungu yote matano ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge lako lipokee maelezo hayo yatakayosaidia majadiliano kuhusu hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi mapema leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Ushauri wa Kamati; nianze na maoni ya Kamati. Kutokana na uchambuzi kama nilivyoeleza, Kamati inayo maoni yanayojenga msingi wa ushauri nitakoutoa. Naomba kubainisha maoni hayo kama ifuatavyo: -

i. Kitendo cha Jeshi la Magereza kuanza ujenzi wa Gereza na Ofisi za Jeshi hilo katika Wilaya ya Kilosa kwa kutumia fedha za fidia ni jambo la kupongezwa. Uamuzi huo umepelekea kuanza kwa ujenzi wa mradi kama ilivyopangwa. Pamoja na hivyo, uzingatiaji wa thamani halisi ya matumizi katika utekelezaji wa mradi ni jambo la kusisitizwa na kupewa uzito stahiki.

ii. Kitendo cha Vyombo vya Ulinzi na Usalama vilivyo chini ya wizara hii kutopewa fedha za maendeleo kwa wakati ni jambo

linaloathiri utendaji wa vyombo hivyo pamoja na utekelezaji wa miradi husika.

iii. kutokutolewa kwa wakati kwa fedha za miradi kunasababisha miradi kushindwa kutekelezwa na kukamilika kwa wakati na hivyo kutofikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa wakati Bunge linaidhinisha fedha za miradi kwa niaba ya wananchi.

iv. Juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali katika kuimarisha vyombo vya ulinzi na usalama chini ya Wizara hii ni jambo la kupongezwa. Ili kuendelea kuimarisha utendaji kazi mtiririko wa fedha kwa ajili ya vyombo hivyo ni suala la kuzingatiwa na kupewa umuhimu stahiki kwa kuzingatia mpango wa utekelezaji wa bajeti ya vyombo hivyo.

v. Uhaba wa vyombo vya usafiri na usafirishaji ni jambo linaloathiri utendaji kazi wa Majeshi yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

vi. Ujenzi wa Ofisi za Vyombo vya Ulinzi vilivyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ni muhimu ukazingatia maeneo makubwa yatakayokidhi miundombinu ya kisasa na mahitaji ya baadaye.

vii. Ukosefu na uchakavu wa vifaa na vitendea kazi kwa majeshi yaliyo chini ya Wizara hii kwa kiasi kikubwa unaathiri ufanisi wa vyombo hivi ikiwemo ukusanyaji wa maduhuli.

viii. Vyuo vya Mafunzo vinavyomilikiwa na Majeshi yaliyo chini ya Wizara hii vina miundombinu chakavu, duni na isiyokidhi hitaji la mafunzo ya kisasa. Hali hii inaathiri ubora wa mafunzo yanayotolewa na vyuo hivyo.

ix. Kukosekana kwa hati za maeneo yanayomilikiwa na majeshi yaliyo chini ya Wizara hii ni jambo linalochangia kuwavutia baadhi ya wananchi kuvamia maeneo hayo na baadaye kuibuka kwa migogoro ya umiliki.

x. Kutokupatikana kwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa wakati kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa vyombo vya ulinzi na usalama vilivyo chini ya Wizara hii ni jambo linaloathiri tija iliyokusudiwa na mpango wa mradi.

xi. Kitendo cha malipo ya stika za usalama barabarani kufanyika kwa njia ya fedha taslimu ni suala ambalo kwa namna moja linachangia kupotea kwa mapato kwani kunatoa fursa ya Askari wasio waaminifu kutumia utaratibu huo kwa maslahi yao binafsi.

xii. Kuhudumia wahamiaji haramu 2609 ambao wamemaliza kutumikia vifungo na bado wapo magerezani kunagharimu shilingi 2,348,100,000 kwa mwaka. Kiasi hicho kinatosha kujenga madarasa 117. Hali hiyo inaonesha umuhimu kwa Serikali kuendelea kutekeleza mkakati wa kuwarejesha wafungwa hao katika nchi zao ili kuelekeza fedha hizo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

xiii. Serikali imetoa zaidi ya asilimia 70 ya fedha za maendeleo kwa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)*. Kamati inashauri kiasi hicho cha fedha kiakisi uhalisia kwa mamlaka hiyo kuongeza kasi ya kuandikisha na kugawa Vitambulisho vya Taifa hasa ikizingatiwa kuwa vitambulisho hivyo kwa sasa vimeungwanishwa na huduma muhimu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa jumla; kwa msingi wa Maoni niliyotoa, ufuatao ni ushauri wa Kamati: -

i. Wizara iweke utaratibu wa kufuatilia mtiririko wa fedha za maendeleo na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mafungu yake yote matano;

ii. Serikali iendelee kuboresha hali ya vyombo vya usafiri na usafirishaji kwa Majeshi yaliyo chini ya Wizara hii. Kufanya hivyo, kutaboresha utendaji kazi wa majeshi haya;

iii. Serikali iendelee na mkakati wake wa kuboresha hali ya vifaa na vitendea kazi kwa Majeshi yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Kufanya hivyo kutaongeza ufanisi wa Majeshi hayo ikiwemo ukusanyaji wa maduhuli;

iv. Serikali iongeze kasi ya utekelezaji wa mkakati wa kupima na kupata hati za maeneo yote ya Majeshi ambayo hayajapimwa; kufanya hivyo kutaepusha migogoro baina ya wananchi na Majeshi.

v. Serikali izingatie umuhimu wa kutoa fedha za miradi ya maendeleo kama ilivyoidhinishwa na Bunge. Kwa kufanya hivyo, itasaidia kufanikisha utekelezaji wa miradi hiyo na kupatikana kwa tija ya miradi inayotekelezwa chini ya mafungu yote ya Wizara hii.

vi. Serikali iendelee kuviwezesha vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuajiri askari wengi zaidi ili kuimarisha utendaji kazi wa vyombo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushauri Mahsusi; Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

i. Jeshi la Zimamoto na Uokoaji liandae mpango kazi unaotekelezeka wa ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Zimamoto na Uokoaji kilichopo Chogo Handeni. Kufanya hivyo kutasaidia ujenzi wa chuo hicho kutengewa fedha na kujengwa kwa kuzingatia mpango husika.

ii. Ujenzi wa Ofisi za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji unaoendelea katika mikoa mbalimbali nchini uzingatie upatikanaji wa eneo kubwa ambalo litakidhi ujenzi wa miundombinu ya kisasa na mahitaji ya baadaye.

iii. Jeshi la Zimamoto na Ukoaji lijipange kutumia mbinu za kiteknolojia na za kisasa katika kupambana na majanga mbalimbali. Kufanya hivyo, kutasaidia jeshi hilo kutoa huduma katika miradi mikubwa ya kimkakati na kupambana na majanga kwa mbinu za kisasa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 28- Jeshi la Polisi.

i. Jeshi la Polisi liandae mpango maalumu wa ukarabati na uendelezaji miundombinu ya Chuo cha Polisi Moshi. Kufanya hivyo kutasaidia kutenga fedha, kukarabati na kuendeleza miundombinu kwa kuzingatia mpango husika.

ii. Serikali iweke utaratibu wa kuhakikisha kuwa malipo ya stika za usalama barabarani yanafanyika kupitia namba maalum za malipo *(control number)*.

iii. Askari wa Jeshi la Polisi wasimamiwe inavyostahili ili kuzingatia Sheria, taratibu, miiko, weledi na maadili ya Jeshi la Polisi katika utendaji kazi wao.

iv. Dhana ya Polisi Jamii itekelezwe kwa ukamilifu katika kupambana na uhalifu hususani katika makazi ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 29 - Jeshi la Magereza

i. Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iendelee kutekeleza mkakati wa kuwarejesha katika nchi zao wafungwa waliomaliza vifungo na bado wapo magerezani. Bila kufanya hivyo, hali hiyo itaendelea kuchangia msongamano Magerezani na kutumia fedha za walipakodi kuwahudumia.

ii. Pamoja na kuipongeza Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya kuendeleza na kujenga magereza mapya 12 katika mwaka wa fedha 2023/2024, bado kuna umuhimu kwa Serikali kutoa fedha hizo kwa kadri zitakavyoidhinishwa na Bunge. Aidha, upatikanaji wa fedha hizo ulingane na ratiba ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa ili kuwezesha tija inayokusudiwa.

iii. Jeshi la Magereza liandae mkakati wa kuanzisha na kutekeleza kilimo cha mazao ya chakula ikiwemo kilimo cha umwagiliaji. Mkakati huo uwe ni sehemu ya huduma ya urekebu na kujitosheleza kwa chakula.

iv. Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kutoa msamaha wa wafungwa 376 katika Sikukuu ya Muungano tarehe 26 Aprili, 2023. Msamaha uliotolewa kwa wafungwa umeipunguzia Serikali gharama ya takribani 940,000 kwa siku ambapo kwa mwaka ni shilingi 338,400,000. Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha zote zitakazoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka 2023/2024 kwa ajili ya vikao vya Bodi ya Taifa na za Mikoa za *Parole* ili wafungwa wengi zaidi wanaostahili kupewa msamaha kwa mujibu wa Sheria ya Parole wapunguzwe Magerezani na hatimaye kuokoa fedha za Serikali zinazotumika kuwatunza.

v. Serikali iliwezeshe Jeshi la Magereza kupata magari hususan kwa ajili ya kusafirisha mahabusu pamoja na magari kwa ajili ya shughuli za utawala, ambapo kwa sasa mahitaji halisi ni magari 800. Upatikanaji wa magari hayo, pamoja na mambo mengine, utasaidia mahabusu kupata nafasi ya kusikiliza kesi zao kwa wakati uliopangwa na hivyo kuamuliwa mapema.

vi. Jeshi la Magereza lishiriki kikamilifu katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kupanda miti na kuitunza katika magereza yote katika miji ambayo magereza hayo yapo. Aidha, kufanya hivyo kunaweza kuwa pia ni sehemu ya huduma ya urekebu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 51- Wizara.

i. Wizara iisimamie kwa karibu Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)* kuhakikisha kuwa inatekeleza majukumu yake ipasavyo ikiwemo kuongeza kasi ya uandikishaji na ugawaji wa Vitambulisho vya Taifa kuendana na mahitaji.

ii. Serikali ifanye mapitio ya Sheria ya Parole ili kubaini changamoto za kisheria zinazoathiri ufanisi na lengo la kutungwa kwake kwa madhumuni ya kufanya marekebisho.

iii. Wizara ifanye tathmini ya mfumo uliopo wa usajili wa jumuiya za kidini kwa lengo la kuona kama mfumo na utaratibu uliopo unakidhi mazingira ya sasa ambapo kumekuwa na jumuiya nyingi ambazo zimesajiliwa lakini zinaendesha shughuli zake kinyume na malengo ya yaliyokusudiwa.

iv. Serikali iandae mkakati maalumu wa kuwatafuta, kuwatambua na kuchukua hatua kwa Wakimbizi walio nje ya makazi na makambi ya wakimbizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 93 – Jeshi la Uhamiaji.

i. Jeshi la Uhamiaji liandae mpango wa ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya Chuo cha Uhamiaji Raphael Kubaga kilichopo kichaka miba, Mkinga - Tanga. Kufanya hivyo kutasaidia kutenga fedha na kuendeleza ujenzi kwa kuzingatia mpango huo.

ii. Serikali iendelee kutekeleza mkakati wake wa kuwarejesha makwao wafungwa wahamiaji haramu waliomaliza kutumikia vifungo vyao na bado wapo magerezani.

iii. Serikali iliwezeshe Jeshi la Uhamiaji kupata vyombo vya usafiri ili kuwabaini wahamiaji wasio na vibali na kuwachukulia hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kuwalipisha ada husika na faini.

iv. Serikali iandae mkakati wa kuliwezesha Jeshi la Uhamiaji vifaa vya kisasa ikiwemo kupata boti kwa ajili ya kufanya misako na doria katika Mwambao wa Bahari ya Hindi ambayo imekuwa ni njia kubwa ya kupitisha wahamiaji haramu.

v. Serikali ichukue juhudi za makusudi za kudhibiti mianya ya njia zisizo rasmi zaidi ya 1000 katika mikoa mbalimbali ya mipakani. Kufanya hivyo ni sehemu ya jitihada za muda mrefu za kudhibiti uingiaji wa wahamiaji haramu nchini.

vi. Ujenzi wa Ofisi za Jeshi la Uhamiaji unaondelea katika mikoa mbalimbali nchini uzingatie upatikanaji wa eneo kubwa lenye kukidhi mahitaji ya sasa na baadaye na jengo litakalokidhi matumizi ya vifaa vya kisasa vya kiteknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha taarifa hii. Aidha, Nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo orodheshwa katika taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa *Engineer* Hamadi Yusuf Masauni, Naibu Waziri, Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini, Katibu Mkuu Ndugu Kasper Mmuya pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, *ndc*, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati ya Bunge. Aidha, nawashukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Michael Chikokoto, *ndc,* Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Gerald Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Omary Magwinza na Bi. Victoria Mizengo, wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii ili lijadili na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI (FUNGU 14, 28, 29, 51 NA 93) KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SURA YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika**, awali ya yote kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuvisimamia na kuviimarisha vyombo vyote vya ulinzi na usalama nchini.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na kuliomba Bunge liipokee taarifa hii, kuikubali na kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hiyo kama ilivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, msingi wa taarifa hii ni majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (3) na Kifungu cha 7 (1) (a), cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, pamoja na masharti ya Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Bunge. Kwa mujibu wa Kanuni hizo, kabla ya taarifa ya utekelezaji na Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kujadiliwa Bungeni, zilipaswa kuchambuliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Naomba kulijulisha Bunge lako kuwa, uchambuzi huo ulifanyika baada ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara hii kama ilivyoelekeza Kanuni ya 117 (1) hadi 117 (2) ya Kanuni za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kwa madhumuni ya kuweka bayana mawanda ya Taarifa hii, nalikumbusha Bunge lako tukufu kuwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inajumuisha
Mafungu matano (5) ya kibajeti yafuatayo:-

1) Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji;

2) Fungu 28 - Jeshi la Polisi;

3) Fungu 29 - Jeshi la Magereza;

4) Fungu 51 - Wizara (Makao Makuu) ikiwemo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA); na

5) Fungu 93 - Jeshi la Uhamiaji.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu 6 zifuatazo:- Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi; Sehemu ya Pili ni Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo; Sehemu ya Tatu ni Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa

Mwaka wa Fedha 2022/2023; Sehemu ya Nne ni Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; Sehemu ya Tano ni Maoni na Ushauri wa Kamati; na Sehemu ya Sita ni Hitimisho.

## SURA YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua miradi minne (4) ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara hii katika Mikoa ya Morogoro, Tanga na Manyara.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu hii ya Taarifa inaeleza mambo makuu mawili ambayo ni:-

1) Muhtasari wa maelezo ya Miradi iliyotekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023; na

2) Uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Lengo la sehemu hii ni kuliwezesha Bunge kufuatilia hali ya utekelezaji na upatikanaji wa fedha lilizoziidhinisha na kupata mantiki ya uamuzi wake wakati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii.

### 2.1 Maelezo Kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara hii ilipaswa kutekeleza jumla ya miradi 12 katika Mikoa mbalimbali nchini. Hata hivyo, kwa madhumuni ya masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilitembelea miradi minne inayotekelezwa katika Mikoa ya Morogoro, Tanga na Manyara. Naomba kueleza kwa muhtasari kuhusu miradi hiyo kama ifuatavyo:-

### 2.1.1 Mradi Na. 6305 – Ujenzi wa Gereza la Wilaya na Ofisi za Magereza, Kilosa

Mradi huu unahusu ujenzi wa Gereza la Wilaya na Ofisi za Jeshi la Magereza katika Wilaya ya Kilosa, Mkoani Morogoro. Mradi huu unatekelezwa chini ya Fungu 29 -Jeshi la Magereza.

### 2.1.2 Mradi Na. 6582 – Ujenzi wa Chuo cha Zimamoto na Uokoaji Chogo, Handeni – Tanga

Mradi huu unahusu ujenzi wa majengo na miundombinu kwa ajili ya mafunzo ya Maafisa na Askari katika Chuo cha Zimamoto na Uokoaji kilichopo Chogo, Handeni. Mradi huu unatekelezwa chini ya Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

### 2.1.3 Mradi Na. 6582 – Ujenzi wa Ofisi za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Manyara;

Mradi huu unahusu ujenzi wa Ofisi za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika Mkoa wa Manyara mradi huu unatekelezwa chini ya Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

### 2.1.4 Mradi Na. 6302 – Ujenzi wa nyumba 12 katika Chuo cha Uhamiaji, Boma Kichakamiba – Wilayani Mkinga

Mradi huu unahusu ujenzi wa nyumba 12 za watumishi katika chuo cha Uhamiaji kilichopo Boma Kichakamiba Mkoani Tanga. Mradi huu unatekelezwa chini ya Fungu 93 – Jeshi la Uhamiaji.

## 2.2 Matokeo ya Ukaguzi

**Mheshimiwa Spika**, baada ya muhtasari wa maelezo kuhusu miradi ya maendeleo iliyokaguliwa, naomba kutoa taarifa kuhusu matokeo ya ukaguzi na uchambuzi wake kama ifuatavyo:-

### 2.2.1 Fungu 29- Jeshi la Magereza

**(a) Mradi wa Ujenzi wa Gereza la Wilaya na Ofisi ya Jeshi la Magereza Kilosa**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa, mradi huo ulianza kutekelezwa rasmi Februari, 2022 kwa kutumia utaratibu wa *Force Account*. Wakati wa ukaguzi, Kamati ilielezwa kuwa hadi kukamilika kwake ujenzi wa mradi utagharimu **Shilingi Bilioni 8.3**. Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Jeshi lilitengewa Shilingi **757,200,108/=** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa mradi huu. Hadi wakati Kamati inatembelea mradi Jeshi halikuwa limepokea Fedha yoyote kwa ajili ya mradi.

Kamati ilielezwa kuwa fedha inayotumika katika ujenzi ni sehemu ya fidia ambayo Jeshi limepokea kutokana na eneo lake kutwaliwa kwa ajili ya ujenzi wa SGR; ambapo Jeshi lilipwa kiasi cha **Shilingi 461,497,022.16.**

Wakati wa ukaguzi Kamati ilielezwa kuwa mradi una awamu nne za utekelezaji; ambapo hadi wakati Kamati inakagua awamu ya kwanza ilikuwa imekamilika na kiasi cha **Shilingi 410,326,554** kimeshatumika**.**

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa ukaguzi Kamati ilibaini kuwa mradi huu unakabiliwa na changamoto zifuatazo;-

1) Ukosefu wa fedha; Hadi Kamati inatembelea mradi huu tarehe 14 Machi, 2023 ikiwa ni muda wa miezi mitatu kabla mwaka wa fedha 2022/2023 haujaisha, fedha za kuendeleza mradi huu zilikuwa bado hazijapokelewa;

2) Ubovu wa barabara inayoelekea katika mradi; na

3) Ukosefu wa nishati ya umeme katika eneo la mradi.

### 2.2.2 Fungu 93- Idara ya Uhamiaji

**Ujenzi wa nyumba 12 Chuo cha Uhamiaji, Boma Kichakamiba – Wilayani Mkinga**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu katika mwaka wa fedha 2022/2023 ulitengewa kiasi cha **Shilingi 600,000,000.00** Hadi wakati kamati inatembelea mradi Tarehe 16 Machi, 2023 ujenzi wake haukuwa umeanza. Kamati ilielezwa kwamba sababu za kutoanza ujenzi wa mradi ni kutopokelewa kwa fedha kutoka Hazina. Kamati ilidadisi kujua kama Wizara imekamilisha taratibu zote na kuomba fedha

Hazina; ambapo ilielezwa kuwa taratibu zote zimekamilika na fedha kuombwa Hazina.

**Mheshimiwa Spika**, mbali ya kwamba kamati ilikwenda kukagua mradi wa ujenzi wa nyumba za watumishi; lakini ilibaini chuo hiki kinakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo;-

1) Uhaba wa maji safi na salama kwa matumizi yote ya binadamu na Wanyama;

2) Upungufu wa Vifaa Tiba katika Zahanati ikiwa na hitajio la Jengo la Mama na Mtoto ili kutoa huduma za Afya kwa Watumishi Katika Chuo na Wananchi wanaozunguka chuo hicho;

3) Uhaba wa Miundombinu ya Umeme;

4) Uwanja wa Gwaride unahitaji maboresho kwa kiwango cha lami au zege;

5) Miundombinu ya barabara ndani ya Chuo bado ni duni; na

6) Ukosefu wa vyombo vya usafiri ikiwemo mabasi na magari ya utawala.

**Mheshimiwa Spika**, mradi wa ujenzi wa Nyumba za watumishi katika chuo hiki ni moja ya mikakati ya kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi. Kutokutolewa kwa fedha za ujenzi wa mradi huu kunasababisha watumishi hao kuendelea kufanya kazi katika mazingira ambayo si rafiki na hivyo kuathiri ufanisi wa kazi zao.

### 2.2.3 Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

#### a) Ujenzi wa Chuo cha Zimamoto na Uokoaji Chogo, Handeni – Tanga

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa mradi huu ulipaswa kuanza kutekelezwa tangu tarehe 21 Novemba, 2022 kwa uratatibu wa *Force Account* na ungekamilika tarehe 30 Oktoba, 2023. Aidha, mradi huu hadi kukamilika kwake unatarajiwa kutumia jumla ya

**Shilingi 1,553,000,000/=**. Ujenzi unajumuisha Jengo la Utawala, Jengo la Ukumbi wa Mihadhara, Jengo la Maktaba na Jengo la Amari.

**Mheshimiwa Spika,** Hadi wakati Kamati inatembelea mradi huu tarehe 15 Machi, 2023 ikiwa imebaki miezi mitatu kabla Mwaka wa Fedha 2022/2023 haujaisha; fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa mradi huu hazikuwa zimepokelewa.

**b) Ujenzi wa Ofisi za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Manyara;**

Mradi huu ulitarajiwa kuanza Tarehe 21 Novemba, 2022 na kukamilika Tarehe 30 Oktoba, 2023. Aidha, hadi kukamilika kwake mradi ulitengewa jumla ya **Shilingi 600,000,000/=** na utatekelezwa kwa utaratibu wa *Force Account.* Aidha, hadi Kamati inatembelea mradi huu Tarehe 19 Machi, 2023 ujenzi haukuwa umeanza. Kamati ilielezwa kuwa kutokuanza kwa ujenzi kulitokana na kutokupokelewa fedha za ujenzi kutoka Hazina; japokuwa Jeshi limekamilisha taratibu zote na kuomba fedha Hazina.

## SURA YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

### 3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipofanya uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, ilizingatia makusanyo ya maduhuli ikilinganishwa na lengo lililokusudiwa, upatikanaji wa fedha za matumizi kwa shughuli zilizopangwa kutekelezwa hususan fedha kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mafungu yote Matano ya Wizara.

Vilevile, Kamati ilizingatia taarifa muhimu na za ziada zilizopatikana kupitia mahojiano wakati wa vikao vya Kamati. Uchambuzi huo ni kama ifuatavyo:-

### 3.1.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara ikijumuisha Mafungu yake yote matano (5) ilikadiria kukusanya mapato ya **Shilingi 356,600,000,000/=** ikilinganishwa na **shilingi 331,591,585,600/=** zilizokadiriwa kukusanywa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Kamati ilielezwa kuwa, hadi kufikia Mwezi Februari 2023, kiasi kilichokusanywa kilikuwa ni **Shilingi bilioni 199,834,373,735**/= sawa na **asilimia 56** ya lengo la mwaka lililopangwa**.** Kamati ilibaini kuwa makusanyo hayo yameongezeka kwa **Shilingi Bilioni 24,794,373,735/=** sawa na **asilimia 14.16** ikilinganishwa na makusanyo yaliyokusanywa katika kipindi kama hicho kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ambayo yalikuwa **Shilingi Bilioni 174.04**.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kufanya uchambuzi wa kina, Kamati ilibaini kuwa Mafungu yote matano (5) ya Wizara yalikusanya mapato kwa kiwango cha kuridhisha ikilinganishwa na makusanyo ya kipindi kama hiki kwa kila Fungu katika Mwaka wa Fedha 2021/2022.


**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu mwenendo wa makusanyo kwa kipindi cha miaka mitano na kufanya ulinganisho wa makusanyo hayo kwa miaka mitano kuanzia Mwaka 2018/2019. Kamati ilibaini kuwa makusanyo ya Mapato yamekuwa yakiongezeka kila Mwaka hadi Mwaka 2019/2020 na kupungua katika Mwaka wa fedha 2020/2021. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa changamoto mbalimbali ikiwemo ukosefu wa vitendea kazi, uchakavu wa vitendea kazi na uhaba wa rasilimaliwatu ni kati ya sababu zilizochangia makusanyo hayo kupungua.

**Mheshimiwa Spika,** Mwenendo huo wa Makusanyo unadhihirika katika **Jedwali Na. 1 & 2** na **Grafu Namba 1** hapa chini.

**Jedwali Na. 1: Mwenendo wa Makusanyo ya Wizara 2018/2019 – 2022/2023**

| MWAKA | 2018/2019 | 2019/2020 | 2020/2021 | 2021/2022 | 2022/2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| MAKUSANYO | 185.53 | 229.81 | 149.65 | 175.05 | 199.83 |

**Grafu Na. 1: Mwenendo wa Makusanyo ya Wizara 2018/2019 - 2022/2023**




***Chanzo: Randama za Wizara 2018/2019 - 2022/2023***

**Mheshimiwa Spika**, vilevile Kamati ilifanya uchambuzi na kuainisha mchanganuo wa makusanyo kwa kila Fungu hadi kufikia mwezi Februari, 2023 ikilinganishwa na lengo la Mwaka lililowekwa. Aidha, Kamati ilifanya ulinganisho wa Makusanyo yaliyopatikana hadi kufikia Mwezi Februari 2023 na Makusanyo yaliyopatikana katika kipindi kama hicho, Mwaka 2022 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 2** na **Grafu Na. 2** hapa chini.


**Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Mapato hadi kufikia Februari 2023**

| FUNGU | MAKADIRIO 2022/2023 | % YA JUMLA YA LENGO | MAKUSANYO FEB 2023 | % YA JUMLA YA MAKUSANYO |
|---|---|---|---|---|
| 14 – Zimamoto | 11,000,000,000 | 3 | 7,136,168,341.49 | 3.57 |
| 28 – Polisi | 94,500,000,000 | 25.8 | 58,808,408,547.39 | 29 |
| 29 – Magereza | 1,500,000,000 | 0.4 | 2,063,948,831.62 | 1.0 |
| 51- Wizara | 500,000,000 | 0.10 | 336,000,000 | 1.12 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 93- Uhamiaji | 260,100,000,00 0 | 70.7 | 131,489,848,014.36 | 65.8 |
| **JUMLA** | **367,600,000,00 0** | **100** | **199,834,373,735** | **100** |

***Chanzo: Randama ya Wizara 2022/2023***

**Grafu Na. 2: Ulinganisho wa Makusanyo kwa Mwaka wa Fedha**




***Chanzo: Randama ya Wizara 2020/2021na 2021/2022***

**Mheshimiwa Spika**, katika mchanganuo huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

**(a) Makusanyo ya Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto,** yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 3** lakini Taarifa ya Makusanyo ilionesha kuwa Fungu 14 limechangia kwa **asilimia 3.57** ya kiasi kilichokusanywa;

**(b) Makusanyo ya Fungu 28 - Jeshi la Polisi,** yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 25.8** na Taarifa ya Makusanyo ilionesha kuwa Fungu 28 limechangia kwa **asilimia 29** ya kiasi kilichokusanywa;

**(c) Makusanyo ya Fungu 29 - Jeshi la Magereza,** yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 0.4** na Fungu hilo limechangia kwa **asilimia 1.0** ya kiasi kilichokusanywa;

**(d) Makusanyo ya Fungu 51 - Wizara,** yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 0.10** na Taarifa ya Makusanyo

ilionesha Fungu hilo limechangia kwa **asilimia 1.12** ya kiasi kilichokusanywa;

**(e) Makusanyo ya Fungu 93 - Jeshi la Uhamiaji,** yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 70.7** lakini Taarifa ya Makusanyo ilionesha kuwa Fungu hilo limeshachangia asilimia **65.8** ya kiasi kilichokusanywa.

**Mheshimiwa Spika**, ulinganisho huo wa makadirio ya makusanyo kwa kila Fungu ikilinganishwa na mapato halisi ya kila Fungu, umeisaidia Kamati kubaini kuwa Jeshi la Uhamiaji ndilo linalochangia kwa asilimia kubwa katika makusanyo yote ya Wizara. Hadi mwezi Februari, 2023 Wizara ilikuwa imekusanya **asilimia 54** ya lengo; ingawa kwa kipindi hicho angalau wangekuwa wamefikia **asilimia 65** ya lengo. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa kutofikiwa kwa lengo la makusanyo kumechangiwa na sababu mbalimbali ikiwemo ukosefu wa vitendea kazi, uchakavu wa vitendea kazi na uhaba wa rasilimaliwatu.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi uliofanyika, Kamati ina maoni kuwa mwenendo wa makusanyo kwa Mwaka huu wa fedha ni wa kuridhisha kwani kiujumla Wizara kwa mafungu yote imekusanya **asilimia 54** ya lengo lililowekwa.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na mwenendo wa makusanyo ya Mapato kwa Mwaka huu kuwa wa kuridhisha ni dhahiri kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kufikiwa kwa lengo lilowekwa. Pamoja na kwamba ukusanyaji unaridhisha bado ukusanyaji wa maduhuli unakabiliwa na changamoto mbalimbali kama ilivyoelezwa katika taarifa hii.

Ni rai ya Kamati kuwa Serikali itazingatia changamoto hizo na kupanga makadirio ya makusanyo kwa kuzingatia uhalisia katika Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**3.2 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika,** Katika Bunge la Kumi na Moja Kamati iliendelea kuishauri Serikali kupitia Hazina kuona umuhimu wa kutoa fedha hizo kama zinavyoidhinishwa na Bunge. Hata hivyo utengwaji wa fedha za maendeleo na mtiririko wa upatikanaji wa fedha hizo

uliendelea kuwa si wa kuridhisha kwa baadhi ya Mafungu hasa Fungu 29 na Fungu 14 na hivyo kuathiri ratiba ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo hususan inayohusu Ujenzi wa Chuo cha Zimamoto kilichopo Chogo, Handeni Mkoani Tanga, Ujenzi wa Ofisi za Zimamoto katika Mikoa mbalimbali hapa nchini, Ujenzi na ukarabati wa Magereza pamoja na kuimarisha usalama magerezani ikiwemo ununuzi na usimikaji wa vifaa maalum vya ulinzi na usalama magerezani.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia changamoto hiyo, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kufanya ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na kiasi cha fedha kilichopokelewa hadi kufikia Mwezi Februari, 2023. Kupitia uchambuzi huo, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

1) Hadi kufikia Mwezi Februari 2023, Wizara ilikuwa imepokea **asilimia 62.5** ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara.

2) Kati ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara hadi kufikia mwezi Februari 2023, **asilimia 39.4** ilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo, **asilimia 51.4** ilikuwa ni mishahara na **asilimia 7.97** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

3) Hadi kufikia Mwezi Februari 2023, Asilimia ya fedha za maendeleo zilizotolewa kwa kila Fungu ilikuwa kama ifuatavyo: Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji - **asilimia 20;** Fungu 28 - Jeshi la Polisi - **asilimia 36.2**; Fungu 29 - Jeshi la Magereza - **asilimia 0.5;** Fungu 51- Wizara - **asilimia 63.5** na Fungu 93 – Jeshi la Uhamiaji lilipokea **asilimia 46.**

4) Hadi kufikia Mwezi Februari, 2023 Fungu 29 lilikuwa limepokea asilimia ndogo ya fedha za miradi ya maendeleo kuliko Mafungu yote ya Wizara hii; na


5) Hadi kufikia Mwezi Februari, 2023, ni Fungu 51 tu lilolopokea fedha za maendeleo **zaidi ya asilimia 50;** na Fungu 14, 28, 29 na 93 yamepokea fedha za maendeleo **chini ya asilimia 50.**

**Mheshimiwa Spika**, mchanganuo wa upatikanaji wa fedha za mishahara, matumizi mengineyo na maendeleo, umeoneshwa dhahiri katika **Jedwali Na. 3** na **Grafu Na. 3** hapa chini.

**Jedwali Na. 3: Mchanganuo wa upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2022/2023 kwa matumizi ya Wizara**

| Matumizi | Fedha iliyotengwa | Fedha iliyopokelewa hadi Februari, 2023 | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Mengineyo | 471,249,055,000 | 298,468,903,924.02 | 63.3 |
| Mishahara | 600,219,122,000 | 389,103,672,716.25 | 64.8 |
| Maendeleo | 140,412,900,000 | 60,373,163,768.31 | 43 |

**Grafu Na. 3: Mchanganuo wa upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2022/2023 kwa ajili ya Matumizi ya Wizara**




***Chanzo: Randama ya Wizara 2023/2024***

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa mtiririko wa fedha kwa ajili ya Mishahara na Matumizi Mengineyo kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ni wa kuridhisha kwani imepokea **zaidi ya asilimia 50** ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya mishahara na mengineyo. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa mtiririko wake sio wa kuridhisha kwani Fungu 14, 28, 29 na 93 yamepata fedha za maendeleo **chini ya asilimia 50.**

**Mheshimiwa Spika,** Ili idhini ya Bunge kwa bajeti ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya Maendeleo iwe na tija, upatikanaji wa fedha hizo kwa wakati na kwa kadiri inavyostahili, ni jambo muhimu kufanikisha utekelezaji huo kwa muda uliopangwa. Hivyo, ni rai ya Kamati kuwa Serikali itoe fedha hizo kwa Mafungu yote kwa ukamilifu kufikia tarehe 30 Juni, 2022 ili kutoathiri ratiba ya utekelezaji wa miradi iliyopangwa.

### 3.3 Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kamati ilishauri masuala mbalimbali. Naomba kuliarifu Bunge kuwa, taarifa ya Mtoa Hoja ilionesha kwamba, Serikali imezingatia sehemu ya ushauri kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 1** cha Taarifa hii.

Mfano wa ushauri wa Kamati uliozingatiwa ni kuhusu Serikali kulipa uzito wa kipekee suala la uhitaji wa watumishi katika Idara na Majeshi yaliyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Taarifa iliyowasilishwa ilieleza kuwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Serikali imetoa kibali cha ajira kwa Majeshi hayo; ambapo Fungu 14 limeajiri Askari wapya 79, Fungu 28 Askari wapya 4118, Fungu 29 Askari wapya 1241 na Fungu 93 Askari wapya 521.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na uzingatiaji mzuri wa ushauri, upo ushauri ambao utahitaji kufanyiwa kazi zaidi na Serikali. Mathalani, ushauri kuhusu Serikali kutoa fedha za maendeleo kwa wakati kwa mafungu yote ili kutekeleza kwa ufanisi miradi inayopangwa.

## SURA YA NNE

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

### 4.1 Mpango wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** ili kujiridhisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati

ilipitia majukumu makuu ya Wizara na kubaini kuwa makadirio ya mapato na matumizi yanayopendekezwa yanalenga kuimarisha utendaji kazi na ufanisi wa Wizara katika utekelezaji wa majukumu hayo, ambayo ni pamoja na:-

1) Kuendelea kusimamia uwepo wa amani na usalama wa Raia na mali zao;

2) Kuendelea kusajili na kutoa Vitambulisho vya Taifa kwa Watanzania, Wakimbizi na Wageni;

3) Kuendelea kuzuia na kupeleleza makosa ya jinai na makosa ya usalama barabarani;

4) Kuimarisha shughuli za kilimo na mifugo ikiwa ni pamoja na kutekeleza mkakati wa kujitosheleza kwa chakula;

5) Kufanya mapitio ya Sera na Sheria mbalimbali zinazohusu Wizara ili kuongeza ufanisi katika utendaji wa Wizara; na

6) Kuimarisha na kuendeleza mapambano dhidi ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipopitia majukumu hayo kwa kulinganisha na Bajeti inayoombwa, ilibaini kuwa utendaji kazi na ufanisi wa Wizara katika kutekeleza majukumu yake utaimarika endapo Serikali itatenga fedha za kutosha na kutoa fedha hizo kadri zitakavyoidhinishwa na Bunge kwa ukamilifu na kwa wakati kwa kuzingatia Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara.

**4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka 2023/2024**

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mafungu yote matano inategemea kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 393,500,000,000**. Kiasi kinachotarajiwa kukusanywa ni ongezeko la **asilimia 7.04** ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ambayo yalikuwa **Shilingi 367,600,000,000**. Ongezeko hili linatarajiwa kuwa katika Fungu 28 na Fungu 93. Ambapo Fungu 28 lengo la makusanyo yake limeongezeka kwa **asilimia 17 na Fungu**

**93** lengo la makusanyo yake limeongezeka kwa **asilimia 4.** Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa lengo la makusanyo kwa Fungu 29 na Fungu 14 ni sawa na lengo lilowekwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilirejea sababu zilizochangia Wizara kutofikisha lengo la makusanyo kwa Mwaka 2022/2023 na kubaini kuwa elimu ya usalama barabarani, uchakavu wa vitendea kazi, upungufu wa rasilimaliwatu, na upungufu wa vitendea kazi zilikuwa miongoni mwa sababu zilizochangia kupungua kwa makusanyo katika Fungu 93. Pamoja na changamoto hizo bado lengo la makusanyo ya Fungu hilo limeongezeka kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Ni maoni ya Kamati kuwa, pamoja na nia njema ya kuongeza makusanyo ya Wizara, ni vyema Serikali izingatie changamoto zilizosababisha makusanyo kuwa chini ya lengo na ikalenga uhalisia katika kupanga makisio hayo. Mchanganuo wa lengo la makusanyo kwa Mafungu yote unaonekana katika **Jedwali Na. 4** hapa chini.

**Jedwali Na. 4: Makadirio ya Mapato**

| FUNGU | MAKADIRIO 2022/2023 | % YA JUMLA YA LENGO | MAKADIRIO 2023/2024 | % YA JUMLA YA LENGO |
|---|---|---|---|---|
| Fungu 14 | 11,000,000,000 | 3 | 11,000,000,000 | 2.8 |
| Fungu 28 | 94,500,000,000 | 25.7 | 110,500,000,000 | 28.08 |
| Fungu 29 | 1,500,000,000 | 0.4 | 1,500,000,000 | 0.38 |
| Fungu 51 | 500,000,000 | 0.10 | 500,000,000 | 0.13 |
| Fungu 93 | 260,100,000,000 | 70.8 | 270,000,000,000 | 68.61 |
| **JUMLA** | **367,600,000,000** | **100** | **393,500,000,000** | **100** |

***Chanzo: Randama ya Wizara 2023/2024***

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini yafuatayo:-

(a) **Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji** linategemewa kukusanya **asilimia 2.8** ya makadirio ya makusanyo

ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2022/2023 ambapo lilitegemewa kukusanya **asilimia 3** ki-uwiano ikiwa ni **pungufu kwa asilimia 0.2;**

**(b)** **Fungu 28 - Jeshi la Polisi** linategemewa kukusanya **asilimia 28.08** ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2022/2023 ambapo lilitegemewa kukusanya **asilimia 27.5** kiasi ambacho ki-uwiano ni **ongezeko la asilimia 0.5;**

**(c)** **Fungu 29 - Jeshi la Magereza** linategemewa kukusanya **asilimia 0.38** ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na Mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo ilitegemewa kukusanya **asilimia 0.4** ambayo ki-uwiano ni **pungufu ya asilimia 0.02;**

**(d)** **Fungu 51- Wizara** inategemewa kukusanya **asilimia 0.13** ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2022/2023 ambapo lilitegemewa kukusanya **asilimia 0.10** ambayo kiuwiano ni ongezeko la **asilimia 0.03;** na

**(e)** **Fungu 93 - Jeshi la Uhamiaji** linategemewa kukusanya **asilimia 68.61** ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2022/2023 ambapo ilitegemewa kukusanya **asilimia 70.8** ambayo kiuwiano ni pungufu kwa **asilimia 1.8.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa ufafanuzi huo, ni dhahiri kuwa Fungu 28 - Jeshi la Polisi na Fungu 93 - Jeshi la Uhamiaji, ndio yanayotegemewa katika makusanyo ya Wizara hii kama inavyoonekana katika **Grafu Na. 4** ya Taarifa hii. Kamati imebaini kuwa kwa miaka minne mfululizo Mafungu hayo yamekuwa yakikadiriwa na kukusanya asilimia nyingi zaidi ikilinganishwa na Mafungu mengine.

**Grafu Na. 4: Ulinganisho wa Makadirio ya Makusanyo 2022/2023-2023/2024**




***Chanzo: Randama za Wizara 2022/2023 na 2023/2024***

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inayapongeza Mafungu hayo kwa kuendelea kuwa na mchango mkubwa na muhimu katika makusanyo. Hata hivyo, pamoja na pongezi hizi, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Fungu 93 - Jeshi la Uhamiaji bado halijapewa uzito unaostahili katika kupelekewa fedha za maendeleo licha ya kuwa ndio inakusanya zaidi ya Mafungu mengine ya Wizara. Hadi mwezi Februari, 2023 Fungu hilo lilikuwa limepokea **asilimia 46.05** tu ya fedha iliyotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, ni rai ya Kamati kuwa Fungu 93 lipewe uzito unaostahili katika kutengewa na kupelekewa fedha za maendeleo kwa wakati ili kutekeleza miradi yake ya maendeleo kama ilivyoidhinishiwa na Bunge.

**4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi**

**Mhesimiwa Spika,** maelezo yaliyotolewa na Wizara mbele ya Kamati yalibainisha kuwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inayoombwa kwa Mafungu yote matano ni **Shilingi 1,293,820,903,000/=** Kati ya fedha hizo **Shilingi 678,657,324,000/=** sawa na **asilimia 52.45,** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi 510,135,630,000** sawa na **asilimia 39.43** ni Matumizi Mengineyo na **Shilingi 105,027,949,000/=** sawa na **asilimia 8.12** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, kati ya fedha za maendeleo zinazoombwa, **Shilingi 100,333,364,000/=** sawa na **asilimia 95.5** ni fedha za ndani na **Shilingi 4,694,585,000** sawa na **asilimia 4.6** ni fedha za nje.

Mgawanyo wa fedha za matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ni kama inavyoonekana kwenye **Chati Na. 1** hapa chini.

**Chati Na. 1: Mgawanyo wa Fedha za Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**




***Chanzo: Randama ya Wizara 2023/2024***

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini kuwa Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, fedha za nje za utekelezaji wa miradi ya maendeleo zilikuwa **asilimia 4.7** ambapo hadi kufikia Februari, 2023 fedha hizo hazikuwa zimetolewa. Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 fedha za maendeleo kutoka nje ni **asilimia 4.5**. Kamati inatoa rai kwa serikali isitegemee fedha kutoka nje kwenye miradi ya maendeleo kwani fedha hizo hazina uhakika wa kupatikana na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio hayo kwa kupitia Kasma, Vifungu na Mafungu yote ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha unaoishia Juni, 2023. Katika uchambuzi huo Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

(a) Bajeti inayoombwa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 imeongezeka kwa **asilimia 7** ikilinganishwa na Bajeti iliyotengwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Ongezeko hili lipo katika Mishahara kwa **asilimia 13** na **asilimia 8.25** kwa matumizi mengineyo;

(b) Bajeti inayoombwa kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo imepungua kwa **asilimia 25** ikilinganishwa na Bajeti hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

(c) Bajeti ya Maendeleo inayoombwa imepungua kwa **asilimia 25;** ambapo **Fungu 28** imepungua kwa **asilimia 16.33, Fungu 29** kwa **asilimia 23.4, Fungu 51** kwa **asilimia 32.75** na Fungu 93 kwa **asimila 32.65**

(d) Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kiasi cha fedha za maendeleo kilichotengwa ni sawa na kiasi cha fedha kilichotengwa katika mwaka wa fedha 2022/2023;

(e) Fedha za Matumizi Mengineyo zimeongezeka kwa Mafungu yote ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ambapo: Fungu 14 Jeshi la Zimamoto - imeongezeka kwa **asilimia 8.33,** Fungu 28 - Jeshi la Polisi imeongezeka kwa **asilimia 6.70** Fungu 29 - Jeshi la Magereza imeongezeka kwa **asilimia 7.03**, Fungu 51 - Wizara kwa **asilimia 25.5**, na Fungu 93 - Uhamiaji kwa **asilimia 16.45.**

**Mheshimiwa Spika,** maelezo yaliyoainishwa hapo juu yanatokana na uchambuzi wa Kamati baada ya kupitia na kujadili Randama za Mafungu yote matano ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, naomba Bunge lako lipokee maelezo hayo yatakayosaidia majadiliano kuhusu hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi mapema leo hii.

## SURA YA TANO

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

## 5.1 Maoni ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi kama nilivyoeleza, Kamati inayo maoni yanayojenga msingi wa ushauri nitakoutoa. Naomba kubainisha maoni hayo kama ifuatavyo:-

1) Kitendo cha Jeshi la Magereza kuanza ujenzi wa Gereza na Ofisi za Jeshi hilo katika Wilaya ya Kilosa kwa kutumia fedha za fidia ni jambo la kupongezwa. Uamuzi huo umepelekea kuanza kwa ujenzi wa mradi kama ilivyopangwa. Pamoja na hivyo, uzingatiaji wa thamani halisi ya matumizi katika utekelezaji wa mradi ni jambo la kusisitizwa na kupewa uzito stahiki.

2) Kitendo cha Vyombo vya Ulinzi na Usalama vilivyo chini ya wizara hii kutopewa fedha za maendeleo kwa wakati ni jambo linalooathiri utendaji wa vyombo hivyo pamoja na utekelezaji wa miradi husika.

3) kutokutolewa kwa wakati kwa fedha za miradi kunasababisha miradi kushindwa kutekelezwa na kukamilika kwa wakati na hivyo kutofikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa wakati Bunge linaidhinisha fedha za miradi kwa niaba ya wananchi.

4) Juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali katika kuimarisha vyombo vya ulinzi na usalama chini ya Wizara hii ni jambo la kupongezwa. Ili kuendelea kuimarisha utendaji kazi mtiririko wa fedha kwa ajili ya vyombo hivyo ni suala la kuzingatiwa na kupewa umuhimu stahiki kwa kuzingatia mpango wa utekelezaji wa Bajeti ya vyombo hivyo.

5) Uhaba wa vyombo vya usafiri na usafirishaji ni jambo linaloathiri utendaji kazi wa Majeshi yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

6) Ujenzi wa Ofisi za Vyombo vya Ulinzi vilivyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ni muhimu ukazingatia maeneo makubwa yatakayokidhi miundombinu ya kisasa na mahitaji ya baadae.

7) Ukosefu na uchakavu wa vifaa na vitendea kazi kwa majeshi yaliyo chini ya Wizara hii kwa kiasi kikubwa unaathiri ufanisi wa vyombo hivi ikiwemo ukusanyaji wa maduhuli.

8) Vyuo vya Mafunzo vinavyomilikiwa na Majeshi yaliyo chini ya Wizara hii vina miundombinu chakavu, duni na isiyokidhi hitaji la mafunzo ya kisasa. Hali hii inaathiri ubora wa mafunzo yanayotolewa na vyuo hivyo.

9) Kukosekana kwa hati za Maeneo yanayomilikiwa na majeshi yaliyo chini ya Wizara hii ni jambo linalochangia kuwavutia baadhi ya wananchi kuvamia maeneo hayo na baadae kuibuka kwa migogoro ya umiliki.

10) Kutokupatikana kwa Fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa wakati kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa Vyombo vya Ulinzi na Usalama vilivyo chini ya Wizara hii ni jambo linaloathiri tija iliyokusudiwa na mpango wa Mradi.

11) Kitendo cha malipo ya Stika za Usalama Barabarani kufanyika kwa njia ya fedha taslimu ni suala ambalo kwa namna moja linachangia kupotea kwa mapato kwani kunatoa fursa ya Askari wasio waaminifu kutumia utaratibu huo kwa maslahi yao binafsi.

12) Kuhudumia wahamiaji haramu **2609** ambao wamemaliza kutumikia vifungo na bado wapo Magerezani kunagharimu **Shilingi 2,348,100,000** kwa mwaka. Kiasi hicho kinatosha kujenga **madarasa 117.** Hali hiyo inaonesha umuhimu kwa Serikali kuendelea kutekeleza mkakati wa kuwarejesha wafungwa hao katika nchi zao ili kuelekeza fedha hizo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo nchini.

13) Serikali imetoa **zaidi ya asilimia 70** ya fedha za maendeleo kwa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA). Kamati inashauri kiasi hicho cha fedha kiakisi uhalisia kwa Mamlaka hiyo kuongeza kasi ya kuandikisha na kugawa Vitambulisho vya Taifa hasa ikizingatiwa kuwa vitambulisho hivyo kwa sasa vimeungwanishwa na huduma muhimu mbalimbali.

**5.2 Ushauri wa Jumla**

**Mheshimiwa Spika**, kwa msingi wa Maoni niliyotoa, ufuatao ni ushauri wa Kamati:-

1) Wizara iweke utaratibu wa kufuatilia mtiririko wa fedha za maendeleo na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa Mafungu yake yote matano;

2) Serikali iendelee kuboresha hali ya vyombo vya usafiri na usafirishaji kwa Majeshi yaliyo chini ya Wizara hii. Kufanya hivyo, kutaboresha utendaji kazi wa majeshi haya;

3) Serikali iendelee na mkakati wake wa kuboresha hali ya vifaa na vitendea kazi kwa Majeshi yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Kufanya hivyo kutaongeza ufanisi wa Majeshi hayo ikiwemo ukusanyaji wa maduhuli;

4) Serikali iongeze kasi ya utekelezaji wa mkakati wa kupima na kupata Hati za maeneo yote ya Majeshi ambayo hayajapimwa; kufanya hivyo kutaepusha migogoro baina ya wananchi na majeshi.

5) Serikali izingatie umuhimu wa kutoa fedha za miradi ya maendeleo kama ilivyoidhinishwa na Bunge. Kwa kufanya hivyo, itasaidia kufanikisha utekelezaji wa miradi hiyo na kupatikana kwa tija ya miradi inayotekelezwa chini ya mafungu yote ya Wizara hii.

6) Serikali iendelee kuviwezesha vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuajiri askari wengi zaidi ili kuimarisha utendaji kazi wa vyombo hivyo.

### 5.3 Ushauri Mahsusi

#### 5.3.1 Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

1) Jeshi la Zimamoto na Uokoaji liandae mpango kazi unaotekelezeka wa ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Zimamoto na Uokoaji kilichopo Chogo Handeni. Kufanya hivyo kutasaidia ujenzi wa chuo hicho kutengewa fedha na kujengwa kwa kuzingatia mpango husika.

2) Ujenzi wa Ofisi za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji unaoendelea katika mikoa mbalimbali nchini uzingatie upatikanaji wa eneo

kubwa ambalo litakidhi ujenzi wa miundombinu ya kisasa na mahitaji ya badaye.

3) Jeshi la Zimamoto na Ukoaji lijipange kutumia mbinu za kiteknolojia na za kisasa katika kupambana na majanga mbalimbali. Kufanya hivyo, kutasaidia jeshi hilo kutoa huduma katika miradi mikubwa ya kimkakati na kupambana na majanga kwa mbinu za kisasa zaidi.

### 5.3.2 Fungu 28- Jeshi la Polisi

1) Jeshi la Polisi liandae mpango maalumu wa ukarabati na uendelezaji miundombinu ya Chuo cha Polisi Moshi. Kufanya hivyo kutasaidia kutenga fedha, kukarabati na kuendeleza miundombinu kwa kuzingatia mpango husika.

2) Serikali iweke utaratibu wa kuhakikisha kuwa malipo ya Stika za Usalama Barabarani yanafanyika kupitia namba maalum za malipo *(Control Number)*.

3) Askari wa Jeshi la Polisi wasimamiwe inavyostahili ili kuzingatia Sheria, taratibu, miiko, weledi na maadili ya Jeshi la Polisi katika utendaji kazi wao.

4) Dhana ya Polisi Jamii itekelezwe kwa ukamilifu katika kupambana na uhalifu hususani katika makazi ya watu.

### 5.3.3 Fungu 29 - Jeshi la Magereza

1) Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iendelee kutekeleza mkakati wa kuwarejesha katika nchi zao Wafungwa waliomaliza vifungo na bado wapo Magerezani. Bila kufanya hivyo, hali hiyo itaendelea kuchangia msongamano Magerezani na kutumia fedha za walipakodi kuwahudumia.

2) Pamoja na kuipongeza Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya kuendeleza na kujenga Magereza mapya 12 katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, bado kuna umuhimu kwa Serikali kutoa fedha hizo kwa kadri zitakavyoidhinishwa na Bunge. Aidha,

upatikanaji wa fedha hizo ulingane na ratiba ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa ili kuwezesha tija inayokusudiwa.

3) Jeshi la Magereza liandae mkakati wa kuanzisha na kutekeleza kilimo cha mazao ya chakula ikiwemo kilimo cha umwagiliaji. Mkakati huo uwe ni sehemu ya huduma ya urekebu na kujitosheleza kwa chakula.

4) Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kutoa Msamaha wa **Wafungwa 376** katika Sikukuu ya Muungano **tarehe 26 Aprili, 2023.** Msamaha uliotolewa kwa Wafungwa umeipunguzia Serikali gharama ya takribani **Shilingi 338,400,000** kwa mwaka.

   Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha zote zitakazoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka 2023/2024 kwa ajili ya vikao vya Bodi ya Taifa na za Mikoa za *Parole* ili wafungwa wengi zaidi wanaostahili kupewa msamaha kwa mujibu wa Sheria ya Parole wapunguzwe Magerezani na hatimaye kuokoa fedha za Serikali zinazotumika kuwatunza.

5) Serikali iliwezeshe jeshi la Magereza kupata magari hususan kwa ajili ya kusafirisha mahabusu pamoja na magari kwa ajili ya shughuli za utawala ambapo kwa sasa mahitaji halisi ni magari 800. Upatikanaji wa magari hayo, pamoja na mambo mengine, utasaidia mahabusu kupata nafasi ya kusikiliza kesi zao kwa wakati uliopangwa na hivyo kuamuliwa mapema.

6) Jeshi la Magereza lishiriki kikamilifu katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kupanda miti na kuitunza katika magereza yote katika miji ambayo magereza hayo yapo. Aidha, kufanya hivyo kunaweza kuwa pia ni sehemu ya huduma za urekebu.

### 5.3.4 Fungu 51- Wizara

1) Wizara iisimamie kwa karibu Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kuhakikisha kuwa inatekeleza majukumu yake ipasavyo ikiwemo kuongeza kasi ya uandikishaji na ugawaji wa Vitambulisho vya Taifa kuendana na mahitaji.

2) Serikali ifanye mapitio ya Sheria ya Parole ili kubaini changamoto za kisheria zinazoathiri ufanisi na lengo la kutungwa kwake kwa madhumuni ya kufanya marekebisho.

3) Wizara ifanye tathmini ya Mfumo uliopo wa usajili wa Jumuiya za Kidini kwa lengo la kuona kama mfumo na utaratibu uliopo unakidhi mazingira ya sasa ambapo kumekuwa na Jumuiya nyingi ambazo zimesajiliwa lakini zinaendesha shughuli zake kinyume na malengo ya Jumuiya hizo.

4) Serikali iandae mkakati maalumu wa kuwatafuta, kuwatambua na kuchukua hatua kwa Wakimbizi walio nje ya makazi na makambi ya wakimbizi.

**5.3.5 Fungu 93 – Jeshi la Uhamiaji**

1) Jeshi la Uhamiaji liandae mpango wa ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya Chuo cha Uhamiaji Raphael Kubaga kilichopo kichaka miba, Mkinga - Tanga. Kufanya hivyo kutasaidia kutenga fedha na kuendeleza ujenzi kwa kuzingatia mpango huo.

2) Serikali iendelee kutekeleza mkakati wake wa kuwarejesha makwao wafungwa wahamiaji haramu waliomaliza kutumikia vifungo vyao na bado wapo Magerezani.

3) Serikali iliwezeshe Jeshi la Uhamiaji kupata vyombo vya usafiri ili kuwabaini wahamiaji wasio na vibali na kuwachukulia hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kuwalipisha ada husika na faini.

4) Serikali iandae mkakati wa kuliwezesha Jeshi la Uhamiaji vifaa vya kisasa ikiwemo kupata Boti kwa ajili ya kufanya Misako na Doria katika mwambao wa bahari ya Hindi ambayo imekuwa ni njia kubwa ya kupitisha wahamiaji haramu na Magendo.

5) Serikali ichukue juhudi za makusudi za kudhibiti mianya ya njia zisizo rasmi zaidi ya 1000 katika mikoa mbalimbali ya mipakani. Kufanya hivyo ni sehemu ya jitihada za muda mrefu za kudhibiti uingiaji wa wahamiaji haramu nchini.

6) Ujenzi wa Ofisi za Jeshi la Uhamiaji unaondelea katika mikoa mbalimbali nchini uzingatie upatikanaji wa eneo kubwa lenye kukidhi mahitaji ya sasa na baadae na jengo litakalokidhi matumizi ya vifaa vya kisasa vya kiteknolojia.

## SURA YA SITA

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, Nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo orodheshwa katika Taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Vita Rashid Kawawa, Mb | - Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Vincent Paul Mbogo, Mb | - M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Abdi Hija Mkasha, Mb | - Mjumbe |
| 4. | Mhe. Ali Juma Mohamed, Mb | - Mjumbe |
| 5. | Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb | - Mjumbe |
| 6. | Mhe. Cosato David Chumi, Mb | - Mjumbe |
| 7. | Mhe. Daniel Tlemai Awack, Mb | - Mjumbe |
| 8. | Mhe. Dr. Alfred James Kimea, Mb | - Mjumbe |
| 9. | Mhe. Edwin Enosy Swalle, Mb | - Mjumbe |
| 10. | Mhe. Fakharia Shomar Khamis, Mb | - Mjumbe |
| 11. | Mhe. Felister Deogratius Njau, Mb | - Mjumbe |
| 12. | Mhe. Grace Victor Tendega, Mb | - Mjumbe |
| 13. | Mhe. Jafari Wambura Chege, Mb | - Mjumbe |
| 14. | Mhe. Joseph Anania Tadayo, Mb | - Mjumbe |
| 15. | Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb | - Mjumbe |
| 16. | Mhe. Maulid Saleh Ali, Mb | - Mjumbe |
| 17. | Mhe. Minza Simon Mjika, Mb | - Mjumbe |
| 18. | Mhe. Muharami Shabani Mkenge, Mb | - Mjumbe |
| 19. | Mhe. Mwinyikondo Rajab Mustafa, Mb | - Mjumbe |

20. Mhe. Neema Lugangira, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Nicholaus G. Ngassa, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Zahor Mohammed Haji, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Eng. Hamadi Yusuf Masauni (Mb), Naibu Waziri, Mhe. Jumanne Abdallah Sagini (Mb), Katibu Mkuu Ndugu Kasper Mmuya pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi (*ndc*), Katibu wa Bunge; kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto *(ndc),* Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Omary Magwinza na Bi. Victoria Mizengo wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii ili lijadili na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Vita Rashidi Kawawa, Mb
**MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**

29 Mei, 2023

***Kiambatisho Na. 1***

## 1.0 UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA

Wakati wa kuchambua Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kamati ilishauri masuala mbalimbali ambapo maelezo ya Wizara kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri huo ni kama ifuatavyo:-

***1) Serikali ifanye mapitio ya Sheria ya Parole ili kubaini changamoto za kisheria zinazoathiri ufanisi na lengo la kutungwa kwake kwa madhumuni ya kufanya marekebisho.***

Ni kweli Sheria ya Bodi ya Parole ina changamoto kadhaa. Mfano Kifungu cha 4 (a) na (b) cha Sheria ya Bodi ya Parole, Sura ya 400 Rejeo la Mwaka 2002 kinachotoa masharti ya kuachiliwa mfungwa aliyefungwa kwa miaka zaidi ya minne (4) kuwa ndiye atafaidika na utaratibu wa parole. Katika kushughulikia changamoto hizo, Sheria ya Parole imeanza kufanyiwa maboresho kwa kukusanya maoni kutoka kwa wadau ambao ni wananchi ili kurekebisha Sheria hiyo. Maboresho hayo yatawezesha Bodi ya Taifa ya Parole pamoja na Bodi za Parole za mikoa kutekeleza Majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

***2) Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) iliyokuwa imepanga kununua kadi ghafi kwa ajili ya vitambulisho, iwezeshwe kupata kiasi cha Shilingi bilioni 5.3 zilizosalia kwa mwaka wa fedha 2021/2022.***

Mwaka 2021/22 Mamlaka iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 10,080,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Mwezi Mei, 2022 Mamlaka ilipokea kiasi cha Shilingi bilioni 5.3 ikiwemo Shilingi bilioni 2 kwa ajili ya ununuzi wa kadighafi. Aidha, hadi kufikia tarehe 30, Juni, 2022 Mamlaka ilikuwa imepokea jumla ya Shilingi 10,000,000,000 sawa na asilimia 100 ya fedha zote za ndani za kutekeleza shughuli za maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2021/22.

***3) Pamoja na juhudi za Serikali kuanzisha mfumo wa usajili wa Jumuiya kwa njia ya kielektroniki, Serikali ifungue Ofisi ya Msajili wa Jumuiya kikanda ili kurahisisha huduma kwa wananchi.***

Katika mwaka wa fedha 2022/23, Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Jumuiya imefanikiwa kufungua Ofisi Moja ya Kanda ya Mashariki iliyopo Dar es Salaam, ambayo itahudumia wateja waliopo kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro na mikoa mingine ya jirani. Ofisi hiyo ilifunguliwa rasmi tarehe 05 Septemba, 2022 na inaendelea kutoa huduma hadi sasa. Aidha, katika

mwaka wa fedha 2023/24, Ofisi ya Msajili wa Jumuiya inatarajia kufungua ofisi nyingine tatu ambazo ni Kanda ya Kaskazini katika mkoa wa Arusha, Kanda ya Ziwa mkoani Mwanza na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini mkoani Mbeya.

Ofisi hizo zitawawezesha wananchi kupata huduma kwa ukaribu zaidi na kuongeza tija katika ufuatiliaji na Usimamizi wa Jumuiya za Kidini na zisizo za Kidini zilizopo katika maeneo hayo sambamba na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali yanayotokana na ada na tozo mbalimbali za jumuiya.

***4) Pamoja na kupongeza juhudi za Serikali za kuwarejesha wakimbizi katika nchi zao, Serikali ichukue hatua stahiki na madhubuti kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ili kufanikisha zoezi la kuwarejesha wakimbizi hao nchini kwao.***

Wizara ya Mambo ya Ndani kupitia Idara ya Huduma kwa Wakimbizi imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Serikali ya Jamhuri ya Burundi, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) pamoja na wadau wengine wa ndani na nje ya nchi katika kufanikisha zoezi la urejeshaji wakimbizi kutoka nchi ya Burundi. Kuanzia tarehe 01 Julai, 2022 hadi 28 Februari, 2023 kulikuwa na wakimbizi na waomba hifadhi 255,681 wengi wao wakiwa ni wa kutoka nchi ya Burundi na DRC. Katika kipindi hicho, jumla ya wakimbizi 4,634 walirejea nchini kwao kwa hiari na wakimbizi 3,616 walipelekwa katika nchi ya tatu za Marekani (3,126), Canada (474), Ufaransa (9) na Australia (7).

Jitihada nyingine zilizofanyika katika urejeshaji wa wakimbizi kutoka nchi ya Burundi ni pamoja na kuendesha mazoezi ya kuwahoji wakimbizi wa Burundi juu ya sababu zinazofanya wasirejee kwenye nchi yao ya asili (Intention Survey for Burundian Refugees). Mazoezi hayo yalifanyika kuanzia tarehe 27 Juni, 2022 – 22 Julai, 2022 na kutembelea maeneo ya asili ya wakimbizi wanakotokea nchini Burundi kuanzia tarehe 01 – 06 Agosti 2022. Mazoezi yote mawili yalibainisha kuwa asilimia zaidi ya 90 ya wakimbizi kutoka nchi ya Burundi hawana matishio ya usalama badala yake wanahofia ugumu wa maisha nchini kwao unaosababishwa na uduni wa huduma za kijamii na fursa za kiuchumi. Hivyo, kwa sasa wakati Serikali ya Tanzania ikiendelea

na jitihada za kuwarejesha wakimbizi nchini humo, Shirika la UNHCR na Jumuiya ya Kimataifa inaendelea na jitihada za kuboresha mazingira ya maeneo wakimbizi wanapotokea nchini humo.

Vilevile, kuanzia mwezi Machi, 2023 UNHCR imeahidi kuboresha motisha ili kuvutia wakimbizi kujiandikisha kurejea kwa kuwaongezea fedha za kujikimu wanaporejea. Aidha, mwezi Aprili, 2023, Wizara inakusudia kufanya kikao na Serikali ya Burundi kitakachojadili pamoja na mambo mengine, utekelezaji wa Sera ya Wakimbizi juu ya kutenga eneo salama ndani ya Burundi ambapo inatarajiwa wakimbizi wote walioko kambini na nje ya kambi watarejeshwa kwa mkupuo na kuhifadhiwa eneo husika watakapowezeshwa kupata huduma za kijamii wanazozipata kambini.

Kwa upande wa wakimbizi kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) jitihada za kuitisha Mkutano wa Pande Tatu wa kujadili urejeshaji wa wakimbizi kutoka nchi hiyo walioonesha nia ya kurudi nchini kwao kwenye maeneo salama zinaendelea. Serikali ya DRC imealikwa hapa nchini kushiriki Mkutano huo mwezi Aprili, 2023.

**5) *Serikali iongeze jitihada za kuwafikia kwa urahisi watu wote wenye vigezo vya kusajiliwa na kutambuliwa wanaoishi mbali na makao makuu ya Wilaya.***

Katika mwaka wa fedha 2021/22 NIDA ilitambua na kusajili jumla ya watu 677,573 na hivyo kufikisha jumla ya watu 23,185,729 waliotambuliwa na kusajiliwa tangu kuanza kwa zoezi la usajili na utambuzi mwaka 2012. NIDA inaendelea kutambua na kusajili wananchi kupitia ofisi za usajili za wilaya na pamoja na kuendesha mazoezi ya usajili na utambuzi wa wananchi katika ngazi ya kata na vijiji. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Februari, 2023 NIDA imesajili jumla ya watu 550,358 na hivyo kufikia jumla ya watu 23,736,087 waliosajiliwa tangu kuanza kwa zoezi la usajili mwaka 2012.

Pia Mamlaka imefanya marekebisho ya Kanuni za Usajili na Utambuzi wa Watu za mwaka 2012 ili kuwawezesha Watanzania

kuendelea kutumia Vitambulisho vya Taifa bila kuwa na ukomo wa matumizi na hivyo kupunguza gharama kwa wananchi na Serikali. Vilevile, marekebisho hayo yatawezesha NIDA kusimamia ipasavyo huduma ya ushirikishwanaji wa taarifa na kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli. Sambamba na hilo, marekebisho ya hayo yatawezesha zoezi la usajili kuwa jumuishi kwakuwezesha usajili wa makundi ya Walowezi na Watanzania wanaoishi nje ya nchi. Aidha, katika mwaka wa fedha 2023/24 NIDA inatarajia kusajili watu 1,500,000. Usajili huo utafanyika kwa kawaida katika ofisi za usajili za wilaya na usajili wa pamoja (Mass registration) katika maeneo ya vijijini na hivyo kuwezesha wananchi wengi kupata huduma mbalimbali ikiwemo mikopo inayotolewa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

***6) Pamoja na nia njema ya Serikali kutekeleza mpango wa ujenzi wa nyumba za wahanga wa biashara ya usafirishaji haramu wa binadamu kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali ifanye upembuzi wa kina kabla ya kuanza utekelezaji.***

Serikali imefanya upembuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa mpango wa ujenzi wa nyumba salama za wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu. Upembuzi huo umeonesha umuhimu na uhitaji wa nyumba salama kwa wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu hususan kwa kuzingatia hali ilivyo kwa sasa kuhusu uhalifu huu hapa nchini. Kwa mfano, kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2014 hadi Februari 2023, takwimu zinaonesha kuwa jumla ya wahanga 1,073 wameokolewa, kupewa hifadhi na baadae kuunganishwa na familia zao. Kati yao, watoto ni 956 ambao ni sawa na **asilimia 89** na watu wazima ni 117 sawa na **asilimia 11**.

Wahanga wa jinsia ya kike ni 999 ambao ni sawa na **asilimia 93** na wahanga wa jinsia ya kiume ni 74 sawa na **asilimia 7**. Takwimu hizi zinaonesha kuwa watoto wa kike ndio wahanga wakubwa wa usafirishaji haramu wa binadamu. Wengi wao wanaanzia miaka nane (8) hadi 15. Wahanga hawa husafirishwa kutoka vijijini na kupelekwa mijini na wengine nje ya nchi kutumikishwa kingono; kutumikishwa kwenye ukahaba; kufanya kazi za ndani; kufanya kazi ngumu kwenye mashamba, uvuvi, migodi midogo midogo na viwandani; kuomba mitaani; kutolewa viungo vya mwili kama vile

figo na wengine hususan vijana kutumikishwa kingono kwa kulawitiwa na kulazimishwa kuingizwa kwenye mapenzi ya jinsia moja na wengine pia kuingizwa kwenye vitendo vya ugaidi.

Wahanga hawa wanapookolewa, Serikali inalo jukumu la kisheria la kuwalinda, kuwapa hifadhi, kuwapa huduma muhimu za kibinadamu na urekebu (*Rehabilitation*) na hatimaye kuwaunganisha na familia zao. Hata hivyo, hadi sasa Serikali haina nyumba salama kwa ajili ya kuwahifadhi na kutoa huduma kwa wahanga na mashahidi wa usafirishaji haramu wa binadamu. Uwepo wa Nyumba Salama, kimsingi, ni takwa la kisheria hususan Kifungu cha 20 cha Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu Na. 6/2008. Vilevile, ni utekelezaji wa Ibara ya 6 ya Itifaki ya Umoja wa Mataifa ya Kuzuia na Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu hususan Wanawake na Watoto (The Palermo Protocol, 2000) iliyoridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2006.

Kwa kipindi kirefu sasa tangu kutungwa kwa Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu Na. 6 ya mwaka 2008, Serikali imekuwa ikiwaombea hifadhi na huduma muhimu za kibinadamu wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu kwenye vituo vinavyomilikiwa na Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGOs) kabla ya kuwaunganisha na familia zao. Hata hivyo, kumekuwepo na changamoto mbalimbali zinazotokana na kutumia vituo vinavyomilikiwa na taasisi zisizo za kiserikali kuhifadhi wahanga na mashahidi wa usafirishaji haramu wa binadamu kama ifuatavyo:

(a) Mosi, vituo hivyo havina usalama wa kutosha hivyo wahalifu au mtandao wa uhalifu umekuwa ukienda kwenye vituo hivyo kuwatisha wahanga ambao ni mashahidi muhimu wa kesi za usafirishaji haramu wa binadamu na hivyo kuwafanya wahanga hao kujitoa kwenye kesi zilizoko mahakamani kwa kuhofia usalama wao;

(b) Vituo hivyo havikuanzishwa mahsusi kwa ajili ya kusaidia wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu, hivyo upatikanaji wa nafasi za malazi katika vituo hivyo umekuwa na changamoto na mara nyingi Sekretarieti imelazimika kutafuta *fit persons* au kulipia wahanga kwenye nyumba za kulala wageni;

(c) Vituo vingi vimeanzishwa kwa lengo la kuwahudumia Watoto wa kike, pale ambapo Sekretarieti imeokoa Watoto wa kiume au watu wazima imekuwa ikipata changamoto ya sehemu ya kuwapeleka kwa ajili ya kupata hifadhi ya muda na huduma muhimu za kibinadamu;

(d) Miundombinu ya vituo vingi si rafiki kwa wahanga wenye ulemavu kwa kuwa havijaandaliwa kupokea watu wa aina hiyo; na

(e) Mashirika mengi yanategemea misaada kutoka nje ili kujiendesha, katika kipindi cha hivi karibuni hususan baada ya janga la UVIKO 19 mashirika mengi yalisitisha utoaji wa huduma kutokana na uhaba wa fedha. Hali hiyo imeongeza changamoto ya upatikanaji wa nafasi za malazi kwenye vituo hivyo. Hata pale nafasi inapopatikana mashirika hayo mara nyingi yamekuwa yakiiomba Sekretarieti kuchangia gharama za uendeshaji.

Uzoefu wa nchi nyingine hususan Namibia unaonesha kuwa uwepo wa nyumba salama zinazomilikiwa na Serikali unasaidia kwa kiasi kikubwa mapambano dhidi ya uhalifu huu kwa maana ya kutoa ulinzi kwa wahanga na mashahidi wakati wa uendeshaji wa kesi na kutoa huduma za urekebishaji kwa wahanga kwa kuzingatia sheria na matakwa ya mikataba ya kimataifa. Urekebishaji unapofanyika vizuri husaidia kuwaepusha wahanga wasirubuniwe tena na wahalifu na kusafirishwa, pia huwafanya wahanga kuwa mabalozi wazuri kwa kutoa elimu hii kwa watoto, vijana na jamii kwa ujumla kwenye maeneo yao.

Kutokana na hali hii, nchi ya Namibia ndiyo nchi pekee Barani Afrika ambayo iko kwenye daraja la kwanza - *Tier One* (kwa mujibu wa ripoti ya Serikali ya Marekani iliyotolewa mwezi Juni, 2022) kwa maana ya kuzingatia matakwa ya mikataba ya kimataifa katika mapambano dhidi ya usafirishaji haramu wa binadamu. Tanzania kwa mujibu wa ripoti hiyo, tumepanda kutoka *Tier Two Watchlist,* ambapo tumekaa kwa muda wa miaka mitatu mfululizo, mpaka *Tier Two* kutokana na jitihada mbalimbali ambazo Serikali ya Awamu ya Sita imeonesha katika kupambana

na uhalifu huu ikiwa ni pamoja ya Serikali kutenga fedha za kuanzisha nyumba salama. Ikumbukwe kwamba Mhanga wa usafirishaji haramu wa binadamu anaweza kuwa mtu yeyote ingawa takwimu zinaonesha kuwa watoto na wanawake ndio waathirika wakubwa. Wengi wao husafirishwa kutoka vijijini kwa kudanganywa au kupewa ahadi za uongo na mwisho wa siku hujikuta wanaishia kwenye mikono ya wahalifu ambao huwafanyisha kazi bila malipo tena kwa vipigo na mateso.

Kutokana na madhila wanayopata, kama vile mateso, unyanyasaji, kupata kilema cha maisha au magonjwa yasiyotibika, wengi wao huwa wameathirika kisaikolojia na baadhi kufikia hatua ya kukata tamaa ya maisha na hata kutoa uhai wa Maisha yao. Hivyo, wanapookolewa hupewa hifadhi ya muda kwenye nyumba salama na kupata huduma muhimu za kibinadamu na ulinzi wakati kesi zinazowahusu zikiendelea mahakamani. Vilevile, hupata msaada wa kisaikolojia, huduma za urekebu na mafunzo ya stadi za maisha zitakazowasaidia watakapounganishwa na familia zao.

Ukosefu wa nyumba salama ni kinyume cha matakwa ya sheria ya nchi na mikataba ya kimataifa tuliyosaini na kuridhia kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu usafirishaji haramu wa binadamu.

Hali hii, imesababisha wahanga ambao ndio mashahidi wakubwa kwenye kesi za usafirishaji haramu wa binadamu kusita kutoa ushahidi mahakamani kwa kuhofia kufanyiwa vitendo vya kikatili na mtandao wa uhalifu huo hivyo kusababisha wahalifu wa vitendo hivyo kushinda kesi mahakamani kwa kukosa ushahidi wa kuwatia hatiani. Vilevile, ukosefu wa nyumba salama hupelekea baadhi ya wahanga kutopata huduma za urekebu na hivyo kusababisha baadhi yao kusafirishwa tena na kwenda kutumikishwa. Hali hii inafanya tatizo hili kuendelea na kuonekana kuwa kubwa hapa nchini.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Mkundi kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa maoni na mapendekezo ya Kamati mbele ya Bunge tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Pia nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Vincent kwa kuwashirikisha wajumbe vizuri kwenye Kamati yenu, ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea kuna tangazo dogo kuna wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni Wenyeviti wa Kamati za Usalama Barabarani Mikoa yote ya Tanzania Bara. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa na mjadala uliopo mbele yetu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi nina orodha hapa ya wachangiaji tutaanza na Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, ajiandae.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia kidogo katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Masauni na Naibu wake Mheshimiwa Sagini na timu yao yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuilinda nchi yetu na kulinda mali za wananchi na kwa kuonyesha msimamo wa kutetea wananchi wake hususani nikitolea mfano kwa jinsi alivyochukua hatua za haraka kwenda kupeleka usafiri Sudani Kusini na kuwachukua wanafunzi wa Tanzania ambao walikuwa kule na kuwarudisha nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi pia kwa Trafiki wa Zanzibar, Trafiki wa Zanzibar wamekuwa trafiki marafiki, Trafiki wa Zanzibar unaweza ukamfuata hata kama umepotea njia akakuelekeza, nenda njia fulani. Trafiki wa Zanzibar anaweza akakusimamisha, akakwambia usipite njia hii ina foleni pita njia hii. Trafiki wa Zanzibar anaweza akasimama kwenye *zebra* akasimamisha magari akatoka mwenyewe kwenda kushika wanafunzi au watoto kuwavusha mpaka upande wa pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo mengine tumeona trafiki yuko kwenye *zebra* lakini haangalii kusimamisha magari ili watu wapite macho yake yako kulia anaangalia daladala linalokuja litafanya nini ili nipige mkono. Kwa hiyo hilo pia Mheshimiwa Waziri aliangalie, kuna baadhi ya matrafiki hawako sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze pia Trafiki wa Chanika, Chanika kuna kiongozi anakaa kule, si vizuri kumtaja kwa nafasi lakini huwa anakwenda, lakini kituo kile hakina *raider* ya kuongoza misafara, unakuta kwamba wanatumia tu mikono na taa na wakati kiongozi mkubwa sana huwa anaenda kule. Sasa naomba Wizara hii iangalie kupeleka *raider* kwa Polisi wa Chanika, barabara ile ni kubwa, ina maroli mengi ina mabasi mengi, sasa ni vizuri tuangalie usalama zaidi wa viongozi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitoe pongezi kwa Jeshi la Magereza kwa sasa hivi wanatumia vizuri nafasi za wafungwa. Zamani tulikuwa na kazi tu ya kuwalisha na kuwavalisha nguo kazi hazionekani, lakini sasa hivi tumeona kwamba maofisi mengi na vituo vingi vya Magereza majengo yanajengwa kuna ma-*hall* kuna nini, magereza wanafanya kazi unajua kweli huyu sasa akitoka hapa akashajifunza kitu anaenda kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaniona mtu wa pongezi sana, natoa pongezi sana kwa sababu haya yanayofanyika yanaonekana, nipongeze Jeshi la Uhamiaji katika utaratibu mzima wa utoaji *Passport* kwa sasa hivi kwa maana hati za kusafiria. Zamani ukitafuta hati ya kusafiria yaani unahangaika kama unatafuta kumtoa mtu figo ukaweke kwako, sasa hivi *Passport* ukisema dakika mbili unaambiwa baada ya muda fulani njoo uchukue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeliona hilo Dodoma, tumeliona hilo Dar es Salaam japo kuna maeneo mengine yana matatizo kidogo, basi niombe wawasaidie hususani katika masuala ya kompyuta ikitolewa mfano katika Mkoa wa Iringa, kompyuta zao ni za kizamani, wawarekebishie wawape za kisasa na maeneo mengine ambayo bado yana kompyuta za kizamani, ili waweze

kufanya kazi zao vizuri, watu wapate *Passport* mapema. Nasema hivi kwa sababu kuna wakati mwingine *Passport* unapata kidharura dharura, siyo kwamba kila anayechukua *Passport* kwa ajili ya sterehe zake. Kwa hiyo niwapongeze kwamba wameboresha kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi vile vile kwa Trafiki wa Makumbusho Dar es Salaam, yule kijana anajituma, ile kazi inaonekana kaipenda na ameingia pale kwa dhati, anaongoza magari kwa mbwembwe, watu wanapita pale wanamtunza, lakini nafikiri kuna wengine wameenda kwenye upolisi hawana jinsi ili mradi tu niende nizibe pengo. Kwa hiyo napenda hao mapolisi kweli wanaoenda huko waangalie, huo upolisi wanautaka au wamekwenda tu kwa sababu hamna kitu kingine cha kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa polisi wetu pamoja na pongezi zote tunazowapa, kuna maeneo ambayo wanatupa kero, unaanza na king'amuzi, basi akimshika mmoja mwenye tisini yatapita magari hata ishirini yote yanaonyesha king'amuzi tisini tu, tisini hiyo hiyo haibadiliki wanaoneshwa hiyohiyo. Kama hivyo ving'amuzi vibovu vikatengenezwe au vinunuliwe vipya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, wana mchezo wa kujificha hawa, utaona tu ghafla kakurupuka kwenye mihogo, sasa wewe Bwana Shamba? Uko kwenye mihogo ulifuata nini? Kaa barabarani tukuone kama kuna tatizo tusimame tukwambie, bwana tusaidie hapa, kuna mwingine anamtaka trafiki amuulize hivi kutoka Gairo mpaka manyoni ni kilomita ngapi, lakini yeye yuko kwenye mihogo ghafla tu anaingia ili mradi tu uvunje sheria. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, trafiki wana ucheleweshaji usiokuwa na sababu, wanaweza wakasimamisha mabasi ya abiria, malori na kadhalika, halafu mwenyewe anakaa anachati pale anasubiri dereva au konda atoke amfuate pale akamuulize. Sasa wanawatia hasira madereva, wakitoka pale wanatoka spidi, matokeo yake tunasababisha ajali mbele. Ni afadhali anaposimama aongee naye palepale wamalizane palepale kama kuendelea na safari aendelee kama ni kumwandikia

amwandikie badala ya kumsimamisha kwa muda mrefu na kumpotezea muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matrafiki wengine ni walevi, asubuhi tu analewa. Mimi nimekutana naye Morogoro, kanisimamisha nimesimama, kaniuliza hii namba ya wapi nikamwambia hii namba ya usajili wa Zanzibar, akauliza nitajuaje kama Zanzibar? Dereva wangu akamjibu akamwambia si umeona bendera hiyo ya Mbunge? Akasema, aah, bendera hata mimi ninayo kiunoni, lakini kutokana na harufu yake nilivyomskia nikajua mlevi nikamwambia achana naye tuondoke. Sasa walevi kama wale Wizara iwaangalie asubuhi asubuhi isiwe inawapangia kazi huko barabarani, wanatuletea vituko. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo kuna kazi nyingine ambazo zinakuwa kioo cha jamii wakiwemo Mapolisi, Wanajeshi kwa ujumla kuna Walimu, kuna Madaktari hata Wabunge yaani ni kazi ambazo zinaenda watu wanakuangalia kioo cha jamii. Sasa tunaposikia Polisi yuko katika ule mchezo kwa kweli wanatutia mashaka. Unasikia mtoto kalawitiwa au kabakwa, unamchukua unataka umpeleke polisi, halafu unakuja unasikia polisi mwenyewe ndio walewale, wanatukatisha tamaa na watatugombanisha kwa sababu ukishamchukua mtoto aliyelawitiwa ukampeleka polisi, kumbe polisi mwenyewe ndio yuleyule anakuona mbaya wale waliompeleka huyo mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maadili kwenye Jeshi la Polisi na wengineo liangaliwe kwa kina, kwa sababu licha ya kutia aibu, lakini wanatukatisha tamaa, halafu baadae wanatuambia mbona mnamalizana wenyewe kijamii jamii hukohuko nyumbani, sasa huko polisi tukienda na mambo yenyewe ndio hayo inakuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote niseme kabisa pongezi nyingine kwa Waziri na Mheshimiwa Rais, nyumba za askari sasa hivi nyingi zimeboreshwa tofauti na zamani. Zamani mpaka tunajiuliza yaani chumba kimoja wanapishana kwa mapazia unajiuliza wanapataje watoto pale, lakini sasa hivi tunashukuru nyumba za maaskari zimekuwa nzuri, zinaheshimika,

wamewapa staha. Naomba Wizara waongeze nguvu yale maeneo mengine ambayo hayajapata nyumba, basi wajengewe waendelee kuwa na staha. Pamoja na hayo bado napendekeza vifaa zaidi vinunuliwe vya kisasa kwa ajili ya askari wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo na Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, ajiandae.

**MHE MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa na hali ya uzima na afya, lakini niwashukuru na Wabunge wenzangu wote waliokuwemo katika Bunge hili Bunge Tukufu hii leo na wakaweza kunipigia makofi kwa wingi hivi saa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais wangu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa utekelezaji wake mkubwa anaoufanya katika Wizara zake zote. Mheshimiwa Rais Mwenyezi Mungu amjalie huyu bibi amuondolee kila la shari, amjalie heri, amuondolee nakama, husda, ubaya, amuondolee kila aina ya uadui katika kiwiliwili chake na katika safari zake na ampe heri na busara katika uongozi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuendelea niwapongeze Mawaziri wangu wote, Mheshimiwa Masauni nampongeza sana kwa Wizara hii ni Wizara yake, Wizara mama amejaa na hakuna Waziri mwingine katika Wizara hii kama si yeye Masauni. Pia nimpongeze na Naibu wake hivi sasa ambaye ni Mheshimiwa Sagini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Naibu Mheshimiwa Sagini, nilimwomba hapa katika swali langu tuende kwenye *site* zangu za Mkoa wa Kusini Unguja. Mheshimiwa Sagini hakurudi nyuma, alisema nitakwenda na wewe na nitakwenda kufanya kazi moja baada ya moja. Nimshukuru Naibu Waziri Sagini, tulikwenda Kizimkazi na tukazifanya zile kazi za Kizimkazi.

Hatimaye leo hii katika utekelezaji wao uliosomwa sasa hivi na Mheshimiwa Waziri nimeona mafanikio ya Wizara yetu tuliyokwenda kule na Mheshimiwa Sagini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Sagini tulikwenda kuangalia kwanza Kituo cha Kizimkazi, kilikuwa kinajengwa upya na kituo kile kwa bahati kimeshamalizika na hivi sasa kinaendelea kufanya kazi, isipokuwa tu kituo kile kina wafanyakazi ambao walitolewa katika kituo kingine wakapelekwa kituo kile bado hawajapata mafao yao. Wamepelekwa pale kufanya kazi hawajapata mafao yao na mpaka sasa hivi wanalalamika sana. Hawajapata maposho yao ya kutoka kule na kuja kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika wafanyakazi hawa waliokuwa wamepelekwa pale mafao hawajapata na wanataka mafao yao. Kwa hiyo niomba Serikali, wale wafanyakazi waliopelekwa pale wa polisi kwenda kufanya kazi katika Kituo cha Kizimkazi, wapewe mafao yao na wapewe mahitaji yao yanayohusika katika kuhamishwa kule kuja pale ili waweze kufanya kazi vizuri. Naomba sasa hivi Mheshimiwa Waziri anapokuja ku-*wind* hapa, atuambie kwamba lini utawapatia mafao yao ili na sisi wananchi tuweze kufaidika kwamba wale watu tayari tarehe fulani watapewa mafao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuendelea kuna kitengo cha wanawake katika Wizara…

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwantumu, kuna taarifa

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ataniibia dakika zangu, nilindie dakika zangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba ukae, Mheshimiwa Saashisha taarifa fupi.

**TAARIFA**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka tu kumpa mama yangu kwamba Mheshimiwa anayechangia kwamba si Kizimkazi tu wanaaskari wanaodai mafao. Kule Hai kuna wanaodai *arrears,* posho zao ambazo ni stahiki zao za msingi. Kwa hiyo nilikuwa namwongezea tu kwamba Mheshimiwa Waziri akatazame stahiki za askari wa majeshi yetu yote ili wawalipe, wanafanya kazi kubwa na muhimu sana kwa Taifa letu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mwantumu taarifa unaipokea?

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea kwa mikono miwili mwanangu huyo. Kwa hiyo kadhia zinatoka hizo kwa wengine baadhi ya vituo vingine. Kwa hiyo tunaomba sasa hivi hili suala lifanyike kwa

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani, kuna Kitengo cha Polisi cha Akinamama, kitengo hiki akinamama wanapokuwa wajawazito wengine wanakuwa wanachukua likizo zao mapema, lakini kabla ya kujifungua bado hawa watu wana likizo zao, mara moja ile likizo inakatwa, ikishakatwa ile likizo anapewa likizo yake ya uzazi siku zake arobaini akimaliza arejeshewe likizo yake ya kawaida? Basi anakuwa harejeshewi tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kadhia ipo inayofanyika katika kitengo hiki na kipo hiki kitengo na ndio maana mimi hapa sasa hivi nakizungumzia. Kwa hiyo tunaomba akinamama waliokuwepo katika kitengo hiki wakimaliza likizo zao za uzazi wapewe likzo zao za stahiki zao ili waweze kuwalea watoto wetu vizuri, maana wale tunawategemea keshokutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuendelea, kuna vituo tulivyokwenda na Waziri Sagini kule Makunduchi Zanzibar, tulikwenda kuangalia Kituo cha Polisi daraja C ambacho ni cha Makunduchi kina thamani ya kujengwa milioni mia moja na kumi, lakini pia kuna Kituo cha Polisi cha Dunga C milioni mia moja na

kumi, lakini kuna Kituo cha Polisi daraja *C* Dunga Mitini, Kusini Unguja kina shilingi milioni 48.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo hivi hapa nilikuwa navipigia kelele sana katika Bunge lako hili Tukufu, kwamba hivi vituo vilikuwa vibovu na vichafu na sasa hivi bado hatujapata mustakabali mzima wa vituo hivi kujengwa kwake, isipokuwa nasikia tu Kituo cha Makunduchi kilishaanza kuzungushwa mabati ndio utekelezaji ambao tunautaka, kilishazungushwa mabati ili kwa kuendelea vituo hivi viweze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba, hivi vituo vitekelezwe vizuri na vijengwe vizuri ili wale polisi na wao wapate vituo vizuri vya kufanyia kazi zao kwa sababu wanaazimaazima vituo wanakaa. Kama kule Makunduchi kuna nyumba nyingine mbovu, zinavuja, nazo zitengenezwe, Kituo cha Dunga wamehamia Dunga huku wanataka na wao wamaliziwe kituo chao ili warudi kule kwa kawaida ili waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuendelea, kuna milioni 110 na kuna milioni 44 hizi ambazo tutakazokwenda kujengewa vituo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwantumu malizia mchango wako

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia, kuna vituo vinataka kujengwa ma-*hal,l* kwa hiyo nashukuru kwamba vimeonekana na pia vitakwenda kujengewa hizo kumbi za kuweza kufanya mikutano yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina zaidi, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja kwa Wizara hii ya Mambo ya Ndani. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira na Mheshimiwa Felista Deogratius Njau, ajiandae.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu sana. Awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kulifanyia Taifa letu na mojawapo ya sehemu ya kazi nzuri ni kututeulia viongozi makini kama Waziri wetu wa Mambo ya Ndani pamoja na Naibu wake na timu yake nzima kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kazi inakwenda vizuri kwenye Wizara hii mchango wangu utakuwa mfupi. Nimetazama majukumu ya Wizara hii chini ya *Government Notice* ile namba 383 na namba 385 ya mwaka 2021 kama ambavyo imeboreshwa na *Government Notice* namba 334 ya Julai, 2021. Majukumu ya Wizara hii ni mapana sana, lakini yako *summarized* pale kwamba ni utekelezaji wa sera za usalama wa umma *(implementation of policies on public safety)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu hili si jukumu dogo kwa sababu ni jukumu ambalo wateja wake kuanzia mwanzo mpaka mwisho ni binanadamu. Kama ambavyo watu wanasema kazi ya kuongoza binadamu siyo kazi ndogo, wakati mwingine kuongoza vitu ambavyo havina utashi au haviko hai ni rahisi zaidi kuliko kuongoza binadamu. Kwa hiyo taasisi zote hizi ukianzia Polisi, Magereza, Uhamiaji, Zimamoto zote zinashughulikia binadamu, tena binadamu wenye changamoto au binadamu walioko katika changamoto za matukio mbalimbali. Kwa hiyo si jambo ambalo ni rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tukubali kwamba juhudi zote hizi za uchumi za kukuza uchumi na ustawi wa jamii ambazo Serikali inaendelea nazo bila Wizara hii kukaa sawa sawa hatutaweza kufaidi matunda yake. Tutaomba madarasa yatajengwa lakini vibaka watakuja wataiba madirisha ya kisasa. Tutaomba dawa zitakuja wezi wataiba, mateja wa madawa ya kulevya watavuruga Nchi. Kwa hiyo, Wizara hii ina umuhimu mkubwa sana tofauti ambavyo tunadhani kwamba labda kazi

yao ni kukamata na kuachia watu. Mambo yote ya msingi haki za binadamu zinaanzia Wizara hii, haki jinai zinaanzia Wizara hii. Sijui kufanya siasa, hata sisi kufanya si lazima Wizara hii ikae sawa sawa ili tuweze kufanya siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mpira, Yanga wasingecheza vizuri jana kama kungekuwa hakuna usimamizi wa Wizara hii. Tuende mbele hata suala la *sovereignty,* uhuru wa Nchi ambaye inakupa *right to govern* na *responsibility to protect* (haki ya kutawala na wajibu wa kulinda). Bila kuwa na Wizara hii makini ikalinda watu wako huwezi ukahesabiwa kama ni nchi huru kama watu wanakufa na kuuwawa kila siku kama kuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa la kujiuliza hapa ni kwamba hawa tunaowakabidhi dhamana kubwa nanma hii hali yao ikoje? Hali yao kibajeti kwa mfano iko namna gani? Kamati imeeleza hapa kwamba ukienda kwenye miradi ya Wizara hii *stress* ni msongo wa akili imeeleza taarifa ya Kamati kwamba tumekwenda Handeni kule kwenye kile chuo cha pale Chogo kwa kweli kinatia msongo. Hali siyo nzuri kwa sababu hakuna kinachoendelea pamoja na bajeti kutengwa. Ukienda kituo pale ofisi za uhamiaji pale Babati hakuna kinachoendelea, ukienda kile kituo cha uhamiaji kule Kichakamiba halafu kina nafuu kidogo lakini bado, ukienda Chuo chetu cha Polisi Moshi bado, ukienda gereza kule Kilosa bado, hata ukija kwenye Gereza la Jimbo langu la Mwanga bado hali hairidhishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi ninachokiomba sana ni kwamba fedha zinazotengwa za miardi ya maendeleo kwa Wizara hii ziende tena ziende kwa wakati, vinginevyo tunajiingiza kwenye mazingira ambayo sio mazuri. Hali ikoje kimaslahi, malalamiko juu ya stahiki za askari yamekuwa mengi sana, kila siku wapo kwenye maswali na majibu tunayaona. Hili suala linahitaji kutazamwa sana kwamba tusibaki tubakakia na askari wetu ambao wanaishi kwenye malalamiko kila siku. Suala lingine ambalo ni la muhimu katika taasisi za Wizara hii ni suala la mafunzo na vifaa, taasisi zilizoko chini ya Wizara hii kama nilivyosema zina-*deal* na wahalifu zina-*deal* na wageni zina-*deal* na majanga. Sasa ili uweze kushughulika na mambo kama haya

na bado utimize sheria lazima mafunzo na vifaa uwe navyo vya hali ya juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameweka umuhimu mkubwa sana katika suala la haki jinai ndiyo maana akaunda na Tume ambayo ina wabobezi inazunguka kufanya kazi nzuri, lakini masuala yote yanaanzia kwenye Wizara hii. Mahakama haziwezi kufanya vizuri kwenye mambo ya uhalifu kama Wizara ya Mambo ya Ndani haifanyi vizuri. Tutaweka watu ndani, Magereza watatoka bado majambazi kama suala la urekebu halifanyiki vizuri. Kwa hiyo, tunapokuja kwenye suala la bajeti katika Wizara hii kwa kweli ni vizuri tukatilia kipaumbele kama ambavyo tunatilia kipaumbele Wizara zingine ambazo labda matokeo yao yanaonekana kwa macho, maana ukisema kilimo utaona mashamba kwa macho na chakula utakiona, ukisema madini utaona madini yanachimbwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa wanashughulika na jambo ambalo pengine halionekani kwa macho lakini lina umuhimu mkubwa sana ili hao mengine yaweze kufanyika. Liko suala ambalo limesumbua, Tanzania tu lakini limesumbua hata Dunia hasa Nchi za Afrika na Afrika Mashariki kwa sasa. Ni juu ya suala la hizi taasisi za dini pamoja na *NGOs* ambayo zinafanya mambo ambayo kwa lugha ya mtaani tunasema ni ya hovyo, lakini tuseme ni mambo ambayo ni kinyume cha sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo pamoja na mengine ambayo yapo lakini tatizo moja wapo ni suala zima la kuchuja hizi taasisi wakati wa usajili. Tunafahamu kwamba sheria inataka kabla taasisi haijasajiliwa idhaminiwe na taasisi nyingine ambayo tayari iko inafanya kazi. Sasa udhamini huu uko wa namna gani, siyo suala tu la kusaini *form* tu ambalo nadhani ndiyo linalofanyika. Umefika wakati sasa udhamini huu uende na uwajibikaji kwamba wacha niitolee mfano dini yangu mimi ili ni rahisi zaidi. Kama mimi nakuja nataka kusajili taasisi ya kikristo, nafikiri umefika wakati sasa Wizara ku-*rank* zile taasisi za kikristo ambazo tayari zipo, zile ambazo zimeshadumu miaka mingi na zina sifa ya kudhamini taasisi mpya ndiyo zipewe wajibu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhamini unakuaje? Lazima kusaini *form* ya kusema mimi *so and so* wa taasisi fulani nimesoma Katiba ya mwombaji na mafundisho yake, *Constitution and Doctrines*, nimeridhika kwamba kwa Katiba hii na kwa mafundisho haya huyu mwombaji anaweza akaendesha taasisi au kanisa *whatever* la Kikristo. Sasa akishasaini hivyo tukakubaliana siku naye akianza kuficha watu porini tutamuuliza, atakuwa ni sehemu ya kutusaidia katika ushahidi na katika kuiwajibisha hii taasisi kwamba mbona wewe katiba yako ilisema unafanya haya na haya, haya ya kupeleka watu porini ya kushindisha watu njaa, mbona yalikuwa hayapo katika katiba yako wala kwenye *doctrines* zako. Usipofika hapo tutaendelea kupata shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina fahamu kwamba utaratibu huu unafuata katika maana ya udhamini lakini hauendi *deep* kwenye kuhakikisha kwamba yule anayedhamini ni nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wakati tunaingia *Council of Legal Education* tuwe Mawakili ilikuwa lazima upate *referee,* lazima upate udhamini wa Wakili lakini siyo kila Wakili, ni Wakili ambaye amefikia *level* fulani ya *seniority* ambayo Mahakama inamuani kwamba huyu akituambia huyu kijana anafaa mruhusuni afanye mtihani wa uwakili anaweza, siyo kila mtu tu. Kwa hiyo, hili tunahitaji kuliangalia kwa makini sana lisije likatuvurugia Nchi kama ambavyo tumeona sehemu zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo lakini nisisahahu kupongeza taasisi zilizoko chini ya Wizara hii. Nikianzia Jimboni kwangu Mwanga, Polisi pale Mwanga jengo lao wamelikarabati kwa kuchanga kutoka kwenye mishahara yao na kuwakamata wadau wengine kama sisi, lakini wamelikarabati vizuri. Wananchi wa Jimbo la Mwanga hasa Tarafa ya Usangi wameungana wakajenga Kituo cha Polisi cha kisasa kabisa na hili nikuombe sana Mheshimiwa Waziri kwamba baada ya kukupitishia bajeti yako twende ukakitazame kile kituo ili tujenge na vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho pia niwapongeze Idara ya Uhamiaji, mradi mmojawapo ambao unafanya vizuri ni kile Chuo

pale cha Kichakamiba taarifa ni kwamba walianza kwa kukatana mishahara wachange wao wenyewe kutoka mishahara yao kuanza kujenga na ndiyo maana ile taasisi iko vizuri sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja na nawapongeza kwa kazi nzuri wanayofanya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Neema Kichiki Lugangira, atafuatiwa na Mheshimiwa Felista Njau, Mheshimiwa Ahmed Shabiby ajiandae.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia kwenye hoja hii ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Kwanza kabisa ningependa kuipongeza sana Serikali kupitia Mheshimiwa Rais, *Doctor* Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji mkubwa ambao Serikali inaendelea kufanya kwenye Jeshi la Zimamoto. Tarehe 22 Mwezi wa Tano nikiwa pale Bukoba tulipata ajali la moto kwenye Soko letu la Bukoba na kipekee niwapongeze sana Wanabukoba wenzangu pamoja na Jeshi la Polisi na Jeshi la Zimamoto kwa kazi kubwa waliyoifanya kuhakikisha ya kwamba moto ule unazimwa kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo yote yaliwezekana kutokana na uwekezaji mkubwa ambao umeendelea kufanyika kwenye Jeshi la Zimamoto. Kipekee namshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, maana Serikali imeshatuma shilingi milioni 600 ambazo zinalenga kujenga kituo cha zimamoto kwa pale Bukoba na kituo hiki kitajengwa katika Kata ya Miembeni pale Bukoba Mjini. Kwa hiyo nami kama Mjumbe wa Kamati hii ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama naendelea kuafarijika sana kwamba yale ambayo tunayashahuri yanafanyiwa kazi na uwekezaji mkubwa unaendelea kufanyika kwenye Jeshi letu la Zimamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu katika bajeti hii utakuwa katika maeneo matatu na nitaanza kwanza katika eneo

la idadi ya mahabusu. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayofanya ya kuhakikisha kwamba tunapunguza msongamano kwenye magereza yetu ikiwemo; moja, kutoa maelekezo kwamba mtu asipelekwe mahabusu mpaka upelelezi uwe umekamilika lakini pili, kuunda Tume ya Haki Jinai. Pamoja na hayo hivi sasa kwa takwimu za jana idadi ya mahabusu ni 12,012 na Serikali inatumia takribani milioni 640 kulisha mahabusu hawa kila mwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, milioni 640 kila mwezi zinaenda kulisha mahabusu hao ambao hawafanyi kazi hivyo hawawezi kuzalisha chakula ambacho wanakula. Asilimia kubwa kati ya hawa ni *petty offenders* kwa maana ya kwamba ni wale wenye makosa madogo madogo yenye dhamana lakini dhamana hiyo inakuwa haipatikani. Ili tuweze kuhakikisha kwamba tunaweza kupunguza msongamano kwenye magereza yetu, mimi napenda kupendekeza mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo napendekeza, Wizara itupe taarifa tokea Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan alivyotoa maelekezo kwamba mtu asiende mahabusu mpaka upelelezi umekamilika. Je jambo hilo limefanyika kwa kiwango gani? Ni muhimu sana tupate taarifa kamili ya utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Jeshi la Magereza lifanye tathmini wale mahabusu ambao wako nao 12,012 kati yao ni asilimia ngapi ya mahabusu hao wana makosa yale madogo madogo yenye dhamana kwa maana ya *petty offenders*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa tatu ni kwamba kumekuwa na changamoto kubwa kwamba mtu anakaa mahabusu kwa miaka mingi takribani miaka miwili, mitatu, mwaka na kadhalika lakini pale ambapo hukumu yake inatolewa ule muda aliokaa mahabusu hauhesabiki kama sehemu ya kifungu. Jambo hilo badala yake limeachiwa utashi wa Jaji ama yule ambaye anatoa hukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitarejea hivi karibuni Mfalme Zumaridi kule Mwanza, Jaji alivyotoa hukumu yake alitoa maelekezo kwamba sehemu ambayo ameshakaa mahabusu iwe ni sehemu ya kifungo na baada ya kauli hiyo kilichofanyika yule Mfalme Zumaridi alikaa magereza mwezi mmoja tu, kwa sababu ule muda ambao alishakaa mahabusu ulihesabika lakini jambo hili haliko *uniform*. Jambo hili linategemea wengine wanapata wengine hawapati, jambo ambalo ni hatari kwa usalama wa nchi yetu, kwa sababu inaweza ikaleta vurugu na wale ambao wako mahabusu wakajiona kwamba kuna wengine wanahaki zaidi kuliko wenzao. Kwa hiyo, mimi napendekeza kuwe kuna *uniformity*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne ni hapo kwenye suala la kupunguza msongamano wa magereza, napendekeza ya kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani ije na Mswada wa Sheria ya Dhamana *(Bail Act)*. Kwa sababu hivi sasa masuala ya dhamana ni kifungu kimoja tu katika sheria ya Mwenendo ya Mashauri ya Jinai *(The Criminal Procedures Act)* na ni kutokana na hivyo kumekuwa na mkanganyiko na *loop holes* nyingi ambazo zinapelekea kuchelewesha haki ya dhamana na haki jinai kwa ujumla wake. Kwa hiyo, mimi napendekeza Wizara hii ituletee Muswada wa Sheria ya Dhamana kwa maana ya *Bail's Act.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa eneo langu la pili nitaongelea suala zima pale Mkoani kwetu Kagera kwenye Magereza ya Bukoba. Tuseme mahabusu au magereza ambao wanaumwa ambao wanapata rufaa ya kuja hospitali ya Mkoa wanawekwa kwenye lile Gereza la Bukoba na wengine wanapata Rufaa kwenye Bugando, lakini Gereza la Bukoba halina gari la kuwasafirisha wafungwa hawa na mahabusu pale ambapo wanaenda kupata matibabu, badala yake wanawasafirisha kwenye magari mengine, magari ya kawaida pamoja na raia. Kwa kipekee sana naomba Wizara ione namna gani ambavyo itapatia Magereza ya Bukoba Mjini iweze kupata gari ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho kutokana na miundombinu ya Mkoa wetu wa Kagera na hali ya hewa naomba sana Mkoa wa Kagera uangaliwe kwa jicho la kipekee, ili tuweze

kupata magodoro, blanketi na sweta za kutosha. Maana hivi sasa katika magereza zetu nane za mkoa wa Kagera tuna takribani wafungwa na mahabusu zaidi ya 1900 na lakini tuna upungufu wa magodoro masweta na mablanketi kwa zaidi ya 15,000. Kwa hiyo, naamini sana kupitia ombi hili Magereza za Mkoa wa Kagera zitapata kipaumbele pale ambapo Jeshi la Magereza litaweza kutoa vifaa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na naipongeza sana Wizara, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Hamad Masauni, Mheshimiwa Naibu Waziri Sagini kwa kazi kubwa ambayo wanafanya na Viongozi wote wa vyombo vya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Neema. Mheshimiwa Felista Deogratius Njau, atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi ajiandae.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu sana, kwa maslahi mapana ya Taifa letu. Awali ya yote kwanza nitambue mchango mzuri na kazi, ufanisi, tija pamoja na uzalendo unaofanywa na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. Pia nitambue na nipongeze jitihada za Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye hivi karibuni siku ya Muungano Aprili 26, aliweza kutoa msamaha kwa wafungwa 376. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amekuwa na tabia ya kuingia moja kwa moja kwenye kero na kuzitatua. Mimi kwa hilo nampa hongera lakini si kwamba tu aliwaondoa wafungwa na kupunguza msongamano bali aliweza kupunguza gharama za matumizi ambazo kwa mwaka ni bilioni 338 ambazo zinatumiwa na hao tu 376.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tatizo la msongamano wa wafunga magerezani bado halijapatiwa jibu sahihi, ndiyo maana naona Mheshimiwa Rais alielekeza nguvu zake kule ili kuonyesha

njia ili na sisi wenye dhamana tuweze kupita huko kuona namna gani tunaweza kwenda kupunguza msongamano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi inayotakiwa kwa wafungwa ni 29,902 lakini iliyopo sasa ni 32,140, tayari tumezidiwa. Tusiende tu kukimbilia kwenye kujenga magereza lakini tutafute mwarobaini. Sisi tuliona kwamba Bodi ya *Parole* inaweza ikawa mwarobaini lakini zipo Sheria katika Bodi ya *Parole* ambazo zinakwamisha wasiweze kuchukua hatua. Sheria hizi zinatakiwa bodi ikae iweze kuzichakata ili kuona sheria rafiki zitakazosaidia ili kuweza kupunguza msongamano wa wafunga magerezani. Nikisema hivyo nirejee kipo kifungu ambacho kinaonyesha kwamba lazima aliyemshtaki mtuhumiwa aweze kuridhia na kusaini ndipo mtuhumiwa aweze kupata msamaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna mambo mengi, wanaweza kuwa na chuki, anaweza kuwa na hasira na asikubali. Kwa hiyo, wale watu wanabaki magerezani. Kwa hiyo kwa kiipengele hicho niombe Bodi ya *Parole* itakavyokaa ianze kuchakata sheria ziwe rafiki kwa ajili ya kupunguza msongamano kwa wafungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msongamano huu wa magereza unajumlisha Wahamiaji haramu. Bunge liliopita nilisimama kwenye Bunge lako Tukufu nikazungumza ni namna gani Wahamiaji haramu wanakomba pesa za walipa kodi na kwenda kukaa kwenye *picnic,* kwa sababu watu hawa hawawezi kufanya kazi ya uzalishaji. Tayari wamemaliza vifungo vyao, tuna wahamiaji haramu 2,609 wako wamekaa wanastarehe wanakula chakula, hawa wahamiaji haramu 2,609 wanatumia pesa za walalahoi, pesa za walipa kodi, pesa za watu wadogo wadogo ambao wanalazimishwa kulipa kodi wasipolipa kodi watachukuliwa hatua. Sisi tunachukua hatua gani kuwaondoa wahamiaji haramu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wahamiaji hawa haramu kama ilivyosema Kamati, wanatumia pesa nyingi kwa mwaka, wahamiaji hawa haramu wanatumia bilioni 2.3. Bilioni 2.3 ni pesa nyingi, ni pesa nyingi ukilinganisha na maisha yetu ya sasa, fedha hizi zingeweza kuelekezwa kwenye madarasa zingejenga

madarasa 117 na watoto wetu wangekaa sehemu salama, zingeweza kuelekezwa magereza huko huko zikaenda kwenye miradi ya maendeleo nao magereza wangeweza kufanya mambo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, itumike busara wakati Waziri anakuja ku-*wind up* aweze kuonyesha dira ya wahamiaji haramu, kwa sababu zipo hapa Wizara ya Mambo ya Nje, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Mambo ya Ulinzi, kaeni muone namna gani mnakwenda kutoa hii kansa ambayo imeenea kwenye Nchi yetu. Nikisema hayo naenda ku - *reflect* kwenye bajeti ya magereza, bajeti yao ni ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Maendeleo mwaka 2022/2023 wameomba shilingi 21,300,069,000. Hizi zilitengwa na Bunge, lakini fedha walizopata ni shilingi milioni 100. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Hee! Loh!

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Magereza wana shughuli za kufanya, wana rasilimali watu, wanaweza kufanya mambo makubwa, wamepewa shilingi milioni 100 sawa na 0.46%. Hatuwezi kwenda hivi. Kama tunawapa wahamiaji haramu shilingi bilioni mbili sawa na 20%, tunaachaje kuwapa hawa wazalishaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zetu tumewekeza, tunalisha watu wanaopita wanakuja kukaa hapa wanapunga hewa, tunaacha kwenda kuzalisha. Watu wa magereza waliweka mikakati 2020 wakasema wana vituo tisa wanaweza kuzalisha mazao mbalimbali, wakapunguza *burden* ya mafuta ya kula, wakapunguza *burden* ya mfumuko wa bei. Tungewapa fedha wakalime. Wana ardhi, wameziainisha vituo tisa. Tumeshindwa kuwapa fedha lakini fedha za kulisha wahamiaji haramu, wapita njia tunazo. Kiko wapi cha kumpa mtoto wa kambo chakula ukamwacha mtoto wako? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba lichukuliwe kwa u-*serious* kabisa, wakati Mama yetu anazunguka huku na kule ughaibuni kutafuta fedha, sisi tunakwenda kulisha watoto wa jirani

wanashiba sisi tunalala njaa. Naomba fedha inayotengwa na Bunge kwa ajili ya Bajeti za Wizara hii na Wizara nyingine kwa maslahi ya Taifa zikatolewe kwa wakati. Hazitolewi. Ukiwapa shilingi milioni 100, wakanunue nini katika shilingi bilioni 21? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka ninavyoongea leo, wako tu wako hapo. Vyombo hivi haviwezi kulalamika kutokana na *nature* yao ya kazi, lakini sisi tunakuwa midomo yao, tunawasemea. Wanafanya kazi kwa kinyongo, hawafanyi kazi vizuri, wanafanya kwa kinyongo lakini ni kwa sababu wamejawa uzalendo, wanafanya kazi hii na Taifa linaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Magereza ardhi waliyonayo ni ekari 19,770. Iliyotumika ni 3,850 sawa na 19% halafu mnalalamika hawa Magereza wamekuwaje? Wapeni hela tuwapime kwa kazi zao. Tuwape fedha wakafanye kazi. Wana uwezo mkubwa, wana ufanisi mzuri, wana uzalendo wa kutosha, wanaweza kuliletea tija Taifa, lakini wameshindwa kufanya kwa sababu tu hawana fedha za maendeleo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. muda wako umekwisha. Tunashukuru sana kwa mchango wako.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namalizia kwa kusema, Waheshimiwa hawa Jeshi la Magereza wapate stahiki zao, waweze kununua sare zao wenyewe. Wasinunuliwe, wanunue kwa wakati ili wawe *smart*. Saa nyingine unakutana nao hawaeleweki. Tuwasaidie wakasimame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby atafuatiwa na Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi na Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, ajiandae.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza nawapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakuu wote wa vyombo vya usalama kwa kazi nzuri wanazofanya, lakini nami leo nina michango yangu tu midogo midogo. Nitaanza na Uhamiaji. Pale Gairo mlisema tuwatafutie kiwanja kwa ajili ya kujenga ofisi. Kiwanja kipo, tunasubiri ofisi ije uhamiaji. Mwakani nikija, nakuja kivingine, naomba hiyo ijengwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni masuala ya Zimamoto. Nataka kujua tu, hivi ninyi Mawaziri mnavyopewa hivyo vyeo, mnakuwa waoga, mnakuwa kama sisi tu huku hatuongei na kwenye Mabaraza ya Mawaziri, mnakuwa wenzetu au mnakuwa vipi? Mimi unajua sielewi kabisa! Hili suala la Zimamoto liko chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Ukijenga jengo, yako majengo yanatoa mpaka Shilingi milioni 40, Shilingi 30, Shilingi milioni tano, wanalipia Zimamoto hata jengo hujaanza kujenga. Kwenye magari, kuna kodi ya Zimamoto, lakini ukiangalia kwenye miji yetu, magari ya Zimamoto hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nikupe mfano wa Dodoma, Makao Makuu ya Nchi ina majengo mapya mengi, majengo marefu mengi, ukienda kuangalia pale vigari vya zimamoto vile, hata moto ukiwasha na nyasi havizimi. Tatizo ni liko wapi kwenye upande wa Zimamoto? Ukienda kule Mtumba kuna majengo ya Serikali. Hata kama yale majengo yamewekewa vifaa vya Zimamoto, lakini yako wapi magari ya Zimamoto? Hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Dar es Salaam, ukienda kule Tegeta, wapi, hakuna. Sana sana utayakuta magari ya watu binafsi. Kuna shida gani na fedha ziko nyingi za zaidi ya kununua magari ya Tanzania nzima? Mfano, pale Gairo, amekuja Mheshimiwa Rais, ameongea na wananchi pale, amesema Gairo ijengwe Mahakama, imeshajengwa. Gairo yajengwe madaraja, yamo kwenye bajeti; Gairo ijengwe mfereji wa kuzuia mafuriko, imeshajengwa; Gairo iletwe gari la Zimamoto kwa sababu ni katikati ya Dodoma na Morogoro kwa ajili ya *accidents* zinazotokea pale barabarani, lakini mpaka leo hata mpango

hamna. Mmeleta watu wa Zimamoto zaidi ya sita. Sasa mnataka wazime na mikono?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake mtuambie basi, mtupe *course* wenyewe tu, hamna haja ya kuweka watu wa Zimamoto pale. Kama watu wa Zimamoto wako sita, wanapewa mshahara, lakini hakuna chombo chochote cha kufanyia kazi. Hilo ni agizo la Rais. Mheshimiwa Waziri, nataka ukija uwe na majibu ya kutosha, kwa sababu wakati ule alikuwa Waziri, Mheshimiwa Simbachawene. Sasa sifahamu kila akija Waziri mpya na mambo yanabadilika? Nilikuwa naliomba sana hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la *accidents* zinazotokea hasa kwenye magari yetu, mabasi. Mimi ni msafirishaji wa zaidi ya miaka 27 sasa, nafanya hiyo kazi. Kuna vitu vingine hamtaki kushirikisha wadau. Mkiita wadau, mnaita wapiga debe, wale wadau wahusika kabisa hamtuiti tuwapeni ushauri. Toka enzi ya Hayati Mwalimu Nyerere, akaja Mheshimiwa Mwinyi, akaja Hayati Mkapa, mpaka leo, ukienda *LATRA* kuchukua leseni ya usafirishaji; kwa mfano, kama unatoka Dar es Salaam kuja Dodoma unapewa na kitu kinaitwa *time table* kwamba gari itatoka Dar es Salaam saa ngapi, itafika Chalinze saa ngapi, itafika Morogoro saa ngapi, itafika Gairo saa ngapi, na itafika Dodoma saa ngapi? Zile *time table* zinawekwa kulingana na *speed* ambayo unatembea, unawekewa na kituo, ukiingia dakika tano, utoke, yaani kila kitu inaeleza kwamba gari inatakiwa ifike saa ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadaye mkaleta *speed governor,* zimefanya kazi, zikafeli kwa sababu madereva wanazichezea, wanaweka *switch,* hazina kazi yoyote. Zimefeli *speed governor.* Sasa hivi mmeleta *VTS.* Nayo kuna kipindi inafanya vizuri, kuna kipindi nayo inachezewa. Sasa tena nimekusikia Waziri tena unarudisha tena *speed governor* ambayo ilifeli mwanzoni. Msifanye mchezo jamani. Nani atanunua kila siku? Eti mtu una gari 60 ukanunue *speed governor* shilingi 1,800,000 kwa magari 60 ambayo ilishafeli na unajua kabisa dereva ataichezea. Kwa nini msiweke utaratibu wa kufuata *time table*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mweke *speed* 95. Haya magari ya sasa hivi siyo *speed* 80 na hata ukiangalia Sheria ya *Traffic, speed* 80 haiko kisheria. Inasema iwapo *TANROADS* kama wataweka kibao cha *speed* 100 ndiyo hizo hizo, lakini sisi tumeweka kichwani kwamba ni *speed* 80. Wekeni *speed* 95. Magari ya sasa hivi hayatumii breki tu, yanatumia na umeme ambapo ni kitu kinaitwa *retarder* kuwa kama breki. Wekeni *speed* 95, fuateni *time table,* gari ikitoka Dar es Salaam, Chalinze imewahi weka pembeni gari, piga faini. Inakuja mpaka Morogoro, gari imewahi, piga faini, weka gari pembeni isiondoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kipindi hapa niliona mabasi yamekamatwa pale Same. Askari wa Same walikuwa wanafanya kazi vizuri sana, lakini kuna baadhi hata ya Wabunge hapa wakaanza kupiga kelele, wananchi wanateseka. Siyo wanateseka, Polisi wafanye kazi yao bila kufuata watu wa siasa. Gari imewahi, *time table* inapokuonesha, weka pembeni piga faini. Dereva baadaye atapigwa na abiria, akionekana anawahi wahi tu, mwishowe abiria watambadilikia. Watampiga. Hiyo ndiyo kumaliza *accidents.* Sasa kama tuna Polisi kila kona na wanashindwa kuangalia *time table* na *time table* za kila gari wanazo, haiwezekani kitu kama hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni masuala ya kikotoo. Kwenye Jeshi la Polisi, tunapata taabu, tunawaona ndugu zetu, jamaa zetu, wako kama pale Gairo, wako sehemu nyingine. Kikokotoo wanachotumia cha mafao ni kikokotoo cha watumishi wa Umma. Kwa nini wasitumie kikokotoo kama wanachotumia JWTZ au *TISS?* Leo Askari anamaliza kazi yake, amefanya kazi miaka 30 anakwenda anakuwa masikini wa kutupwa, anakufa hata kabla ya siku zake. Hiyo lazima tufanye haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata uhamisho. Utakuta kwenye uhamisho miaka 10 mnahamisha Askari hapa, mnapeleka pale, miaka 10 hamjawalipa. Wako wanaodai mpaka Shilingi milioni 100, wako wanaodai mpaka Shilingi milioni 80. Kwa hiyo, kwenye Wizara mnazidi kuongeza mzigo. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shabiby, taarifa kutoka kwa Esther Matiko.

**TAARIFA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka nimpe tu taarifa, licha ya kwamba wanapewa kwa kama watumishi wengine na siyo kama JWTZ, lakini pia hata hayo mafao yao kwa maana ya michango wanacheleweshewa kupeleka. Wakistaafu wanaenda kufuatilia mafao yao wanaambiwa, hawawezi kupewa mafao mpaka watoe riba. Yaani wakatwe wenyewe ile adhabu ambayo wanatakiwa walipie waajiri wao ambao ni Serikali, wanalipa wao wenyewe. Kwa hiyo, unakuta Askari hawa wengine mpaka wanafariki hawajapewa mafao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka nimpe tu hiyo taarifa iwe kwenye kumbukumbu yake.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shabiby, taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nilikuwa naitaka hiyo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hawa Askari saa nyingine mnasema wanakula rushwa, hata mimi ningekuwa Polisi ningekula, kwa *style* hii. Ndiyo ukweli huo. Lazima mafao yao jamani wapate. Unajua kuna vitu vingi sana tunachangia tu, tunachukia, lakini tunaangalia kuanzia mishahara yao? Tunaangalia kuanzia maslahi yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Hiyo ni kengele ya mwisho Mheshimiwa?

**MWENYEKITI:** Muda umeisha..

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Ni kengele ya pili?

**MWENYEKITI:** Ndiyo.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Dah, haya bwana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Shabiby. Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi na mchangiaji wa mwisho mchana huu ni Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa fursa hii ya kuweza kuchangia mchana wa leo katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya, pia kwa jitihada kubwa ambazo Mheshimiwa Waziri amezizungumzia hapa; kutafuta fedha mbalimbali katika kuhakikisha kwamba wanaboresha mifumo kwenye Jeshi letu hili la Polisi na majeshi mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana kwa kazi kubwa unayoendelea kuifanya. Mimi kama mdogo wako, nina imani kubwa sana na wewe na uwezo wako ulionao. Wewe pamoja na Naibu Waziri wako. Nataka nikusihi jambo moja tu Mheshimiwa Waziri kwamba utaandika kitabu chenye historia nzuri sana kama utafanya mabadiliko na mapinduzi makubwa sana katika kuliboresha Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi kwa sasa ukienda kwenye mawanda ya ajira utaona kabisa imepewa kipaumbele cha mwisho katika kutafuta ajira ama kuombwa ajira. Uki-*compare* na hapo mwanzoni Jeshi la Polisi lilivyokuwa lilikuwa na heshima kubwa sana. Leo hii tuna baadhi ya Maafisa wa Polisi wakubwa tu akiwemo *IGP* mwenyewe Wambura, wakiwemo akina Msangi, akina Mkumbo nimemwona hapo na wengine, akiwemo *RPC* wangu wa Shinyanga Mama yangu, ni mfano ulio bora kwa maafisa wenye weledi, wanafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kadiri siku zinavyokwenda Mheshimiwa Waziri mwenyewe umeona kumekuwa na sintofahamu ndani ya Jeshi la Polisi. Nidhamu, weledi, rushwa na mambo mengine. Haya yote kama alivyosema kaka yangu Mheshimiwa Shabiby hapo, ni kwa sababu maslahi ya Askari wetu ni mabaya mno. Askari ambao wanatulindia mali zetu, Askari ambao wana-*risk* maisha yao, leo hii Askari anayefanya kazi miaka 60, anapostaafu, anaondoka na Shilingi milioni 18. Hivi hata kama ni wewe Mheshimiwa Waziri, usingefurahi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado hata *pension* utaona, mtu aliyetumikia Taifa kwa miaka zaidi ya 60 anaondoka na Shilingi 40,000. Ndiyo maana nikatanguliza kukuomba kaka yangu, utaandika kitabu kizuri sana kama utaenda kusimamia vizuri kwa weledi maslahi ya hawa watu ili waweze kufanya kazi kwa bidii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kwenye Jimbo langu la Msalala. Wilaya ya Kahama ina Halmashauri tatu, lakini Halmashauri hizi kwa maana ya Ushetu, Msalala na Kahama Manispaa; Msalala tuna *OCD,* lakini *OCD* yule hana gari, *OCD* mwenyewe anakwenda kukagua tukio kwa bodaboda, akishuka pale amejaa vumbi, hata haeleweki. Nakuomba kaka yangu kwa uchungu mkubwa, maeneo yetu hasa sisi tunaotoka kwenye mazingira ya mgodi, cha kushangaza, hawa hawa ndio Askari ambao wanaenda kulinda mali, migodi mikubwa hii. Hivi Mheshimiwa Waziri unashindwa kufanya kikao hata na hawa wawekezaji wakubwa kwenye maeneo yetu kama *Barrick* kuwaomba walau wachangie magari kwa ajili ya maaskari wetu ambao wanalinda mali zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia askari hawa wamekuwa wakidharaulika kwenye maeneo mengine. Leo hii wanaacha kufanya kazi ya uaskari, kwenye maeneo yetu utakuta askari ndiyo mchimbaji anaingia kwenye duara. Kwa nini? Kwa sababu maisha ni magumu, hajielewi. Boresha maslahi Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunazungumzia habari ya rushwa. Rushwa inatokea kwa sababu ya mazingira magumu.

Nenda kaimarishe mifumo kwenye Jeshi la Polisi. Siyo kila kitu kinaweza kikafanywa na watu wenyewe. Leo tunazungumzia habari ya tochi. Kwani hakuna mfumo, hakuna *system* ambayo unaweza ukaifunga Mheshimiwa Waziri? *Cameras* au kukawa na *checking point* walau kutoka hapa kwenda Dar es Salaam kukawa na *checking point* mbili? Funga *camera,* funga vifaa vya kisasa ambavyo vitasaidia kuonesha kwamba vinaweza kulinda usalama wa barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nizungumzie habari ya magari. Naomba sana, kwenye Jimbo la Msalala, Halmashauri ya Msalala, Halmashauri ya Ushetu, tusaidie magari. Bado mpaka sasa utaona, hata kwenye misafara hii, magari yaliyoletwa yale ya *Land Cruiser* wanazotumia ma-*OCD,* ma-*RTO* bado zimechoka mno. Unakuta *Land Cruiser* iko kwenye msafara, tairi inatembea inacheza inakatika, inakatika, inakatika. Naomba sana Mheshimiwa Waziri katika bajeti hii, pia peleka maombi kwa Mheshimiwa Rais aone namna ya kuweza kusaidia kununua magari mapya kwa ma-*OCD* wetu kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nizungumze habari ya vituo vya Polisi. Nampongeza sana *RPC* wangu wa Mkoa wa Shinyanga. Huyu mama anafanya kazi kubwa sana. Nimekuwa nikilia hapa toka mwaka 2022 kupatiwa vituo vya Polisi maeneo yetu hayo ni maeneo hatarishi sana maeneo ya migodi. Mama ameweza kufanya jitihada nami mwenyewe nimemchangia, sasa hivi tunanyanyua vituo vitatu vya Polisi Isaka, kituo kimoja kinanyanyuka na bado hakijakamilika. Naomba kwenye bajeti hii upeleke fedha tukamalize Kituo cha Polisi cha Isaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunanyanyua kituo kingine cha Polisi Kata ya Ngaya, tumeezeka, tunatakiwa tumalizie. Naomba muunge mkono *RPC* wako wa Shinyanga tukamalizie Kituo cha Polisi hiki. Tunajenga Kituo cha Polisi kingine Kata ya Mwaluguru kitahudumia kata tatu. Tayari kiko kwenye lenta. Nakuomba peleka fedha twende tukamalizie vituo hivi. Huyu mama ameona aanze jitihada mwenyewe binafsi kuhakikisha ya kwamba tunakuwa na vituo vya Polisi kwenye maeneo yale ili tuweze kulinda usalama wa raia na mali zao kwenye maeneo hayo. Kwa

hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, hali ya vituo vya Polisi kwenye maeneo baadhi, ni mbaya mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Kata ya Busangi tuna kituo cha Polisi lakini kimebomoka upande. Askari wamekaa mle ndani kwenye gofu. Muda wowote linaweza likadondoka. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri uone namna ya kupeleka upeleke fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nizungumzie habari ya *NIDA*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ahsante sana.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie hili la mwisho. Suala la *NIDA*, bajeti iliyopita ya mwaka 2022 nilizungumza hapa, nikasema suala la *NIDA* ni changamoto kubwa mno na nikatoa mfano nikasema mnazidiwa hata na Klabu ya Yanga! Leo hii kwenye maeneo yetu hakuna jambo lolote linaloweza likafanyika mpaka mtu awe na kadi ya *NIDA*. Mmefeli wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wewe ni rafiki yangu, ni kaka yangu, lakini kwenye hili mimi nashika shilingi. Mheshimiwa Shangazi uko hapo, uniandike. Nashika shilingi ya mshahara wako mpaka uje unieleze, mna mkakati gani wa kuhakikisha ya kwamba mnatatua tatizo la kadi za *NIDA*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, mchangiaji wa mwisho mchana huu.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kunipa hii nafasi ya kuchangia leo kwenye bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani lakini kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kaka yangu *Engineer* Masauni lakini Naibu

Waziri kaka yangu Sagini kwa kazi kubwa mnayoifanya. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Rais kule kwetu Manyoni amefanya mambo makubwa sana. Ameleteta miradi mingi sana lakini vilevile ametusaidia sana kwenye upande wa Jeshi la Polisi. Ninamshukuru vilevile Katibu wa Wizara ya Mambo ya Ndani na Naibu Katibu Mkuu kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya kwa Taifa letu lakini ususani katika Jimbo la Manyoni Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo na maeneo mawili takayoenda kuchangia. Eneo la kwanza tachangia upande wa Jeshi la Polisi lakini nafasi ikininiruhusu tachangia kuhusu Jeshi la Zimamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimshukuru vilevile *RPC* wa Mkoa wa Singida Afande Stella. Kwa kweli huyu dada yetu ametusaidia sana sisi Manyoni. Manyoni kulikuwa na mauaji yaliyokuwa yakiendelea, niliongea hapa Bungeni, lakini vilevile Mheshimiwa Waziri ulitoa maagizo kwa Afande Stella na ukafanya mabadiliko pale Manyoni. Tumepata *OCD* mpya lakini na taarifa tayari mmeleta mmpelelezi bado hajafika. Kwa hiyo nimshukuru sana Afande Stella lakini kipekee nikushukuru sana Waziri na Naibu Waziri kwa kulichukua hili kwa umakini kabisa na hali ya usalama Manyoni inaendelea kuimairika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini upande wa Jeshi la Polisi kuna suala la Vituo vya Polisi vya Kata. Wenzangu wametangulia kusema, Mheshimiwa Idd ameongea hapa, katika Jimbo langu la Manyoni Mashariki maeneo mengi kwanza hayana Vituo vya Kata vya Polisi lakini Vituo vya Kata vingi vya Polisi ni vibovu na ni vichakavu. Kwa mfano na Kituo cha Kata cha Sanza ni kibovu sana, lakini hata pale Heka ni kibovu sana. Mbaya zaidi nilishawahi kuchangia hapa Bungeni, katika Kata ya Kintinku pale Askari na Polisi wanatumia gala la *EFAD* kama kituo cha polisi. Hii ni aibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe kaka yangu *Engineer* Masauni, naomba unisaidie tuanze na hili la Kituo cha Polisi katika Kata ya Kintinku. Lakini pia nina Kata zaidi ya nane ambazo hazina vituo vya polisi, zikiwemo Kata za Sasilo, Chikola,

Makutupora, Kata ya Saranda na Kata ya Majiri. Nafasi itakapo ruhusu niwaombe basi na hizi kata nazo tuweze kuziangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine kwenye hii Kata ya Kintinku ulimuagiza *RPC,* Afande Stella; alishafika katika Kata ya Kintinku akakagua eneo wananchi wametenga ekari tatu kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha polisi cha kata. Kwa hiyo tayari sisi tuna eneo ekari tatu na Naibu Waziri uliniaidi utakuja kuliona hilo eneo, bado ujatimiza kaka yangu Sagini; nakuomba ufike ili uweze kuliona hilo eneo. Lakini ningeomba kwenye bajeti ya mwaka huu twende tukawajengee kituo cha polisi katika Kata ya Kintinku lakini mnifikirie vilevile kwenye kata hizo zingine nilizozitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni uhaba wa vitendea kazi upande wa polisi. Katika Wilaya ya Manyoni kulikuwa na mauaji sana yaliyokuwa yakiendelea lakini hali imeanza kutulia *RPC* wa Mkoa alimua kuchukua gari kutoka Mkoani kulileta Manyoni kwa sababu Manyoni hawana gari. Nikuombe Mheshimiwa Waziri, itakapotookea fursa ya magari utuletee gari la polisi Wilaya ya Manyoni ili liweze kusaidia katika doria mbalimbali. Lakini vilevile umesema hapa mnaende kununua pikipiki kwa ajili ya vituo vya kata. Naiomba hiyo fursa vilevile kwenye vituo vyangu vya kata vya polisi ili anagalau tuweze kupata hizo pikipiki ziwasaidie ndugu zetu na watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu Jeshi la Zimamoto. Kaka yangu Shabiby ameeleza hapa, na mimi naomba niongee hili. Mheshimiwa Rais anazunguka duniani kutafuta wawekezaji. Ile Filamu ya *Royal Tour* imeleta wawekezaji wengi sana, watu wamekuja wanawekeza. Lakini tuna tatizo moja, zimamoto ya Tanzania ni kama mtoto yatima, amesahaulika ndugu zangu. Unaenda kwa mfano mkoani pale tuna gari moja la zimamoto nalo ni bovu. Sisi tuna wilaya takribani sita, hakuna hata gari moja kwenye wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwenye Jimbo langu la Manyoni nina miradi mikubwa. Tuna ujenzi wa shule ya wasichana

ya bilioni nne, tuna mradi wa bilioni 12 wa maji, lakini tuna ujenzi wa *VETA* tumepewa 1.4 bilioni; hii miradi inajengwa, *it's very risk,* hatuna zimamoto pale Manyoni, wamejenga kaofisi utafikiri banda la kuku. Mheshimiwa Waziri naomba ufanye mageuzi kwenye Jeshi la Zimamoto. Huu uwekezaji ambao mnauleta hatutatengeneza *confidence* kwa wawekezaji kama mtu anakuja kuweza *billions of moneys* halafu hakuna uhakika wa Zimamoto, *it's so risks.* Kwa hiyo nikuombe kaka yangu *Engineer* naomba sasa mkatoa kipaumbele sana kwenye Jeshi la Zimamoto huko ndiko ambako tunahitaji kutengeneza *confidence* kwa wawekezaji. Mwekezaji anapokuja akagundua kwamba tuna Zimamoto, tuna mifumo ya zimamoto, tuna magari tuna ofisi, tunawafanyakazi anakuwa na uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tuna pigana kujenga viwanda kila eneo lakini unakuta maeneo mengi hayana zimamoto. Kaka yangu pale Shabiby amesema Gairo pale, hapa penyewe mjini ametolea mfano, tuna majengo mengi ya Serikali kule Mtumba, lakini tukiuliza mifumo ya zimamoto, magari ya zimamoto ni machache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimamoto ni mtoto yatima, sasa tunataka asiendelee kuwa mtoto yatima, kwa sababu Rais amepeka nguvu nyingi kwenye uwekezaji, tunahitaji kuweka nguvu nyingi na sisi katika kuimarisha Jeshi la Zimamoto… *(Makofi)*

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Chaya, taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Saashisha.

**TAARIFA**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nataka nimpe taarifa tu kwamba hapo awali miaka ya 80 Jeshi la Zimamoto lilikuwa linasimamiwa na *local government,* kwa maana ya uendeshaji wake ulikuwa chini ya TAMISEMI. Tumeisha shauri hapa nyingi; kama huku imeshishindikana basi bora warudishe kwenye halmashauri hizi

zenye nguvu ili waweze kuhudumia chombo hiki na ufanisi uweze kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kumpa taarifa hiyo tu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Chaya taarifa unaipokea?

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa hiyo taarifa lakini bado mimi nisinge shauri lirudi halmashauri. Bado Wizara hii hii ya Mambo ya Ndani inayo uwezo wa kusimamia hiki kitengo cha zimamoto kwa sababu uwezo wanao, watalamu wanao, tukipeleka huko halmashauri tunaweza tukaleta matatizo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi bado naendelea kuishauri kwamba tunahitaji kuhakikisha tunaweka nguvu sana kwenye Jeshi la Zimamoto. Huu uwekezaji ambao tumesema tunawekeza Mama Samia amezunguka nchi nzima anavutia wawekezaji wamekuja Tanzania, wanaweka viwanda, wanaweka mitambo lakini hatuna mifumo mizuri ya Zimamoto kwa hiyo niombe Serikali sasa katika bajeti hii na bajeti ijayo… *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Chaya kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Matiko.

**TAARIFA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimi Mwenyekiti, nilikuwa nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Dkt. Chaya kwamba ingefaa kwa zile Majiji au halmashauri zenye uwezo waweze kuchukua hili suala la Zimamoto maana yake tumeo fedha tunatenga kwenye Wizara lakini haziendi. Kwa hiyo ukiacha ile pesa ya Mambo ya Ndani tutaendelea kuona rasilimali za Watanzania zikiteketea kwa sababu hatuna vyombo vya zimamoto, kwenye Halmashauri zenye uwezo zipewe jukumu la kuwa na hizi zimamoto, zitasaidia sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Stephene Chaya taarifa unaipokea?

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa hiyo taarifa na nakubaliana na Esther Matiko kwamba kwa Majiji ambayo yenye uwezo wa kununua hii mitambo ya zimamoto wanaweza wakanunua lakini bado hili ni jukumu la Wizara, ninaamini kaka yangu MheshimiwaMasauni bado hajashindwa na ndiyo maana namshauri sasa, kwenye bajeti hii tunataka kuona mnaenda kuwekeza kwenye zimamoto. Wizara mna uwezo wa kusimamia hii sekta, tunataka uwekezaji mkubwa ambao Mheshimiwa Rais anavutia sasa hivi, tutengeneze *confidence* kwa wewekezaji, hakuwezi kuwa na *confidence* kwa wawekezaji kama kuna *risk* kubwa hususana kwenye suala la zimamoto, kwamba mifumo yetu ni mibovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwakweli kaka yangu Masauni unafanya kazi nzuri sana. Kwanza ni msikivu, pia Mheshimiwa Naibu Waziri ni msikivu, mara nyingi unapokea simu zetu unajibu meseji hata usiku. Baada ya kusema haya naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Chaya, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha mchana. Yako matangazo machache; moja ni wageni waliyoingia muda huu Bungeni. Wageni waliyotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 82 kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara *CBE* Kampasi ya Dodoma. Ahsante karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nawakumbusha tangazo la Katibu wa Bunge kwamba Waheshimiwa Wabunge wote Wizara ya Maliasili na Utalii imendaa semina leo hii baada ya kusitisha shughuli za Bunge kwenye ukimbi wetu wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, jioni tutaendelea na uchangiaji. Tutaanza na Mheshimiwa Almas Athuman Maige, atafuatiwa na Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah na orodha bado iko ndefu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema haya nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja kamili jioni.

*(Saa 7.08 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala ulio mbele yetu wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Tutaanza na Mheshimiwa Almas Athuman Maige, atafuatiwa na Mheshimiwa Maida Hamad Abdalla na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, ajiandae.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniruhusu nichangie hoja hii ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitajikita kwenye jambo moja tu la kujaribu kuelezea Sekta ya Ulinzi Binafsi *(Private Security Industry)*. Sekta hii ilianzishwa huko Ulaya miaka mingi iliyopita, lakini ilianzishwa baada ya kuwa na sheria zake zote na kanuni zake ndipo wenzetu wale wakaanzisha hii sheria. Sekta hii ya ulinzi binafsi hapa kwetu Tanzania imeanza mwaka 1980 yaani miaka 43 iliyopita na hapakuwa na sera wala sheria wala *GN*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii inafanya kazi chini ya mwamvuli wa ulinzi wa raia na mali zao na wakishirikiana na Jeshi la Polisi, lakini sekta hii inafanya kazi zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ulinzi wa watu (*man guarding*), kusindikiza hela (*cash in transit*), ulinzi wa mitambo (*security installation*) kama tunayoiona hapa Bungeni, huduma za zimamoto (*fire rescue),* upelelezi binafsi *(private investigation),* lakini na ulinzi wa watu binafsi ambao unaitwa *bodyguard* au kifupi *bouncers.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta sasa imeajiri ajira karibu 450,000 nchi nzima na hili ni jeshi kubwa sana. Linasaidia sana kupata kodi, lakini pia limesaidia ajira kwa vijana wetu. Sasa yako makampuni elfu mbili na zaidi, wakati ilipoanza mwaka 1980 ilikuwa na kampuni mbili tu, lakini sheria inazotumia ni za kiraia yaani sheria ile ya *BRELA* ya Usajili wa Makampuni, lakini Sheria ile ya Ajira na Mahusiano Kazini ya Mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria zote hizi mbili ni za kiraia na hazifai kutumia kwenye sekta ya ulinzi binafsi kwa sababu sekta ya ulinzi binafsi ni karibu jeshi. Kwanza wanavaa kijeshi, lakini vile vile wanafanya kazi zile zile kama za polisi yaani kulinda raia na mali zao, lakini wanavaa sare za kijeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilianzia wapi hii sekta ya ulinzi binafsi? Ilitokana na ombwe mwaka 1980 wakati Mheshimiwa aliyekuwepo, *IGP* Philemon Mgaya alipomwomba Mheshimiwa Rais wakati ule Mheshimiwa Mwinyi, ili wapate fursa ya kulinda mali ambazo zilikuwa zimetaifishwa na Azimio la Arusha, wakarudishiwa wenyewe mwaka 1980 na kuondoa mgambo au polisi waliokuwa wanalinda mali hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo pakawa na ombwe kubwa sana hakuna sasa walinzi na kwa vile ilikuwa haraka haraka Mheshimiwa Rais Mwinyi akatoa ruhusa ya kuanzisha sekta ya ulinzi na ndipo yakaja makampuni mawili la *Group Four* na *Ultimate Security.* Tangu hapo makampuni yamekua na kuendelea kufanya kazi ambazo nimezitaja hapo juu kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa limejitokeza, yako mapungufu makubwa na mengi kwa sekta hii binafsi kuendeshwa bila sheria, kanuni wala miongozo. Kwa hiyo hatuna sheria wala mamlaka, kule nje kuna mamlaka *(Private Security Industry Authority)* kama vile *EWURA* au *TCRA* na kadhalika. Kwa kukosekana mamlaka hizo *Private Security Industry Authority (PSIA),* kampuni za ulinzi hazina madaraja. Ukitangaza kazi kampuni yoyote inaomba kazi bila madaraja. Tofauti na wakandarasi. Wakandarasi lazima uwe daraja la kwanza mpaka la saba, lakini makampuni haya hayana madaraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni haya ya ulinzi hayatambuliwi na mashirika ya kigeni yanayokuja hapa kwa sababu hayana *certification,* hayana uthibiti. Kwa hiyo makampuni haya yanazurura tu na yanapata tabu sana ikitokea kazi, kwa mfano, kwenye gesi kwenye *oil,* lakini pia kwenye migodi, lazima yajiunge na kampuni nyingine ya nje ili yapate kazi huko na imekuwa hasara kubwa sana na huduma kwa kampuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako matukio mengine mabaya sana katika sekta hii kutokana na kutokuwepo kwa sheria, kwa mfano, walinzi kushtakiwa kwa mauaji. Watu wamevamia lindo na askari ana bunduki, akipiga akaua jambazi anashtakiwa kwa mauaji, wakati polisi wakipiga jambazi wanapongezwa na kupewa vyeo, lakini wote wanafanya kazi zile zile. Hili ni pungufu moja kubwa sana. Bahati nyingine wakati fulani hawa askari walinzi binafsi walitoka kwenye Jeshi la Polisi au Jeshi la Wananchi. Wana vyeo vikubwa wale walinzi kuliko wale walinzi ambao wako pale pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, wateja wa sekta kuumizwa na kukosa pa kukimbilia. Kwa hiyo wako watu sana waliajiri walinzi, lakini wakaumizwa. Walinzi kugeuka majambazi, wakawaibia wateja wao, lakini pia walinzi kuwadhulumu wateja kwa mfano, wizi wa Tawi la *CRDB* Azikiwe, mabilioni yalichukuliwa kwa mpango wa kupanga, lakini pia kesi ya Kasusula mnaifahamu, alitumwa kwenda kuchukua dola 2,000,000 akaondoka nazo kutokea *Airport*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wizi wa *NBC* Moshi mabilioni yalichukuliwa. Walinzi wa shule ya sekondari ya wasichana huko Tabora mchana wanalinda, usiku wanaenda wanawaibia wasichana, wakampiga mlinzi akafa, lakini walinzi kuuawa malindoni huko Temeke, walinzi waliuawa pamoja na mlinzi mmoja wa polisi na mlinzi mmoja aliyekuwa Sajenti Mstaafu wa sekta ya ulinzi binafsi. Mambo mabaya yalitokea pale. Yule Polisi aliyekuwa *junior staff* akazikwa kwa bendera ya Serikali huyu wa sekta binafsi akatupwa kama maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tiba ya kasoro hizi ni kuwezesha sekta ya ulinzi binafsi iwe na sheria yake. Iwe na mamlaka yake *Private Security National Authority* na hii itatokea tu kwa kuleta sheria ndani ya Bunge lako. Nilileta sheria ya sekta hii hapa mwaka 2016 na Serikali iliipenda sana ikaichukua sheria hiyo kwa mategemeo kwamba wangeiletea haraka iwezekanavyo lakini nashangaa mpaka leo haijaja. Kwa hiyo nimwambie Waziri nina mpango wa kukamata shilingi niende nayo Uyui aifutae huko Tabora Uyui ili atueleze, nataka tu *commitment* ya Serikali, Serikali itoe ahadi lini sheria hii itakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, nakushukuru sana kwa muda wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maige. Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah atafuatiwa ma Mheshimiwa Hamida Mohammed Abdallah na Mheshimiwa Martha Festo Mariki ajiandae.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na afya njema na hadi kuweza kusimama katika Bunge hili tukufu jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya katika Taifa letu na kuimarisha majeshi yetu haya kuhakikisha kwamba changamoto wanazokabiliana nazo zimeondoka ili kuimarisha suala la amani na utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote, lakini pia niwapongeze majeshi yetu yote nchini kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya ya kuhakikisha kwamba usalama wa raia pamoja na mali zao umepatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze katika Jeshi letu la Polisi lakini kupitia ufinyu wa bajeti, wastaafu wa Jeshi la Polisi, pamoja na mifumo ya kumbukumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jeshi letu hili tunatambua kwamba limekuwa likifanya kazi kubwa na ya mfano katika Taifa letu na wanafanya kazi usiku na mchana, lakini la kusikitisha wana changamoto kubwa kutokana na ufinyu wa bajeti katika utekelezaji wa majukumu yao. Kitengo cha mafuta kinasuasua, mishahara yao inasuasua, magari mabovu, ofisi hazijulikani, vifaa vya ofisi havijulikani. Tumekuwa tukipitisha bajeti hapa na kuona kwamba angalau kutakuwa na unafuu katika utekelezaji wa majukumu yao katika utekelezaji wa bajeti hiyo, lakini baada ya bajeti ile kupitishwa tu changamoto zile zinaendelea kuwepo siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yetu kwamba katika bajeti hii ambayo Mheshimiwa Waziri ameiwasilisha hapa, taarifa ya bajeti ni nzuri, imepangika vizuri, ni mategemeo yetu kwamba utekelezaji wa bajeti hii utaweza kwenda kulenga changamoto zote zile zinazowakabili jeshi hili katika maeneo yote Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Serikali kwa juhudi zake ambazo zinaongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya hadi kuhakikisha kwamba jeshi letu hili au majeshi yetu haya yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Mkoa wa Kaskazini Pemba pamoja na changamoto hizo nilizozitaja, zipo changamoto kadhaa ambazo jeshi hili wamekuwa wakikabiliana nazo. Katika changamoto hizo moja ilikuwa ni magari, tunaishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mkoa wa Kaskazini Pemba tumeweza kupatiwa magari mawili. Gari

moja liko pale Makao Makuu ya Mkoa, lakini gari lingine limeelekezwa katika Kituo cha Polisi Mchanga Mdogo. Wanafanya kazi kwa kuhudumia wananchi kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa ni mafuta, hawana mafuta ya kufanyia kazi, uchakavu wa ofisi pamoja na vifaa vya ofisi, lakini pia majengo chakavu. Majengo yote ya Mkoa wa Kaskazini baadhi tu lakini askari wengi wanakaa uraiani. Si vema Askari Polisi pamoja na kazi zao kukaa uraiani kwa sababu kuna kazi zingine wanazofanya wanarudi usiku lindoni na mambo mengine. Kwa hiyo ni vema tukakarabati zile ofisi hasa pale polisi *line,* kuna ofisi nzuri tu ambazo majengo yake tumeyarithi kwa kipindi kirefu, kwa hiyo ningeomba yafanyiwe ukarabati mkubwa kwa sababu majengo yale ni mazuri. Pale kuna Mesi na mambo mengine, huduma za afya na mambo mengine. Kwa hiyo yakikarabatiwa majengo yale na majengo mengine yaliyoko Michewene na vituo hasa kituo kingine Matangatuani na Konde kwa hiyo Mkoa wa Kaskazini Pemba tutakuwa tumeondoa changamoto kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wastaafu. Kumekuwa na ukwasi mkubwa kuhusu suala la wastaafu wa Jeshi la Polisi. Mara nyingi unapotegemea kustaafu unategemea kwamba utapata haki ambayo itaweza kukusaidia katika maisha baada ya kustaafu. Askari wetu hawa wamekuwa wakidhalilika katika hali ya umaskini sana na wanaodhalilika sana ni kuanzia cheo cha Kuruta, Koplo, Sajenti, *Senior* Sajenti mpaka *Inspector* kidogo kumekuwa kama kuna makundi fulani kati ya huku na huku. Kwa hiyo ningeomba sana changamoto hii iweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna wastaafu ambao wameshalipwa haki zao kupitia mafao yao ambayo *PSSSF* tayari wameshawalipa, lakini kuna fedha za kusafirisha mizigo pamoja na nauli. Malalamiko ni makubwa, askari ni wengi sana wanaodai hizo haki, ni wengi mno, sasa hivi wanadai haki zao za kusafirisha mizigo ambapo wengine walikuwa wanafanya kazi Morogoro, wengine walikuwa wanafanya kazi mikoa mingine tofauti tofauti, lakini fedha zao hawajalipwa. Kwa hiyo inasikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi juzi tu walipeleka malalamiko maeneo tofauti tofauti ikashindikana, wakapeleka malalamiko kwa Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, mmojawapo katika Wakuu wa Mikoa wangu waliopo, akawatishia kuwapeleka kwa Mheshimiwa Rais. Matokeo yake haki zile waliweza kupatiwa mara moja. Nauliza hizi fedha zilitoka wapi na katika bajeti gani? Walipolalamika tu na kutishiwa na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, basi waliweza kulipwa hizi haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sasa hivi utaratibu uliopo jeshini ni kuwa, ndani ya miezi mitatu kabla ya kustaafu, watumishi hawa wanalipwa haki zao za kusafirisha mizigo pamoja na nauli, lakini wale waliostaafu kipindi cha mwaka 2020/2021, haki zao hadi leo hawajapewa. Kwa hiyo hao watawekwa katika bajeti ipi? Nauliza, haki zao zitaingizwa katika bajeti ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la mifumo ya kumbukumbu. Kumekuwa na ukwasi mkubwa katika mifumo ya kumbukumbu Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na watendaji wa Wizara tunaomba masuala ya kumbukumbu yaangaliwe upya katika jeshi hili kwa sababu kunakuwa na utofauti sana katika ulipaji wa haki, lakini pia katika suala zima la utekelezaji, yaani tunamfanya mpaka yule askari husika, aweze kutokuwa na imani na jeshi lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna askari naomba baadaye nimkabidhi Mheshimiwa Waziri. Askari huyu ambaye alikuwa anafanya kazi katika kituo cha Morogoro, alikuwa katika cheo cha *Senior* Sajenti. Askari huyu aliugua akiwa kazini, lakini pia pamoja na kuugua akiwa kazini, jeshi halikuangalia kuugua kwake wala namna ya kujua matibabu yake. Familia ikamsafirisha ikampeleka nyumbani Zanzibar, askari yule kwa bahati mbaya alifariki dunia, lakini alifariki dunia mwaka 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo mwaka mmoja baadaye inakuja barua ya kustaafu askari yule, pamoja na kupeleka vitambulisho na mambo mengine anaambiwa anastaafu kwa umri wa lazima wa miaka 55, lakini pia arejeshe vitambulisho pamoja na sare na mambo mengine, wakati askari

yule ameshastaafu, mwaka mmoja baadaye ndio inakuja barua ya kustaafu, wakati amefariki.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maida muda wako umekwisha.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Festo Mariki na Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki ajiandae.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa maandalizi ya bajeti ya 2023/2024. Bajeti ambayo inatupa afueni wa kwenda kupunguza changamoto mbalimbali. Sina mashaka na bajeti hiyo na naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Kamati kwa taarifa yao, lakini kwa ushauri wao mzuri walioutoa na naomba Wizara kuzingatia ushauri wa Kamati ili waweze kuufanyia kazi na hatimaye ikiwezekana bajeti inayokuja, basi tuone mabadiliko ya changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze vilevile Koplo Hamisi Masana kwa kukataa kupokea rushwa wakati anatekeleza kazi zake. Amekuwa ni mfano mzuri, lakini sio rahisi kwa watu wengine. Huyu ameonesha mfano mzuri na ni mzalendo wa kweli. Tuhakikishe basi wenzetu wengine wanafuata nyayo za Koplo Hamisi kwa kutopokea rushwa wakati wakiwa kazini ili tuweze kupunguza changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la Polisi. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri wetu kwa sababu nilikwenda kupeleka kilio cha Polisi. Lindi Manispaa tulikuwa hatuna Kituo cha Polisi, tulikuwa na Kituo cha Polisi lakini walikuwa

wanatumia nyumba za kupanga. Ninamshukuru Waziri Masauni kwa wema wake wa kutupatia shilingi milioni 900 na tumeweza sasa kuendeleza ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja A, kituo hiki kitakuwa cha mfano Kanda nzima ya Kusini. Kwa hiyo, nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri wetu kwa wema wako na kwa huruma ambayo umeionesha kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia suala la Wilaya ya Lindi, Lindi ina Majimbo matatu na jiografia yake Mheshimiwa Waziri anaifahamu vizuri kwa sababu ameshawahi kuja na anajua mazingira yaliyopo. Changamoto tunayoipata ni vitendea kazi, ukiangalia ukubwa wa eneo tuna Jimbo la Mtama, Jimbo la Lindi Mjini na Jimbo la Mchinga, ukiangalia hayo maeneo hatuna magari ya kutosha. Panapotokea dharura yoyote Polisi wanashindwa namna ya kwenda kushughulikia changamoto ambazo zinajitokeza. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nikuombe sana katika eneo hili ambalo umeagiza magari yaliyoingia nchini na magari ambayo tunategemea yatakuja, uitazame Lindi kwa jicho la huruma kuhakikisha kwamba, tunapata gari na Polisi waweze kufanya kazi yao vizuri kwa sababu kuna doria nyingine za usiku wanashindwa kufanyakazi kwa sababu ya kukosa vitendea kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi ile ya Polisi haina viti, haina fenicha, mazingira ya kazi ni magumu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nikuombe sana tutakapokamilisha ofisi mpya basi tupate vitendea kazi kuendana na hali ya ofisi na mazingira ya ofisi yatakavyokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto hiyo, niiombe Kamati ije kutembelea Lindi kuona mazingira ya nyumba za Polisi wanazoishi. Nyumba zile ni chakavu, nyumba zimepitwa na wakati, vijumba vidogo utafikiri mabanda ya kufugia Wanyama, ni huruma sana. Ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri pamoja na kwamba, ziko fedha ambazo zimetengwa katika kujenga nyumba za Polisi, hebu rudi tazama Lindi, mazingira yaliyopo kuhakikisha kwamba, Polisi Lindi wanapata nyumba. Japokuwa tusiwezeshe nyumba za kukamilisha wafanyakazi wote, lakini kila mwaka tukipata kiasi cha kujenga nyumba za Polisi basi tuweze kupata nyumba za Polisi…

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamida kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Matiko.

**TAARIFA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nilikuwa nataka nimpe Taarifa Mheshimiwa Hamida kwamba, uhaba wa nyumba kwa Askari Polisi na Magereza ni Tanzania nzima. Pale Tarime mvua ikinyesha Askari Magereza anafanya kuhamisha godoro kutoka sehemu moja kupeleka nyingine na ni vijumba ambavyo vimejengwa toka enzi za mkoloni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nampa taarifa hiyo ili Serikali ione ni kwa namna gani itenge bajeti ya kutosha kuboresha makazi ya Askari Polisi kwa maana ya Magereza na wengine wote. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hamida taarifa unaipokea?

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Taarifa ninaipokea kwa sababu changamoto hiyo ni kubwa na ipo katika maeneo mbalimbali kama Mheshimiwa Mbunge alivyotolea taarifa, katika maeneo yote nchini Tanzania utakuta miundombinu mbalimbali imekuwa ni mibovu kwa hiyo, tunaomba Serikali kuhakikisha kwamba, kila mwaka wa fedha tunaendelea kupunguza changamoto ili hali ya ndugu zetu Jeshi la Polisi na Jeshi la Ulinzi na Usalama waweze kufanya kazi katika mazingira mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la uhamiaji. Ninajua kwamba, Serikali imeendelea kujenga majengo ya ofisi za Uhamiaji katika kuhakikisha kwamba, tunatoa huduma mbalimbali katika Mikoa mbalimbali, lakini nimshukuru pia Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya muungano wa Tanzania kwa kutupatia fedha na kuweza kujenga Ofisi ya Uhamiaji ya Mkoa wa Lindi. Nimshukuru sana Mheshimiwa

Waziri kwa kusimamia hilo, lakini changamoto iliyopo, bado vitendeakazi ni kizungumkuti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna changamoto kubwa ya kutokuwepo magari. Hawa ndugu zetu wa Uhamiaji wana doria za mchana na usiku, ukisema Ofisi ya Mkoa maana yake wanatembea Wilaya mbalimbali kuhakikisha kwamba, wanaangalia mambo yanavyokwenda, kuona wavamizi ambao siyo raia wa Tanzania wanaendelea kuingia bila kuwa na *passport*. Kwa hiyo, ni suala sasa la Serikali kuona namna gani wanasaidia, kama tumeboresha ofisi zetu, basi sasa vitendea kazi viboreshwe katika Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Lindi, tupatiwe magari ili waweze kufanya kazi usiku na mchana, lakini waweze kuhudumia wananchi ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali kwa huduma ya utoaji wa *Passport,* imekuwa ni suala zuri sana. Changamoto nyingi zimepungua, hakuna usumbufu kama ambavyo miaka ya nyuma ilikuwa inatokea, tuongezee kuwapa vitendea kazi vya kisasa, kutumia mifumo ya TEHAMA na kuharakisha huduma. Siyo Afisa Uhamiaji anakusanya hapa makaratasi ya maombi anapeleka Dar-es-Salaam, badala yake angeweza kutia kwenye *computer* na yakaweza kufika Dar-es-Salaam wananchi wakashughulikiwa na wakatapa *passport* kwa wakati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hamida. Muda wako umeisha.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Martha Festo Mariki, atafuatiwa na Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki. Mheshimiwa Deo Sanga ajiandae.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya katika Taifa letu, pili nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Naibu Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja ninachangia kuhusu changamoto katika Mkoa wangu wa Katavi. Katika Mkoa wangu wa Katavi Jeshi la Zimamoto tuna takribani zaidi ya miaka 12 katika Mkoa wetu wa Katavi hatuna gari la uhakika la zimamoto. Mkoa wetu unakua, Serikali imewekeza vitu vingi sana ikiwepo bandari, lakini Mkoa wetu wa Katavi pia ni Mkoa ambao unapokea wafanyabiashara wengi kutokana na biashara ya kilimo. Hivyo, niiombe sana Wizara hii kupitia Mheshimiwa Waziri katika Mkoa wetu wa Katavi gari letu tulilokuwa nalo lilipata ajali mwaka 2012 likaenda kufanyiwa matengenezo, lakini mpaka hii leo ninapoongea gari hilo halijaweza kurudi katika Mkoa wetu wa Katavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuamini katika Mkoa wetu wa Katavi gari ambalo wanasema tunalitegemea ni gari dogo na ambalo liko *airport*. Sasa unajiuliza ikitokea ajali ya moto na ndege wakati huo inatua, je, gari hilo litaweza kufanya kazi ya kuzima moto? Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, Mkoa wetu wa Katavi tuna uhitaji mkubwa sana wa gari hilo ukizingatia Mkoa wetu unakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ninalopenda kuchangia jioni hii ya leo nitachangia katika upande wa Jeshi la Magereza. Jeshi la Magereza linafanya kazi nzuri, lakini katika Mkoa wetu wa Katavi tumekuwa na msongamano mkubwa sana wa mahabusu na wafungwa. Mfano katika gereza letu pale Wilaya ya Mpanda Mjini ambapo ndiyo gereza linalochukua *almost* wafungwa wote katika Mkoa, gereza lina uwezo wa kupokea wafungwa 100, lakini ukiangalia kwa sasa kuna takribani wafungwa zaidi ya 400. Wafungwa hawa wamesongamana, hivyo tujiulize je, ikitokea mlipuko wa magonjwa nini kitatokea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo niombe sana Wizara, katika Mkoa wetu wa Katavi tumeshaleta maombi yetu na

tumeshatenga eneo ambalo liko Mpimbo katika Kata ya Useja, tuna eneo kubwa lenye ekari za kutosha kwa ajili ya kujenga magereza. Tunaomba sana Wizara muweze kutukumbuka. Katika Mkoa wetu wa Katavi *almost* tuna kama magereza moja tu ambayo ni ya maana pale mjini, tunaomba sana tuweze kujengewa magereza hiyo, ili kuweza kuepusha huu msongamano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalopenda kuchangia ni kuhusiana na Shirika la Magereza la Uzalishaji (SHIMA). Mheshimiwa Waziri, shirika hili hapo nyuma lilikuwa halifanyi kazi vizuri, tunalipongeza kwamba kuna *improvement* ambazo zimeongezeka kidogo, shirika hili tunataka lije na mkakati, mfano, ukiangalia katika Mkoa wetu wa Katavi katika Mkoa wetu wa Rukwa tuna mashamba ambayo ni makubwa sana, ambayo ni mashamba yanamilikiwa na Magereza, lakini mpaka hivi sasa shirika hili limeshindwa kutumia *resource* hizo kwa kulima chakula cha kutosha ili kuweza kuipunguzia Serikali adha ya kuhudumia wafungwa ambao wamekuwa na upungufu mkubwa sana wa chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Wizara waweze kulisimamia Shirika hili la SHIMA liweze kufanya kilimo, ikiwezekana kilimo cha umwagiliaji ili waweze kuendana na nyakati. Wakitumia kilimo ipasavyo hawatakuwa na upungufu mkubwa wa chakula. Ni aibu kwa Taifa kama hili ambalo lina maeneo makubwa sana kushindwa kutumia ardhi tuliyopewa na Mwenyezi Mungu kulima chakula cha kutosha, matokeo yake kuipa Serikali mzigo wa kwenda kuwahudumia wafungwa kwa kusema kwamba, chakula hakitoshi magerezani. Wanayo nguvu kazi ya hawa wafungwa, waweze kuitumia, lakini waweze kutumia *resource* tulizopewa na Mwenyezi Mungu waweze kupata chakula cha kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, tunaomba shirika hili lirudi nyuma ikiwezekana lifuge, pia liweze kupata mifugo ambayo itasaidia, kuna akinamama ambao wako Magereza, kinamama waliofungwa na watoto wadogo, wale watoto hawana hatia, shirika hili tukiweza kufuga mifugo wakaweza kupata maziwa hata wale watoto wadogo wataenda kupata maziwa. Tuombe sana Wizara waweze kulisukuma shirika hili liweze kufanya kazi vizuri

kwani wale watoto waliopo kule magereza hawana hatia yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia jioni hii ya leo ni kuhusiana na makazi ya Askari Polisi pamoja na Askari Magereza. Ukiangalia makazi yao kwa kweli, yanasikitisha na unaweza ukalia machozi. Tuwape heshima Askari hawa kwani ndio wanaotulinda, kama wanatulinda ni kwa nini tusiboreshe mazingira yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuweze kuwapatia vifaa vya kufanyia kazi, lakini upande wa magari, hawana magari, ikiwezekana tuweze kuwabadilishia *uniform* zao mara kwa mara ili waweze kuwa nadhifu na waweze kuipenda kazi yao. Niiombe sana Wizara muweze kuangalia mfano nyumba tu za maaskari ukiziangalia kwa kweli unaweza ukalia machozi. Hawa watu ni muhimu katika Taifa letu, wanatulinda, wanasababisha tunakuwa na amani ni kwa nini tusiweze kuwatetea watu hawa waweze kupata mazingira mazuri katika kufanya kazi zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ningependa kuzungumzia suala la Polisi Jamii. Kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo Polisi Jamii inafanya kazi katika Kata zetu. Sote ni mashahidi tulivyokuwa likizo iliyopita tuliona Polisi Jamii ikifanya kazi kila Kata wakituhusisha sisi akinamama wa UWT, ninaipongeza sana Serikali. Ili Polisi Jamii waweze kufanya kazi vizuri katika nchi yetu ni lazima kuhakikisha kwamba, Serikali tunajipanga kuhakikisha tunajenga vituo vya Polisi kila Kata, pia ni lazima tuwapelekee vitedea kazi. Mfano watu hawa hawana vitendea kazi, sasa watafanyaje kazi hiyo? Kazi wanayoifanya ni kubwa na ukizingatia uhalifu mkubwa unafanyika katika Kata zetu, tukiwaboreshea mazingira wakafanya kazi vizuri tutaweza kukomesha uhalifu kuanzia kwenye ngazi za Kata na hivyo kupunguza uhalifu mkubwa sana katika Wilaya zetu na *level* za Mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kushauri ni kuhusiana na wao kuweza kutenga pesa kwa ajili ya kutoa elimu. Tukiangalia katika maeneo yetu mengi, ukiangalia ni kweli wananchi wengi hawana uelewa kuhusiana na masuala ya

ukatili, lakini kupitia Polisi Jamii tukitenga pesa kwa ajili ya elimu, hususan vijijini, wananchi wengi watapata uelewa kuhusiana na mambo yanapotokea ni wapi waende kushtaki na badala yake waache kuficha mambo yanayokwenda kufanya uhalifu katika maeneo yetu. Mfano, masuala ya ulawiti kwa watoto wetu, masuala ya ubakaji na ukatili wowote ule wa kijinsia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuongelea ni kumpongeza *RPC* wangu wa Mkoa wa Katavi kwa jinsi ambavyo anafanya kazi nzuri, kazi iliyotukuka. *RPC* wangu wa Katavi napenda kumpongeza sana kwa namna jinsi alivyo-*deal* na vijana wanaoitwa damu chafu, walikuwa wanatusumbua sana wananchi wa Katavi, lakini nampongeza kwa jinsi ambavyo ame-*deal* na vijana wale ili kuhakikisha kwamba wananchi wa Mkoa wa Katavi tunaenda kupata amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na ninawatakia utekelezaji mwema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Martha. Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, atafuatiwa na Mheshimiwa deo Sanga. Mheshimiwa Venant Daudi ajiandae.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nami kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji siku hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nitumie fursa hii kumpongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan kwa uzalendo wake mkubwa aliouonesha jana, licha ya kwamba Dar-es-Salaam Young Africans walipoteza mchezo, lakini hakurudi nyuma aliweza kuweka mzigo mezani kama alivyoahidi. Pia nitumie fursa hii kumpongeza sana Rais wa Zanzibar Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa kudumisha misingi ya haki na utawala bora katika uongozi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Taifa lolote raia ili ajulikane kwamba yeye ndiye mwananchi wa Taifa hilo hakuna kinachomtambulisha zaidi ya kitambulisho. Kitu kinachoshangaza katika Taifa letu hili mambo ni tofauti. Kumekuwa na ukakasi mkubwa katika upatikanaji wa vitambulisho vya uraia, vitambulisho vya Mtanzania. Mheshimiwa Waziri ningependa sana Kaka yangu utakapokuja hapa kuhitimisha ni lazima utueleze mkakati wa Serikali mlionao juu ya upatikanaji wa vitambulisho vya Mtanzania. Kama siyo hivyo, mimi sitaondoka na shilingi, lakini nitaondoka na mshahara wote na mamilioni yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo ambalo linaendelea sasa hivi, kule Zanzibar tunapozungumzia suala la upatikanaji wa leseni za udereva ni tofauti sana na huku. Zanzibar ili upate leseni ya udereva wanaohusika na masuala ya leseni ya udereva ni mawasiliano. Maana inawezekana mawasiliano wakaidanganya Wizara ya Mambo ya Ndani, lakini Tanzania Bara ili upate leseni ya udereva ni lazima upite kwa Jeshi la Polisi. Jeshi la Polisi wao ndiyo wanaotoa leseni za udereva. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni kumekuwa na zoezi la unyang'anyaji wa leseni za udereva kwa madereva hata kama wameendesha miaka 20. Unajua napata suala kitu kimoja, leseni walizokuwanazo zinathibitisha wazi kwamba wao walikuwa na leseni, lakini kwa nini wanyang'anywe leseni? Sifa gani waliyoikosa? Kama kumrejesha darasani kwa nini msimrejeshe wakati ule ambapo alikuja kuomba leseni, mumrejeshe sasa hivi kakosa sifa gani? Je, kapunguza uwezo wa kuona au kigezo kipi mnachotumia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nimkumbushe Kaka yangu Mheshimiwa Masauni na Mheshimiwa Jumanne kwamba, mwaka jana niliuliza swali hapa Bungeni kuhusiana na ujenzi wa nyumba za Askari kule Nungwi na upanuzi wa kituo cha Polisi. Majibu niliyojibiwa ni kwamba, mnawaruhusu wananchi waliozunguka maeneo yale waweze kukodisha nyumba zao ili Askari wale wapate sehemu ya kukaa. Kusema kweli, nilikaa nikatafakari mara sita, hivi kweli askari tunamtakia mema? Turuhusu raia aende akamkodishe tena maeneo ya Nungwi ambayo ni maeneo ya uwekezaji? Chumba kimoja unaweza

kukodi kwa laki, je, leo Askari ana familia nyumba moja atakodi kwa shilingi ngapi? Kwa mshahara gani anaoupata atakaoweza kujikimu kama siyo kumtengenezea misingi ya rushwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibaya zaidi, ulikataa kupanua nyumba za Askari, ulikataa kupanua eneo la Kituo cha Polisi, kinachonisikitisha na kinachonihuzunisha, umeenda kuchukua kituo changu cha afya Nungwi na kuweka Askari Utalii, hili jambo halikubaliki. Hili jambo halikubaliki! Kituo cha afya kile wananchi walikuwa wanakitegemea sana, kuweka Askari wako katika maeneo yale kumesababisha usumbufu mkubwa. Kama ulishindwa kujenga vituo vya polisi basi ilikuwa huna haja ya kwenda kung'ang'ania kituo cha afya, mlitumia njia moja mkatuchezea mchezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri tuliuliza kwa nini kituo chetu kimefungwa? Hoja mkasema kwamba, kituo kile mashimo yake ya choo yamejaa, ninachotaka niulize wale Askari wako wanajisaidia wapi? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, sababu ya pili ukaniambia kwamba, pindi ikinyesha mvua katika maeneo yale maji yanaingia mpaka ndani yanaweza kusababisha maradhi juu ya wagonjwa, hivi Askari wao wana kinga juu ya maradhi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuelewe ya kwamba, kabla ya kuanzishwa Polisi Utalii, Nungwi sisi tulikuwa na Polisi Shirikishi, Polisi Jamii. Polisi Jamii walikuwa wanafanya kazi kubwa mno kwa sababu, ulinzi wa kwanza wa raia na mali zao unategemea zaidi wananchi wanaozunguka maeneo yale. Leo hii mmetuletea Askari Utalii, sipingani nao, Rais alianzisha kile kikundi kwa lengo mahsusi na lengo madhubuti kabisa, lakini leo hii kimebadilika kikundi kile, kimekuwa ni kikundi cha manyanyaso, kimekuwa kikundi cha wala rushwa, kimekuwa ni kikundi ambacho kinasababisha shaghalabaghala, zogo, kafara, sijui hata kitu gani kwa wananchi wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine lazima tukae tutafakari sisi kama Taifa, hivi tuseme Askari Jamii wakiwezeshwa

hivi wanaweza kushindwa kweli kulinda fukwe zao? Hivi Askari Jamii tukiwapatia vifaa kuna haja gani ya maeneo yale yanayozunguka fukwe kuleta Askari Utalii kulinda *beach*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Uhifadhi lilikuwa na dhamira nzuri kuanzishwa, kama nilivyotangulia kusema, lakini sasa hivi Mheshimiwa Waziri, wanalichafua Jeshi letu la Polisi. Misingi na utaratibu wa uchukuaji wa rushwa na kunyang'anya kwa kutumia nguvu imekuwa mtihani katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kitu kimoja, wakati mlipokuja kujenga kituo Nungwi, wananchi waliamini kwamba mtawalinda raia na mali zetu, lakini kumbe mmekuja kutuwinda raia na vitu vyetu. Mmekuja kuwawinda raia na wasio kitu, kwa sababu vituo vya Polisi vimekuwa vina-*base* zaidi kuwaweka ndani wale watu masikini. Masikini wananyanyasika. Kile Kituo cha Polisi pale Nungwi kimekuwa kikitumika na watu kuonesha mamlaka waliyokuwa nayo. Watu wanaweza kuwekwa ndani kituoni, lakini sababu za msingi hazijulikani. Tunaongoza kwa kuwa na *unreported case. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibaya zaidi kinachonisikitisha, unaleta kesi za watu wanaohusika na dawa za kulevya; wananchi wetu wanajitolea kuwaonesha maaskari nani na nani anayehusika na dawa za kulevya, kumbe tunawatafutia kula! tunaleta ripoti leo, kesho mtu huyo katoka. Halafu anakuja kukutajia, sasa nimeambiwa na afande moja, mbili, tatu. Kusema kweli tunalikosesha uaminifu Jeshi letu la Polisi na tunaliondolea ushirikiano baina ya raia wema na Jeshi hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati walala hoi, waendesha bodaboda na wavuvi wananyanyasika; wakati hawa wanalia; cha kushangaza, wauza unga, wavuta bangi na wanaokwepa kodi za Serikali, wao wanalindwa pamoja na kuhifadhiwa. Tunaelekea wapi? Mara ngapi Kituoni kwetu Nungwi tunapeleka watu ambao wanahusika na tuhuma mbaya lakini mnawaachia? Mheshimiwa Waziri mimi nimekuwa nikikutumia *messages* mara nyingi juu ya mwenendo mzima wa Kituo cha Polisi, Nungwi, lakini hakuna moja linalotekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazuia mshahara wa Mheshimiwa Waziri kama hajanipigia msasa kituoni kwangu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Simai. Malizia sekunde 30.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deo Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Venant Daud na Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, ajiandae.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Waziri wakati anawasilisha bajeti yake hapa, ameeleza kwamba bajeti kutoka mwaka 2022 mpaka sasa mwaka huu 2023 imeongezeka maradufu. Kwa hiyo, kwa kuongezeka kwa bajeti hii, la kwanza, lazima tumshukuru mama kwa kukuongezea ma-bi na ma-bi na kuwa na ma-ti. Kwa hiyo, tunampongeza sana mama kwa kujali kuongeza bajeti ya Wizara hii ya Mambo ya Ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ameongeza, ni kwa sababu Waziri mwenye dhamana na Naibu Waziri mko vizuri. Ndiyo maana mmeongezewa ma-bi, sasa mmekuwa na ma-ti. Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wako, pamoja na *IGP,* Afisa Uhamiaji, Makamishna wote pamoja na Katibu Mkuu, kazi mnayoifanya ni kubwa na nzuri sana. Ndiyo maana umesema uhalifu pia kutoka asilimia fulani ya mwaka 2022 na mwaka huu imepungua, ni kwa sababu ya kazi nzuri unayoifanya kuiongoza Wizara hii. Tunakupongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi, unajua Waheshimiwa Wabunge wenzangu, ukitaka kujua kazi ya Jeshi la Polisi na taasisi zake zote wanafanya kazi nzuri, hebu siku moja vituo vya Polisi vifungwe kwa masaa kadhaa, tuone kitakachotokea. Ndiyo maana tunawapongeza, kazi

mnayoifanya ni nzuri ya kutulinda sisi na mali zetu. Ongeza jitihada za kuhakikisha unaendelea kutulinda sisi na mali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri inayofanywa, Mheshimiwa Waziri na timu yako, wapo baadhi ya Askari wanaoliharibia sifa Jeshi la Polisi. Ndiyo maana leo umewaonesha pale zaidi ya watu wanne, umewatunuku kwa sababu ya kufanya kazi nzuri. Kwa hiyo, tunakupongeza kwa kuwatunuku wale kuwa mfano kwa Jeshi la Polisi kufanya kazi nzuri. Wengine pia watakaoendelea kufanya kazi nzuri, wape motisha ili waweze kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ombi. Kituo cha Polisi cha Makambako kina eneo ambalo wananchi walishalitoa. Nimekuelezea mara nyingi, mwaka 2022 mwezi Agosti alipokuja Rais nilisema, wanahitaji fidia yao kwa sababu hawawezi sasa hivi kufanya kazi ya aina yoyote. Hawawezi kuezeka nyumba zao hata kama mabati yameharibika, walizuiliwa. Fidia yao ni Shilingi milioni 250, sito B, ni milioni 235. Nakuomba Mheshimiwa Waziri, jambo hili lichukulie maanani, ukiongea na Waziri wa Fedha ili wananchi hawa waweze kulipwa fidia yao na waweze kuondoka katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la pili, Kituo cha Makambako ni kituo kilichopo *center* ambapo wako wahalifu wanatoka sehemu nyingine; Songea, Mbeya, Iringa nakadhalika, pale ni kama *center*. Tunaomba kituo hiki kwa sababu ni kituo kamili cha Wilaya ya Kipolisi, tunaomba vitendea kazi kama magari, kituo cha Polisi chenyewe kiimarishwe, kijengwe vizuri ili waweze kudhibiti uhalifu unatokea katika eneo letu pamoja na Mkoa wetu wa Njombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ni lazima tulipongeze Jeshi la Uhamiaji kwa kudhibiti wahalifu wanaoingia nchini. Maana bila kusimamia hawa, ndio wanaogeuka kuwa majambazi na ndiyo wanaotuharibia, lakini Jeshi hili limesimamia vizuri na hatimaye kila wakati tunapata taarifa kwamba wamekamatwa wahalifu mahali fulani, wamekamatwa wahamiaji kutoka sehemu fulani. Kwa hiyo, tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi upande wa Magereza. Makambako tulitenga eneo kwa ajili ya kujenga eneo la Magereza katika Mji wa Makambako. Tunaomba, katika kutenga bajeti yake, Mheshimiwa Waziri aone sasa umuhimu wa kujenga Magereza Makambako ili kupunguza msongamano mkubwa uliopo katika Wilaya ya Njombe. Wilaya ya Njombe ni kubwa sana, kwa hiyo, tunaomba sana utenge fedha kwa ajili ya kujenga Magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo ambalo wenzangu wamelisema hapa, kwa upande wa *NIDA*. Vitambulisho hivi vimekuwa tatizo. Baadhi ya watu sasa wanatoka Makambako kwenda kufuata Njombe, na wakifika kule wanaambiwa waje kesho, keshokutwa na nini, kwa hiyo, nadhani tatizo hili inawezekana liko nchi nzima. Tunaomba jambo hili hebu mliwekee umuhimu kuhakikisha raia wa Tanzania wanapata vitambulisho vyao ili wajulikane kama ni raia wetu wa maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamezungumza juu ya malimbikizo ya Askari na mengine, pamoja na kwamba mnakwenda vizuri, hebu mwone namna ya kuhakikisha changamoto hizi za Askari wetu mnaziondoa ili kusiwe na tatizo juu ya Askari wetu ambao wanakuwa wamestaafu na wengine wanakuwa wakati fulani wanadai haki zao. *(Makofi)*

*(Hapa Mhe. Deo K. Sanga alinyamaza kwa sekunde chache)*

**MBUNGE FULANI:** Alikuwa anatafuta ma-bi na ma-bi. *(Makofi)*

**MHE. DEO K. SANGA:** Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaona hapa natafuta ma-B, *amount* ile ili niweze kuitaja hyapa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiujumla nirudie tena, Waziri kazi yako ni nzuri. Unajua mtu anapofanya kazi vizuri ni lazima tumpongeze. Kabisa, unafanya kazi yako vizuri, pamoja na timu yako ya Makamishna wote pamoja na *IGP* wako, mnafanya kazi

nzuri. Endeleeni. Hawa Askari wachache wanaochafua, mwadhibiti waweze ku…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sanga.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Venant Daud, atafuatiwa na Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa na Mheshimiwa Sylvia Sigula, ajiandae.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami kuwa mmoja ya wachangiaji katika Bajeti hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa, hasa ya Mheshimiwa Rais, ya kuhakikisha wananchi wanalindwa saa 24. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa kweli wanafanya kazi kubwa na wanajitahidi sana kusikiliza changamoto za wananchi kupitia wawakilishi wao, hasa Wabunge. Hiyo ndiyo sifa ya viongozi ambao sisi kama wenzao tumewatanguliza mbele kwa niaba ya kwenda kuwasikiliza wananchi waliotutuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache sana ambayo nataka nichangie. Jambo la kwanza katika Jimbo langu la Igalula, pamoja na ulinzi wa nchi kuwa imara, ambao Mheshimiwa Rais anaendelea kuuimarisha, tuna haja ya kuongeza upatikanaji wa ulinzi zaidi. Katika Jimbo langu la Igalula tuna ujenzi wa vituo vya Polisi ambapo wananchi waligundua kuwa ili waendelee kuwa salama, lazima waanzishe ujenzi wa vituo vya Polisi. Naiomba Serikali, Mheshimiwa Rais amekuwa akisaidia sana ujenzi unapofika katika hatua ya maboma, hata katika zahanati, vituo vya afya na shule, tunaletewa fedha, lakini sasa tuna maboma mengi ya vituo vya Polisi hayaletewi fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba, tuna Mfuko wa Tuzo na Tozo, usiwe tu unahusika kwenye mikoa, basi ushuke na kwenye kata na vijiji ili kwenda kuimarisha vituo vya Polisi katika maeneo yetu. Hii itatusaidia kuondoa mitafaruku ambayo inawakumba wananchi wetu katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata vituo hivyo ambavyo viko katika hatua ya maboma ni Kituo cha Tura na Goweko. Naomba Serikali, Mheshimiwa Waziri nilishakwambia, na nimeshauliza maswali kadhaa hapa mkaniahidi mtatenga fedha za bajeti ili ziweze kwenda kule, lakini kwenye bajeti hii sijaona fedha hizo zimetengwa. Naomba kupitia Bunge hili, unitengee fedha ili vituo vya Polisi viweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto kubwa ya Polisi wetu. Wanafanya kazi kubwa sana. Kazi ya kumlinda binadamu ni kubwa sana. Ninyi wenyewe mnafahamu, binadamu ana mbinu nyingi, lakini Polisi pamoja na uchache wao, wanajitahidi kuwalinda binadamu ili wasifanye madhara katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamekuwa na shida ya mambo mawili; jambo la kwanza, hawalipwi stahiki zao kikamilifu. Leo tunalalamika Polisi wanakula rushwa, lakini rushwa nyingine zinasababishwa na hali duni ya maisha yao. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nakuomba, waimarishieni Polisi mapato, hasa zile posho zao stahiki zilizopo kwa mujibu wa sheria zikiwemo kodi za nyumba, kulipia bili za maji na umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikia leo hii Polisi wakienda kuomba bili za umeme wanaambiwa waende na risiti wakati sasa hivi mtandao umekuwa mkubwa, luku wananunua kwa kutumia simu zao za mikononi, maji wanalipia kwa kutumia simu zao za mkononi. Sasa unapomwomba risiti ni kwenda kuwadidimiza na kuwanyima haki yao ambayo ipo kwa mujibu wa sheria. Kama mlipanga kuwalipa shilingi 50,000 walipeni fedha zao, wao watajua watafanyaje huko. Kama analala kwenye pagale ambalo halina umeme, ni yeye na maisha yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni vitambulisho vya *NIDA*. Mheshimiwa Waziri hili jambo mimi naomba mfanye

*assessment* ya uhakika, muone kama hili zoezi mnaliweza au tulisimamishe kwa muda ili tujipange upya. Kwa sababu gani nasema hivyo? Tuna changamoto kubwa ya vitambulisho vya Taifa. Leo tumesema kila mwenye laini ya simu lazima asajiliwe kwa kutumia namba ya *NIDA,* lakini fanya takwimu, simu zipo zaidi ya milioni 50, lakini namba za vitambulisho mmetoa ngapi? Ndiyo maana unakuta namba ya mtu mmoja anasajiliwa mtu mwingine ambalo ni kosa na kinyume cha sheria. Kwa hiyo, mimi namwaomba Mheshimiwa Waziri, hebu angalia hili jambo, kama mnaliweza tuendelee nalo, lakini mwongeze kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitambulisho hivi mmeacha kusajili tangu mwaka 2012. Sasa kuna vijana wamefikisha umri wa miaka 18 mpaka leo hamjaweza kusajili upya. Rudisheni zoezi mkasajili upya tena ili sasa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Venant, muda wako umeisha. Malizia.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, atafuatiwa na Mheshimiwa Sylvia Sigula, na Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib, ajiandae.

*(Hapa microphone haikuwaka)*

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naona watu wa Igunga walikuwa wana-*test* mitambo lakini imeshindikana. Mambo yanakwenda vizuri. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi jioni hii nami niweze kuchangia Bajeti ya Wizara ya Mambo ya ya Ndani ya Nchi. Kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa kuunda Tume ya Haki Jinai nchini. Ukifuatilia

kwa haraka haraka, ukifanya utafiti, hii Tume ya Haki Jinai, asilimia takribani 60 ni wanufaika wa taasisi na vyombo vilivyoko chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa maana ya taasisi zote zilizopo chini ya Wizara, asilimia 30 ya wanufaika ni Wizara ya Katiba na Sheria na asilimia 10 ni taasisi nyingine. Tunamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuona, tunaamini tume hii italeta mabadiliko makubwa sana kwenye vyombo vyetu vilivyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri, kaka yangu Mheshimiwa *Engineer* Masauni, kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kuifanya kwenye hii Wizara pamoja na Naibu wake, kaka yangu, Mheshimiwa Jumanne Sagini. Hongereni, mmeendelea kuaminiwa, mnaendesha vizuri Wizara, mnatoa mwongozo mzuri, nasi kama Wabunge tupo nanyi, tunawaunga mkono na kuhakikisha yale yote ambayo mmepanga yanatimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie nafasi hii kuvipongeza vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vilivyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Nampongeza Inspekta Jenerali wa Jeshi la Polisi, Afande *IGP;* Kamishna Jenerali wa Uhamiaji; Kamishna Jenerali wa Magereza; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa na pia niwapongeze Maafisa wa Bunge, wale ambao wanahudumia Jeshi la Polisi na Magereza ambao wako hapa Bungeni, wanatupa ushirikiano mkubwa katika kuhakikisha mambo yetu yanakwenda vizuri. Nami kwenye bajeti nimeona Gereza langu la Igunga litakamilishwa, kwa kuwa mwaka 2022 nilitoa fedha pale kwa ajili ya *cement* kama Mbunge, na mwaka huu nashukuru Serikali mmetuunga mkono, mtalikamilisha gereza letu tuwe na gereza la kisasa kwa sababu Wilaya ya Igunga ni ya kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie maeneo matatu, manne, lakini kabla ya kuchangia, niseme naunga mkono hoja Taarifa ya Mheshimiwa Waziri na Taarifa ya Kamati ambayo pia mimi ni Mjumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na Jeshi la Polisi. Waheshimiwa Wabunge wengi wameongelea suala la makazi, sitalisema, mimi napenda kusemea Chuo cha Polisi pale Moshi, kuna miundombinu imechakaa, namwomba Mheshimiwa Waziri alipe kipaumbele katika kuhakikisha anaifanyia maboresho. Ni chuo cha kisasa, kimekuwa cha muda mrefu. Kuna mabweni pale tulijengewa na wahisani kwa kupitia Wachina pale, lakini pia na sisi sasa tuweke jitihda kuhakikisha tunaboresha bwalo letu pale la chakula na yale mabweni kwa ajili ya wanafunzi kwa maana ya maafisa wetu wanapokwenda kozi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, jambo lingine ambalo napenda kuchangia jioni hii ni sare la Polisi. Tumefika pale tukaona kwa sasa tunazalisha sare zetu wenyewe. Imewapa heshima sana kama Wizara, hongereni. Kwa hilo, ni hatua kubwa. Zamani tulikuwa tunakutana na Askari Polisi, unakuta *uniform* imechanika, lakini kwa sasa wanazalisha pale kwa ustadi mkubwa, kwa ufanisi. Afande *IGP* pamoja na wasaidzii wake walituonesha na sisi tumeridhika. Mabadiliko haya sasa yaende pia kwenye majeshi mengine yaliyoko chini ya Wizara hii ili tuweze kuendelea kuzalisha *uniform* zetu nchini. *Uniform* zinazalishwa vizuri, zinatoka mpaka na majina na vyeo vya Askari wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kuchangia jioni hii ni kuhusu vyombo vya usafiri na doria na *patrol*. Mheshimiwa Waziri, mama yetu Amiri Jeshi Mkuu, ametenga fedha kwa ajili ya kununua magari. Nasi Jimbo letu la Igunga tunaamini litakuwa miongoni mwa majimbo ambayo yatapewa kipaumbele katika kupata haya magari kwa ajili ya kuimarisha *patrol. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru *OCD* wa Igunga, anatupa ushirikiano mkubwa sana. Mwaka 2022 mimi kama Mbunge niliwachangia matairi, mwaka huu nimeona Serikali inatupatia gari mpya. Basi tunasema *Insha'Allah,* mama anaupiga mwingi, vijana wanasema apewe maua yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la mwongozo wa ujenzi wa hivi vituo vya polisi vya kwenye kata *(police posts);* sisi pale tumeanza jitihada pale Jimboni kwetu Igunga, nilipewa fedha

kwa ajili ya kuanzisha ujenzi wa Kituo cha Polisi pale sehemu moja inaitwa Mwanzugi eneo ambalo lina uchumi mkubwa sana na mzunguko wa fedha. Naomba na ninyi Serikali basi mtuingilie muongeze nguvu tuweze kukamilisha kile kituo cha Mwanzugi ili tuweze kupata na kuhakikisha raia na mali zao zinakuwa salama. Lakini pia Kata ya Igurubi ambayo ni makao makuu ya tarafa, kule kuna uchimbaji mkubwa wa madini, pia tuna kituo pale cha polisi cha nguvu za wananchi ambacho kimeshafikia hatua ya kupauliwa. Naomba mtuongezee fedha kama Serikali tuweze kukikamilisha mtuletee askari wetu pale waendelee kutusaidia kulinda wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ukweli mnafanya kazi nzuri, tunawapongeza kwa hilo. Lakini pia kuna huu utaratibu wa polisi kata mmesema mnawapatia pikipiki. Ilikuwa ni hoja niliyotaka niijenge hapa, kwamba tuweze kuwasaidia usafiri ili angalau basi wawe huru ili wanapokuwa wanafanya shughuli zao kwenye hizi kata waweze kutembea sehemu moja kwenda nyingine. Mmejitahidi sana polisi kata wanatupa ushirikiano hata sisi tunapokuwa kwenye ziara zetu Waheshimiwa Wabunge tunapata ushirikiano mkubwa Mheshimiwa Waziri tunakushukuru kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la msingi kwenye Jeshi la Polisi ningependa kuchangia pia kamera. Muweke sasa, kama mlivyosema, kwamba mtaweka kamera za usalama barabarani ili zinapotokea ajali au uhalifu mweze ku-*track* kirahisi. Hili namkumbuka hata Mheshimiwa Kenethy Nola alinisisitiza, akaniambia asubuhi kuwa yeye hatapata nafasi ya kuchangia lakini aliomba niweze kulichangia. Hongereni lakini tunawapa msisitizo miji yetu imekuwa kama Makao Makuu ya Dodoma sasa inahitaji kamera kwa ajili ya usalama barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikimaliza Jeshi la Polisi, naomba niende Jeshi la Uhamiaji. Niongelee suala la Chuo pale cha mafunzo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ngassa muda umeisha, naomba malizia.

**MHE.NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa pamoja na yote niliyoongelea ningependa kuchangio la mwisho, upande wa mamlaka ya vitambulisho vya Taifa. Mheshimiwa Waziri naomba nishauri, muwapatie fedha za kutosha ili waweze kukamilisha waweze kununua *card* ghafi ili wananchi waweze kupatiwa vitambulisho vya Taifa. Lakini pia ukijaribu kufatilia suala la vitambulisho vya Taifa linasaidia utambuzi wa walipa kodi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nashukuru sana, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ngassa. Mheshimiwa Sylivia Sigula atafuatiwa na Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib, Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza ajiandae.

**MHE. SYLIVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mungu Mwingi wa Rehema kwa kuniwezesha kusimama katika Bunge lako hili tukufu. Nitumie nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri kaka yangu Masauni na Naibu Waziri, kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana na tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kuipongeza Serikali. Sasa hivi askari wetu wanapokuwa kwenye mafunzo haya ya *refresher course* mambo ni mazuri. Serikali imechukua suala lile la chakula na sasa hivi inaligharamia Serikali. Tunaipongeza sana Serikali na waendelee kufanya hivyo ili askari wetu wafanye kazi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ulinzi wa raia na mali zao tumewapa jukumu hili Jeshi la Polisi. Ni ukweli usiofichika Jeshi la Polisi wanafanya kazi kubwa sana, lakini mazingira yao ni magumu mno. Leo ukienda Mkoa wa Kigoma, ukienda Wilaya ya Kibondo ukaambiwa hizi ndizo nyumba za askari, utatoa machozi, lakini utaungana na mimi Wabunge hapa wanasimama kila mmoja anaelezea makazi ya askari, makazi ya askari. Mimi naomba nikuombe Mheshimiwa Waziri, utakapokuja kumalizia

hapa hebu tupe mkakati wa Serikali ni namna gani tunaenda kukabiliana na hili jambo la nyumba za askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kuchangia kuhusu hii inaitwa *Police General Order (PGO)*. Kama kuna changamoto ambayo polisi wanakutana nayo basi ni hii *PGO*. *PGO* hii imeanzishwa zaidi ya miaka kumi iliyopita, na huenda lengo lake lilikuwa zuri, kuwapa motisha askari, lakini jambo hili kulingana na mazingira ya sasa limekuwa tena halina uhalisia na hivyo ni wakati mwafaka sasa wa kufanya mapitio yahii *PGO*. *PGO* hii ni sheria zinazoongeza Jeshi la Polisi, na zimekuwa zimeeleza mambo mengi sana. *PGO* hii ina kurasa zaidi ya 900 lakini mimi nitaomba nijielekeze kwenye *PGO* namba 132. *PGO* hii namba 132 inazungumzia posho za askari. *PGO* hii imeeleza posho nyingi ambazo askari anastahili kupewa. Kuna posho ya pango, kuna posho ya mavazi, kuna posho ya upelelezi, kuna posho ya utaalam lakini kuna posho nyingine nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini masikitiko yangu ni kwamba posho hizi haziendani na uhalisia wa sasa kwa mfano, ukizungumzia posho ya pango inasema askari atapewa asilimia kumi ya mshahara. Huenda kwa kipindi hicho ilikuwa ina maana sana. Leo kwa askari anayepata mshahara wa laki tano asilimia kumi ni shilingi elfu 50, sasa uniambie ni nyumba gani askari atapata kwa shilingi 50,000? Hii haiwezi kukubalika. Lakini *PGO* hii haijaeleza ni namna gani hii posho wanapewa. Sasa ninashauri Serikali tufanya mapitio, tupitie hii ili tutoe utaratibu rasmi ni namna gani askari wanapata posho hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunazungumza hapa, unapozungumzia suala la posho ya mavazi, maisha yamebadilika kila mmoja anafahamu. Miaka kumi iliyopita leo uhalisia ni tofauti…

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE.SYLIVIA F. SIGULA:** …leo unampa posho ya mavazi askari, unasema posho ya mavazi apewe shilingi 30,000, kwa mavazi gani atakayo nunua?

Mheshimwia Mwenyekiti, kwa hiyo mimi niombe, ni wakati sasa Mheshimiwa Waziri wa kufanya mapitio ya hii *PGO* kwa sababu ina mambo mengi mengi sana ambayo yanahitaji kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la rushwa kwa askari polisi. Mimi nilikaa nikatafakari sana, lakini nikaona kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya rushwa kwa askari na uhaba au ufinyu wa mishahara yao. Haiwezekani leo upate mshahara ambao hauwezi kukidhi mahitaji yako. Kitakachofanyika ni nini? Kwa hiyo mimi niombe Mheshimiwa Waziri, ni wakati sasa wa kuboresha maslahi, ni wakati sasa wa kuboresha mishahara ya askari ili nao waweze kufanya vizuri. Tusikae kuwalaumu rushwa, rushwa, rushwa wakati maslahi yao ni madogo. Mwaka jana ilitembea video hapa ya askari amechukua elfu kumi kama rushwa …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia.

**MHE.SYLIVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,lakini askari yule ile video ilinitoa machozi. Askari yule elfu kumi ile alipewa adhabu kali, alifukuzwa kazi lakini leo ukisoma ripoti ya *CAG* kuna wezi wa mabilioni bado wako ofisini. Hili jambo haliwezekani. Kwa hiyo mimi niombe Mheshimiwa Waziri, askari wanafanya kazi kubwa sana na wanafanya kazi ngumu sana hebu ifikie hatua tuwape thamani yao. Ikitokea kesho askari wakagoma ndio utaelewa kwa nini askari ni muhimu katika nchi hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante, malizia.

**MHE. SYLIVIA F. SIGULA:** Tuna amani sasa kwa sababu askari wanafanya kazi yao vizuri. Naunga mkono hoja ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, ahsante. Mheshimiwa Munira Khatib atafuatiwa na Mheshimiwa Agnesta kaiza, Mheshimiwa Vicent Mbogo ajiandae.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi kwa kuweza kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Nimpongeze sana amepambana sana na panya *road* na sasa hivi Tanzania yetu imetulia, majangili wamepungua. Kwa hiyo nimpongeze sana kaka yangu Masauni, endelea kufanya kazi sisi tunakuamini na Taifa linakuamini pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti,napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wizara yote kwa ujumla, hakika mnafanya kazi nzuri sana, nawapa pongezi sana. Lakini niwapongeze sana sana Wizara kwa kuanza ujenzi wa kituo changu cha Wilaya Mkoani. kituo hiki kilikuwa kimezungushwa mabati tangu mwaka jana lakini huu mwezi wa tano sijui kwa ajili ya bajeti ya leo tayari kimeanza msingi na tayari kimeanza kufanyiwa kazi. Niombe Serikali, itakapo pita bajeti hii kile kituo basi kiendelee pia na ujenzi wake usije ukasita. Iendelee na kile kituo pale kimalize kwa sababu kituo hiki ni kituo muhimu, ndicho kituo ambacho kimezungukwa na Bandari ya Mkoani pale, kwa hiyo ni kituo muhimu sana. Ujenzi wake naomba uendelee na uharakishwe zaidi kwa sababu ni kituo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na kituo hiki, niombe nyumba za Wilaya Mkoani, Waheshimiwa Wabunge karibu wote wamezungumzia hapa suala la nyumba. Suala la nyumba limekuwa ni tatizo kwa Tanzania nzima. Niombe basi Wizara iweze kuangalia upya suala la nyumba ya makazi ya askari hawa. Hasa ukiangalia mazingira ya Pemba. Mazingira ya Pemba si rafiki askari kukaa uraiani. Ukiangalia mwaka sasa hivi tulionao tunapitisha bajeti ya 2023/2024. Mwaka kesho tu kuna uchaguzi. Si mazingira rafiki kwa askari wetu kukaa katika nyumba za uraiani. Niombe sana Serikali iweze kuangalia upya suala la nyumba za mapolisi, naamini Serikali yangu ni Sikivu.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mheshimiwa Saashisha taarifa ya tatu leo inatosha hiyo. Mheshimiwa Mnura endelea na mchango wako.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala la nyumba hili Serikali yangu Sikivu itasikia na itafanyia kazi. Mheshimiwa Waziri tunakuamini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la dawati la jinsia. Nipongeze sana. Serikali kwa kuamua kwa makusudi kuunda hili dawati la kijinsia la watoto ndani ya Jeshi la Polisi. Kwa kweli mmetusaidia wazazi na hili dawati linafanya kazi nzuri sana. Lakini niombe Serikali, dawati hili liwe na kamisheni, liweze kujitegemea lenyewe na liwe na bajeti ya kutosha. Hatuwezi dawati hili kulichanganya ndani ya askari jamii kwa sababu dawati hili linafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri akae aangalie dawati hili lina wasaidia watoto. Mimi binafsi nimeshaenda kulitembelea dawati hili, linatoa elimu, linawasaidia akina mama, linafanya kazi zake vizuri. Dawati hili linatakiwa liweze kujitegemea. Kama ilivyo kwa askari jamii ndivyo dawati hili linatakiwa lijitegemee lenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tunataka kumaliza suala la udhalilishaji kwa watoto basi ni lazima kuweza kuwapa kamisheni iweze kujitegemea wenyewe lakini pia dawati hili lipatiwe fedha ya kutosha ndipo litaweza kufanya vizuri. Kwa sababu sasa hivi tunapokwenda kuna mambo mengi ya udhalilishaji wa kijinsia kama tutalisaidia dawati hili, yale masuala mengi ya ukatili wa watoto naamini yatapungua…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Munira ahsante sana muda…

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naomba niunge mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza atafuatiwa na Vicent Mbogo, Mheshimiwa Juma Hija ajiandae.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Wizara hii ya Mambo ya Ndani. Kabla sijaenda katika mchango wangu kwa moyo kabisa wa dhati naomba nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan. Pamoja na mambo mengine mazuri sana ambayo anaendelea kuyafanya, Mheshimiwa Rais ameweza kuweka utulivu katika nchi, ameweza kuweka amani na ametengeneza mshikamano. Lakini zaidi sana Mheshimiwa Rais ametufanya Watanzania kuwa wamoja bila kujali itikadi zetu za vyama lakini pia bila kujali itikadi zetu za dini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa leo nitakwenda kujikita katika hoja moja inayohusiana na uraia pacha. Mnamo tarehe 15 mwezi wa tano, 2023 nilisimama mbele ya Bunge lako tukufu nikihitaji kupata ufafanuzi kutoka kwa Serikali ni kwa nini inapata kigugumizi kuhusiana na suala zima la kuwapatia wenzetu diaspora haki yao ya msingi kwa maana ya uraia pacha. Majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ndiyo yanayonisababisha hivi leo nisimame kuchangia kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua hoja yangu ya leo itakwenda kugusa Wizara ya Mambo ya Ndani lakini pia itakwenda kugusa Wizara ya Mambo ya Nje. Sasa kwa sababu Wizara ni moja kila Waziri atanisikiliza kinacho muhusu basi atakwenda kukijibia katika eneo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema nitakwenda kuchangia suala zima la uraia pacha. Tunafahamu na tunatambua wazi wazi kwamba wapo watanzania wenzetu ambao tunawaita ma diaspora ambao walizaliwa katika nchi hii ya Tanzania, wamezaliwa katika Mikoa hii ya Tanzania katika vijiji na vitongiji ndani ya Tanzania. Diaspora hawa, hawa Watanzania wenzetu wazazi wao uhalisia wao ni Utanzania ni Watanzania na kwa

lugha nyingine Watanzania hawa na wenyewe ni Watanzania kwa kuzaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunatambua kwamba wapo diaspora ambao wamekulia ndani ya nchi hii kwa maana ya kukulia, wamelelewa lakini Watanzania hawa wamepata elimu zao ndani ya Tanzania, na wengine wamesomeshwa na kodi za Watanzania wanyonge wakiwa ndani ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua na tunafahamu kwamba hata sisi tulio katika Bunge hili tumeacha mikoa yetu, vijiji vyetu tunakwenda katika miji mingine kama ni Dar es Salaam Mbeya au ni wapi kwa lengo moja la kutafuta maisha kwa sababu Mtanzania yeyote ana haki ya kwenda popote kwa ajili ya kutafuta maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania hawa waliondoka ndani ya Tanzania wakiwa wamepitia *process* zote za kiusalama kwa maana ya uhamiaji. Watanzania hawa walipewa *passport* na uhamiaji. Na kwa lugha nyingine, watanzania hawa Serikali iliwathibitisha kwamba ni Watanzania safi, ni Watanzania wazalendo, na ikawapa kibali cha kwenda kutafuta ng'ambo ili mwisho wa siku waje kuifaidisha nchi yao au Taifa lao la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua suala zima la ajira nchini ni changamoto sugu. Kwa hiyo tunapopata Watanzania wenye elimu, wenye uwezo wa kwenda kule kwenye mataifa mengine ili waweze kutafuta tunapaswa kama Taifa kuhakikisha watu hawa tunalinda uraia wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwamba zipo nchi ambazo ili uweze kupata kazi, ili uweze kufanya biashara, ili uweze kufanya lolote ndani ya nchi hiyo huna budi kuwa na uraia wa pale. Wakati naongelea hili naomba tujikumbushe. Nimesema Watanzania hawa walitoka nchini wakiwa ni salama salimini, kwa maana ya vyombo vyote vya usalama vilithibitisha kwamba hawa watu ni safi kabisa. Sasa, walipofika katika mataifa yale, kwa sababu wameingia katika nchi hizo na wanaonekana ni watu safi na wana *passport* za Tanzania na ni wazalendo

wakaamua wawape uraia ili waweze kufanya maisha yao kuwa mazuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukubaliane jambo moja; kwamba hakuna sababu yoyote ile ya kisheria inayopaswa kumwondolea Mtanzania uhalisia wake wa kuzaliwa. Nayasema haya kwa sababu gani? Mnamo mwaka 1995 ndani ya Bunge hili ilitungwa sheria kandamizi inayohusiana na uraia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana muda wako umeisha.

**MHE.AGNESTA L. KAIZA:** *How can it be?*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba umalizie. Ahsante sana. Mheshimiwa Vincent Mbogo atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mheshimiwa Vita Kawawa ajiandae.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi anayoifanya ya kuendelea kutoa ajira mpya ili kuliboresha Jeshi letu na Majeshi yetu nchini. Niwapongeze Mheshimiwa Waziri Naibu pamoja na timu nzima ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kazi kubwa mnayoifanya, ni kazi ya kiuzalendo; pia askari kazi wanayofanya ya kulinda mali na kuhakikisha nchi yetu inakuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naenda kujikita kwa maeneo machache sana, hasa Jeshi la Zimamoto. Wabunge wengi wameongelea masuala ya makazi lakini Jeshi la Zimamoto lisipoanza na kuwa na mfumo wa zimamoto jamii; zimamoto jamii katika maeneo mengi miji inakua hata taarifa za majanga zinapotokea Jeshi la Zimamoto mpaka lifike kuna malalamiko kwamba *either* maji hamna ama wamechelewa kufika. Kwa hiyo wasipoanzisha zimamoto jamii katika maeneo ambayo ni hatarishi ili wanapopata taarifa ya majanga tayari wanakuwa na taarifa kutoka kwa wale zimamoto jamii kwamba ni vifaa gani vinatakiwa

viende katika tukio linalotokea. Kwa sababu sasa hivi wanaweza wakaenda na vifaa ambavyo havifai kwenye tukio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakianzisha sera ya kuwa na zimamoto jamii wataweka *coverage* kubwa sana ambayo itawapunguzia kazi askari wa zimamoto. Hata ile ajali ya ndege ya Ziwa Victoria tungekuwa na zimamoto jamii maeneo yale wangeweza kuchukua hatua mapema zaidi; kabla ya Jeshi halijafika tayari. Hakungekuwa na hata mgongano wa wananchi kulalamika kuwa hawajafika; wanakwenda kuongezea nguvu tu kwenye zimamoto jamii. Vilevile wanakuwa tayari na taarifa. Kwa hiyo kazi itafanyika vizuri kwa sababu tayari wana taarifa kamili na nini hatua ya kuchukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye upande wa *NIDA,* Wabunge wengi wamechangia, lakini nitoe ushauri kwa upande wa taarifa kwa wananchi wanaoishi vijijini. Wizara waje na mkakati maalum namna ya kuwapelekea taarifa wananchi ambao wanaishi vijijini kwa sababu wanatembea umbali mrefu, wanatumia gharama, hawana taarifa, akifika wanamwambia kitambulisho chako, bado, rudi. Mwananchi anatumia hata nauli elfu 30 mpaka 40, mwisho anakata tamaa anaacha, kwa hiyo watumie *local radio, tv,* Viongozi wa Serikali, Madiwani na hasa Madiwani wa Chama cha Mapinduzi ndio watapata taarifa kamili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitembelea kwenye vyuo vyetu, bado vina hali ngumu ukizingatia Jeshi la Uhamiaji pamoja na Jeshi la Zimamoto tumeuhisha sasa hivi ndio wanaanza kujitegemea kama majeshi, hawana vyuo ndio wanaanza kujenga. Kwa hiyo Wizara itenge fedha, wapewe bajeti ili waweze kumaliza vyuo vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna Sheria ya *Parole;* Sheria hii ndio itapelekea kupunguza msongamano wa wafungwa magerezani na hili Mheshimiwa Rais ameliona na ndio maana amemchagua Mwenyekiti wa Bodi ya *Parole* Mheshimiwa Kagasheki kuwa wakatazame walete sheria ya mabadiliko itakayowezesha wafungwa kupata unafuu na kupata msamaha

ili waweze kupunguziwa kesi pamoja na kupunguza msongamano magerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo kata za kimkakati ambayo jiografia imekuwa ni ngumu, uhalifu unapotokea mpaka askari polisi wafike inakuwa ni tatizo hasa katika Jimbo langu la Nkasi Kusini, Kata ya Sintali, Kata ya Kizumbi, Kata ya Myula, pamoja na Kata ya Nyinde. Hizi kata zote ziboreshwe, vituo vya polisi vimechoka, vina hali ngumu pamoja na makazi. Wabunge wengi wamechangia kuhusu makazi ya askari wetu, kwa kweli ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anapokuja kumalizia, kwa kuwa yeye ni msikivu mzuri, safi kabisa, anatenda kazi vizuri, aje na mkakati wa namna ya kuboresha makazi ya askari wetu, yako katika hali ngumu sana pamoja na Ofisi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Juma Othman Hija, atafuatiwa na Mheshimiwa Vita Kawawa na Mheshimiwa Rashid Abdalla Rashid, ajiandae.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nikushukuru kwa kunipatia nafasi jioni hii ili kutoa mchango wangu katika Wizara hii muhimu katika nchi yetu. Pili, niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliompongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyoiongoza nchi yetu kwa umakini na kwa ufasaha zaidi. Mimi pamoja na wapigakura wangu wa Jimbo la Tumbatu, tunamwombea dua Mwenyezi Mungu amjalie afanye kazi zake kwa wepesi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wetu pamoja na Naibu wake kwa namna walivyotayarisha hotuba yao na baadaye kuiwasilisha kwa umakini kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu leo naenda katika michango ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, viongozi wetu wa Wizara hii ni miongoni mwa viongozi wasikivu sana, wanasikiliza maoni ya Wabunge tunapokwenda na kutuelekeza. Kinachotakiwa katika hili ni sisi Wabunge kuwa wasitahimilivu tu lakini ukiwa unakwenda unaomba, unakwenda unaomba, unajibiwa vizuri, basi ustahimili tu unaloliomba utalipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mwaka 2016 nimekuwa nikisimama hapa kuiomba Wizara hii kujengewa Kituo cha Polisi katika Jimbo langu la Tumbatu. Kwa muda wote wa miaka mitano nimekuwa nikionana na viongozi hawa, majibu yao yalikuwa ni mamoja, nayo ni kuniambia kwamba Mheshimiwa subiri itafika siku *Insha Allah* na wewe tutakujengea Kituo chako cha Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeweza kustahimili, na nimestahimili nikijua kwamba mahitaji ya nchi hii katika kujenga vituo hivi ni makubwa, siyo kwangu mie tu, lakini katika nchi nzima mahitaji ya kujenga vituo hivi ni makubwa sana. Sasa unapokwenda kuomba kitu kwa mwenzako lakini asikukatalie anakwambia subiri, basi ni vyema ukasubiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima naishukuru Serikali hii kwa kupitia Wizara hii kwamba ombi langu hili limekubaliwa na Kituo cha Polisi katika Jimbo langu la Tumbatu ujenzi umeshaanza. Kwa hiyo nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali yangu inayoongozwa na Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa namna ombi langu hili lilivyokubaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo naomba mambo mawili katika hili, masafa kutoka Mkokotoni mpaka Tumbatu, jiografia yake ni lazima u-*cross* bahari, sasa basi maaskari wetu pale watakuwa wanakwenda Tumbatu kwa kutumia vidau au viboti vya wananchi. Naiomba Serikali na ni vyema itafutie boti maalum kwa ajili ya maaskari wetu ambao wanakwenda kule Tumbatu, kuwe na boti maalum kwa ajili ya maaskari ambao wanakwenda katika Kituo chetu cha Tumbatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, katika kutatua hili ni vyema pamoja na kituo cha polisi ambacho kitajengwa kule pia

tunaomba maaskari wetu kule wajengewe makazi ili waweze kufanya kazi kule kule. Sisi wananchi wa Tumbatu kwa kushirikiana na Ofisi ndogo ya utawala kule Tumbatu tumeshatenga eneo maalum kwa ajili ya kuwapa Serikali wajenge makazi hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la pili ambalo linafanana kabisa na hili ni kuhusu Kituo changu cha Mkokotoni. Mwaka 2018 nilisimama hapa kutoa masikitiko yangu makubwa kwa namna ya kituo kile kilivyokuwa, lakini nashukuru Serikali imechukua juhudi kituo kile sasa hivi kipo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kutoa mfano, niliwahi kusema ule ukweli ulivyo kwamba, kipindi kile maaskari wetu walikuwa wanafanya kazi, inaponesha mvua wana-*shift,* kutoka ofisini kwao wanafanya kazi katika chumba cha mahabusu lakini *alhamdulillah* hali ni nzuri, wanafanya kazi vizuri na jengo liko vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililokuwepo pale ni moja ambalo ni kubwa, kuhusu makazi ya maaskari pale Mkokotoni…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hija, malizia, muda wako umeisha.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vita Kawawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Abdalla Rashid na Mheshimiwa Rita Kabati, ajiandae.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na Viongozi wote Wakuu wa Majeshi walio chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza Wabunge mbalimbali ambao wameweza kueleza maeneo mbalimbali katika majeshi yetu na kazi wanazozifanya, lakini naomba tu niwaambie majeshi yetu haya yanafanya kazi nzuri sana, sisi tunaosimamia Kamati

tunajua umuhimu, Jeshi la Polisi wanafanya kazi saa 24 kwa siku saba na ndio maana leo tuna amani katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi linalinda usalama wa raia na mali zake, lakini tuna Jeshi la Magereza linahifadhi wale ambao wanakuwa wakorofi na wanawahifadhi vizuri na wanarekebishwa. Tuna Jeshi la Uhamiaji ambalo linakaa, lipo mipakani mwetu, linafanya kazi masaa 24 siku saba au wiki, kuangalia kila mtu anayeingia nchini na linaruhusu watu wanaokuja waliokuwa wema, waliokuwa wabaya wanaondoka, ndio maana nchi yetu leo hii inaendelea kuwa na amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna budi kuyapongeza majeshi yetu haya. Tuna Jeshi la *Fire* basi ikitokea moto, linakuja kuzima, kwa hiyo tunaomba sana Mheshimiwa Waziri na Waheshimiwa Wabunge tutambue majeshi yetu haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Kamati tulibahatika kutembelea na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani tulitembelea nchi moja sitaweza kuitaja, nchi hiyo hakuna amani. Tumefika nchi ile pale tumewekwa sehemu moja na tunatakiwa twende sehemu nyingine, umbali wa kutoka hapa mpaka Morogoro lakini kwa gari ni siku nne, umbali wa kutoka hapa mpaka Morogoro, siku nne na njiani humo kuna vikundi vitatu, kila kikundi kinafanya kazi yake ya uhalifu, kwa sababu hakuna amani. Kwa hiyo tulishindwa kwenda kwa chini na tukashindwa kwenda kwa kuruka kwa sababu hakuna amani. Kwa hiyo sisi hatuna budi kuyapongeza majeshi yetu na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa kazi nzuri inazozifanya za kulinda amani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, naomba nimpongeze na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwanza kwa kukubali na kuridhia maombi ya Wizara chini ya Mheshimiwa *Engineer* Masauni, kuridhia kutoa shilingi bilioni 42.5 kwa *NIDA,* Taasisi yetu ya Vitambulisho vya Taifa kwa ajili ya kuchapisha vitambulisho milioni 13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii *NIDA* imeshapokea fedha hizo na imesha-*order* vitambulisho, kwa hiyo tunachosubiri ni ujio wa vitambulisho ghafi na kuanza kuzalishwa milioni 13. Naamini kabisa maneno yote ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu, Taasisi ya *NIDA* ikikamilisha, kelele zitapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mategemeo yetu kwa Taasisi yetu hii ya *NIDA* ikisimamiwa vizuri chini ya Wizara na ikafanikisha zoezi hili la kuzalisha vitambulisho milioni 13, tutavuka hapa tulipo kwa sababu vitambulisho ni jambo muhimu sana kwa Taifa letu, lakini pia na kwa dunia yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna haja ya kuboresha sheria ili kuona taasisi zetu muhimu zinazohusika na utambuzi kwa watu wetu na kwa ajili ya shughuli za kimsingi za kijamii na kiuchumi zisiachwe nyuma kutokana na vitambulisho hivi vya *NIDA,* kwanza ni vitambulisho janja kwa maana vina *smart card*, vina *chip* ndani yake ambayo inahifadhi taarifa zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunafanya kazi ya *duplications* katika taasisi mbalimbali ya utambuzi wa watu, lakini ushauri wangu ni kwamba lazima tuwe na *uniform* au tunakuwa na *universal identity data bank* kwa ajili ya vitambulisho vyetu vyote ili kupata taarifa zilizo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano leo tumesikia hapa kwa Mheshimiwa mkongwe Maida kwamba kuna mtu aliumwa, akapelekwa Zanzibar, alipofika Zanzibar akafariki na alipofariki baada ya mwaka akaletewa barua ya kuambiwa amestaafu na anatakiwa arudishe vifaa vyote vya Jeshi la Polisi. Hii yote ni kwa sababu ya kukosa mfumo unaounganika pamoja ulio sahihi. Kwa hiyo tuuboreshe mfumo huu wa *NIDA,* tukipewa vitambulisho vyote watu wote wakapata tujitahidi sana taasisi zetu zote ziunganishe mfumo uwe mmoja kwenye mfumo huu wa *NIDA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Rashid Abdalla Rashid atafuatiwa na Mheshimiwa Rita Kabati na Mheshimiwa Asia Halamga ajiandae.

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii. Niungane na wenzangu kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuongeza mafungu ndani ya bajeti za Wizara zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri *Engineer* Masauni pamoja na Naibu Waziri wake kwa kazi kubwa anazozifanya na hasa *Engineer* Masauni, nimwambie kwamba ana Naibu Waziri wa kazi sana, ameshatembelea katika maeneo yetu na kuona matatizo mbalimbali ikiwemo Kituo cha Polisi Kengeja. Kaenda kukishuhudia mwenyewe na kuona kwamba kituo hiki kina hali ngumu sana. La kushukuru ni kutuambia kwamba ndani ya mwaka huu wa bajeti zimetengwa kiasi cha shilingi milioni 247 ili kwenda kuanza ujenzi wa kituo kile ambacho kimejengwa zaidi ya miaka 50 iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nije katika upande wa Polisi Jamii, Polisi Jamii katika jimbo langu wamefanya jitihada kubwa na jitihada hizi zilifanyika kwa sababu ya kuahidiwa na *RPC* wa wakati huo ndani ya miaka 10 iliyopita na tukaweza kama wananchi kujenga zizi pale na sasa limefikia hatua ya kuezekwa na tayari hili nimeshaliombea sana tangu akiwa Mheshimiwa Simbachawene ambaye aliniahidi kwamba tutatumia Mfuko wa Tuzo na Tozo kwenda kukuezekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Masauni pia ameshaniahidi kwamba ujenzi huu wa Polisi Jamii tutakwenda kumaliza kuezekea, lakini mpaka sasa hivi ninapozungumza hakuna kinachoendelea. Nimwombe sana Mheshimiwa Masauni akanimalizie jengo langu hili la Polisi Jamii katika huu Mfuko wake wa Tuzo na Tozo ili wananchi waweze kuona umuhimu wa nguvu zao walizozitumia pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo kingine ni Kituo cha Polisi Mkoani, ni kweli kituo hiki sasa hivi kinaendelea kujengwa, lakini

nadhani changamoto zake Mheshimiwa Waziri anazijua kwamba amepata fedha tangu mwezi Desemba, 2022 na ujenzi wake umekwenda kuanza juzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni vizuri Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha akatuambia alikumbwa na tatizo gani hata kituo hiki kutoka Desemba hadi ujenzi umeanza Mei na ujenzi wenyewe nimwambie Mheshimiwa Waziri unahitaji usimamizi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamejengwa lakini ukuta umekaa upande, jana ukuta wameubomoa, nadhani Kamishna wa Zanzibar na yeye yupo hapa, afuatilie aone ni kwa nini huyo *Engineer* anaendeleza ujenzi huo pasi na umadhubuti, pesa milioni 700, ni pesa za kutosha kwa ajili ya huo ujenzi, lakini inaweza kutokea kwamba fedha zisitoshe kwa hali hiyo ambayo inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni Ofisi ya *NIDA,* Wilaya ya Mkoani, Mheshimiwa Waziri anajua kwamba *NIDA,* Wilaya ya Mkoani hakuna Ofisi kuna kaofisi kadogo, kachumba, kastoo wameazimwa pale wilayani, shughuli zote zinafanyika humo humo. Nimwombe Mheshimiwa Waziri hili ni afadhali atoke mwenyewe aje akague ile ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba, kuna suala zima la Ofisi ya Uhamiaji ambayo inaendelea kujengwa katika Wilaya ya Mkoani. Ofisi hii mkataba wake wa ujenzi kati ya Wizara na mkandarasi unamalizika Agosti, 2023. Ujenzi bado uko katika hatua nzuri, lakini niombe mkandarasi wampatie fedha ili aweze kumaliza ile ofisi kwa wakati ili wananchi wa Wilaya ya Mkoani tuweze kupata huduma kutoka katika Jeshi letu la Uhamiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna matatizo makubwa katika Jeshi letu la Polisi Mkoa wetu wa Kusini Pemba. Jeshi linafanya kazi vizuri, lakini pesa za *Other Charge* kwa maana ya *OC* hawapati fedha za kutosha. Tunajua kule tuna Viongozi Wakuu wa Serikali ambao wanaenda Pemba na huduma ambayo inatakiwa kutoka Jeshi la Polisi ni kuongoza misafara na mambo mengine, lakini inapotokea hizo shughuli kwa kweli ma-*RPC* wale

tunawapa wakati mgumu sana wa kuona namna gani misafara ile wataiongoza kwa sababu fedha hawana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba, hili suala la *OC* Mheshimiwa Waziri alifanyie jitihada za kutosha kwa hawa ma-*RPC,* wanapata shida kubwa kwelikweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la mwisho ni kwamba, tunaomba tupate usafiri kwa *patrol* za hawa askari wetu. Askari wanafanya kazi za kutosha, lakini wakati mwingine wanaenda kwa miguu au watumie usafiri wa hizi bodaboda za kawaida, haipendezi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatamani sana kuona askari wetu wa kule Pemba au Zanzibar kwa ujumla wanafanya kazi za doria kama ambavyo wanazifanya askari wenzao wa huku bara. Inapendeza na inatia moyo, lakini unamkuta askari anatembea kwa miguu kufuata mhalifu ni shida. Hilo naomba Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi, bodaboda milioni tatu, milioni tatu na nusu, Waziri atupatie angalau bodaboda 12 kule Pemba, kila mkoa upate bodaboda sita ziweze kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa Asia Halamga na Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil ajiandae.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Wanasema moyo usiokuwa na shukrani hukausha mema yote, kwa niaba ya familia ya Mwamoto naomba nitoe shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Spika na Wabunge wote wa Bunge hili la Muungano kwa kutufariji wakati wa msiba. Kwa kweli hatuna cha kuwapa lakini Mwenyezi Mungu awabarika sana na marehemu alikuwa ni Mume wa Askari wa Gereza Kuu la Iringa. Pia, naomba nishukuru sana Mheshimiwa Waziri ulipiga simu na ukatuletea na mchango Mungu akubariki sana lakini naomba pia niwashukuru *RPC* pamoja na Uongozi mzima wa Magereza Mkoa wa Iringa kwa

ushirikiano wao mkubwa ambao waliuonesha wakati wa msiba wa Kaka yetu mpenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais ambaye ndiye Amiri Jeshi Mkuu kwa maboresho makubwa sana katika Jeshi hili, pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa ushirikiano wao mkubwa katika Wizara hii, wamekuwa watu wa msaada sana wakati wako tayari. Naomba pia niwapongeze Wakuu wote wa Majeshi ambao wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana bila kumsahau Anna Makakala ambaye anatuwakilisha wanawake vizuri katika jeshi hilo. Naomba pia nimpongeze *RPC* wetu wa Mkoa wa Iringa amekuwa na ushirikiano mzuri sana katika Mkoa wetu wa Iringa na kazi nyingi zinakwenda kwa sababu yuko tayari wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Polisi pale Kihesa tumekuwa tukiongea muda mrefu sana, wameanza angalau kujenga, japokuwa nyumba zile hazitoshi, bado maboresho yanahitajika sana katika nyumba zile za *FFU* Kihesa. Pia nyumba zilizopo Makao Makuu pale Iringa, kambi zao kwa kweli ni mbovu sana. Wakinamama, watoto ambao wanakaa katika zile kambi wanaishi kwa shida sana, tunaomba kwa kweli pia ziboreshwe ili waweze kuishi vizuri kwa sababu Askari wengi wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie kuhusu Wilaya ya Kilolo. Wilaya ya Kilolo imeanza siku nyingi sana toka 2022 lakini haijajengewa Makao Makuu ya Polisi katika Wilaya ya Kilolo. Sasa utakuta *OCD* anakaa Kata ya Lugalo karibu kilometa 70 kutoka yalipo Makao Makuu lakini Serikali inatumia gharama kubwa sana kusafirisha mahabusu kutoka huko Lugalo mpaka katika Mahakama ambayo ni Makao Makuu. Kwa hiyo, ungefanyika utaratibu mzuri kwamba Makao Makuu kwanza ijengwe ili *OCD* akae na *DC* sehemu moja, kupunguza hata gharama za Serikali lakini pia hata mahabusu wasiwe wanasafirishwa kwa muda mrefu kwa sababu hata kuna uhaba mkubwa sana wa magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa ni kulipia tu lile eneo kwa sababu eneo lipo lakini halijalipiwa, tulisikia Serikali ilishaanza kutenga pesa kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu ya Polisi Kilolo lakini eneo halijalipiwa, kwa hiyo, ufanyike utaratibu lile eneo walipe fidia kwa wananchi ili waweze kujenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kituo cha Polisi cha Ruaha Mbuyuni kipo mbali sana na Makao Makuu hakina gari lakini kumekuwa na ajali nyingi sana katika ile Barabara, sasa tunaomba Serikali iangalie umuhimu wa kutoa gari katika Kituo cha Polisi cha Ruaha kwa sababu kiko karibu kabisa na Jimbo la Mikumi. Pia, tunaomba Serikali itoe pesa kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi Idodi ambacho ni lango kuu la utalii kwa ajili ya kusaidia Mikumi *National Park.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalipongeza pia Jeshi la Magereza linafanya kazi nzuri sana, kuna mashamba makubwa ambayo kwa kweli kama yatafanyiwa kazi nzuri nafikiri Jeshi la Magereza litakuwa na uchumi wa kutosha. Kuna lile Gereza la Isupilo, kuna Gereza la Pawaga, wana mashamba makubwa ambayo yamekaa hayana kitu chochote, sasa kama hawawezi basi waweke hata wawekezaji waweze kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ritta muda wetu ndio umeisha, unga mkono hoja.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Asia Halamga atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil, Mheshimiwa Abubakari Asenga ajiandae.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi ya kuweza kuchangia kwa ufupi katika Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wote ambao wameweza kumpongeza Mheshimiwa Rais pamoja na Waziri,

Naibu Waziri, Wizara nzima kwa ufanisi wao wa kazi na utendaji wao wa kazi. Nichukue nafasi hii kutoa pole sana kwa wananchi wa Endasak, Wilaya ya Hanang kwa kuunguliwa na soko usiku wa kuamkia juzi, lakini niendelee kuwapa pole kwa sababu wafanyabiashara wengi ni wa hali ya chini kabisa hususani akina mama ambao wameweza kupteza mitaji yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Mkuu wa Wilaya pamoja na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya lakini kubwa zaidi wananchi wa Endasak na wa Wilaya ya Hanang' kwa kukabiliana na moto ule japo umeweza kuleta hasara lakini walihangaika usiku kucha na kufanikiwa kuuzima japo hawakuweza kufanikiwa kuokoa vitu. Adha hii ambayo imeweza kuwakuta wananchi hawa ni kwa sababu Mkoa wa Manyara kwanza kijiografia kutoka Wilaya na Wilaya, Wilaya iliyopo karibu ni kilometa 75, kwa hali ya kawaida Wilaya nyingi unatembea takribani kilometa zaidi ya 300 na hivyo kunapotokea janga na kwa sababu hatuna gari la zimamoto madhara yanakuwa ni makubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ninamuomba Mheshimiwa Waziri uzingatie jiografia ya Mkoa wa Manyara ukubwa wake na uzingatie sasa tuweze kupata gari kwa sababu hatuna gari la zimamoto, gari lililopo lipo Babati Mjini na hatuna visima maalum kwa ajili ya maji, pia hatuna mabomba maalum kwa ajili ya uzimaji wa moto. Kwa hiyo, tunakuomba sana unapokuja kuhitimisha hoja yako basi uhakikishe kwamba Mkoa wa Manyara tupate usafiri huo ili kuweza kukabiliana na majanga yanapotokea ndani ya Mkoa wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru kwa kunipa nafasi.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil atafuatiwa na Mheshimiwa Abubakari Asenga, Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. AHMED YAHYA ABDULWAKIL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote nakushukuru kwa udhati wa nafsi yangu kunipa nafasi hii adhimu ambayo nilikuwa naamini

nitaipata. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, napenda sana kumshukuru Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna usukani alivyoukamata barabara kutuongoza katika nchi yetu. Nchi imetulia, nchi ina amani wawekezaji wanakuja, hakuna longolongo ndogondogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo kwamba Zanzibar nimewahi kusikia hotuba moja ya Mheshimiwa Dkt. Samia kwamba ni eneo maalum tengefu kwa kuwa limezungukwa na *square* mita 2,800 za mraba na zote hizi *square* mita zimezungukwa na bahari yote. Kwa hiyo, nikawahi kumsikia kwamba linahitaji kupata zana za kisasa ili liwe na ulinzi wa kisasa kuepukana na maharamia ambao wanaidowea nchi yetu. Kwa hiyo, naamini timu nzuri inayoongozwa na Ndugu yangu Mheshimiwa Masauni na Mheshimiwa Jumanne wanaweza wakakidhi haja ya nchi yetu kupata ulinzi imara ndani ya bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ni mbaya mno, walishawahi kunyemelea nyemela eneo la Kaskazini Pemba lakini Majeshi yetu ya Ulinzi yalikuwa imara na yakawafukuza wale maharamia. Kwa hiyo, ipo haja kupata mgao maalum wa zana za baharani pamoja na zana za nchi kavu ili shughuli za Jeshi la Polisi ziweze kuimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu niingie katika Bunge hili nilizungumza kuhusu Kituo cha Polisi cha Chukwani ambacho ni cha ghorofa, nikapata matumaini katika bajeti iliyopita kwamba kitajengwa au kitamaliziwa maana yake wananchi wamechangia milioni 60 wenyewe kukijenga. Nikapata matumaini kwamba katika bajeti tunayoendelea nayo, ziko zimetengwa milioni 60. Nimekwenda panda shuka Makao Makuu ya Jeshi la Polisi nimeonana na Kamishna wa Polisi, sijapata matumaini ya aina yoyote kiasi kwamba nimeanza kuvunjika moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo natumia nafasi hii kuwaambia kwamba mimi sina nia hata siku moja ya kuzuia shilingi ya mtu yeyote, hata mia! Naomba nipate maelezo kamili ya kituo kile juu ya wananchi waliochangia milioni 60 nguvu zao na baadhi ya wengine ni wageni baada ya matokeo makubwa

ya uvunjifu wa amani. Wameshakufa watu watatu na akitaka nani na nani nitamuambia, Wazungu wawili wamekufa mwaka jana, kwenye uchaguzi kuna Mzungu alivamiwa na mmoja Mwanasheria ambae alikuwa anashughulikia uchaguzi, mwanae Mwanasheria Hamili kadhalika alivyamiwa. Kwa hiyo, hali ni mbaya mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache naomba sana nipate jibu rasmi ya kuwa kile kituo ni lini kitamalizika lakini yote kwa yote naunga hoja mkono asilimia 100. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ahmed, Mheshimiwa Abubakari Asenga atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Jumanne Sagini ajiandae.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, ahsante sana kwa nafasi hii. Nami ninamshukuru Mheshimiwa Rais, Waziri na Watumishi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani, moja kwa kufahamu kwamba katika dunia tunayoenda sasa ya sayansi na teknolojia ni aibu sana kuendelea kutumia Askari barabarani kuongoza magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona katika bajeti ya Waziri kwamba mmeanza kufunga taa katika Majiji makubwa kama Dar es Salaam, Arusha na Mwanza, hii programu ni nzuri sana na ni muhimu ikaendelea katika maeneo mengine kama Morogoro na kwingineko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika dunia ya sasa haiwezekani hata kidogo kwa kweli tuna upungufu wa Askari karibu asilimia 40 ya nchi yetu halafu tunaendelea kutumia Polisi kwenda kuongoza magari barabarani. Tunaomba hii teknolojia iendelee mbele watu wakae sehemu wachache wa-*control computer* watazame magari yanaoenda *speed*. Mtu anakamatwa hata kama mbele ya kilometa 50 anapewa faini kuliko Askari kukaa kila kichochoro, wakati huo wananchi katika vijiji wananchi katika Kata wanalalamikia wapate Askari wa kuwalinda. Kwa hiyo, hili ni jambo zuri na ni jambo kubwa, mpango huu Mheshimiwa Waziri ni

vizuri ukawekewa fedha za kutosha ukaenda katika Majiji yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mimi kushika shilingi ya Kaka yangu Mheshimiwa Masauni nitashika kwa mambo mawili. Kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wote wamefika Jimboni kwangu. Mheshimiwa Waziri tumeenda nae Jimboni mpaka tumepita vichochoroni mpaka kwenye Magereza ya Idete ameenda mpaka Gereza la Kiberege ameenda kule, tumeingia ndani kona zote. Leo Watanzania wa Kilombero wa Ifakara wanaangalia hivi ninavyochangia, ahadi yao ya Wilaya ya Kilombero kukosa Kituo cha Polisi cha Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile ni Wilaya kongwe sana, haina Kituo cha Polisi cha Wilaya, tumeshatafuta eneo tumelipata na mimi Mbunge nimepeleka tofali, anapokaa *OCD* wetu hapafai, wakati wa mafuriko maji yanaingia. Kwa hiyo, kama ni kushika shilingi Mheshimiwa Waziri mimi nitataka ufafanuzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni Kituo cha Polisi Tarafa ya Mwaya Kata ya Mwaya. Mheshimiwa Waziri umefika umekuta kituo cha Polisi cha mbao, katika dunia ya sasa hivi Kata ambayo inaongoza kwa watu wengi, mimi nina tofali za kuchangia pale Wizara inanipa nini? Tujenge Kituo cha Polisi ama tukarabati tuondoe zile mbao katika Kata ya Mwaya Askari wetu wapate Kituo cha Polisi chenye sifa ya kukaa vizuri. Kituo cha Polisi cha Mwaya kila mwaka Waandishi wa Habari wanaenda wanakipiga picha wanakisambaza hizo picha. Kwa hiyo, siyo vizuri jambo hili ni baya sana katika Kata yetu ya Mwaya, Mheshimiwa Waziri nakuomba sana chondechonde haya mambo mawili makubwa unisaidie Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Kilombero na Kituo cha Polisi cha Kata ya Mwaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, *NIDA* imekuwa usumbufu kama baadhi ya Wabunge walivyosema. Wananchi wetu walishakubali kupata Namba za *NIDA* achana na haya mambo ya kitambulisho. Namba hizi haziji kwa wakati, sasa kama kweli mmeweka bilioni 42.5 Mheshimiwa Waziri tafauteni utaratibu ambao namba hizi watazi-*print* kwa wakati. Mimi kila siku

napokea meseji hapa 10, 15, 20, nimekwama nimekuja Wilayani nimetafuta *NIDA* nimekosa. Nikatafuta na mimi operesheni nikaongea na Mkurugenzi wa *NIDA* na mimi nikatafuta chochote kitu, tukawachukuwa watu wa *NIDA* wakaanza kuzunguka katika Kata kufanya operesheni ya kuandikisha, haijasaidia kitu bado watu wengi hawajaandikishwa na watu wengi hawajapata namba. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba sana jambo hilo utusaidie sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Ifakara inaonekana inaongoza katika utapeli wa kimitandao. Kuna vijana wachache ambao wamekuja kutuharibia Mji wetu wa Ifakara. Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana kwa kuniletea *OCD* mpya na Mkuu wetu wa Wilaya wameanza operesheni maalum ya Kamati ya Ulinzi na Usalama kuhakikisha kwamba Ifakara inasafishika na tunaondoka katika hiyo *rank* ya kwanza ya utapeli wa kimitandao kama juzi nilivyomuona Afande *RPC* wa Morogoro anachukua hatua na tunasafisha Mji wetu na Kilombero inakuwa safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Esther Matiko atafuatiwa na Mheshimiwa Jumanne Sagini, mtoa hoja ajiandae.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nitaanza na Serikali kulipa malimbikizo ya madeni ambayo yanatokana na safari za kikazi na uhamisho kwa Askari wetu.

Pili, Serikali ihakikishe inawapa fedha askari kununua *uniform*. Wamekuwa wakijinunulia *uniform* wao wenyewe na mtakapoanza kuwapa fedha mhakikishe mnapa na *arrears* zote za nyuma ambazo wamekuwa wakitoa hela zao kununua *uniform* maana yake mshahara wao wenyewe ni mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni kuhusiana na manyanyaso wanaopata Askari wenye vyeo vya chini kazini. Nimepokea malalamiko mengi sana kwa Askari Magereza na hata Askari wa Jeshi la Polisi, Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu wako nimeshafikisha baadhi ya manyanyaso hayo.

Unakuta Askari wengine wananyanyasika wanahamishwa hata zaidi ya mara 10 kisa tu mkubwa wake anamchukua mwenza wa huyu Askari, kitu ambacho siyo haki kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna kesi nyingine ambayo nitaenda kuitoa kama *case study* ili muweze kufanya kama ni tafiti au muunde Tume kuhakikisha kwamba hawa Askari ambao wanajitoa wasinyanyasike. Kuna Askari ambaye alikuwa ni Askari Magereza wa Gereza la Karanga anaitwa George Mkonda alikuwa ni Koplo *by then* 2014. Mkuu wake wa Magereza kukawa na mgongano wa kimaslahi akamuundia zengwe, Askari huyo akapeleka malalamiko yake kwenye Ofisi ya Rais, Maadili ya Viongozi wa Umma, wakamuandikia huyu Mkuu wa Gereza onyo. Hakuishia hapo akaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri sana huyu Mkuu wa Gereza akapandishwa cheo kuwa *RPO* wa Kilimanjaro. Mheshimiwa Waziri Masauni unajua na Naibu Waziri unajua na hata Katibu Mkuu wa Wizara unajua, alivyokuwa hivyo akamuundia zengwe huyu Askari akashushwa cheo akapewa adhabu ya miaka mitatu akahamishwa kuja Dodoma. Kuanzia 2016 adhabu kwa kawaida ni miaka mitatu mitatu, amekaa na adhabu mpaka 2021, miaka mitano ndiyo akarudishiwa cheo chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hawa Askari wanajitoa, mimi nimeshawahi kwenda gerezani jamani, hawa Askari wana-*risk* maisha yao sana hasa Askari Gereza. Nimekaa gerezani miezi minne naona jinsi wanavyojitoa, kule gerezani mnapeleka watu wa tabia mbalimbali, *yet* akitoka hapo apate *frustration* ya mkubwa wake wa cheo anamnyanyasa katika kazi, *is not fair*! Huyu Askari amehangaika hebu mtendeeni haki. Msikilizeni, kwanza mmlipe hela yake. Hii adhabu yenyewe amepewa ya magumashi tu, kwamba eti alikuwa anachukua simu za ndugu za mahabusu anawachaji shilingi mia tano, mia tano, hao ndugu wenyewe hawakuwahi kuitwa kuja kutoa *testimony*, amelalamika mtoto wa watu hamjamsikiliza, mmemshusha cheo miaka mitano, hamjampa malimbikizo. Wenzake sasa hivi ni *Staff Sergeant*, yeye bado ni Koplo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri msikilizeni, amehangaika sana, Katibu Mkuu wenu ana hii kesi, hebu isikilizeni muifanye kama *case study* muweze kuwasaidia Askari Magereza, Askari Polisi na wengine wote ambao wananyanyasika kwa sababu vyeo vyao ni vidogo hawawezi wakaongea kwa maadili. Najua kwa maadili yao hawawezi wakaongea, wasaidieni, apewa *arrears* zake zote, maana yake alitakiwa arudishiwe cheo chake 2019 lakini wamemrudishia 2021, lakini anatakiwa apandishwe kila baada ya miaka mitatu, mkijua kwamba ilikuwa ni zengwa mrudishieni vyeo vyake vyote nae aende kuwa kwenye *Staff Sergeant*. Nilimsikia Mheshimiwa Rais analalamika kwamba unakuta Askari wanakuwa mpaka wazee wakiwa kwenye *Staff Sergeant*! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mambo yenyewe ndiyo haya wanatumikia wanabaki na vyeo vidogo kwa sababu wananyanyasika *they cannot say anywhere*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kabisa Serikali ichukue hili, iunde kama ni Tume Maalumu wafuatilie watu wanaonyanyaswa..

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Esther.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Wafuatilie watu wanaonyanyaswa Askari hawa wa chini waweze kutendewa haki. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Waziri, Naibu Waziri na viongozi wote kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka wa Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Spika, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi kinachoishia Aprili, 2023 Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani imesimamia kwa uadilifu na ufanisi mkubwa masuala yote ya usalama wa raia hasa kurudisha uwajibikaji kazini iliyopelekea kupungua kwa uhalifu. Pia kwa kusimamia vizuri rushwa na upendeleo umepungua kwa kiasi kikubwa kupelekea wananchi kushiriki kikamilifu shughuli za ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo makubwa ya ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Mbalizi kwa kushirikisha wananchi, askari bado wanaendelea kufanya kazi katika mazingira magumu kutokana na kutokuwepo kwa nyumba za askari hasa katika eneo jirani na Kituo cha Polisi. Ni vigumu sana kwa Wilaya yenye askari zaidi ya 150 na inatoa huduma kwa wakazi karibu 500,000. Kunapotokea dharula, viongozi na hata askari inakuwa vigumu kujikusanya kwa muda muafaka. Pia wananchi wameanza ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja C, pia wananchi katika Tarafa zingine wameonesha nia ya kushiriki kujenga vituo vingine katika Miji Midogo ya Ilembo, Isuto na Ikukwa. Kuna uhitaji mkubwa wa kuwepo vituo vya polisi katika maeneo haya kutokana na shughuli za kichumi na pia umbali kutoka makao makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Serikali ianze mchakato na itenge bajeti ya angalau shilingi milioni 300 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vipya vya Igoma, Ilembo, Isuto na Ikukwa. Kwa vile wananchi katika baadhi ya kata wameanza ujenzi na wamehamasika kushiriki ujenzi wa vituo vinne vipya vya polisi, bajeti hii inayoombwa ya shilingi milioni 300 kwa kila kituo itachochea kumaliza ujenzi wa maeneo muhimu ya vituo hivi na kuwezesha motisha na ufanisi kwa askari. Pia napendekeza kuongeza magari kwa ajili ya usafiri hasa ukizingatia jiografia ya Wilaya ya Kipolisi ya Mbalizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza, Naibu Waziri na uongozi mzima wa Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kazi nzuri ya kulinda wananchi na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto ya Wizara ni kwa baadhi ya Wilaya kutokuwa na vituo vya polisi vyenye hadhi hasa katika makao makuu ya Wilaya kwa baadhi ya maeneo nchini mfano ni Wilaya ya Kilindi, Mkoani Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Mambo ya Ndani ametembela Wilayani kwangu na kujionea hali halisi ya ubovu, uchakavu na udogo wa kituo cha polisi. Naomba leo Mheshimiwa Waziri anieleze, je, ni lini Wizara itatujengea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe shukrani za dhati kwa Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kazi kubwa wanayofanya ya kulinda raia na mali zao. Hata hivyo nina mambo kadhaa ya msingi sana ya kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhusu kuwajumuisha polisi kutumia kikokotoo kama watumishi wengine wa Serikali tofauti na askari wengine wa majeshi mengine. Yapo malalamiko makubwa miongoni mwa askari kutoridhika na utaratibu huo. Askari hawa wa Wizara hii wanaona ni vyema utaratibu unaotumika kutoa mafao au kikokotoo kinachotumika kwa askari wengine mfano toka Wizara ya Ulinzi utumike na kwao pia kwani mazingira yao ya ufanyaji kazi yanalingana na askari wengine, lakini pia hawana muda wa kufanya mambo yao wanapokuwa katika ajira ukilinganisha na watumishi wengine wa umma, hivyo hawana muda wa kutafuta fedha nyingine kwa ajili ya kujiandaa na maisha ya kustaafu kama ilivyo kwa watumishi wengine wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia viinua mgongo vyao au pensheni zao kwa walio wengi sio kubwa, hivyo, kutumia

kikokotoo cha asilimia 33 hakiwasaidii kujiweka vizuri kwa maisha ya kustaafu, na pia umri wao wa kustaafu ni tofauti na wastaafu wengine wa kada nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ni vyema kwa ufanisi bora wa majukumu yao wakiwa na afya nzuri ya akili wawapo kazini na baada ya kustaafu, tunaiomba Serikali ilipe uzito jambo hili la kutumia utaratibu wa kuwalipa mafao kama askari wengi wa Wizara ya Ulinzi na sio kikokotoo hiki cha asilimia 33 kama kinavyotumika kwa watumishi wengine wa umma ili kuweka heshima sawa kwa askari wetu wote na kuimarisha usalama wa raia na mali zao.

Pili, Serikali iweke mpango mahususi kwa kutumia nguvu kazi yake wakiwemo wafungwa na mahabusu kuhakikisha inaboresha makazi ya askari. Mfano makazi ya askari polisi ndani ya Jimbo la Iringa hayaridhishi. Hata makazi ya askari polisi wa Dodoma Kituo Kikuu cha Polisi *Iringa Road* hayaridhishi, ni aibu kwetu kama viongozi kuridhika kuwa na makazi duni namna hii ya askari wetu ambao ndiyo wanalinda mali na wananchi wetu wote yakiwemo mahoteli makubwa, maghorofa na roho zetu Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, wenza au wanawake wa askari polisi waangaliwe kwa namna ya kipekee katika kuwawezesha kiuchumi ili kusaidia ustawi wa familia za askari wetu. Kwa kuwa mara nyingi kupata ushirikiano wa kukopeshwa kwenye vikundi mitaani inakuwa ni changamoto kutokana na kazi za wenza wao. Uwepo mpango mahsusi wa kuzisaidia familia za askari kiuchumi kwa kuwawezesha wenza wao.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa inayoendelea kufanya kwa kuhakikisha ulinzi na usalama unaendelea kuimarika katika pande zote za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, polisi wanafanya kazi kubwa sana ila idadi ya polisi ni wachache, naiomba Serikali kuendelea kuajiri askari ili kuendelea kuimarisha ulinzi katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Igalula lina changamoto kubwa ya vituo vya polisi, kwa kutambua hilo wananchi wameanzisha ujenzi wa vituo vya polisi katika Kata za Tura na Goweko; naiomba sana Serikali kutupatia pesa ili tuweze kukamilisha ujenzi wa vituo vya polisi vya Tura na Goweko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na polisi kufanya kazi kubwa sana ila kumekuwepo na kutokulipwa kwa stahiki zao ambazo zipo kwa mujibu wa sheria, kwa mfano pesa ya pango yaani kodi za nyumba kila mwezi. Polisi wamekuwa hawalipwi pesa hizi kwa muda sana, naiomba Serikali itusaidie kuwalipa ili kupunguza rushwa kwa sababu ya maisha magumu ya polisi. Polisi wamekuwa wakidai malimbikizo mengi sana, niiombe Serikali iwalipe polisi ili waweze kuwa na moyo kwa kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto kubwa sana kwenye upatikanaji wa Vitambulisho vya Taifa, wananchi wanapata changamoto kubwa sana, kwanza ofisi za *NIDA* ipo moja kila Mkoa, sasa ipo moja tu wananchi kutoka Kata za Mmale, Loya na Tura wanasafiri umbali zaidi ya kilometa 180 - 200 kufuata vitambulisho mkoani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali naomba sana zoezi la vitambulisho warudie tena kuandikisha kwenye kata zetu ili wananchi wengi wapate vitambulisho kuliko usumbufu wanaoupata wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko mengi ya *OCD* wangu wa Wilaya ya Uyui, unyanyasaji wa kituo cha polisi wamekuwa wanawabambikia kesi sana hasa waganga wa kienyeji. Naomba sana Serikali kuchunguza juu ya mwenendo wa *OCD* Uyui amefikia anakamata watu anawaweka ndani mpaka siku kumi bila hata kuwafikisha mahakamani mpaka Diwani na Mtendaji wa Kata ya Miswaki amewakanata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba msaada wako kufanya uchunguzi wa kina juu ya polisi Uyui.

**MHE. SULEIMAN HAROUB SULEIMAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa

kutujaalia afya njema na kuweza kuchangia hotuba hii ya Wizara yetu muhimu kwa ustawi wa Taifa letu. Aidha, naomba kuchukua fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia ni Amiri Jeshi Mkuu kwa kutuongoza kwa umahiri na uweledi mkubwa, ninamuombea kwa Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema na mafanikio mema zaidi.

Pia pongezi kwa Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini pia nampongeza Waziri Mheshimiwa *Engineer* Hamad Yusuf Masauni na Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia *IGP,* Makanda, *RPC, OCD* na maafande wetu wote walio chini ya Wizara hii. Nchi ipo salama na kwa mipango na mikakati ya Wizara hii nina imani thabiti kuwa Tanzania itaendelea kuwa salama na Watanzania tutaendelea kuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo naomba kuchangia na kushauri machache kama ifuatavyo; kwanza kutoa mafunzo ya ukarimu na matumizi ya lugha nzuri kwa wananchi. Kuna baadhi ya askari hasa Zanzibar unapokwenda kutafuta huduma za usalama na ulinzi baadhi ya askari wanawajibu raia lugha zisizoridhisha na zinazovunja moyo, haziendani na heshima ya Jeshi letu

Pili, utoaji wa huduma nzuri hasa katika sehemu za kuingia nchini kwa mfano uwanja wa ndege na bandarini, mfano Zanzibar uchumi wake unategemea zaidi sekta ya utalii hivyo basi askari wa Uhamiaji wa maeneo hayo ni vizuri watoe huduma nzuri na stahiki kwa Watanzania na wasio Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni kuhusu Vitambulisho vya Mtanzania kwa wenye sifa za kupatiwa. Kuna ukakasi kwa baadhi ya maeneo katika upatikanaji wa vitambulisho hivyo.

Nne ni kuhusu doria; ni jambo zuri sana kwa kuimarisha ulinzi na usalama katika maeneo yetu sehemu tofauti za nchi yetu hivyo ninashauri Jeshi la Polisi liendelee na doria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, naipongeza Serikali inayoongozwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan; Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Zanzibar na wasaidizi wao wote. Aidha nikutakie kheri na mafanikio mema zaidi Waziri - Mheshimiwa Hamad Yussuf Masauni na Naibu Waziri - Mheshimiwa Jumanne Sagini katika kutimiza majukumu mliokabidhiwa na Mheshimiwa Rais kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia, ahsante sana.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, magereza nyingi nchini miundombinu ni chakavu, ninaomba Serikali kuona namna yoyote ya kurekebisha jengo la Magereza Lindi, hakuna gari, TAKUKURU walio wengi wanatumia magari binafsi, wasaidiwe Lindi kupata magari, zimamoto vifaa hawana tunahitaji boti ya uokoaji. Lindi tunapata changamoto, Serikali itusaidie.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iimarishe shughuli za Jeshi la Magereza hususani Gereza la King'ang'a kwa kufanya mambo yafuatayo; kwanza, kupima eneo la gereza lote na kupata hatimiliki ili kuepuka uvamizi wa eneo hilo na kulipangia matumizi bora ya ardhi.

Pili, kuwe na ufugaji wenye tija kuliko ilivyo sasa kuna kundi kubwa la ng'ombe lenye tija ndogo sana. Wanafuga kienyeji, hawana shamba la malisho, hawana kisima cha maji, hawana josho la koushea mifugo, hawana wataalam wa kusimamia mifugo matokeo yake hata *product* ya mifugo yao ni kilo chache sana. Wananchi hawana cha kujifunza kutoka Gereza la Mifugo King'ang'a.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumaliza mgogoro kati ya gereza na wananchi wa Kingale, tunapenda kupata askari ambao wataimarisha mahusiano na jamii inayolizunguka gereza tofauti na ilivyo sasa. Askari waliokaa muda mrefu gerezani pale wangehamishiwa maeneo mengine ili kupata askari wengine watakaoleta maarifa mapya ya maendeleo. Tunapenda kupata

askari wenye taaluma ya mifugo, kilimo, umwagiliaji na wachumi ili kulisaidia gereza kujiimarisha kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Mji wa Kondoa umekuwa na unaendelea kukua, tunahitaji kupatiwa vifaa vya Jeshi la Zimamoto ikiwemo gari kwa maana hakuna huduma hiyo hali tukiwa tunashuhudia mali za wananchi zinateketea kwa moto na kusababisha hasara kubwa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tumeshuhudia mabweni ya wanafunzi yakiteketea bila msaada wowote kwenye Shule ya Sekondari *Kondoa Islamic* na kituo cha kulelea mayatima cha Bicha, magari yameungua moto, viwanda vya mafuta ya alizeti vimeteketea na nyumba za wananchi. Tunaomba gari la zimamoto na vifaa vya askari wa zimamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu magari ya polisi yamechakaa sana tunaomba polisi wilaya wapatiwe gari la kufanyia doria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jumanne Sagini, Mheshimiwa Naibu Waziri na mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nikushukuru wewe kwa kuendesha vizuri sana kipindi hiki cha hoja yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia afya na kutuwezesha kukutana hapa leo ili kujadili hotuba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Ninamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini kama Msaidizi wake kwenye nafasi ya Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninamshukuru Makamu wa Rais, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Waziri Mkuu, Waziri wangu Mheshimiwa Injinia Masauni kwa miongozo bora kabisa wanayonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu. Pia

ninawashukuru Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakuu wa Vyombo na Wasaidizi wao kwa msaada ambao wamekuwa wakinipa katika utekelezaji wa majukumu ya Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naishukuru familia yangu kwa msaada na watoto kuvumilia wakati mwingine nakuwa nao mbali. Zaidi niwape shukrani za pekee wananchi wa Butiama kwa kuendelea kunivumilia ninapokuwa natekeleza majukumu haya, wakati mwingine nakuwa nao mbali na hasa siku ya leo wanapomhifadhi katika nyumba yake ya milele aliyekuwa Mbunge wa eneo hilo niliyepokea nafasi yake, Mheshimiwa Nimrod Mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamezungumzwa mengi hapa, lakini mtoa hoja atakuja ayaguse mengi. Mimi mdogo wake niguse yale machache ambayo yametajwa na Waheshimiwa Wabunge. Moja ni kuhusu miundombinu ya majengo ya ofisi, makazi ya Askari wa vyeo tofauti kwa vyombo vyote vilivyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka na katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wangu imesemwa bayana kabisa namna ambavyo dhamira ya Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu Dkt. Samia Suluhu Hassan alivyoamua kushughulikia changamoto zinazokabili vyombo vilivyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwa uchache tu nikiwarejesha Waheshimiwa Wabunge katika ukurasa wa 50 wa Kitabu cha Bajeti mpaka 65, imeelezwa kwa kirefu namna ambavyo Jeshi la Polisi kwenye miradi yake ya maendeleo imegusia ukarabati wa ofisi, makazi pamoja na kujenga vituo vipya vya polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nyumba, mtakumbuka mwaka uliopita, Mheshimiwa Waziri wangu alizindua mkakati wa ujenzi wa nyumba 1,760 kama sehemu ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo wa Sekta ya Usalama wa Raia na mali zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa majengo, imetajwa hapa na Waheshimiwa tofauti tofauti kuhusu Magereza na Polisi. Nilitaka niwatajie maeneo machache ambayo tumefanya kazi kubwa. Kwenye upande wa Magereza imeelezwa vizuri sana kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wangu kwamba yako maeneo yanayomilikiwa na Jeshi la Magereza yalikuwa hayajamilikiwa rasmi kwa maana ya kuwa na hati lakini katika bajeti hii, zaidi ya shilingi bilioni 1.778 zimetengwa kwa ajili ya kulipa fidia, kulipia upimaji wa viwanja na kukabidhi hati kwa ajili ya vyombo vyetu hivi hasa Magereza. Ukurasa wa 19 mpaka 21, aya ya 31 mpaka 34 kwenye bajeti yetu imeeleza bayana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya maeneo hayo kwa mfano, nitaje Chuo cha Kiwira kitanufaika, Chalinze, Namtumbo, Nanyumbu, Hanang', Muleba, Liwale, Kalambo, Mlele, Ikungi, Bahi, *Wazo Hill*, Kimbiji, Namvuti, Chamwino na Kaliua. Kote huko maeneo yameshalipiwa, kinachofuata ni ujenzi na hati tunazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa Jeshi la Zimamoto na Uokozi, zaidi ya shilingi milioni 210 zimetengwa kwa ajili ya kulipa fidia ili hatimaye jeshi hili limiliki maeneo hayo ili fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi ziweze kujengwa na kuepusha migogoro iliyopo kati ya wananchi na vyombo vyetu. Uhamiaji kadhalika wametengewa zaidi ya shilingi milioni 120 kwa ajili ya kulipa fidia. Polisi wametengewa zaidi ya shilingi milioni 554.8 kwa ajili ya kulipia fidia maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeelezwa juu ya uimarishaji wa Magereza, Magereza chakavu na mengine yanahitaji kujengwa upya. Niwakumbushe kwamba imeelezwa katika hotuba ya Waziri wangu kwamba mwaka huu unaokuja, Magereza 12 yafuatayo yatajengwa na kukamilishwa yale yanayoendelea kujengwa; Gereza la Msalato, Kaliua, Kakonko, Karatu, Kilosa, Kyabakari, Gairo, Kingurungundwa, Mpimbe na Sengerema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya ujenzi maeneo ya Zimamoto na Uokozi imeelezwa kwa ufasaha na Mheshimiwa Kichiki Neema Lugangira. Tumesema katika eneo hilo zaidi ya shilingi bilioni 2.3 zimepokelewa ili kuendeleza ujenzi eneo la Songwe, eneo la

Simiyu, Manyara, Kagera, Katavi, Geita na Njombe na ujenzi unaendelea kutekelezwa na kwa mwaka ujao zimetengwa zaidi ya shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa majengo ya mikoa hiyo saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vitendea kazi kwenye upande wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, zaidi ya shilingi bilioni tatu zimetengwa kwa ajili hiyo na kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri mmesikia majadiliano yanayoendelea na moja ya nchi wahisani ili kupata zaidi ya shilingi bilioni 100 kwa madhumuni tu ya kuimarisha vitendea kazi kwa ajili ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji hususan magari na vifaa vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameeleza Mheshimiwa Mbunge kutoka Manyoni juu ya nini tufanye? Nimhakikishie Mheshimiwa, katika Wilaya yake ya Manyoni tumetenga gari. Atapewa gari la lita 1,000 kwa ajili ya ku-*support* shughuli za Zimamoto na Uokozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la Uhamiaji, mwaka 2022/2023 wamepata zaidi ya shilingi bilioni 5.6 kwa ajili ya kununua magari 30 kuwezesha utekelezaji wa majukumu yao. Mwaka ujao tumetenga shilingi bilioni 3.8 kununua magari 23 kusaidia utendaji hasa misako na doria ambayo imelalamikiwa kwa kiwango kikubwa hapa na baadhi ya Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usalama barabarani. Imetolewa hoja hapa na Mheshimiwa Shabiby kuhusu umuhimu wa kuzingatia ratiba za magari yale badala ya kutegemea tu *speed governor* na vitu kama hivyo. Pamoja na kutumia hizo teknolojia, ushauri wake tunauchukua na tunaanza kuufanyia kazi. Baraza la Taifa la Usalama Barabarani eneo hilo ni eneo linalosisitizwa sana ili ratiba inayotolewa na *LATRA* izingatiwe na mabasi yote na basi litakalo-*overspeed* kwa maana ni mwendo hatarishi hata kwa usalama wa abiria na wenye mali, wadhibitiwe ili waende kama ratiba zao zinavyoonyeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa hapa kwamba baadhi ya Askari wetu wa Usalama Barabarani wanapungukiwa maadili na kufanya vitendo vinavyokiuka nidhamu na maadili

ipasavyo. Niweze kusema *IGP* kupitia Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani, kwa kweli amekuwa madhubuti sana kusimamia nidhamu ya Askari wa Usalama Barabarani. Mtakumbuka *IGP* alivunja ile Kamati inayohusika na utoaji wa leseni za udereva na kuiunda upya baada ya kuonekana wanakiuka maadili. Nikwambieni, *IGP* amewaondoa baadhi ya Askari wasio na maadili kwenye kikosi hiki na kupeleka wengine ili kuhakikisha kwamba nidhamu inakuwa nyenzo namba moja katika utendaji wa jeshi letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge mmoja amezungumzia juu ya uhakiki wa leseni. Mheshimiwa nimekuona. Leseni zile zinahakikiwa kwa sababu uvunjwaji wa kile Kikosi cha Leseni cha Jeshi la Polisi ni baada ya kubaini kwamba zipo leseni zilizokuwa zinatolewa kinyume cha taratibu na wengine walizipata bila hata ya kufanya mafunzo.

Mheshimiwa Mewnyekiti, nikwambie, katika leseni zaidi ya 29,000 zilizohakikiwa katika muda huu mfupi, tumebaini uwepo wa leseni zaidi ya 2,000 ambazo hata wenye nazo walikiri kwamba hawakuzipata kwa utaratibu unaokubalika. Sasa ukishakuwa na watu wanaendesha vyombo vya moto, wanabeba abiria, hawakuhudhuria mafunzo yoyote na ukabaini, lazima uchukue hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo tuvumiliane. Hatuna dhamira ya kumnyang'anya mtu leseni aliyeipata kwa njia za halali na ni mtu ambaye anajua hiyo kazi ya uendeshaji wa magari. Kwa hiyo, nikuondoeni shaka kwamba, wale ambao watakuwa na leseni zao, hawatanyang'anywa kama wamepitia mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Mtoa hoja, Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa *Eng.* Hamad Masauni, karibu uhitimishe hoja yako.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe kwa dhati kabisa kwa namna ambavyo umeongoza na kusimamia vyema majadiliano haya ya kupitisha Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2023/2024.

Pia nichukue fursa hii kuwashukuru kwa dhati kabisa Waheshimiwa Wabunge wote kwa usikivu, kwa uchangiaji wenu makini uliofanywa kwa kuzungumzwa moja kwa moja katika Bunge hili Tukufu pamoja na kwa njia ya maandishi. Naomba niseme kwamba, tunatambua na kuthamini dhamira na nia njema ambayo mnayo ambayo kimsingi inalenga kuboresha mikakati na mbinu za kufanya kazi katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya NUU chini ya Mheshimiwa Mwenyekiti Vita Rashid Kawawa pamoja na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Vincent Mbogo na Wajumbe wote kwa jinsi ambavyo walivyoweza kuwasilisha Taarifa ya Kamati iliyosheheni na yenye maelekezo na ushauri mzuri. Nao niwaahidi kwamba ushauri huo tutauchukua na kuufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja za Wabunge ni nyingi na waliochangia ni wengi. Naomba nizijibu hoja hizi, zile ambazo nitaweza kuzijibu sasa hivi kuzifafanua bila kuorodhesha majina tuweze kuzijibu kwa pamoja kutokana na wingi na wengi wake. Nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jinsi ambavyo ameweza kutoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali kabla yangu mimi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru tena kwa mara nyingine tena Waheshimiwa Wabunge kwanza kwa kuthamini jitihada kubwa sana za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu. Hii inadhihirisha kwamba Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Rais na Serikali yake tunazungumza lugha moja, tunacheza wimbo mmoja, tunatembea pamoja. Tunashukuru sana kwa kuunga mkono jitihada hizo ambazo Mheshimiwa Rais

amekuwa akizifanya toka ameingia madarakani za kuhakikisha kwamba anashughulikia changamoto za Askari na vyombo vya usalama katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Kiongozi Mkuu wa nchi yeye amekuwa ndio mpambanaji namba moja wa kuhakikisha kwamba vyombo hivi vya usalama vinatekeleza majukumu yake katika mazingira mazuri na kwa weledi. Nadhani sisi tunapaswa kufuata nyayo zake. Waheshimiwa Wabunge mmelionesha hilo katika michango yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa jinsi ambavyo wametupongeza na wamependezwa na vyombo hivi vinavyofanya kazi zake vizuri, lakini hawajasita kuonesha maeneo ambayo wanadhani ni vyema yakafanyiwa kazi ili tuweze kuviimarisha vyombo vyetu vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii sasa kuweza kutoa ufafanuzi wa mambo hayo, lakini kabla sijafanya hivyo, kuna hoja moja naomba nianze nayo ambayo nimeona siyo sawa nianze ufafanuzi bila kuizungumzia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Waheshimiwa Wabunge wamezungumza kwa uchungu na hasira kutokana na jinsi ambavyo wanaona kuna haja ya kufanya jitihada zaidi za kuweza kuimarisha vyombo na Askari wetu. Katika mazingira yoyote yale, hakuna namna ambavyo tunaweza kuhalalisha rushwa, hakuna namna ambavyo tunaweza kuhalalisha uzembe, hakuna namna ambavyo tunaweza kuhalalisha uonevu, hakuna namna ambavyo tunaweza kuhalalisha kupora haki ya watu kwa kisingizio chochote. Iwe kwa maslahi madogo, iwe kwa kucheleweshwa kwa haki hizo na maslahi hayo. Kwa hiyo, hili naona nilizungumze likae kwenye rekodi na nina hakika Waheshimiwa Wabunge nao pia wanaamini kama ambavyo ninaamini mimi kwamba tuna haja ya kuhakikisha kwamba tunawatendea haki wananchi wa nchi hii kwa kuepuka vitendo vyote ambavyo ni kinyume na maadili na uadilifu kwa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. Hilo niliona nilizungumze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanya hivyo, ndiyo maana kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri tutaendelea kuhakikisha tunachukua hatua za kisheria kwa yeyote yule, iwe Askari, iwe mtumishi raia katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambaye atakiuka maadili mema ya utendaji kazi wake lakini hatutaacha kuwapongeza wale wote ambao wanafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi ni mashahidi. Leo kuna Askari mmoja mwenye cheo kidogo tu alifanya kitendo cha kishujaa na cha kupigiwa mfano. Tulimleta hapa Waheshimiwa Wabunge mmemwona na tumemtambulisha kwenu na baadaye jioni tukitoka hapa tuna tafrija, yeye pamoja askari wengine waliofanya vizuri kwenye kata, tukiona kwamba ni utaratibu mzuri wa kuweza kutoa motisha kwa Askari wengine; naamini waliofanya vizuri ni wengi, lakini tutaendelea kufanya hivi kila mwaka ili kuweza kutoa motisha kwa Askari wengine ili watambue kwamba tunathamini juhudi za Askari waadilifu, tunathamini juhudi za askari ambao wanafanya kazi zao kwa kujituma na kwa ubunifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zilizozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge kwa uchungu kabisa ni nyingi. Wamezungumzia kwa mfano masuala ya vitendea kazi. Wako waliozungumzia masuala ya usafiri, magari, boti, vitendea kazi vingine mbalimbali kama pikipiki, hata *helicopter* naongezea hiyo, lakini wako Waheshimiwa Wabunge walizungumzia juu ya changamoto ya vituo vya Polisi katika maeneo yao, nyumba za makazi ya Askari. Kuna masuala ya stahiki na madeni ya muda mrefu ya Askari Polisi, masuala ya mafunzo, masuala ya vitendea kazi vya kisasa, mifumo, TEHAMA, vifaa, zana, sare na kadhalika. Mambo mengi yamezungumzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba kutokana na dhamira njema ya dhati ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tokea ameingia madarakani, amefanya kazi kubwa sana ya kuboresha vitendea kazi katika vyombo vyetu vya usalama. Ndiyo maana katika bajeti hii ambayo tunamaliza nayo, ambayo imetekelezwa kwa zaidi ya 80% na ni historia katika Wizara hii kutekeleza bajeti za Mambo ya Ndani kwa zaidi ya 80%, kuna ziada ya zaidi ya Shilingi bilioni 300.

Amekuta bajeti ya shilingi bilioni 900 kufikia Shilingi trilioni 1.1 na mwaka huu tumeongezeka kidogo. Kwa hiyo, dhamira ya Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu inadhihirishwa kutokana na namba zilizopo katika bajeti yetu. Namba hazisemi uongo. Kwa hiyo, hili Waheshimiwa Wabunge nataka niwahakikishie kwamba dhamira ya Mheshimiwa Rais tokea ameingia madarakani ni dhamira ya dhati na dhamira ya vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika suala la ulipaji wa madeni na stahiki mbalimbali, katika mwaka huu wa fedha, shilingi bilioni 82.52 zimetolewa kwa ajili ya kazi hiyo. Ni fedha nyingi, najua fedha hizi zinaweza zisiwe zimekidhi kuweza kutatua matatizo au changamoto ya miaka mingi sana ya madeni ya Askari na kadhalika, lakini angalau kuna kazi na hatua imepigwa. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea kuhakikisha kwamba tunachukua maoni yenu na kufanya jitihada zinazowezekana kupunguza madeni haya ya askari kwa kadiri ya hali ya kiuchumi itakavyoruhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ambalo linadhihirisha juu ya dhamira ya dhati ya Serikali katika kwenda sambamba na dhamira ambayo Waheshimiwa Wabunge wanayo ni kwamba katika kipindi cha mwaka huu tunaomaliza nao, tumeweza kutekeleza miradi 23. Nimekuwepo katika Wizara hii kwa muda mrefu. Ni kwa miaka mingi sana katika kumbukumbu yangu ambapo miradi 23 imekamilika. Miradi hii imekamilika; nazungumza kwa taarifa zilizopatikana mpaka mwezi huu. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kuna miradi kadhaa ambayo inafikiwa katika hatua ya mwisho, kabla ya mwisho wa mwaka huu kumalizika itakuwa imekamilika na hivyo kuongeza hata idadi ya miradi 23 na kuwa miradi mingi zaidi. Miradi hiyo nimeitaja kwa kina katika hotuba yangu, sina haja ya kuirejea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumzia stahiki za Askari, unazungumzia mambo mengi. Kuna masuala kwa mfano ya upandishwaji vyeo. Kumekuwepo malalamiko ya muda mrefu ya Askari kutokupandishwa cheo lakini katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, watumishi zaidi ya 1,696 wamepandishwa vyeo, lakini mwaka huu ambao tunazungumza nao hali kadhalika tunatarajia kupandisha vyeo askari wengi zaidi. Askari hao ambao

wamepandishwa vyeo ni miongoni mwao ni wale Askari ambao tumewapeleka katika kata, wenye vyeo hivi vya ukaguzi na ambao wanaendelea kufanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika ajira, tumeweza kutoa ajira kwa watumishi 6,608 katika kipindi hiki, katika mwaka ambao unamalizika; na mwaka huu ambao tunaomba bajeti muipitishe, tunatarajia kutoa ajira kwa askari 3,117. Lengo ni kuhakikisha kwamba tunapunguza mzigo wa Askari wetu ambao wanatekeleza majukumu makubwa wakiwa na idadi ndogo. Askari wengi wanastaafu lakini Askari kwa muda mrefu walikuwa hawajaweza kuajiriwa hivyo pungufu hilo sasa linaenda kupungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo niliona nataka nilizungumzie ni kwenye eneo la mafunzo. Suala la mafunzo ni suala la msingi sana kwa vyombo vyetu vya usalama na katika hili nataka nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa maelekezo yake mahususi aliyotoa ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeyapongeza ya kuhakikisha kwamba Askari ambao wanakwenda mafunzo hawakatwi posho yao. Hili limefanyika katika mwaka wa fedha huu ambao unamalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusisitiza tena, katika mwaka huu wa fedha maelekezo ya Mheshimiwa Rais ni kuhakikisha kwamba hakuna Askari hata mmoja anakatwa posho yake ya aina yoyote kwa ajili ya mafunzo. Ndiyo maana katika bajeti yetu ya mwaka huu tumetenga zaidi ya Shilingi bilioni 29 kwa shughuli hiyo. Kwa hiyo, hakuna sababu yeyote kwa askari yeyote kukatwa posho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hakuna sababu yeyote kwa askari yeyote kukatwa posho. Lakini nipongeze wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama kuhakikisha kwamba wanaimarisha mafunzo vyuo vyetu vya kuwafundishia askari, na niipongeze vilevile Serikali kupitia Mheshimiwa Rais wetu kwa kutenga bajeti nzuri ya kuimarisha miundombinu ya vyuo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningetoa mfano wa Chuo cha Zimamoto na Uokoaji mwaka huu wa fedha tunavyozungumza

tuna takribani bilioni 1.1 lakini kazi nzuri inaendelea kukamilika katika Chuo cha Raphael Kubaga cha Uhamiaji kule Tanga vilevile, na upande wa Jeshi la Polisi halikadhalika. Kwa hiyo katika eneo la mafunzo kuna jitihada kubwa ambazo zinaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika eneo la uimarishaji wa miundombinu ya usafiri, nimezungumza katika bajeti hii kuna fedha ambayo tumetenga takriban milioni. Kwanza nizungumze, katika bajeti iliyopita mtakumbuka kwamba nilieleza bilioni 15 ilitengwa na kufedha ambayo tayari imeishatolewa kununua magari hayo, na mwaka huu wa fedha tunatarajia kununua magari mengine 24 zaidi kwa shilingi bilioni 7.6. Lakini magari ambayo yako njiani kufika ni magari 101 366 ni pikipiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia kuhusu umuhimu wa kuimarisha usafiri katika ngazi za chini za Kata. Lakini si katika suala la usafiri tu, mwaka huu tumekuja na mpango kabambe. Mheshimiwa Naibu Waziri alizungumza hapa, kwa mwaka jana mtakumbuka tulizindua mpango kabambe wa kuhakikisha kwamba tuna kabiliana na changamoto ya usafiri, makazi ya askari kwa vyombo vyote vya ulinzi na usalama ambapo lengo lilikuwa ni kuja na nyumba na vituo vya polisi 51,760. Tumefanya mpango huo kwa mafanikio makubwa kwa mwaka huu mmoja. Hata hivyo tumeona kuna haja ya kuupitia tena mpango huo na kujikita zaidi katika ngazi ya chini. Baada ya kuona mafanikio makubwa ya Askari Kata katika kata zetu ambapo wamekuwa wakifanya kazi kubwa sana, wamekuwa wakifanyakazi ya kutoa elimu na kuelimisha, wamekuwa karibu na wananchi na kuweza kuyakabili matukio kwa haraka yanapotokezea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge kwahiyo nawapongezeni sana kwa jinsi ambavyo mmeona juu ya umuhimu wa kuwawezesha askari wetu kata hawa, ambapo kata hizi zipo katika majimbo yenu yote. Ndiyo maana tukapewa maelekezo na Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha kwamba si tu tunapeleka magari katika wilaya lakini tupeleke pikipiki katika kata zote ambako kuna askari kata. Na gari na pikipiki hizi ambazo ziko njiani zitakapofika tutaanza kuzitawanya katika kata

na Wilaya hizo. Si tu pikipiki na magari, hata mafuta yatakwenda sasa moja kwa moja kwenye kata na Wilaya, hayatabakia Mkoani. Na ukiangalia bajeti hii imeonesha kiasi cha fedha ambacho kimetengwa kwa ajili ya mafuta kimeongezeka kwa kiwango kikubwa sana *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama hiyo haitoshi, kwa eneo hili la kata tumeweza kufanya maboresho makubwa sana ya Mfuko wetu wa Tozo na Tozo. Kama mnvyotambua Mfuko wa Tuzo na Tuzo umekuwa ukifanya kazi kubwa sana ya kuchangia jitihada za kuimarisha vituo vya polisi na nyumba za askari ili kutoa msukumo zaidi na nyongeza ya kazi kubwa ya fedha ya bajeti ya Serikali inayotengwa kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu nichukue nafasi hii kumpongeza *IGP* kwa kuweza kutoa msaada mkubwa sana katika kufikisha azma hii ya kuleta maboresho makubwa katika matumizi ya mfuko wetu wa Tozo kwa kushirikiana na Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi. Tunakwenda kufanya maboresho makubwa ambayo yatapelekea sasa kuhakikisha tunapata fedha za kujenga vituo vya polisi vya kata zote nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako Wabunge mbalimbali ambao walizungumza hapa, nimeandika majina yao, wale ambao walikuwa wamezungumzia kuhusu habari ya vituo vya polisi kata. Walisema wameishaanza hizo kazi za kujenga vituo vya polisi kata katika kata zao lakini vimeshia njiani kabla ya hata mpango huu. Niwapongeze, najua na wengine hamjapata nafasi ya kusema, lakini mmefanya kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge hawa nitakao wataja wamefanya. Mheshimiwa Chaya, Mheshimiwa Iddi, Mheshimiwa Vicent, Mheshimiwa Jah *People* haa hili jina nadhani halina shida Mheshimiwa, Mheshimiwa Nicholas, Mheshimiwa Munira, niliwasikia mkizungumzia habari ya vituo vya kata. Nataka niwahakikishie, kwamba tutakapoanza kutekeleza mpango huu najua yatahitajika mabadiliko ya sheria, lakini tutaharakisha. Tunadhani katika kipindi kisichozidi miezi sita tuanze utaratibu huu. Tutaanza na kata zenu na tutaanza na kata zile za Waheshimiwa Wabunge ambao watakuwa wameenda kwakushirikiana na wananchi wao

kuanza jitihada za kutafuta maeneo na kuanza kazi za awali. Hilo nataka niwahakikishie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nadhani tutakapoweza kufanikiwa kuweka miundombinu imara katika kila kata katika nchi hii hali ya usalama itaendelea kuimarika katika maeneo yenu na hatimaye katika Taifa kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya Magereza ameyazungumza vizuri Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa hiyo mengine ambayo niliona niyachangie ni kwamba, kuna hoja ambazo zimezungumzwa kuhusiana na suala la uhamiaji haramu, lakini wengine wakalinasibisha jambo hili na msongamano wa mahabusu. Wamesema kwamba wahamiaji haramu hawa wako wengi, hususani hawa ambao wanatoka nchi ya Ethiopia, wamekuwa wakijaza magereza na hivyo kusababisha msongamano. Sitaki nikatae, changamoto ya Wahamiaji haramu hususani wa Ethiopia kwa kwakweli ipo, ingawa imepungua kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba nieleze takwimu mpya ambazo tunazo sasa hivi tunavyozungumzwa. Wahamiaji haramu waliyopo sasa hivi katika magereza ni 1,600. Tumefanikiwa kuwaondosha wahamiaji haramu 3,100 katika siku za hivi karibu. Tumefanya hivyo kwa jitihada na ushirikiano na msaada kwanza wa Shirika, nichukue fursa hii kulishukuru sana Shirika Uhamiaji la Kimataifa *(IOM)* kwa kuweza kutusaidia kuwasafirisha wahamiaji haramu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nipongeze jitihada ambazo zimeendelea kufanyika kwa ushirikiano wa Idara yetu ya Uhamiaji pamoja na Ubalozi wa Ethiopia hapa nchini kwa kuhamasisha ndugu wa hao wahamiaji haramu katika nchi yao kuweza kutoa fedha za kuwaondoa. Jambo hili limetusaidia sana kama Serikali kupunguza gharama za kuwasafirisha watu hawa ambazo hazina sababu yeyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua mna uchungu sana, kwamba watu hawa wakikaa magerezani wanakula bure. Lakini watu hawa vilevile tukitoa hela za wananchi ambazo zingeenda

kujenga shule, zingeenda kujenga hospitali, tukawasafirisha watu ambao waliyokuja hapa kwa hiyari na yenyewe vilevile ni kutumia rasilimali vibaya. Ndiyo maana tukaamua kutuma jitihada hizi; jitihada za kuhakikisha kwamba tunazungumza na Shirika la *IOM* watusaidie kuwaondosha na wamefanya hivyo na kuzungumza na ndugu zao ambao wamefanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la muhimu zaidi ni nini ilhali unaweza ukawaondosha leo wakaja wengine kesho? Jambo la muhimu ni kuhakikisha kwamba tunatafuta ufumbuzi wa kudumu la tatizo la kudumu la Wahamiaji haramu ususani ambao wanatoka Ethiopia ambao ni wengi. Katika kufanya hivyo, katika Hotuba yangu nimesoma imeeleza kwamba, tumefanya marekebisho ya kanuni na kuiondoa nchi ya Ethiopia kutoka katika listi ya nchi ambazo zinatumia viza rejea. Sasa hivi raia wa Ethiopia anaweza akaja na *passport* yake akaingia kwenye mpaka, akatoka bila ya bughudha yeyote. Jambo hili limesaidia sana kutupatia ufumbuzi wa kudumu. Najua ni mapema mno kuweza kusema tunajivunia kwa kiasi gani. Lakini tunavyozungumza sasa hivi takwimu zinaonyesha kwamba tunapata wahamiaji haramu kutoka Ethiopia kwa mwezi hawazidi 40, wakati ilikuwa kwa mwezi wahamiaji haramu zaidi ya 300 wanaingia nchini. Kwa hiyo ni dhahiri kwamba utaratibu huu umeweza kusaidia na pengine utaweza kusaidia zaidi kuliondosha kabisa kama siyo kulimaliza tatizo la wahamiaji haramu katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la msongamano wa Mahabusu lina mambo mengi; na ndiyo maana nataka nichukue fursa hii tena, mimi leo sisemi mnyonge maana Mheshimiwa Rais hawezi kuwa mnyonge; nitasema tumpe haki yake Amiri Jeshi Mkuu kwa jinsi ambavyo anaguswa na changamoto za vyombo vyetu lakini na wananchi wa nchi hii ambao wanahitaji huduma kwa vyombo hivi. Kitendo chake kwa kuunda Tume ya Haki Jinai ambayo hivi karibuni itawasilisha ripoti tunategemea Tume hii itakuja kutupa mapendezo mengi ikiwemo hayo mliyoyazungumza, maboresho ya haki na stahiki za askari, masuala ya mafunzo ambayo nimeelezea na mengineno, lakini hata utaratibu wa jinsi ambavyo mifumo na miundo ya Taasisi zetu za Haki Jinai. Kwa mfano katika jambo moja ambalo lilikuwa lina

changia ongezeko la Magerezani kuwa na msongamano, kama ambavyo mnajua, kuna idadi kubwa ambayo inakaribia idadi ya wafungwa ya mahabusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo unaweza ukakabiliana na tatizo la kuondosha wafungwa ambalo tunakwenda nalo vizuri. Mheshimiwa Rais amefanya jitihada kubwa ya kutoa msamaha kwa wafungwa nimetoa Takwimu, wakati ambapo nawasilisha taarifa yangu. Amefanya kupitia Katiba katika Ibara ya 45(1)(c) cha Katiba kimempa Mamlaka Mheshimiwa Rais ya kutoa msamaha wa wafungwa ambao katika kipindi kilichopia wafungwa 12,515 wameweza kutolewa, kwa mwaka 2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hizi taarifa zisiingie kwenye *Hansard* lakini nataka tu mtambue tu kwamba kuna Idadi kubwa ya wafungwa katika kipindi cha kuanzia miaka hiyo ambayo tangu utaratibu huu umeanza wa wafungwa kuachia. Pia kana kwamba hii haitoshi kupitia Sheria ya Bodi ya *Parole* Sura Na. 400 inazungumzia wafungwa 1,046 ambao wameachiwa lakini kwa huduma ya jamii inazungumzia wafungwa 5,339 ambao wametumikia vifungo vya nje pamoja na kufaidika na huduma hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo utaona, takwimu hizi zinaonyesha jinsi ambavyo sheria hizi; Sheria ya Bodi ya *Parole,* Sheria ya Huduma ya Jamii pamoja na Sheria ya Kifungo cha Nje, pamoja na Mamlaka ya Mheshimiwa Rais Kikatiba inavyosaidia kutupungumzia msongamano wa wafungwa magerezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hii haigusi maabusu. Kwa hiyo lazima kuna haja ya kuangalia namna ya kufanya ili kuhakikisha kwamba tunawaondoa na kuwapunguza mahabusu katika Magereza; na ndiyo maana nimezungumza hapa suala la Tume ya Haki Jinai ambayo naamini kabisa itakuja na mapendekezo ambayo pengine yatatusababishia tuweze, sitaki nilisemee, lakini najua, kwa sababu hata sisi kuna mambo ambayo tumeyaona na tumeyatolea maoni na tutaendelea kuyatolea maoni ili yaweze kuingizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ni namna ambavyo utaratibu wa jinsi mifumo na miundo yetu itakavyoharakisha masuala ya upelelezi, kuepusha mianya ya kutokuwa na upelezi usiokuwa na mapungufu. Wakati mwingine unaweza kusema sasa hivi tumejitahidi sana, Jeshi la Polisi limejitahidi. Kwa mfano ukienda Magereza leo hakuna hata mahabusu mmoja ambao upelelezi wake haujakamilika, lakini bado kuna msongamano. Kuna mahabusu ambao pengine bado wako ndani kwa sababu tu ya sheria zetu zilivyo, kuna mahabusu ambao wako ndani pengine wamekosa dhamana kwa kushindwa kutimiza vigezo vya dhamana, kuna mahabusu pengine wapo ndani leo kwa sababu wanamakosa ambayo kwa mujibu wa sheria hawapaswi wapate dhamana. Kuna mahabusu wapo ndani kwa utashi wao tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mambo haya yanahitaji ufumbuzi wa pamoja, na ndiyo maana nichukue fursa hii kupongeza sana ile Kamati ya Haki Jinai, ambayo iko chini ya *DPP* ambayo imekuwa ikipita kwenye Magereza mbalimbali na kupitia kesi za mahabusu moja baada ya nyingine na kusaidia wale ambao pengine walikuwa wanahitaji msaada wa kisheria, msaada wa mawazo, na wengine ambao kwa sababu ya uelewa mdogo wameshindwa kuzifahamu haki zao; na mahabusu wengi wamekuwa wakiachiliwa kwa utarabu huo. Kwa hiyo niliona nizungumzie hizo ni kama sehemu ya jitihada ambazo tunazichukua za kuhakikisha kwamba tunapunguza msongamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaendelea kuimarisaha Magereza yetu. Wakati nchi hii inaundwa idadi ya watu walikuwa ni wachache sana, sijui kama bado walikuwa wanafika milioni 12. Sasa unazungumzia watu milioni sitini na kitu. Kwa hiyo lazima maeneo haya haya ambayo tumerithi kutoka kwa wakoloni tukubaliane ukweli kwamba hayawezi kutosha kulingana na idadi ya watu walio hapa. Na ndiyo maana katika bajeti yetu mwaka huu tumeongeza. Mwaka jana tulitenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Magereza sita na fedha yote hiyo imetoka na kazi inaanza, mwaka huu tumeongeza Magereza 12. Tunaamini kabisa tutakajenga Magereza mengi zaidi na kuongeza mabweni si tu itasaidia kupunguza msongamano lakini itasaidia dhamira tuliyokuwa nayo katika kuhakikisha kwamba kwenye hii hoja ya

maboresho tuanayoendelea nayo katika Wizara ya kuangalia utaratibu wa urekebu ili tuhakikishe kwamba wafungwa wanaotoka magerezani hawarudii makosa. Na moja katika jambo ambalo linasaidia kuwa na urekebu uliyo bora ni mazingira mazuri ya wafungwa hawa wanapokaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ukiwa na magereza ya kutosha yenye nafasi utaweza kutenganisha wafungwa kulingana na uzito wa makosa yao, usugu wa uhalifu waliyokuwanao umri na kadhali. Kwa hiyo hoja hii ya ujenzi wa Magereza ni hoja ya msingi na hoja endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine ambalo limezungumzwa vilevile, naomba niliunganishe hapa hapa; hoja ya kuimarisha vitendea kazi. Hakuna namna ambavyo tunaweza tukaimarisha usalama wa nchi katika karne hii bila kuwa na vyombo vya kisasa; ikiwemo Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Zimamoto na Jeshi la Uhamiaji. Na ndiyo maana niungane sana na Waheshimiwa Wabunge ambao mmezungumza kwa uchungu sana kuhusu eneo la Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Mmezungumza kwamba Jeshi hili limesahaulika, Jeshi hili linaonewa, wako ambao waliofikia wakasema kwamba kuna haja ya turudishe kwenye Halmashauri, wamesahau changamoto zilizotokea wakati huo ambazo zilikuwa zinasababisha ikaletwa kwenye Jeshi. Lakini najua mmesema hivyo kwa sababu ya uchungu mlio kuwanao, ambapo mko sahihi kabisa, wala mimi siwezi kuwa Waziri ambaye nasema uongo hapa mbele ya Bunge, nikasema kwamba eti Jeshi la Zimamoto letu liko vizuri, lina vifaa vya kutosha; nitakuwa ni Mbunge mwongo, Waziri mwongo na siwezi tena kuingia kwenye rekodi hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nakubaliana na ninyi juu ya kilio chenu hicho. Lakini Waheshimiwa Wabunge nataka niwaambie kitu kimoja; kwamba mkipitia bajeti yangu niliyoisoma mtagundua kuna maeneo mawili ambayo nimeyaeleza na maeneo hayo nadhani yanakwenda sasa kutupatia suluhisho la kudumu kwenye matatizo ambayo ninyi yanawaumiza kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa jambo la kwanza, kwamba tunatarajia kupata magari ya Zimamoto 12 hivi karibuni

kupitia mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya Austria. Nadhani hii nyimbo ya mkopo huu wa Austria ni ya miaka mingi sana, na ninyi Waheshimiwa Wabunge mtakuwa ni mashahidi. Hakuna siku nilivyokuwa Naibu Waziri katika miaka yangu mitano sikuwa nimeimba mwimbo huu; lakini leo santuri hii inafikia mwisho, hayo magari yapo njiani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa zaidi ni kwamba, kupitia Wizara ya Fedha na Mipango Serikali inakamilisha mkopo mwingine wa masharti nafuu. Nichukue fursa hii kumpongeza tena Mheshimiwa Rais, kwanza kwa kuimarisha demokrasia ya uchumi. Ndiyo maana leo tunazungummzia mikopo hii mizuri kabisa ambayo haitakuwa mzigo kwa Watanzania, lakini inakwenda kutoa na kuongeza thamani ya maisha yao na uhai wao, maana uhai uwezi kununua kwa hela na pia inakwenda kuokoa mali zao. Kama mlivyosema Waheshimiwa Wabunge mlio wengi; kwamba leo hii nchi imefunguka, wawekezaji wanaongezeka. Mmeona takwimu nilivyoisoma kwenye Uhamiaji, jinsi idadi ya watu wanaoingia, jinsi vibali vya *class* A vilivyozidi kiwango, inadhihirisha kwamba sasa kuna wimbi kubwa sana la uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuwa na uwekezaji mkubwa halafu tuwe na Jeshi la Zimamoto kama tulilo nalo sasa hivi. Lakini kupitia mkopo huu ambao nina imani kabisa upo katika hatua za mwisho tutakuwa na Jeshi la Zimamoto la kisasa. Kama tulipata shida sana kuzima moto uliokuwa unawaka Mlima Kilimanjaro sasa hivi tutakuja kuleta helkopta kwenye Zimamoto mkopo huu ukikamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, kwamba Serikali ya Awamu ya Sita imeliona hilo na *Insha Allah* kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu jambo hili litakwenda vizuri na litakwenda kuondosha changamoto ambazo Wabunge wamezieleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ni mengi, najua nimeletewa hapa *note* kwamba nimalizie, lakini nataka nizungumzie uraia pacha. Hili nililizungumza juzi, majibu yangu yanabakia vile vile kwamba waheshimiwa ni Watanzania wenzetu

ambao wako nje, tunawathamini sana, michango yao ni muhimu, hapa ni nyumbani kwao japokuwa wameamua kwenda kuchukua *passport* nyingine kwa sababu zozote waliokuwa nazo, tunawahitaji sana waweze kuja kutoa michango kwa uchumi wa nchi hii. Ndio maana Serikali kwa kupitia Wizara ya Mambo ya Nje, ilifanya majadiliano nao na wakaona kwamba kwa sasa na kulingana na uhitaji uliopo, wanaweza wakatimiza azma yao hiyo kwa kuweza kupewa hadhi maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana katika hotuba yangu hii nimeeleza juu ya mpango wa marekebisho ya sheria nyingi ikiwemo Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54 ambayo inalenga kwenda kutibu tatizo na kero moja kubwa ya watu hawa, ili kuwa wanaingia hapa kama wageni, lakini sasa kama jambo hili litapita, basi wataingia hapa bila *visa,* wataingia hapa kama anavyoingia Mtanzania mwingine. Kwa hiyo hiyo ndio kauli yangu, nasisitiza katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona amenitoa katika mstari nilikuwa nataka nieleze kitu kimoja cha muhimu sana, kwamba hii dhana ya maboresho na kuwa na vyombo imara, nikisema hapa nizungumze mipango na mikakati ambayo aidha imeshafanyika au inaendelea kufanyika nahitaji muda mwingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo nataka niyagusie ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeyazungumza kabla sijamaliza. Wamezungumzia hoja ya kuwa na umuhimu wa kuwa na mifumo ya kisasa ya kubaini kushughulikia, pamoja na kuzuia uhalifu ikiwemo kuweka mifumo ya miji salama. Nimezungumza katika hotuba kwamba tunaenda sasa kuweka kamera kwenye miji yetu mitatu kwa kuanzia, lakini nimezungumza najua kuna Waheshimiwa Wabunge wana changamoto hata Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti kwenye Kamati alikuwa analizungumza sana hili na tatizo pamoja na Mheshimiwa Aida kule Nkasi kwenye Maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwenda juzi kwa Mheshimiwa Chege, tatizo hili la vifaa, boti kwenye Maziwa yetu kwenye Bahari, kwenye bajeti hii kuna boti 10 tunaenda kununua. Kwa hiyo mambo ni mengi, lakini kwa sababu muda ni mchache

naomba nimalizie labda jambo moja tu ambalo nisingeomba niliache kutokana na jinsi ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamelizungumza kwa hisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *NIDA*. Ni kweli tumekuwa na changamoto kubwa kwenye upatikanaji wa vitambulisho na changamoto hiyo ilitokana na sababu nyingi. Kwanza, ilikuwa, hatukuweza kununua kadi ghafi za kutosha kwa wakati, lakini sababu ya pili ilichangiwa na kutokea mambo ya UVIKO, tuliweka fedha kwa ajili ya kuomba hizi kadi na mlolongo wa foleni ya mahitaji ulikuwa mkubwa, ikawa tumechelewa kuzipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichukue fursa hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na wananchi wanaonisikiliza hapa, kwamba fedha zote za kadi na ziada zimeshalipwa, yaani sasa hivi hatuna deni la kadi hata moja. Kwanza tulitoa bilioni 28 ambazo kadi zake ziko njiani na nyingine zimeshaanza kuingia nimeambiwa mpaka mwezi huu kuna kadi zimeingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunakwenda kukata mzizi wa fitina. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati amezungumza vizuri, tunakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kulieleza vizuri Mheshimiwa Vita Kawawa. Shilingi bilioni 42.5 na hii ndio fedha ambayo tulitenga kwenye bajeti ya mwaka jana kwa ajili ya ununuzi wa kadi. Maana yake ni kwamba tumetumia fedha ya ziada vile vile kupata kadi nyingi zaidi. Hivyo itakavyofika mwezi Desemba mwaka huu, tunategemea kadi zote zilizokuwa zimeshalipiwa zitakuwa zimefika na hivyo kuanzia wakati huo hatutarajii hata Mtanzania mmoja kuwa hana kitambulisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nisisitize kitu kwamba kwa hivi tunavyozungumza kwa wale Watanzania wenzetu ambao hawana *ID* hizi za *NIDA*. Najua wanazo zile namba za utambulisho waendelee kutumia namba hizo, namba hizo zinatambulika, namba hizo ni halali. Hakuna sababu yoyote ya kumkosesha haki yake Mtanzania yeyote popote pale alipo eti kwa sababu hana kipande kile cha *NIDA*. Kwa sababu namba hii inatumika na inaendelea kutumika kwa taasisi za Serikali, kuendelea kutoa taaluma na kuzitumia ili wananchi waendelee kupata huduma

zao mpaka pale tutakapotarajia ambapo ni Desemba mwaka huu, kuwa tutaweza kufikisha kadi kwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana tukasema sasa tunataka tupeleke mwelekeo wetu kwenye ule utaratibu wa kuwa na kadi moja. Najua mchakato wake siyo mwepesi, lakini tutaanza nao. Tusingeweza kusema hivyo kama hata watu kadi zenyewe hawana. Inaleta matumaini sasa kadi watakuwa nazo, hivyo hata tukija na mpango kwa baadaye kwamba sasa tupunguze gharama za Serikali, za kuwa na rundo la makadi kwenye kipochi na kumsumbua mwananchi kupata huduma, tuwe na utaratibu huo wa kuwa na kadi moja kwa ajili ya matumizi ya huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa fursa hii. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge kuna tangazo la wageni walioko Bungeni jioni hii. Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya Mafunzo ambao ni wanafunzi 150 kutoka Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini cha Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu la 51 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ukurasa 460, kwenye kishkwambi ni ukurasa wa 459.

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 51 - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*......................Sh. 23,169,088,096

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge Kifungu hicho kina mshahara wa Mheshimiwa Waziri na hapa nina orodha ya Waheshimiwa Wabunge wanaotaka ufafanuzi wa hoja mahususi na za kisera.

Mheshimiwa Nicholaus Ngassa hayupo, Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nitumie nafasi hii kukushukuru, lakini pia lazima niseme kweli. Kaka yangu leo Mheshimiwa Waziri ameweza kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa ufasaha sana kiasi ambacho alitaka kunifilisi na kuweza kunishawishi kwamba hoja yangu ya kutaka kushika shilingi niiondoshe. Hata hivyo, nitakuwa na suala dogo tu, nahitaji *commitment* ya Serikali kuhusiana na masuala mazima ya vitambulisho vya Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingi duniani zikiwemo Australia zimefanikiwa kuwarahisishia wananchi wao kwa kupunguza mzigo wa kuwa na kadi nyingi na kuweka katika mfumo wa kukusanya taarifa zote muhimu na kuwa na kadi moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka nifahamu ni lini sasa na sisi tunaweza kufikia huko pamoja na kuhakikisha nchi hii kila Mtanzania anakabidhiwa kitambulisho chake cha Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Simai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tumepokea pongezi tunashukuru sana. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Simai kwamba maelezo niliyoyatoa kwamba tunatarajia Mwezi wa 12 kadi zote ziwe zimeshaingia kwa sababu tumeshalipa fedha zote. Naomba achukulie kama ni *commitment* ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nimhakikishie vilevile dhamira ya dhati ambayo tunayo ya kuhakikisha kwamba tunakuwa na mfumo huo wa kuwa na kadi moja. Ingawa mfumo huu siyo jambo la kusema linatokezea leo na kesho kwa sababu linahitaji *engagement* ya taasisi mbalimbali, inahitaji elimu, linahitaji mabadiliko ya sheria lakini ni kwamba hiyo ni dhamira yetu na mchakato huo tunauanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati iliyo njema ni kwamba hivi karibuni kama chini ya wiki moja nyuma, nilishiriki Mkutano ulioandaliwa na Taasisi ya *Aid Africa* ambapo tumeweza kufanya mazungumzo na taasisi mbalimbali ikiwemo taasisi ya *Melinda and Bill Gates Foundations* na wameahidi kutusaidia kuanza mchakato huu, kama Mbunge alivyosema ziko nchi ambazo zimenufaika, sisi tutachukua nchi hizo zilizonufaika kama ni sehemu ya kujifunza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Naona Mheshimiwa Simai ameridhika, nashukuru. Mheshimiwa Sylivia Sigula.

**MHE. SYLIVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wakati nachangia niliongea kuhusu *Police General Order (PGO)* na katika maelezo yangu nilisema hii *PGO* imekuwa ni ya muda mrefu sana, lakini pia vifungu vingi havina uhalisia wa sasa. Kwenye maelezo yangu nilitoa mfano kwenye *PGO* hiyo hiyo kwenye kifungu cha 132, kinaelezea posho za askari, ikiwemo posho ya mavazi, posho ya pango, posho ya upelelezi na posho zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi kanuni zimekuwa ni za muda mrefu sana na hazina uhalisia kwa maisha ya sasa. Sasa naomba *commitment* ya Serikali kwa sababu kanuni nyingi hizi katika hii *PGO* zinawakandamiza sana askari. Naomba *commitment* ya Serikali ni lini itafanya marekebisho ya hii *PGO* ili kuleta ahueni kwa

askari wetu na nisiporidhika kwa maelezo ya Waziri nitaomba Wabunge wenzangu waniunge mkono hoja yangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemsikia Mheshimiwa Sylivia Sigula na kama Waziri wangu alivyojibu wakati anatoa ufafanuzi wa hoja, ni kwamba kwa kweli hoja zote ni muhimu, zilikuwa hoja nyingi asingeweza kuzijibu zote hapa, lakini tumezitilia maanani sana. Kwa kweli alichosema Mheshimiwa Mbunge ni sahihi *PGO* ni ya muda mrefu ina umuhimu wa kufanyiwa mapitio kama ambavyo nyaraka nyingine za Serikali hufanyiwa mapitio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe tu hakikisho Mheshimiwa Mbunge na kwa sababu tunakutana tena vikao vijavyo kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani kupitia Jeshi la Polisi chini ya *IGP* wataanza mapema iwezekanavyo hata baada ya Bunge lako hili kuanza kufanya mapitio ya *PGO* kwa madhumuni ya kuboresha maeneo ambayo yanaonekana kupitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Naona Mheshimiwa Sylivia ameridhika. Waheshimiwa Wabunge tunaingia kwenye *guillotine*.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 51 - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*......................Sh. 23,169,088,096
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.................Sh. 810,968,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*.............Sh. 1,466,497,000
Kifungu 1004 – *Probation Services Division*.............Sh. 3,809,573,348
Kifungu 1005 – *Government Communication Unit*….Sh. 568,624,000
Kifungu 1006 – *Information and Communication Technology Unit*……..............................Sh. 717,827,703

Kifungu 1007 – *Internal Audit Unit*……………………..…..….Sh. 661,108,553
Kifungu 1008 – *Procurement Management Unit*...…..Sh. 757,161,000
Kifungu 1009 – *Complaints Unit*……………..........................Sh. 441,074,000
Kifungu 1010 – *Legal Services Unit*……………………..Sh. 718,427,500
Kifungu 1011 – *The Police, Prisons, Fire & Rescue and Immigration Services Commission*…....Sh. 802,806,800
Kifungu 2001 – *Registrar of Societies Unit*.....................Sh. 772,550,000
Kifungu 4001 – *Refugees Services Division*………….Sh. 1,822,587,000
Kifungu 4002 – *Anti-Trafficking in Person Secretariat*..Sh. 660,722,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji**

Kifungu 2001 – *Immigration Zanzibar*……..............Sh. 10,612,656,000
Kifungu 2002 – *Immigration Head Quarter*............Sh. 75,836,352,000
Kifungu 2003 – *Immigration Ilala*…...............................Sh. 57,505,000
Kifungu 2004 – *Tanzania Regional Immigration Training Academy*………….....………Sh. 441,140,000
Kifungu 2005 – *Immigration Kinondoni*…......................Sh. 57,505,000
Kifungu 2006 – *Immigration Temeke*………......................Sh. 57,505,000
Kifungu 2007 – *Immigration Arusha*…………………..….Sh. 129,385,000
Kifungu 2008 – *Immigration Dar Es Salaam*…..…………Sh. 112,085,000
Kifungu 2009 – *Immigration Dodoma*………………........Sh. 117,405,000
Kifungu 2010 – *Immigration Geita*……………………….Sh. 113,885,000
Kifungu 2011 – *Immigration Iringa*………...…………….Sh. 115,685,000
Kifungu 2012 – *Immigration Kilimanjaro*…….....………Sh. 134,525,000
Kifungu 2013 – *Immigration Kigoma*……………..…….Sh. 136,165,000
Kifungu 2014 – *Immigration Katavi* ………….....………Sh. 118,085,000
Kifungu 2015 – *Immigration Kagera*……….....…………Sh. 146,980,000
Kifungu 2016 – *Immigration Lindi*……………......…..…Sh. 109,655,000
Kifungu 2017 – *Immigration Mwanza*…..………………Sh. 120,125,000
Kifungu 2018 – *Immigration Manyara* ……....…………Sh. 116,805,000
Kifungu 2019 – Immigration Mbeya…………...………Sh. 121,580,000
Kifungu 2020 – *Immigration Morogoro*…………....……Sh.123,325,000
Kifungu 2021 – *Immigration Mtwara*……...….…………Sh. 123,245,000
Kifungu 2022 – *Immigration Mara*…………....………....Sh. 117,880,000
Kifungu 2023 – *Immigration Njombe*………….....……Sh. 112,805,000
Kifungu 2024 – *Immigration Pwani*…………....…………Sh. 116,485,000

Kifungu 2025 – *Immigration Ruvuma*……………..……Sh. 117,775,000
Kifungu 2026 – *Immigration Rukwa*………..……..…….Sh. 119,005,000
Kifungu 2027 – *Immigration Simiyu*………..…...........Sh. 110,565,000
Kifungu 2028 – *Immigration Singida*……..……….…… Sh. 117,245,000
Kifungu 2029 – *Immigration Shinyanga*…….…..…..…Sh. 114,605,000
Kifungu 2030 – *Immigration Tanga*………….……..….Sh. 128,150,000
Kifungu 2031 – *Immigration Tabora*……….................Sh. 122,005,000
Kifungu 2032 – *Immigration Songwe*……………..……Sh. 124,545,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

Kifungu 3001 – *Fire and Rescue Services*.............Sh. 11,401,892,464
Kifungu 3002 – *Fire and Rescue Services Training Institute*..................................Sh. 606,016,328
Kifungu 3003 – *Fire Safety*…….....................................Sh. 659,546,308
Kifungu 3004 – *Operations*……………………..…………Sh. 890,366,476
Kifungu 3005 – Dar es Salaam *Regional Office*......Sh. 1,823,550,628
Kifungu 3006 – Arusha *Regional Office*……..............Sh. 1,413,776,040
Kifungu 3007 – Dodoma *Regional Office*…………Sh. 2,042,959,756
Kifungu 3008 – Mwanza *Regional Office*…..……….Sh. 1,681,480,800
Kifungu 3009 – Mbeya *Regional Office*……………..Sh. 1,207,896,800
Kifungu 3010 – Kinondoni *Regional Office*………. Sh. 1,353,306,800
Kifungu 3011 – Mara *Regional Office*……….…….….Sh. 651,302,100
Kifungu 3012 – Kigoma *Regional Office*.…….……….Sh. 856,920,100
Kifungu 3013 – Pwani *Regional Office*……………...Sh. 1,415,438,100
Kifungu 3014 – Manyara *Regional Office*…………....Sh. 896,810,100
Kifungu 3015 – Geita *Regional Office*………..………Sh. 759,138,100
Kifungu 3016 – Temeke *Regional Office*.……….......Sh. 1,669,826,800
Kifungu 3017 – Singida *Regional Office*…..…………..Sh. 701,267,600
Kifungu 3018 – Tabora *Regional Office*…….…………Sh. 919,554,800
Kifungu 3019 – Iringa *Regional Office*……………..……Sh. 992,449,700
Kifungu 3020 – Rukwa *Regional Office*…………..…...Sh.635,914,900
Kifungu 3021 – Ruvuma *Regional Office*……..….….Sh. 830,480,100
Kifungu 3022 – Kagera *Regional Office*…………..….Sh. 877,844,100
Kifungu 3023 – Mtwara *Regional Office*………….......Sh. 792,821,900
Kifungu 3024 – Lindi *Regional Office*……………..……Sh. 733,022,100
Kifungu 3025 – Njombe *Regional Office*……………....Sh. 728,658,900

Kifungu 3026 – Shinyanga *Regional Office*…………....Sh. 773,814,100
Kifungu 3027 – Ilala *Regional Office*………..….....Sh. 1,647,636,200
Kifungu 3028 – Kilimanjaro *Regional Office*……..……Sh. 924,768,800
Kifungu 3029 – Morogoro *Regional Office*…….…....Sh. 1,236,659,600
Kifungu 3030 – Katavi *Regional Office*……………..….Sh. 715,766,100
Kifungu 3031 – Tanga *Regional Office*………………Sh. 1,395,792,100
Kifungu 3032 – Simiyu *Regional Office*…………...…..Sh. 516,190,100
Kifungu 3033 – Songwe *Regional Office*………………Sh. 735,914,100
Kifungu 3034 – Fire and Rescue Training College…Sh. 1,828,652,100

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 29 – Jeshi la Magereza**

Kifungu 1001 – *Prisons Headquarters*…………...…Sh. 40,497,214,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…..……Sh. 3,212,237,000
Kifungu 2001 – *Parole Department*………….………Sh.1,283,373,000
Kifungu 2002 – *Prisons Welfare and Rehabilitation*………….………....Sh. 117,605,437,000
Kifungu 2003 – *Resettlement of Offenders*…....…....Sh. 1,690,933,000
Kifungu 2004 – *Prisons Arusha*…..............................Sh. 4,428,970,000
Kifungu 2005 – *Prisons Dar Es Salaam*…………...….Sh. 10,953,644,000
*Kifungu 2006 – Prisons Dodoma*……………………..….Sh. 5,387,040,000
Kifungu 2007 – *Prisons Kigoma*…………...………....Sh. 2,653,460,000
Kifungu 2008 – *Prisons Tanga*…………………...……Sh. 1,733,874,000
Kifungu 2009 – *Prisons Kagera*…………………...……Sh. 2,751,726,000
Kifungu 2010 – *Prisons Mwanza*...............................Sh. 1,413,548,000
Kifungu 2011 – *Prisons Tabora*……………………..……Sh. 1,449,606,000
Kifungu 2012 – *Prisons Mbeya*…………...……………Sh. 4,682,230,000
Kifungu 2013 – *Prisons Singida*.................................Sh. 2,089,642,000
Kifungu 2014 – *Prisons Coast*...................................Sh. 5,386,964,000
Kifungu 2015 – *Prisons Lindi*……………..……………...Sh. 665,674,000
Kifungu 2016 – *Prisons Manyara*……....…………………Sh. 2,326,822,000
Kifungu 2017 – *Prisons Mtwara*.................................Sh. 2,908,196,000
Kifungu 2018 – *Prisons Ruvuma*...............................Sh. 1,032,480,000
Kifungu 2019 – *Prisons Rukwa*……………………..……Sh. 1,830,161,000
Kifungu 2020 – *Prisons Mara*………………………...……Sh. 3,324,972,000
Kifungu 2021 – *Prisons Iringa*...................................…Sh. 2,532,746,000
Kifungu 2022 – *Prisons Kilimanjaro*...........................Sh. 2,381,470,000

Kifungu 2023 – *Prisons Morogoro*……….....…….…Sh. 5,010,196,000
Kifungu 2024 – *Prisons Geita*……………..…..………Sh. 1,691,106,000
Kifungu 2025 – *Prisons Katavi*....................................Sh. 1,109,090,000
Kifungu 2026 – *Prisons Njombe*.................................Sh. 1,217,114,000
Kifungu 2027 – *Prisons Simiyu*……………..…………Sh. 1,769,666,000
Kifungu 2028 – *Prisons Shinyanga*………….…..……Sh. 1,066,440,000
Kifungu 3001 – *Ukonga Prisons Staff College*…..…..Sh. 3,368,988,000
Kifungu 3002 – *Kingolwila Prisons Driving School*........Sh. 619,766,000
Kifungu 3003 – *Ruanda Prisons Trade School*.............Sh. 920,684,000
Kifungu 3004 – *Prisons College Kiwira*……..……...Sh. 1,368,124,000
Kifungu 4001– *Prison Building Brigade*……...……….Sh. 492,271,000
Kifungu 4002 – *Prison Industries*...................................Sh. 674,957,000
Kifungu 4003 – *Prison Farms*........................................Sh. 793,800,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 28 – Jeshi la Polisi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*......................Sh. 93,542,870,963
Kifungu 1002 – *Finance And Accounts*…..…….…Sh. 238,824,931,283
Kifungu 1003 – *Internal Monitoring and Evaluation Unit*……………..……….........................Sh. 337,949,719
Kifungu 1004 – *Legal and Research Services Unit*…………..........................………Sh. 375,152,350
Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit*….............................Sh. 364,130,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*….....Sh. 306,660,000
Kifungu 2001 – *Police Main Force*………….....………Sh. 6,173,263,200
Kifungu 2002 – *Police Marine*……………..……........Sh. 1,473,877,200
Kifungu 2003 – *Railway Police Division*……………......Sh. 3,690,032,000
Kifungu 2004 – *Police Signals Branch*……………..….Sh. 2,754,493,800
Kifungu 2005 – *Police Zanzibar*…………....………....Sh. 8,395,865,770
Kifungu 2006 – *Police Air Wing*……………..………......Sh. 2,268,712,477
Kifungu 2007 – *Tazara Police*……………..…...………Sh. 1,848,911,020
Kifungu 2008– *Field Force Unit*……………..…..………Sh. 1,962,436,240
Kifungu 2009 – *Traffic Police* ……………..…..…………Sh. 894,591,570
Kifungu 2010 – *Police Airport*……………...…..………Sh. 3,201,488,720
Kifungu 2011– *Police Dog and Horses*……………..……Sh. 994,358,000
Kifungu 2012 – *Dar Es Salaam Special Zone*…….…Sh. 8,901,024,369

Kifungu 2013 – *Police Ilala*.......................................Sh. 12,368,973,908
Kifungu 2014 – *Police Kinondoni*………….................Sh. 15,694,590,587
Kifungu 2015– *Police Temeke*………………..…………Sh. 7,047,675,736
Kifungu 2016 – *Police Arusha*……...........................Sh. 13,677,175,778
Kifungu 2017 – *Police Iringa*……………………..…..…Sh. 9,048,429,000
Kifungu 2018 – *Police Kilimanjaro*……….................Sh. 13,073,730,332
Kifungu 2019 – *Police Kigoma*………………...............Sh. 10,995,097,000
*Kifungu 2020 – Police Kagera*………………..............Sh. 11,576,997,244
Kifungu 2021 – *Police Lindi*…………….......…………....Sh. 7,407,351,920
Kifungu 2022 – *Police Mwanza*……………..........…….Sh. 16,834,106,979
Kifungu 2023 – *Police Mara*…………….........…………..Sh. 8,340,153,000
Kifungu 2024 – *Police Tarime - Rorya*………..………Sh. 7,503,979,000
Kifungu 2025 – *Police Mbeya*……...........................Sh. 11,793,656,750
Kifungu 2026 – *Police Mtwara*……………......………Sh. 9,632,074,972
Kifungu 2027 – *Police Morogoro*……….…………..…..Sh. 15,077,736,996
Kifungu 2028 – *Police Manyara*……………………....Sh. 10,291,392,992
Kifungu 2029 – *Police Singida*……………….....………Sh. 9,465,644,792
Kifungu 2030 – *Police Pwani*……..............................Sh. 9,595,704,988
*Kifungu 2031 – Police Ruvuma*……………................Sh. 8,713,626,000
Kifungu 2032 – *Police Rukwa*……………..…….........Sh. 7,048,635,000
Kifungu 2033 – *Police Tarime - Rorya*………….....….Sh. 9,502,336,000
Kifungu 2034 – *Police Tabora*……………....…………Sh. 9,318,266,348
Kifungu 2035 – *Police Tanga*……………...................Sh. 11,901,322,344
Kifungu 2036 – *Police Mjini Magharibi*……………......Sh. 11,507,534172
Kifungu 2037 – *Police Kusini Unguja*……………........Sh. 3,846,426,000
Kifungu 2038 – *Police Kaskazini Unguja*………….…Sh. 3,711,086,984
Kifungu 2039 – *Police Kusini Pemba*…………….......Sh. 3,326,398,400
Kifungu 2040 – *Police Kaskazini Pemba*……….….....Sh. 3,277,161,400
Kifungu 2041 – *Police Dodoma*…………….............Sh. 18,347,464,375
Kifungu 2042 – *Police Geita*…………………….......Sh. 9,270,569,610
Kifungu 2043 – *Police Katavi*……………………..........Sh. 5,298,263,987
Kifungu 2044– *Police Njombe*…..……………………....Sh. 6,560,910,342
Kifungu 2045 – *Police Simiyu*…………….….............Sh. 6,302,049,753
Kifungu 2046 – *Police Songwe*…………..…...............Sh. 5,343,071,361
Kifungu 2047 – *Police Rufiji*…………………………....Sh. 4,725,899,000
Kifungu 2048 – *Tpf Corporation Sole Unit*……….........Sh. 158,364,000
Kifungu 2049 – *Police Bandari*……………………..…Sh. 2,583,554,000
Kifungu 2050 – *Police Band*……………......................Sh. 1,399,970,749
Kifungu 2051 – *Police Bohari*…………………….........Sh. 13,626,481,000
Kifungu 3001 – *Police College Moshi*………………Sh. 23,502,814,766

Kifungu 3002– *Police College*…………………………..….Sh. 2,575,728,000
Kifungu 3003 – *Operations and Training*……….......Sh. 1,754,527,380
Kifungu 3004 – *Zanzibar Police College*……….……Sh. 1,028,342,600
Kifungu 3005 – *Mwanza Marine Police College*……..Sh. 884,918,800
Kifungu 3006 – *Tanzania Police Staff College–Kidatu*..............................…Sh. 1,537,167,000
Kifungu 4001 – *Police Vehicles Maintenance Unit*..Sh. 2,520,354,000
Kifungu 5001 – *Police Medical Unit*………………......Sh. 2,702,468,000
Kifungu 6001 – *Police Ujenzi*…………………….........Sh. 1,062,639,200
Kifungu 7001 – *Criminal Investigation Division*….…..Sh. 5,482,236,387
Kifungu 7002 – *Stock Theft Prevention Unit*…..............Sh. 660,175,000
Kifungu 7003 – *Criminal Intelligence Bureau*…...…..Sh. 1,805,976,800
Kifungu 7004 – *Forensic Intelligence Bureau*…..…..Sh. 2,767,343,027
Kifungu 7005 – *Community Engagement*……..……....Sh. 979,917,560

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

Kifungu 3001 – *Fire and Rescue Services*.................Sh. 9,930,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 28 – Jeshi la Polisi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…...................................Sh. 0
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts*……..............Sh. 15,665,927,723
Kifungu 2004 – *Police Signals Branch*…....................Sh. 1,286,000,000
Kifungu 2005 – *Police Zanzibar*……..............................................Sh. 0
Kifungu 2006 – *Police Air Wing*……..............................................Sh. 0
Kifungu 2015 – *Police Temeke*…………….......……Sh. 126,457,320
Kifungu 2016 – *Police Arusha*……….………………....Sh. 139,000,000
Kifungu 2020 – *Police Kagera*….……………….......Sh. 1,000,000,000
Kifungu 2023 – *Police Mara*……...................................................Sh. 0
Kifungu 2025– *Police Mbeya*.……................................Sh. 100,000,000

Kifungu 2026 – *Police Mtwara*……...............................................Sh. 0
Kifungu 2028 – *Police Manyara*……....……………..….Sh. 1,383,849,000
Kifungu 2029 – *Police Singida*……...............................................Sh. 0
Kifungu 2031 – *Police Ruvuma*……..............................................Sh. 0
Kifungu 2034 – *Police Tabora* ……................................................Sh. 0
Kifungu 2035 – *Police Tanga*……....................................................Sh. 0
Kifungu 2036 – *Police Mjini Magharibi*……………........Sh. 822,370,953
Kifungu 2037 – *Police Kusini Unguja*…………….….…Sh. 554,401,700
Kifungu 2038 – *Police Kaskazini Unguja* ……................................Sh. 0
Kifungu 2039 – *Police Kusini Pemba*……........................................Sh. 0
Kifungu 2040 – *Police Kaskazini Pemba* ……………….Sh.178,086,000
Kifungu 2041 – Police Dodoma…………………….……Sh. 302,249,004
Kifungu 2044 – Police Njombe ………………………….........…Sh. 0
Kifungu 2045 – Police Simiyu…..…………………….....Sh. 220,000,000
Kifungu 2047 – Police Rufiji……………………….………Sh. 300,000,000
Kifungu 2051 – Police Bohari…………………………..Sh. 3,865,910,256
Kifungu 3004 – Zanzibar Police College……………......Sh. 178,803,205
Kifungu 5001– *Police Medical Unit*…………………..…Sh. 528,000,000
Kifungu 7004 – *Forensic Intelligence Bureau*………...…Sh. 442,183,839
Kifungu 7005 – *Community Engagement*……..………Sh. 100,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 29 – Jeshi la Magereza**

Kifungu 1001 – *Prisons Headquarters*........................Sh. 3,730,000,000
Kifungu 4001– *Prison Building Brigade*……..…..….Sh. 7,379,600,000
Kifungu 4002 – *Prison Industries*....................................Sh. 500,000,000
Kifungu 4003 – *Prison Farms*.......................................Sh. 4,760,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 51 - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

Kifungu 1001 – *Administration and Huma Resources Management Division*......................Sh. 41,094,585,000
Kifungu 4002 – *Anti-Trafficking in Person Secretariat*..........................................Sh.2,200,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji**

Kifungu 2002 – *Immigration Head Quarter*…………Sh. 8,240,525,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. RUTH MAKUNGU - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2020, Kanuni ya 123(3)(a) na (b), naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi yake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Naamini walioafiki wameshinda. Kwa hiyo Bunge limepitisha rasmi Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Nichukue nafasi hii kukupongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na tunawatakia utekelezaji mwema wa haya yote mliyoahidi mbele ya Waheshimiwa Wabunge.

Pia nichukue nafasi hii kukupongeza Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti, pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa kazi kubwa mliyoifanya lakini na Waheshimiwa Wabunge ambao pia mlipata nafasi pia ya kuchangia katika hoja hii iliyokuwa mbele yetu. Nawapongeza sana.

Baada ya kusema haya, naahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.58 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 30 Mei, 2023, Saa Tatu Asubuhi)*